
ARIGATOU INTERNATIONAL
All for Children

Ethics Education

GNRC

# Kujifunza Kuishi Pamoja

## Programu ya Utamaduni na Muingiliano wa Dini Mbalimbali kwa Elimu ya Maadili



UNESCO
United Nations
Educational, Scientific and
Cultural Organization

unicef

# Kujifunza Kuishi Pamoja

## Programu ya Utamaduni na Muingiliano wa Dini Mbalimbali kwa Elimu ya Maadili

**Baraza la Dini Mbalimbali Kuhusu Elimu ya Maadili kwa Watoto**

**Mtandao wa Kimataifa wa Dini kwa Watoto**

**Arigatou International**

**Kwa Ushirikiano na kwa kuridhiwa na UNESCO na UNICEF**

Sekretarieti ya Baraza la Dini Mbalimbali inakaribisha maombi ya idhini ya kunakili na kutafsiri sehemu au kitabu chote. Maombi na maulizo yapelekwe kwa Arigatou International, 1 rue de Varembé, 1202 Geneva, Switzerland ambayo itafurahi kutoa taarifa za karibu zaidi kuhusu mabadiliko yaliyofanywa kwenye matini.

Usanifu, mpangilio na michoro na services-concept.ch
na Sekretarieti ya Baraza la Dini (Geneva).

Kimechapwa Dar es Salam, Tanzania na Jamana Printers Limited.

Kitabu hiki kinaweza kurejewa na kupakuliwa kwenye tovuti ifuatayo:
http://www.ethicseducationforchildren.org

© Arigatou International 2008 ISBN: 978-92-806-4677-1

# Yaliyomo

## Kujifunza Kuishi Pamoja


**Watoto na Elimu ya Maadili** ... **1**
Namna kitabu cha *Kujifunza Kuishi Pamoja* kilivyotayarishwa ... 1
Mahali *Kujifunza Kuishi Pamoja* kinapoweza kutumika ... 2
Watoto Kama Wajibu wa Kimaadili wa Pamoja ... 3
Watoto – Zawadi na Wajibu ... 4
Watoto hujifunza wanachoishi ... 5
Elimu ya Maadili na Haki za Binadamu ... 6

**Maadili na Elimu ya Maadili** ... **7**
Maadili, Unyofu na Uadilifu ... 8
Maadili inahusu uhusiano ... 8
Je, kuna unyofu wa kudumu? ... 9
Kanuni za Kimaadili na Unyoofu wa Maadili ya Msingi kwa Elimu ya Maadili ... 10
Uwezo wa kuchagua: Tunu kubwa na wajibu wenye changamoto nzito kuliko zote ... 10
Kulinda na kutetea hadhi ya binadamu ... 11
Heshima na kuelewana ... 11
Ushirikali na uwezo wa "kuchukua madhila ya mtu mwingine" ... 12
Wajibu wa Mtu mmoja na wa Pamoja ... 13
Upatanisho na mbinu za kujenga mahusiano ... 13
Elimu ya Maadili ... 14

**Ubinadamu wetu** ... **15**
Maelezo thabiti kuhusu ubinadamu wetu ... 15

**Ulimwengu wenye dini mbalimbali** ... **16**
Rasilimali za dini kwa maisha ya kiadilifu ... 16
Vipimo vinne vya dhima ... 16
Mchamungu na asiye na dini ... 17
Kujifunza Kuhusiana baina yetu ... 17
Kusali Pamoja au Kuja Pamoja Kusali ... 18

**Mambo ya Kiroho** ... 19


## Sehemu ya 1 Mwongozo wa Mtumiaji 21


**Upeo na Madhumuni** ... **21**

**Moduli za Kujifunza** ... **21**
Unyofu wa Aina nne ... 22
Moduli ... 23
Kulea vijana wajenge mambo yao ya kiroho waliyozaliwa nayo ... 24
Waelimishaji wa Wawezeshaji – kiini cha mchakato wa kujifunza ... 24

**Mchakato wa kujifunza** ... **25**

**Mbinu za ufundishaji** ... **27**
Njia zilizopendekezwa ... 28
Mbinu zilizopendekezwa ... 29

**Kujenga Mazingira Yanayofaa** 32
Kuwa Mfano wa Kuigwa 32
**Namna ya Kuanza Moduli za Kujifunza** 33
**Je, *Kujifunza Kuishi Pamoja* kitumiwe pamoja na nani?** 35
**Je, *Kujifunza Kuishi Pamoja* kitumiwe wapi?** 35
**Je, ni nani anaweza kutumia *Kujifunza Kuishi Pamoja*?** 36
**Kijitabu cha Washiriki** 37
**Je, Naweza kufanya nini kama…** 38
Sina kikundi chenye dini mbalimbali. 38
Nataka kutatua masuala ya kijamii badala ya masuala ya kidini 38
Nina mivutano kwenye kikundi kwa sababu ya tofauti za kidini. 39
Washiriki wamekabiliwa na hali za vurugu 40
Mada za Warsha zinasababisha jazba za hatari kwa Washiriki 41

## Sehemu ya 2 Moduli za Kujifunzia 43

**Moduli ya 1 Kujielewa Binafsi na Wengine** 44
Kukubali uanuwai 45
Kujitambua mwenyewe Kuhusiana na wengine 45
Ubinadamu Wetu 46
Je, tunaweza kupatana? 46
Kujiweka katika nafasi ya mtu mwingine 47
Kushughulikia mahitaji ya kuelewana 47
**Moduli ya 2 Kuubadili Ulimwengu Pamoja** 48
Inakuwaje wakati tunaposhindwa Kuheshimiana? 49
Kuelewa migogoro, ugomvi na uonevu vinavyonizunguka 49
Amani inaanzia kwangu 50
Mibadala isiyo na ugomvi 50
Matembezi ya Usuluhishi 51
Kujenga madaraja ya kuaminiana 51
Kushirikiana kuubadili Ulimwengu 52

## Sehemu ya 3 Usimamizi wa maendeleo 53

**Logu ya Kujifunza** 53
**Njia za Kupima Kujifunza kwa Washiriki** 54
Njia ya Rika kwa Rika 55
Njia ya Kushirikiana kwa Kikundi 56
Njia ya Mimi na Ulimwengu 57
Njia ya Ushauri 58
Njia ya Chati ya Kuhakiki 59
**Njia za Kupima ya 'Kipima Joto'** 60
**Tathmini ya Athari** 61

## Sehemu ya 4 Shughuli 63

Jedwali la Shughuli 63

## Sehemu ya 5 Nyenzo 123

Hadithi 123
Uchunguzi Kifani 138
Mitanziko ya Uadilifu 143
Filamu na Video 149
Nyimbo 156
Mashairi 159
Sala za Amani 167
Igizo Dhima 175
Kadi za Habari za Amani 177
Muhtasari wa Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto 179
Muhtasari wa Tamko la Kimataifa la haki za Binadamu 182
Namna ya Kukunja Korongo wa Karatasi 183

## Sehemu ya 6 Tulifanya Kama Hivi 187

## Sehemu ya 7 Marejeo 219

Nyenzo 219
- Hadithi 219
- Mashairi 219
- Sala za Amani 220
- Uchunguzi kifani 220
- Mitanziko ya Uadilifu 220
- Maandiko ya Msaada kwa Ajili ya 220
- Shukurani na Marejeo kwa Ajili ya Shughuli 221

Faharasa 222
Vifupisho 224
Orodha ya Wajumbe wa Baraza la Dini Mbalimbali 225
Orodha ya Wajumbe wa Kamati ya Baraza la Dini Mbalimbali Kuhusu Elimu Maadili kwa Watoto 226
Waratibu wa GNRC 227

Viambatisho 228
- Fomu ya tathmini 228
- Matriki kwa ajili ya tathmini ya matokeo 230

## Shukurani

*Kujifunza Kuishi Pamoja* imenufaishwa na msaada wa asasi nyingi na marafiki. Tunatoa shukurani kwa mashirika mengi, wataalamu, waandisi wa vitabu, wapitiaji wa rika, washauri, waelekezi, watu wa kujitolea, wahitimu walio mafunzoni na Sekretarieti ya Baraza la Dini Mbalimbali, ambao kujituma na kujitolea kwao kwa dhati kumewezesha kukamilika kwa kitabu hiki.

## Baraza la Dini Mbalimbali kuhusu Elimu ya Maadili kwa Watoto

Mshauri wa Heshima: HRH Prince El Hassan bin Talal.

Wajumbe wa Baraza: A.T. Ariyaratne, Adolfo Perez Esquivel, Kul Gautam, Hans Kung, Bibifatemeh Mousavi Nezhad, Alice Shalvi, Didi Athavale Talwalkar, Anastasios Yannoulatos, Nour Ammari na Emanuel Mathias.

Wajumbe wa Kamati: Hasan Abu Nimah, Swami Agnivesh, Charanjit Ajit Singh, Farida Ali, Ibrahim Al-Sheddi, Kezevino Aram, Wesley Ariarajah, Alicia Cabezudo, Meg Gardinier, Andres Guerrero, Magnus Haavelsrud, Heidi Hadsell, Vinod Hallan, Stuart Hart, Azza Karam, Method Kilaini, Marlene Silbert, Hans Ucko, Deborah Weissman na Sunil Wijesiri wardhana.

## GNRC

Waratibu: Mustafa Ali, Vinya Ariyaratne, Razia Ismail, Marta Palma, Marcedes Roman, Qais Sadiq na Dorit Shippin, na wafanyakazi wenzao katika kanda.

Wajumbe wa GNRC katika Kanda.

Katibu Mkuu Arsushi Iwasaki na wenzao katika Sekretarieti ya GNRC, Tokyo.

## Watoto na Vijana

Wawezeshaji wote wa watoto, vijana na wawezeshaji vijana, waliohusishwa katika utayarishaji wa nyenzo ya kufundishia kupitia warsha mbalimbali za majaribio na mafunzo katika sehemu mbalimbali za dunia.

## Umoja wa Mataifa na Mashirika ya Kimataifa

Mfuko wa Watoto wa Umoja wa Mataifa (UNICEF), hasa Tanya Turkovich, pamoja na wenzake bila ya kuwasahau waliotajwa hapo awali.

Shirika la Elimu Sayansi na Utamaduni la Umoja wa Mataifa (UNESCO), hasa Hélène Gosselin na Linda King.

## Wataalamu Walioalikwa

Gana Dash, Mahal da Costa Soto na David Arond.

## Wasomaji Walioalikwa

Soho Machida, Adib Saab, Halim Nujaim, May Sadiq, Amada Benavides, Jenny Nemko, Heather Jarvis na Leilah Omar.

## Utayarishaji wa Kitabu

Arnaud Dubouchet na wenzake katika Services Concept, kwa usanifu, mpangilio na michoro.

Suraj Vaidya na wenzake katika Jamana Printers Limited, kwa uchapaji.

## Picha

Picha za jalada na kwenye kurasa 189-191, 195, 204-207, 209 na Mustafa Ali

Picha za kurasa 210, 212 na Rolando Calle

Picha za kurasa 198-200 na Satish Kanna

Picha za jalada na kwenye kurasa 216-218 na Peter Williams

Picha za jalada na kwenye kurasa 192-197, 200-203, 207-216, 218 na Maria Lucia Uribe

## Arigatou International

Katibu Mkuu Shozo Fujita na wenzake Makao Makuu Tokyo.

Peter Billings, mhariri na mwandishi.

## Sekretarieti ya Baraza la Dini Mbalimbali

Katibu Mkuu Agneta Ucko na wenzake, Maria Lucia Uribe Torres na Djénane Tosbath de los Cobos, pamoja na waelekezi wengine na wahitimu walio mafunzoni.

## Dibaji

*Kujifunza Kuishi Pamoja* ni mafanikio ya kwanza ya juhudi za elimu ya maadili ya dunia iliyozinduliwa na Arigatou Foundation na Mtandao wa Kimataifa wa Dini kwa Watoto (GNRC).


Baraza la Dini Mbalimbali kuhusu Elimu ya Maadili kwa Watoto lilianzishwa na Arigatou International na kuwa kama kituo cha taarifa na kiungo cha kimataifa kwa mazungumzo, ushirikiano na hatua za uhimizaji elimu ya maadili kwa watoto na kujifunza dini mbalimbali.

Tangu lilipoanzishwa, Baraza la Dini Mbalimbali kuhusu Elimu ya Maadili kwa Watoto limelenga kazi zake katika utayarishaji wa kitabu hiki muhimu kwa ajili ya kuzinduliwa kwenye Mkutano wa Tatu wa GNRC, Hiroshima, mwezi Mei, 2008. Uhimizaji wa elimu ya maadili unafanywa kwa ushirikiano na wale wote wanaokubaliana na dira ya juhudi ya elimu ya maadili – jamii za kidini, mashirika ya Umoja wa Mataifa, Asasi zisizo za Serikali (AZISE) na mengine mbalimbali – katika juhudi za kutimiza haki za mtoto na maendeleo kamili na yenye afya ya mwili, akili, roho, uadilifu na kijamii, pamoja na haki ya mtoto ya kupata elimu kama ilivyoandikwa kwenye Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto.

Mchakatao shirikishi wa kutayarisha kitabu hiki umekutanisha uzoefu wa waelimishaji na wasomi kutoka dini mbalimbali, utamaduni wa kiroho na usio na dini, mashirika ya kimataifa, AZISE, asasi za kielimu na watoto. Tunatoa shukurani maalumu kwa muda na juhudi zilizotumiwa na wenzetu wa UNICEF na UNESCO katika kutayarisha na kuwasilisha kitabu hiki.

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kinakabili suala la Elimu ya Maadili kwa mitazamo ya kujifunza kwa njia ya utamaduni na dini mbalimbali, haki za binadamu na elimu bora, ambapo maadili na unyoofu vinaelimishwa na ambapo watoto wanapewa nafasi ya kuendeleza uwezo wao wa kuzaliwa kwa mambo ya roho. Ni matarajio yetu kwamba nyenzo hii mpya itatupatia zana zinazohitajika kuzidi kukuza maadili na unyofu kwa watoto na kusaidia kujenga dunia bora zaidi.

Sote tuna dhima ya kuitekeleza.



**Takeyasu Miyamoto**
Raisi muadhimiwa wa Arigatou International
Mwasisi wa GNRC



**Keishi Miyamoto**
Raisi wa Arigatou International

**Arigatou International** ni AZISE ya kidini ya kimataifa yenye dhamira ya kubuni mazingira mazuri kwa watoto wote duniani.

**Mtandao wa Kimataifa wa Dini kwa Watoto (GNRC)** ni moja kati ya juhudi muhimu za taasisi ya Arigatou kwa ushirikiano kati ya dini mbalimbali.

**Baraza la Dini Mbalimbali kuhusu Elimu ya Maadili kwa Watoto** ni kituo cha taarifa cha kimataifa na kama kiungo cha mazungumzo, ubia na hatua kuhusu elimu ya maadili kwa watoto.

***Kujifunza Kuishi Pamoja*** ni Programu ya utamaduni na dini mbalimbali kwa elimu ya maadili, iliyotayarishwa kwa kuchangia katika utimizaji wa haki za mtoto na maendeleo kamili na yenye afya ya mwili, akili, roho, uadilifu na kijamii na kupata elimu kama ilivyoandikwa kwenye Makubaliano ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto (CRC), katika ibara ya 26.1 ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu (UDHR), katika Azimio la Dunia kuhusu Elimu kwa wote na Malengo ya Maendeleo ya Milenia. Ni nyenzo kwa waelimishaji na viongozi wa vijana.

## Madhumuni

Madhumuni ya ***Kujifunza Kuishi Pamoja*** ni:

1. Kuimarisha uwezo wa watoto na vijana kufanya uamuzi wa kimaadili uliofundishwa vizuri kwa misingi ya unyofu unaohimiza heshima kwa utamaduni na imani nyingine.
2. Kuwawezesha watoto na vijana kushiriki katika mazungumzo – kusikiliza na kuzungumza kama njia ya kuendeleza hisia zaidi za kujali tofauti na kuelewa watu wengine.
3. Kuendeleza uwezo wa watoto na vijana kutekeleza mahitaji ya jamii zao kwa mtazamo wa upatanishi na heshima kwa uanuwai na kuchangia kwa hali hii katika utamaduni wa amani.
4. Kuwaruhusu watoto na vijana kutambua na kuendeleza mambo yao ya kiroho.
5. Kukubali hadhi ya binadamu kama ilivyoelezwa katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu, CRC na katika mafundisho ya mila na desturi za dini zote.
6. Kukubali uwezekano wa kuishi pamoja, kuheshimiana katika ulimwengu wa dini, mbari na mila na desturi tofauti.
7. Kuwapa waelimishaji zana za kufanyia kazi katika kujifunza utamaduni na dini mbalimbali kwenye kanda tofauti na katika mazingira ya uanuwai.
8. Kutayarisha na kuhimiza desturi zilizofanikiwa za kuishi pamoja na watu, utamaduni, mbari, imani na dini tofauti.

# Watoto na Elimu ya Maadili

Mwezi Mei, 2000 Arigatou International ilizindua **Mtandao wa Kimataifa wa Dini kwa Watoto** (GNRC) kuhimiza ushirikiano miongoni mwa watu tofauti wanaoshiriki katika shughuli za kutimiza haki za watoto na kuchangia katika ustawi wao.

GNRC inashirikiana kwa karibu na wachamungu pamoja na mashirika ya kimataifa, serikali, AZISE, wasomi, viongozi wa biashara, na wanaume, wanawake na watoto kutoka hali mbalimbali za maisha. Kwa ushirikiano na huduma za kufikia, GNRC inaendeleza harakati za kimataifa za kuanzisha mazingira bora zaidi kwa watoto katika karne ya 21.

Jumuiya ya kimataifa imekaribisha kwa mikono miwili juhudi za dini mbalimbali zinazowalenga watoto, na Arigatou International inashirikiana kwa karibu sana na Umoja wa Mataifa katika kazi yake ya kutetea haki za watoto. Katika kikao maalumu cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kuhusu Watoto, mwezi Mei, 2002, Mchungaji Tekeyasu Miyamoto, Kiongozi wa Myochikai na Raisi wa Arigatou International na mwasisi wa GNRC, alitoa hotuba kwa niaba ya GNRC katika Kikao cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Katika hotuba yake, Mchungaji Miyamoto alipendekeza kuanzishwa kwa **Baraza la Dini Mbalimbali kuhusu Elimu ya Maadili kwa Watoto**. Baraza hilo litakuwa na watu wa dini, waelimishaji na wengine wanaofanya kazi, pamoja na Umoja wa Mataifa kukuza mambo ya kiroho kwa watoto – maadili yao na heshima kwa watu wa dini na ustaarabu tofauti sehemu muhimu ya "elimu bora" iliyoahidiwa katika Waraka wa Matokeo ya Mkutano Mkuu Maalumu, *"Ulimwengu Unaowafaa Watoto"*.

Katika kutafakari wazo la baraza hilo, GNRC ilifanya mikutano ya mara kwa mara ambapo iliwaalika wataalamu wa maadili na elimu, wawakilishi kutoka UNICEF na UNESCO na viongozi wengine wanaohusika na wanazuoni. Katika Mkutano wa Pili wa GNRC uliofanyika Geneva, Switzerland, Mei, 2004 na kwa kuidhinishwa na Mchungaji Miyamoto, Baraza la Dini Mbalimbali kuhusu Elimu ya Maadili kwa Watoto lilianzishwa rasmi.



## Namna kitabu cha *Kujifunza Kuishi Pamoja* kilivyotayarishwa

Baraza la Dini Mbalimbali kuhusu Elimu ya Maadili kwa Watoto linahimiza elimu ya maadili kwa njia ya kujifunza utamaduni na dini mbalimbali kusaidia jamii na jumuiya kuishi pamoja kwa amani, na kuwaheshimu wengine na hadhi ya utu kwa binadamu wote. Ni kutokana na moyo huu ndipo kitabu cha *Kijifunza Kuishi Pamoja* kilivyotayarishwa.

Baraza la Dini Mbalimbali kuhusu Elimu ya Maadili kwa Watoto likiwa na shauku ya kuhimiza ushirikiano wa kweli kati ya watu na dini mbalimbali, liliwashirikisha wasomi, waelimishaji na wataalamu wa elimu kutoka dini tofauti na mila na desturi zisizo na uhusiano wa dini kukutana kuanza kutayarisha nyenzo hii. Kikundi hicho kilivutwa sana kwa uelewa kwamba uanuwai una manufaa si kutuwezesha sisi kujua zaidi kuhusu watu wengine, bali pia kujielewa zaidi sisi wenyewe.

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kinaongozwa na wito wa pamoja wa kulinda utu na heshima ya binadamu. Shabaha yake ni kuimarisha dhamira ya watoto kwa haki, kuheshimu haki za binadamu na kujenga uhusiano wenye amani na utulivu kati ya watu wa ndani ya jamii. *Kujifunza Kuishi Pamoja* kinawapa viongozi wa vijana na waelimishaji duniani kote zana kwa ajili ya programu ya utamaduni, na dini mbalimbali itakayowawezesha watoto na vijana kukuza hisia imara ya maadili. Kimesanifiwa kuwasaidia vijana kuelewa na kuheshimu watu kutoka utamaduni na dini nyingine na kukuza hisia yao ya duniani kama jumuiya moja. Kitabu hiki kimetayarishwa kwa ushirikiano wa karibu na UNICEF na UNESCO.

Jina la kitabu la *Kujifunza Kuishi Pamoja* limechaguliwa kutokana na moja ya nguzo kuu za *Kujifunza: Dafina Iliyomo*, ripoti ya UNESCO ya Tume ya Kimataifa kuhusu Elimu kwa Karne ya Ishirini na Moja iliyoelezwa na Jacques Delors.[1]

## Mahali *Kujifunza Kuishi Pamoja* kinapoweza kutumika

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kimetayarishwa kwa kutumika kwenye miktadha mbalimbali ya dini na isiyo ya dini kama kitabu cha marejeo kwa kila anayehusika na uhimizaji wa maadili na unyofu. Madhumuni yamekuwa ni kutayarisha kitabu cha marejeo kitakachofaa kutumika katika ngazi ya kimataifa na kuweza kubadilishwa kwa urahisi kulingana na utamaduni wa jamii husika.

Kitabu hiki kimefanyiwa majaribio katika kanda na utamaduni tofauti kuhakikisha kwamba kinafaa kulingana na muktadha wa kanda na mahali husika (angalia “Tulifanya Kama Hivi”, uk. 187). Warsha za majaribio zilifanywa kwenye nchi 10 tofauti ambazo GNRC iliweza kuwakutanisha mashirika mbalimbali ya dini na yasiyo ya mfungamano wa dini yanayoshughulikia watoto. Katika warsha hizo za majaribio, kitabu hiki cha marejeo kilitumika kwa manufaa ya watoto na vijana zaidi ya 300 waliowakilisha Dini za Jadi za Kiafrika, Madhehebu ya Bahai, Kibuddha, Kikristo, Kihindu, Kiislamu, Dini ya Kiyahudi, wajumbe wa Brahma Kumaris na watu mbalimbali wenye uwakilishi usiokuwa na dini. Warsha za majaribio pamoja na mapendekezo na maoni kutoka kwa wataalamu wa maeneo na fani za elimu, maadili, mambo ya kiroho, kujifunza utamaduni na dini mbalimbali na haki za watoto walichangia uzoefu muhimu na fursa za kujifunza kwa uboreshaji na matayarisho ya kitabu hiki.

*Kujifunza Kuishi Pamoja* tayari ina mafanikio. Katika programu ya GNRC nchini Israel, kitabu hiki kilitumika katika ziara ya siku sita ya kikundi cha vijana wa dini ya Kiyahudi, Wakristo na Waislamu kwenye maeneo ya kihistoria ya Israel na Palestine, yote yana umuhimu mkubwa kwa migogoro kwenye ukanda wao. Katika kila kituo, washiriki vijana walijadili maadili yao na mitazamo tofauti kuhusu historia yao ya pamoja. Walihitimisha uzoefu wao kwa maneno yafuatayo:

> *“Tumeshirki pamoja katika kujifunza kwa kina uzoefu – kujua zaidi kuhusu historia ya kila mmoja, utamaduni na imani wakati huo huo tuliimarisha kujua sisi ni kina nani, utambulisho wetu, kujenga uelewa imara na wenye misingi madhubuti zaidi. Tulishughulikia masuala magumu na yenye changamoto kubwa bila kuathiri uhusiano wetu ndani ya kikundi na bila kutumia ubishani na hoja zinazoumiza na kukatisha tamaa. Ziara hii ingeweza kuwa mwanzo wa kuvunja kuta za tofauti na kujitenga zilizojengwa kati ya makundi mbalimbali ya mataifa na dini nchini mwetu, hata hivyo ilikuwa ziara muhimu na yenye mafanikio. Katika hali ya sasa ya kukata tamaa, hatua ndogo kama hizi ni nadra na zenye thamani kubwa na sote hatuna budi kuona fahari na wenye kupendelewa kwa kushiriki.”*

Kijana Kalpana mwenye umri wa miaka 15 kutoka New Delhi, India, aliyehudhuria warsha ya elimu ya maadili ya wiki moja nchini India ambako kitabu hiki kilitumika, alikuwa na haya ya kusema:

> *“Nilijua kuhusu kuwaheshimu watu wengine wakati nilipofika hapa, lakini sasa nimeanza kujua maana yake nini hasa na tunachotakiwa kufanya kimtazamo na vitendo sisi kama vijana wa Kihindu, Kiislamu na Kikristo kwa pamoja kuboresha jamii zetu.”*

Naye kijana Mohamed mwenye umri wa miaka 16 kutoka Kenya, alitumia maarifa aliyojifunza katika warsha ya majaribio kuhusu elimu ya maadili kuunda Klabu ya Amani kaskazini mwa Kenya. Amewakusanya vijana katika kijiji chake wapange afua zisizotumia nguvu kwa changamoto mbalimbali zinazokabiliwa na kijiji, kuhamasisha harakati za vijana zenye mwamko wa kuleta mabadiliko ya amani.

1 http://www.unesco.org/delors/Itolive.htm

Warsha ya elimu ya maadili ilifanywa kwa walimu, wazazi na vijana katika maeneo ya mpakani yenye migogoro kati ya Colombia na Ecuador. Kwa kutumia uchunguzi kifani, maigizo na majadiliano, washiriki waliyabainisha masuala yanayosababisha migogoro, wakachunguza hatua mbadala zisizotumia nguvu na waliahidi moyo wa kujitolea kwa ajili ya kujenga amani. Mmoja wa wawezeshaji kutoka Colombia alitoa maoni haya kuhusu matokeo ya warsha.

> *"Athari za migogoro ya kivita nchini Colombia zimejengeka sana katika tabia, mienendo na mitazamo ya baadhi ya vijana walioathiriwa moja kwa moja na hali hiyo. Hali hiyo inaweza kuwajengea chuki na kutowavumilia wenzao. Nilifurahi kuwaona watoto wakimbizi wa Colombia wanaoishi Ecuador wakieleza uzoefu wao, hofu yao na wao wenyewe kupendekeza namna ya kuwaheshimu na kuwathamini wengine, kuridhia tofauti zao, kuridhika kwa namna isiyotumia nguvu wala ugomvi hata kama haki zao zimekiukwa. Waligundua kuwa wanaweza kuwa sehemu ya ufumbuzi kuliko kuwa sehemu ya tatizo."*

*Kujifunza Kuishi Pamoja* ni kitabu kinachoweza kutumika kulingana na hali ya mahali husika na kutumiwa na watoto kutoka dini, utamaduni na jamii tofauti kukuza unyofu wa pamoja na kuheshimu tofauti zao za kihistoria na mila na desturi. Kitabu hiki kinatoa fursa ya kuimarisha uwezo wa kuzaliwa wa watoto kwa mambo ya kiroho na matarajio ya maisha bora zaidi duniani, kama mchango wa kubadili hali kwa watoto duniani kote. Sehemu ya 1, Mwongozo wa Mtumiaji inatoa maelezo yote muhimu kwa matumizi ya kitabu hiki.

UNESCO na UNICEF wameshirikishwa kwa karibu sana katika utayarishaji wa *Kujifunza Kuishi Pamoja* na wameridhia kitabu hiki kuwa mchango muhimu kwa elimu bora inayozingatia jamii yenye dini na utamaduni mwingi[2]. Mwongozo wa UNESCO kwa elimu yenye utamaduni tofauti inasisitiza falsafa na mkabala wa kitabu hiki.

> *"Elimu ya dini inaelezwa kuwa ni kujifunza kuhusu dini na desturi za kiroho za mtu binafsi au kujifunza kuhusu dini na imani nyingine. Elimu ya dini mbalimbali, kinyume chake, inalenga kujenga uhusiano kati ya watu kutoka dini tofauti".*[3]

## Watoto Kama Wajibu wa Kimaadili wa Pamoja

> *"Wakati wowote duniani kuna takriban watoto bilioni mbili wanaoishi miongoni mwetu. Vijana na akili bilioni mbili wenye uwezo mkubwa wa binadmu na ambao kwa pamoja ni muhimu hustahili malezi yetu".*[4]

Tunaishi katika lindi la uzuri wa maajabu ya viumbwa, miujiza ya maisha na uwezo mkubwa wa binadamu kutayarisha maisha – kuyafanya kuwa baraka kwa wote. Hata hivyo tunaishi katika ulimwengu uliotawaliwa na ghasia na vita, umaskini na ukiukwaji wa haki au dhuluma.

Ukuaji na maendeleo ya watoto ni pamoja na kimwili, kiakili, kijamii, kiutamaduni, kiroho, kidini na kimazingira. Cha kusikitisha, umaskini, kukosekana kwa mahitaji ya msingi na elimu, maradhi na utapiamlo bado vinaathiri watoto wetu wengi.

Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto (CRC) inabainisha haki za mtoto kusema na kusikilizwa (ibara ya 12) kuhusu masuala yanayowakera na kutamka kwa dhati kuwa:

> *"Mtoto hana budi kuandaliwa kwa ukamilifu kuishi maisha binafsi katika jamii na kulelewa katika moyo wa matazamio makubwa yaliyotajwa katika Katiba ya Umoja wa Mataifa, na hasa moyo wa amani, hadhi, uvumilivu, uhuru, usawa, haki na mshikamano."*

2 www.unesco.org/education

3 UNESCO *Guidelines for Intercultural Education*, uk. 14

4 Kul Gautan,Towards a World Fit for Children, *WCC Journal on Health and Healing*, Issue No 179, January 2005, uk. 5.

Pia imeelezwa kuwa*:*

> *Uzingatiaji mkubwa hauna budi kufanywa kuhusu umuhimu wa maadili ya mila na desturi na utamaduni ya kila mtu kwa ajili ya ulinzi na ukuaji wenye mpangilio mzuri wa amani na utulivu wa mtoto."*[5]

Kila mtoto ni ahadi na zawadi takatifu, alama hai ya maisha ya baadaye. Kwa hiyo changamoto iliyo mbele yetu ni namna ya kuwawezesha watoto na kuimarisha uwezo wao wa kuzaliwa kwa maisha yenye matarajio na matumaini.

Katika kukabili changamoto hii, juhudi ya Elimu ya Maadili ya Dini Mbalimbali inaongozwa na dira yake mahususi.

> *"Tunatarajia kuwa na ulimwengu ambao watoto wote wanawezeshwa kuendeleza mambo yao ya kiroho – kuzingatia misingi ya maadili, kujifunza kuishi katika mshikamano na watu wa dini na utamaduni tofauti, na kujenga imani ambapo watu wanamzingatia Mungu, Mwenye Uwezo wa Mwisho au Uwezo wa Kimungu"*[6]

Juhudi ya Elimu ya Maadili ya Dini Mbalimbali pia inatetea imani kwamba:

> *"Elimu ya Maadili itaimarisha uwezo wa watoto wa kuzaliwa wa kutoa michango chanya kwa ustawi wamarika yao, familia na jamii na kwamba hali hii itasaidia familia yote ya binadamu kutononoka katika mazingira yenye haki, amani, huruma, matarajio na utu"*[7]

Melezi ya kila mtoto si kama ni muhimu tu, bali pia ni wajibu wa kimaadili wa pamoja.

## Watoto – Zawadi na Wajibu



Kwa upande mmoja watoto wetu ni "mali yetu". Tunawaleta duniani, tunawalea wenyewe. Hata hivyo, hatuwamiliki. Wao ni watu binafsi wenye haki zao walio tayari kuinukia vyovyote watakavyokuwa. Kama alivyosema Khalih Gibran katika "*The Prophet*".

> *Na kama mwanamke alivyomkumbatia mwanawe kifuani kwake alivyosema, "tuambie kuhusu watoto."*

*Na alisema:*

> *Watoto wenu si watoto wenu,*
> *Ni wavulana na wasichana, wa Maisha yanayotaka kujibainisha yenyewe, Wanakuja kupitia kwenu bali si kutoka kwenu, Na hata kama wako pamoja nanyi, bado si mali yenu.*
> *Mnaweza kuwapa upendo wenu lakini si mawazo yenu,*
> *Kwa kuwa wana mawazo yao.*
> *Mnaweza kulea miili yao lakini si roho zao, Kwa kuwa roho zao zinaishi katika nyumba ya kesho, Ambayo hamtaweza kutembelea, hata katika ndoto zenu Mnaweza kujitahidi kuwa kama wao, lakini msijaribu kuwafanya wafanane kama ninyi, Kwa kuwa maisha hayarudi nyuma wala hayakawii kama jana…*[8]

5 Utangulizi wa mkataba juu ya haki za mtoto
6 Hati ya maono ya baraza la mahusiano ya dini mbalimbali juu ya elimu ya maadili kwa mtoto
7 Ibid
8 Khalil Gibran, *Mtume,* sura ijulikanayo kwa jina: Watoto, Arrow Books Ltd, New York, 1991.

Kila mzazi, kila mtu mzima anakabiliwa na mtanziko. Kwa upande mmoja, tunapewa tunu ya watoto, wako chini ya ulezi wetu, na tuna wajibu na fursa ya kuwaongoza wakati wanapoelekea kuwa watu wazima. Wakati huo huo, hatutakiwi kulazimisha maoni yetu kwa watoto wetu yanayoweza kukwaza uhuru wao wa maisha pale wanapoyabaini, kujifunza kutokana nayo na kuunda unyofu wao wenyewe. Tunawaachia wao wenyewe, na ulimwengu, kwamba tunawalea na kuwaelimisha watoto kwa hisia ya uwajibikaji, utambuzi na unyenyekevu.

## Watoto hujifunza wanachoishi

Mchakato wa kujifunza kwa watoto unaanza mara anapozaliwa, mazingira anayoishi, uzoefu anaopata na mifano ya tabia na mienendo tunayompa vyote vinachangia uelewa wake kuhusu yeye mwenyewe na ulimwengu. Shairi maarufu sana la watoto hujifunza wanachoishi linaeleza ukweli huu:

*Kama watoto wanaishi kwa kukosolewa*
*Watajifunza kulaani;*
*Kama watoto wanaishi katika uhasama*
*Watajifunza kupigana;*
*Kama watoto wanaishi katika dhihaka*
*Watajifunza kuona aibu;*
*Kama watoto wanaishi katika fedheha*
*Watajifunza kuhisi wana hatia;*

[Lakini]

*Kama watoto wanaishi kwa ustahimilivu*
*Watajifunza kuwa wenye subira;*
*Kama wanaishi kwa kutiwa moyo*
*Watajifunza kujiamini;*
*Kama watoto wanaishi kwa sifa*
*Watajifunza kuthamini;*
*Kama watoto wataishi bila ya upendeleo*
*Watajifunza haki;*
*Kama watoto wataishi kwa usalama*
*Watajifunza kuwa na imani;*
*Kama watoto wanaishi kwa idhini*
*Watajifunza kujipenda wenyewe;*
*Kama watoto wanaishi kwa ukubalifu na urafiki*
*Watajifunza kutafuta upendo duniani.*[9]

Katika kiini cha kujifunza kote kuna uzoefu – mwalimu mkubwa sana – ukweli huu hauhitaji kusisitizwa. Watoto hawazaliwi katika ulimwengu ulio kamilifu – na mchakato wao wa kujifunza unahusisha kuchunguza, kuzoea, kutathmini, kufungamanisha na kukabili mikinzano mingi ambayo wao na wazazi wao, hawatakuwa na kitu cha kudhibiti. Uhalisia tata, maadili yanayokinzana, madai yanayopinga kuhusu ukweli na mibadala inayokanganya hushindania uaminifu. Ndani ya uhalisia huo, kuna haja ya haraka kwa njia ya kulea na kuwawezesha watoto kwa maadili yatakayowasaidia kufanya uchaguzi sahihi.

9 Doroyhy Law Nolte, *Children Learn What They Live*, Workman Publishing Company, New York, 1998.

## Elimu ya Maadili na Haki za Binadamu

Dira na Dhamira ya Baraza la Dini Mbalimbali zinarejea hasa ibara ambazo Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu limeshughulikia: haki ya uhuru wa kutoa mawazo na kuamini, maoni na kujieleza; kupata elimu, kupumzika na burudani; kupata kiwango cha kutosha cha maisha na matibabu, na kushiriki maisha ya utamaduni wa jamii. Baraza la Dini Mbalimbali linaunga mkono zaidi Makubaliano Kuhusu Haki za Mtoto. *Kujifunza Kuishi Pamoja* kinashughulikia hasa Ibara ya 29, inayoeleza kwamba elimu ya mtoto itaelekezwa kwa:

a) *Kuendeleza haiba ya mtoto, vipaji na uwezo wa kiakili na kimwili hadi ukomo wao.*

b) *Kuendeleza heshima kwa haki za binadamu na uhuru wa msingi na kanuni zilizomo kwenye Mkataba wa Umoja wa Mataifa.*

c) *Kuendeleza heshima kwa wazazi wa mtoto, utambulisho wa utamaduni wake, lugha na maadili, kwa maadili ya taifa ya nchi anamoishi mtoto, nchi ya asili yake na kwa ustaarabu ambao ni tofauti na wa kwake.*

d) *Utayarishaji wa mtoto kwa maisha ya uwajibikaji katika jamii huru, kwa moyo wa maelewano, amani, ustahamilivu, usawa na haki za jinsia, na urafiki miongoni mwa watu wote, vikundi vya kitaifa na kidini na watu wa asili ya nchi hiyo.*

e) *Kuendeleza heshima kwa mazingira asilia.*

Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto yanatoa hati ya kisheria kwa mkabala wenye uwajibikaji kwa watoto. Makubaliano ya CRC, yaliyotiwa saini na mataifa yote na kuridhiwa na mataifa yote isipokuwa mawili, yana onyesha maeneo matatu ya haki za watoto. Watoto wote wana haki ya:



- Kuishi, afya, elimu na maendeleo.
- Ulinzi na usalama.
- Ushirikishwaji.

CRC ina kanuni nne za jumla kwa ulinzi wa jumla wa haki za watoto.

- Haki ya kuishi na kuendelezwa.
- Haki ya kutobaguliwa.
- Haki ya kusikilizwa.
- Maslahi bora kwa watoto.

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kimetayarishwa kama mchango wa kufanikisha haki za mtoto kwa kupata elimu na maendeleo kamili ya afya ya kimwili, kiakili, kiroho, kimaadili na kijamii, kama ilivyoandaliwa katika Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto.

# Maadili na Elimu ya Maadili

Kwa kuwa watu wamekuwa wakiishi pamoja katika jamii, urekebishaji wa tabia na mwenendo kiuadilifu umekuwa wa lazima kwa ustawi wa jamii – hii ndiyo maana ya maadili. Ni muhumu kwa watumiaji wa kitabu cha *Kujifunza Kuishi Pamoja* kukubaliana kuhusu maana ya maadili, unyofu na elimu ya maadili.

Kama tukiuliza swali, "je, maadili yana maana gani kwako?" kutakuwa na majibu mengi tofauti:

> "Maadili yanahusu hisia zangu zinazoniambia nini ni sahihi na nini si sahihi".
> "Maadili yanahusu imani zangu za dini".
> "Kuwa mwadilifu ni kufanya kile kinachotakiwa kisheria".
> "Maadili ni viwango vya tabia na mwenendo vinavyokubaliwa na jamii".

Watu wengi wanaelekea kuhusisha maadili na hisia zao. Lakini kuwa mwadilifu si jambo la kufuata hisia za mtu tu, kwa kuwa hisia si msingi wa kuamulia maana ya kilichoadilifu.

Wala mtu hawezi kubainisha kwa ukamilifu maadili na dini. Dini nyingi zinahimiza viwango vya juu vya kiadilifu. Hata hivyo kama maadili yatakomea kwa dini, yatatumika kwa waumini tu. Maadili yanatumika kwa tabia na mwenendo wa muumini kama yanavyofanya kwa mtu asiye muumini.

Kuwa mwadilifu pia ni zaidi ya kufuata sheria tu. Kwa kawaida sheria inashirikisha viwango vya kiadilifu ambavyo raia wengi wanafuata. Lakini sheria kama zilivyo hisia, zinaweza kukengeuka kutoka kile ambacho ni cha kiuadilifu. Historia inafahamu jamii zenye sheria zilizohalalisha utumwa. Katika jamii nyingi, wajibu wa pili wa mwanamke umeandikwa kwenye sheria. Pengine wapo wanawake wanaokumbuka zamani wakati sheria ilipowazuia kupiga kura.

Kuwa mwadilifu si kufanya "kile kinachokubalika na jamii". Viwango vya tabia na mwenendo katika jamii vinaweza kukengeuka kutoka kile ambacho ni cha kiuadilifu. 

Aidha, kama kutenda maadili ni sawa na kufanya "kila kitu ambacho jamii inakikubali" mtu hana budi kutambua kwanza kiwango hiki kilipo. Kwa masuala yenye ubishi, yale yanayotustaajabisha sana, hakuna kinachofaa zaidi ya utafiti. Hata hivyo kukosa mwafaka katika jamii kutazuia kueleweka kwa ufasaha tabia na mwenendo wa kimaadili.

Je, maadili ni nini? Kwanza maadili yanahusu kuangalia kwa makini viwango vya kilicho sahihi na kisicho sahihi kinachofafanua wanachotakiwa kufanya binadamu, hasa kwa upande wa haki, wajibu, manufaa kwa jamii, kutokuwa na upendeleo, au matendo mema maalumu. Maadili yanahusu viwango vile vinavyoweka wajibu unaofaa kuepuka ubakaji, wizi, uuaji, shambulio, kashfa na udanganyifu. Viwango vya kimaadili, pia vinahimiza matendo mema kama vile uaminifu, huruma na utii, na utimizaji wa mahitaji ya msingi ya binadamu. Mtaalamu wa sosholojia Johan Galtung aliwauliza watu katika kiasi cha nchi 50, ni nini hasa wasichokubali kukikosa, na kuhitimisha kutoka katika utafiti huu, mahitaji ya msingi ya binadamu kama vile ustawi, utambulisho na uhuru.[10]

Pili maadili yanahusu kujifunza na kuendeleza viwango vya kimaadili. Kwa sababu hisia, sheria na kanuni za kijamii zinaweza kukengeuka kutoka katika kile ambacho ni cha kimaadili, inakuwa muhimu kuchunguza viwango vya mtu kuhakikisha kuwa vinafaa. Maadili ina maana pia kwamba juhudi za mfululizo za kuchunguza imani zetu za uadilifu na mwenendo wa kiuadilifu, na kujitahidi kuhakikisha kwamba sisi na mataifa na asasi tunasaidia kutengeneza kufuata viwango vinavyofaa na vyenye msingi thabiti, iwe katika mifumo ya imani za kiutamaduni au kidini au vyombo vya kimataifa.[11]

10 Johan Galtung, Human Needs, Humanitarian,Human security and the War in Iraq", key note address, Sophia Universirty, Tokyo, 2004. http//www.transnational.com/forum/meet/2004/Galtung_Human Needs.html

11 Imedhaminiwa kutoka kwa Hans Ucko, "Ethics law and commitment", Current Dialogue, Issue 46, December 2005, Http//wcccoe.org/wcc/what/interreligious/cd46-09.html

## Maadili, Unyofu na Uadilifu

Kwa ghafla inakuwa vigumu kutofautisha kati ya dhana ya "maadili" "unyofu" na "uadilifu"

Maana zifuatazo zimo kwenye Compact Oxford English Dictionary.[12]

> Maadili: Utafiti wa kifalsafa wa unyofu wa uadilifu wa mwenendo wa binadamu na misingi na kanuni inayotakiwa kutawala maadili.
>
> Unyoofu: Misingi ya uadilifu au viwango vinavyokubalika vya mtu au kikundi
>
> Uadilifu: Unahusu au kuhusiana na tabia na mwenendo wa binadamu, hasa utofautishaji kati ya baya au zuri, au lililo sahihi au lisilo sahihi.

Maadili ni imani, mawazo na nadharia zinazowezesha uwekaji wa viwango. Uadilifu unahusiana kwa karibu zaidi na tabia na mwenendo. Unyofu unahusu kinachokubaliwa na jamii, kikundi au jumuiya. Vipengele vyote ni muhimu na vinahusiana. Mtu anaweza kuwa na viwango vya juu lakini anashindwa kuvifuata au kuvitimiza, na hivyo kuwa na maana ya maadili makali lakini uadilifu dhaifu. Unyofu wa kikundi fulani mahususi unaweza usikubaliwe na kikundi kingine.

Kwa mfano, Wanafalsafa wa Kifaransa, Paul Ricoeur[13] na Guy Bourgeault[14], kwa kawaida wao wanatumia neno "maadili" kwa mambo ya msingi kuhusu masuala ya lazima ya tabia na mwenendo wa kibinadamu (km, mwisho na maana ya Maisha, msingi wa wajibu na dhima; hali ya wema na uovu, thamani au umuhimu wa dhamiri ya uadilifu) na kuacha neno "uadilifu" kwa matumizi, uthabiti na kitendo. Zaidi ya hayo "maadili" yanaelekea kuwa na maana ya kudadisi au kuwa tayari kupokea ushauri au ari, hali ya kuwa "uadilifu" mara nyingi una maana ya mifumo bainifu ya desturi, tafsiri kuwa kanuni zitakazoleta kitendo.

## Maadili inahusu uhusiano



Matakwa ya maadili, kwa namna yoyote tunayofikia, yanahusu uhusiano. Mwanatheolojia wa Denmaki, K.E. Loegstrup anaeleza kuwa matakwa ya kimaadili kwa binadamu yanachepukia kama nuru katika mche na kubainisha njia zote zinazotutofautisha sisi na wengine katika uhusiano.[15]

Mtu anavyochagua kujihusisha yeye mwenyewe, na wengine na dunia, inayodumisha maisha yote, ni dalili zote za msingi za maadili na unyofu. Chanzo cha desturi za kimaadili na tabia na mwenendo kitadhaniwa kutokana na uwepo wa Mungu, au ufunuo uliotolewa na Mungu au mwalimu wa kiroho aliyejaliwa hekima ya kutosha au kwa misingi ya haki za binadamu.

Vinaweza kuwapo vyanzo vingi vya tabia au mwenendo wa kimaadili na swali la msingi ni je, maadili yana thamani gani katika kutusaidia kutambua na kushughulikia uhusiano wa maisha yote, je zina manufaa gani katika kukuza unyofu wa ubinadamu na katika kukuza na kujenga hisia ya kijamii.

Jumuiya zote za dini zinaona maadili kama eneo la maisha yasiyozuiliwa bali hutumika kwenye aina zote za maisha: maisha ya mtu binafsi, maisha ya ndani ya familia, mahali pa kazi na katika jamii. Kwa mfano, maadili ya Kiislamu yana nemsi zote za kiuadilifu zinazofahamika. Yanajihusisha na upeo wote wa maisha ya mtu binafsi na maisha ya pamoja – uhusiano wake wa nyumbani, maadili mema ya utumishi, na shughuli katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kisheria, kielimu na kijamii. Yanahusisha maisha ya kila mtu, kuanzia nyumbani, hadi katika jamii, kuanzia kwenye meza ya chakula hadi kwenye medani ya kivita na mikutano ya amani – yana maana kutoka kwenye chimbuko hadi kaburini.

---

12 *Compact Oxford English Dictionary*, Oxford University Press, 2005.

13 Paul Ricoeur, *Soi-même come un autre*, Paris, Seuil, 1990.

14 Guy Bourgault, *l'éthique et le droit face aux nouvelles technologies médicales*, Les Press de l'Université de Montréal, Montréal, 1990.

15 K. E. Leogstrup, *Ethical Demand*, University of Notre Press, Notre Dame and London, 1997.

Katika kukubaliana na msisitizo huu kwa mtu binafsi na jumuiya, dini nyingi za jadi barani Afrika zina usemi: " Mtu anaonekana kuwa mtu tu kuhusiana na watu wengine."

Kwa kuzingatia uhusiano huu, tunatafuta unyofu wa kimaadili utakaosaidia watoto kukuza hisia ya jumuiya, siyo wale tu walio kwenye mazingira yao ya karibu, bali pia kwenye vipingamizi vya kimbari, kitaifa, kikabila, kiutamaduni na kidini. Tunatafuta na kuendeleza unyofu unaokuza hisia ya uwajibikaji wa pamoja miongoni mwa mtu na mtu katika ulimwengu wa kutegemeana.

## Je, kuna unyofu wa kudumu?

Jumuiya nyingi zinaeleza unyofu wa kimaadili kwa maana thabiti itakayoamua mitazamo na mipangilio ya tabia na mwenendo, kama vile upendo na huruma, haki na kutopendelea, uaminifu na ukarimu, kutokuwa na ugomvi na kujidhibiti. Jumuiya hizi zinaweza kusisitiza kanuni za kimaadili zinazoingiliana – kama vile "kumpenda jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe" au "kutowafanyia wengine kila ambacho hutaki wengine wakufanyie" – kwa imani kwamba kuishi kwa misingi hii kunazaa matunda ya kimaadili. Msisitizo wa kudhamiria kuhusu kukuza stadi mahususi na uwezo kwa watoto kwa kawaida utakuza tabia na mwenendo wa kimaadili.

UNESCO imebainisha baadhi ya unyofu wa kimataifa wa maendeleo ya mtu binafsi unaomwezesha mtoto kuhusisha ubunifu wake na ulimwengu wake: kumsaidia mtoto kujenga kujistahi, kuwezesha uwezo wao wa kufanya uchaguzi na kuchukua wajibu wa uchaguzi waliofanya, uwezo wao wa kufanya uamuzi wa haki usio na upendeleo, utayari wa kuwaheshimu wengine na mawazo yao; kuwa tayari kutoa ahadi na kutetea ahadi zao. Hii ni mifano ya sifa nyingi zilizobainishwa kama unyofu unaohitaji kuendelezwa katika mtoto ili kumsaidia kufikiri na kutenda kimaadili.[16]

Uhusiano mara nyingi unajenga na kuunda utambulisho wa mtu. Wasichana na wavulana wana aina tofauti za uhusiano na mama au baba, akiwa mwanafunzi katika shule kunamsaidia kuunda sehemu nyingine ya utambulisho, kama inavyofanya familia na mazingira ya utamaduni. Mila na desturi – za kifamilia, kijiji na kitaifa – huunda utambulisho wa mtu, imani na unyofu. Matukio – binafsi kitaifa, kikanda na kimataifa – huchangia pia katika mchakato wa maendeleo ya utambulisho.



Utambulisho wa kidini, kiroho na kiutamaduni unaundwa kwa namna moja. Kukabiliana na aina mbalimbali za imani na dini, utamaduni na mila na desturi na upekee wa kila dini na utamaduni hakuzuii uaminifu wa kidini, kiroho au mila na utamaduni wa mtu. Kama uhalisia wa wingi wa kidini na kiutamaduni unadhihirishwa katika mazingira ya wazi, upendo, mapenzi, upatanifu, ambapo mamlaka yataongeza heshima na kupendana kuliko ujumuishwa na dhana ya kufahamiana, ukubalifu wa pamoja na uhalali sawa, ambapo hakuna imani au utendaji wa mtu unaopewa upendeleo na kuonekana kama bora zaidi. Katikati ya uanuwai, kilicho muhimu zaidi ya vyote – ubinadamu wetu unahitaji kusisitizwa sana. Taswira inayojitokeza siyo ile ya chungu cha kuyeyushia ambapo kila kitu kinachanganywa pamoja lakini ni chenye picha au nakshi ya mpangilio ambapo kila utambulisho wa kitamaduni una umuhimu wake wa kutambuliwa kuthibitisha utajiri wa uanuai.

Kuwa na hisia ya utambulisho wa mtu kunahitaji kujitawala: uhuru, uhuru wa mawazo, kuzungumza na kutenda na uhuru wa kutokuwa na hofu au woga wa kulaumiwa au adhabu endapo imani za mtu zitakinzana na imani za wengi au za mamlaka inayotawala. Kujiheshimu na kujistahi ni muhimu, siyo kama kuhalalisha heshima kutoka kwa wengine tu, bali kama msingi wa kuwaheshimu wengine.

Ni kawaida kudhani kuwa maadili ni jambo la unyofu wa mtu unaofanywa katika maisha yetu ya kila siku. Lakini ulimwengu tunaoishi unatulazimisha sisi tufikirie na kutenda pia kimataifa. Umaskini na kunyimwa kwa mamilioni, unyonyaji wa rasilimali za duniani, matatizo ya ikolojia, ugomvi na vita vya mara kwa mara na utamaduni wa choyo na ulimbikizaji vinaongeza shinikizo jipya kwetu

16 Orodha ya UNESCO, hizi na nyingine kadhaa "thamani za utu" katika *Eliminating Corporal Punishment: The Way forward to constructive Child Discipline*, Stuart N. Hart (Ed), Paris, UNESCO, 2005. Maudhui haya ya yaliyoandaliwa na jopo la wataalamu wa kimataifa watano kwa matumaini kwamba wataangaza/wataakisi maudhui ya kimaadili itakayozingatia mipaka ya kitamaduni.

kufanya unyofu wa kimaadili katika maisha yetu ya kilimwengu. Sisi – na watoto wetu – tunahitaji hisia za kimaadili kutusaidia kuhusisha na kwenye utamaduni na ustaarabu, kwenye vipingamizi vya kitaifa na kimaadili, na kwenye utambulisho wa kidini na ahadi. Wengi wanaanza kuangalia maelekezo ya kwenda na wakati na kujiandaa kwa siku zijazo.

## Kanuni za Kimaadili na Unyoofu wa Maadili ya Msingi kwa Elimu ya Maadili

Kumekuwa na juhudi za kupata unyofu wa kimaadili ambao jumuiya zote za kidini zinaweza kuthibitisha na kufuata. Miongoni mwa juhudi hizo ilikuwa waraka uliotolewa katika Miaka Mia Moja ya Bunge la Dini za Dunia, Chicago 1993, chini ya uongozi wa Hans Kung. Waraka huo unaojulikana kama *Kuelekea Maadili ya Kimataifa,* hivi sasa unafahamika na umekubalika duniani kote, unatoa msukumo kwa makubaliano yanayowezekana kati ya watu kutoka mitazamo tofauti kuhusu unyofu wa kawaida utakaoongoza jumuiya ya binadamu kwa jumla.[17]

Tangu mwaka 1993, kumekuwa na juhudi zaidi za kuweka vipengele vya kimaadili kwa watu wa aina mbalimbali ambao watathibitishwa na jumuiya ya kimataifa. Uanuwai mkubwa wa dini, utamaduni na namna za maisha zilizowakilishwa duniani, hufanya makubaliano ya pamoja na utekelezaji wake kuwa kazi ngumu. Hata hivyo, yaelekea kuwapo na mwafaka wa pamoja ambao sisi kama jumuiya ya binadamu, hatuna budi kujitahidi kutafuta msimamo wa pamoja kuhusu kanuni za kimaadili, kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

Mwelekeo wa pamoja wa kujenga maisha mazuri ya baadaye unawasaidia watoto kujenga unyofu wa kimaadili. Hata hivyo unyofu uliokuzwa kimataifa, hauna budi kuwa na umuhimu nchini, kwa kuwa jumuiya katika sehemu na tamaduni mbalimbali bila shaka zina nafasi nzuri kuamua kuwa ni maadili ya msingi yanayohitaji kukuzwa kwa mtoto wao. Hata hivyo tunaweza kushangazwa kiwango huru kilichofikiwa cha kanuni za maadili za pamoja.



## Uwezo wa kuchagua: Tunu kubwa na wajibu wenye changamoto nzito kuliko zote

Uwezo wa kuchagua kati ya mibadala ni miongoni mwa tunu kubwa za maisha ya binadamu. Bila shaka daima huwa hatupati kila tunachochagua, lakini tuna uwezo wa haki ya kubagua, kukataa na kuchagua. Katika mojawapo ya tafsiri kutoka katika mila na desturi za Kiyahudi, katika kisa cha kuumbwa kwa binadamu. Adam na Hawa, mwanamke na mwanamume wa kwanza, waliwekwa katika Bustani ya Edeni, kulikokuwa na miti miwili – Mti wa Maisha na Mti wa Maarifa ya Kujua Wema na Uovu. Walifahamishwa athari za kula matunda ya miti hii. Walikula kutoka matunda ya Mti wa Maarifa ya Kujua Wema na Uovu. Je, lilikuwa kosa au lilikuwa uchaguzi wa makusudi?

Harold Kushner anapendekeza kwamba uchaguzi huu ndio unaotufanya binadamu:

> *"Wahenga wetu wa kwanza walichagua kuwa binadamu kuliko kuishi milele. Walichagua hisia ya uadilifu, maarifa ya kujua wema na uovu kuliko ubaya. Walidharau Mti wa Maisha, ambao ungewapa maisha ya milele na kutaka Mti wa Maarifa ya Kujua Wema na Uovu, uliowapa dhamiri. Kama fidia, Mungu kawapa binadamu ambao kwa sasa, wanashirikiana naye, uwezo wa kujua wema na uovu, kipaji cha uwezo wake wa Kimungu cha kuumba maisha mapya. Tunaepuka kifo, si kwa kuishi milele bali kwa kuzaa, kulea na kuelimisha watoto kudumisha roho zetu, unyofu wetu na hata majina yetu"*[18]

17 Declaration towards a Global Ethic. The Council of a parliament of the World Religions, at http://www.parliamentof religions.org_includes/FCKcontent/ File/Toward AGlobalEthic.pdf

18 Harold S. Kushner, *The Lord is My Shepherd*, New York, USA, First Anchor Books Edition, 2004, uk. 23-24.

Uwezo wa binadamu kuchagua kati ya mibadala unatambuliwa na kuthibitishwa katika dini zote. Uwezo wa kuchagua wakati huo huo ni changamoto kubwa na wajibu mgumu. Unahitaji uwezo wa kuchagua, kutambua na kufanya uamuzi wakati huo huo kukabili mtanziko wa kushindwa kuona na kukubali athari kamili ya uamuzi huu unaofanana, ambao si kama unatuathiri sisi wenyewe tu, bali wengine pia na ulimwengu unaotuzunguka. Kanuni za kimaadili na unyofu vina mchango mkubwa katika kutusaidia kufanya uchaguzi huu.

## Kulinda na kutetea hadhi ya binadamu

Dhana ya hadhi ya binadamu inadhihirisha kile ambacho elimu maadili inatafuta kuhimiza katika kukuza unyofu na kanuni za maadili. Ubinadamu wa mtu unakosekana iwapo hadhi yake inaathiriwa. Hadhi ya binadamu inaweza kuathiriwa kutoka pande nyingi.

Kukosekana kwa mahitaji ya msingi ya maisha ni fedheha kwa hadhi ya mtu. Usemi wa Kisingasinga unasema kwamba, "Mdomo wa maskini ni kisanduku cha hazina cha Mungu" Kwenye msemo huu kuna mojawapo ya maadili ya msingi ambayo ni muhimu kwa mila na desturi za kidini, hasa, hadhi ya binadamu. Usemi wa Kisingasinga unaona umaskini, njaa na kunyimwa kama fedheha kwa Mungu. Kila ibada ya Kisingasinga inaishia na *langar*, mlo wa jumuiya, wanaokaribishwa ni wote, bila ya kujali tabaka, hadhi ya kijamii, dini unayofuata na taifa. Kusema kweli, Gurdwaras, ambayo ni mahekalu ya ibada ya Kisingasinga yana jiko linalofanya kazi siku nzima, si kuwahudumia waumini tu, bali mtu yeyote anayehitaji chakula.

Dini ya Kiislamu imefanya kukidhi mahitaji ya maskini kuwa moja ya nguzo zake tano za imani, na kumtaka kila muumini kutenga sehemu ya mapato yake kuwasaidia wale wenye shida. Kumpenda Mungu na Kumpenda jirani yako kama unavyojipenda wewe mwenyewe ni amri kuu katika Dini ya Kiyahudi na Kikristo. Aidha mila na desturi ya Kiyahudi zinazungumzia kuwa binadamu wameumbwa kwa taswira na kufanana na Mungu; wafuasi wa Kivedant wa dini ya Kihindu wanamwona Brahman, Uhalisia wa Juu, na Atman, Uhalisia kwa binadamu kama kitu kimoja, wala si viwili. Mafundisho ya Kibudha yanahoji pia kuhusu ubaguzi wa kitabaka na kuhimiza usawa wa wanawake na wanaume.



Mila na desturi za dini hazijafuata mara zote mafundisho haya, na wakati mwingine zimeweka zenyewe miundo na desturi zinazoathiri hadhi ya watu wa ndani na nje ya jumuiya yao. Lakini mila na desturi zote za dini zinaona kunyimwa hadhi ya binadamu kama upotofu. Hadhi ni sehemu ya maana ya kuwa binadamu.

## Heshima na kuelewana

Haki ya mtu kupata hadhi na heshima ni muhimu katika nyaraka za haki za binadamu kama vile Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu na Makubaliano kuhusu haki za Mtoto.

Haki za Kimataifa za kuishi, kuendelea, ulinzi na ushiriki wa wote zimekubaliwa na nchi za mataifa bila ya kujali umri, jinsia, mbari au dini. Kamati ya Kimataifa inafuatilia utimizaji wa haki za wale wenye umri wa chini ya miaka 18, wanaotegemea sana hatua na uamuzi wa watu wazima na hutoa maoni yake na ukosoaji kwa kila nchi na taifa katika waraka kamili. Haki zilizomo kwenye nyaraka hizi na nyingine za haki za binadamu za Umoja wa Mataifa hazihamishiki kwa mtu mwingine na ni za kimataifa, na hazina budi kufundishwa kwa wote bila ya kujali utamaduni au dini. Haki hizi ndizo ulimwengu ulizokubaliana kuwa na kanuni na misingi ya ubinadamu na zisipunguzwe uzito, zisimilikiwe au kurekebishwa na mtu au shirika lolote.

Dini nyingi na mila na desturi zisizofuata dini zinaridhishwa na ukweli wa imani zao na baadhi zinaweza kuhisi umuhimu wa kushirikiana na mengine. Lakini hivi leo, mila na desturi nyingi zinatambua kuheshimiana ni muhimu kwa sababu inathibitisha tofauti na haichanganyi tofauti na au huruhusu 'tofauti' za kiasili na halali kuishia katika migawanyiko. Kuheshimiana kunakuwa na kuelewana zaidi na kukubali tofauti na kufanana. Inadai kujenga uhusiano ingawa tunatofautiana, na kusaidia katika mchakato wa kusahihishana, kuimarishana na kujikosoa.

Kuheshimu hadhi ya watu wote, kunaweza bila ya shaka kuwa unyofu wa msingi na kanuni za kimaadili katika elimu ya maadili kwa watoto. Kulindana, kushikiliana hadhi ya binadamu inamaanisha seti ya unyofu inayowasaidia watoto na vijana kuheshimu na kukubali watu wengine na wao wenyewe kama binadamu, kutumia mitazamo na fikra zinazosaidia kujenga uhusiano wa jumla na wengine

Hadhi ni muhimu katika muktadha wa wingi unaosisitizwa kwa sababu, kihistoria baadhi ya mila na desturi za dini zimechukua mtazamo wa aina hii – au kuhusiana na wengine, kuonyesha mitazamo hiyo, kama vile tuko sahihi, wengine wamekosea; kama tuna ukweli wengine hawana, kama njia yetu ni kutimiza hadhi ya binadamu, nyingine zinapotosha.

## Ushirikali na uwezo wa "kuchukua madhila ya mtu mwingine"

Katikati ya uhusiano wote wa kujali wengine kuna ushirikali – uwezo wa kuingiza uzoefu wa mtu mwingine na kuelewa na kuhisi furaha na huzuni zao, furaha kubwa na machungu.

Ushirikali unajumuisha uwezo wa aina mbili kwa binadamu; kuchambua na kuhurumia, kutumia akili zetu na mioyo yetu. Kuchambua ni kukusanya hoja zote zinazohusu tatizo, kuchunguza hali, kubainisha chanzo na kupendekeza ufumbuzi. Kuhurumia ni kumfikiria mtu mwingine, kuhisi maumivu ya mtu mwingine anayeteseka au kuhisi hasira ya mtu mwenye ghadhabu.



Sala ya zamani ya Kihindi cha Sioux inasema, "Ewe Roho Mkuu, nipe busara na hekima ya kuwa katika nafasi ya mtu fulani kabla ya kulaumu au kuhukumu". Kama tunashirikali, tunaacha matarajio yetu kwamba watu wengine lazima wawe kama sisi, tunakubali ukweli kwamba mtu mwingine ameleta kitu cha pekee kwenye uhusiano. Wakati huo huo ni ushirikali ndio unaomsaidia mtu kuona na kutambua uonevu wanaofanya watu wengine na kupata ari ya kushughulikia uonevu huo.

Mila na desturi za dini zinawataka watu washirikali na maskini, wasiobahatika na waliokandamizwa. Mila na desturi ya Kiyahudi wanaifanya kuwa bora kwa kusema "… kwa kuwa mmekuwa watumwa nchini Misri. " Mila na desturi ya Kikristo inawahimiza wafuasi 'kuwakumbuka walio magerezani kana kwamba ni wafungwa wenzao, na wale wanaoteswa kana kwamba ninyi wenyewe mnateseka.'

Katika mila na desturi za Kiislamu, mwezi wa Ramadhani unaitwa mwezi wa Subra, Ushirikali na Kujitakasa. Uelewa wa dini ya Kibudha kuhusu ushirikali ni kupenda wema, kunako kwenda zaidi ya ushirikali – ni aina fulani ya kumwonea mtu huruma – na badala yake inahimiza utambulishaji kamili na haraka wa watu wengine, tunaoita ushirikali. Haki za binadamu zimejengwa kwenye usawa kamili; haki za kimataifa, baadhi zina dhima mahususi kutimiza haki za wengine kama ilivyo kwenye Makubaliano ya Haki za Mtoto. Kujali kuhusu utimizaji wa haki za wengine ni muhimu kwa mila na desturi za kidini na zisizo za kidini.

Wito wa kushirikali na uzoefu wa watu wengine pengine ni miongoni mwa unyofu mkubwa tunaoweza kuwarithisha watoto wetu.

## Wajibu wa Mtu mmoja na wa Pamoja

Tunazidi kugundua umuhimu wa neno 'wajibu katika kushughulikia matatizo mengi ya duniani. Watu wengi ni wepesi kudai haki zao lakini wanashindwa kuona wajibu unaoambatana na upendeleo huu. Tuna wajibu wa namna tunavyowalea watoto wetu; tunapopuuzia wajibu huu, wanaweza kupotoka. Serikali zina wajibu wa kudumisha mshikamano wa jamii na amani, kama wajibu huu unapuuzwa tunaweza kukabiliwa na mgogoro wa kijamii. Ni wajibu wa jamii kuhakikisha ugawaji wa rasilimali wa haki na mahitaji ya msingi yanatimizwa, kama hili linapuuzwa kunaweza kutokea ugomvi na migogoro. Kila mmoja ana wajibu wa kuzingatia kwa ajili ya dunia, kupuuzwa kwa wajibu huu kumetusababisha kukaribia maafa ya ikolojia.

Orodha inaweza kuwa ndefu kushughulikia takriban uhusiano wote wa mtu, jamii na kimataifa. Mahusiano yote yanategemea wajibu wa wote na kila mtu kutekeleza wajibu wake kwa jamii. Wajibu wa pamoja wa kumjali kila mmoja unaweza kuhakikisha kuwa tunaishi kwenye ulimwengu wenye haki zaidi na amani.

Wajibu sio jambo la hiari, ni maadili ya msingi, na yanahitaji kutunzwa katika mioyo na akili za watoto kuanzia wakati walipoanza kuunda uhusiano na wengine na ulimwengu uliowazunguka.

## Upatanisho na mbinu za kujenga mahusiano


Watu wengi wanaona upatanisho kuwa hatua mojawapo katika kuleta amani na katika kurekebisha uhusiano katika ngazi za jamii na mtu. Leo, kuna ongezeko la utambuzi kwamba upatanisho si hatua kwa vitendo tu, bali ni mkabala kwa maisha. Kwa maneno mengine usuluhishi si tabia tu, ni maelekezo yatakayosaidia kudhibiti matatizo yasiyoepukika, ukengeukaji mkubwa na migogoro ya maisha ya jumuiya. Upatanisho umekuwa mstari wa mbele kama maadili kwa sababu ya tabia ya binadamu kutanzua tofauti na kutokubaliana kwa kutumia nguvu. Matumizi ya nguvu inaelekea kufikiriwa kama njia rahisi na ya haraka ya kushughulikia migogoro, lakini haitoi ufumbuzi endelevu. Kinyume chake inaongeza uadui na malalamiko. Moyo wa upatanisho unahitaji kusisitizwa kuwa ni maadili yasiyoepukika siku hizi.

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kinazingatia zaidi maadili manne ambayo ni lazima yaunde sehemu ya elimu ya maadili kwa watoto, katika jamii ya kimataifa yenye dini na utamaduni mwingi. Maadili hayo manne ya heshima, ushirikali, upatanisho, na wajibu, sio yote na hayaachi maadili mengine. Elimu ya maadili kwa watoto si hatua ya kuingiza orodha ya unyofu kwa watoto, bali kuendeleza mambo ya kiroho yanayotakiwa kwa maisha katika ulimwengu kwenye mfumo unaotambua mawazo mbalimbali.

Pia hatuna budi kuzingatia kwamba maadili na mambo ya kiroho si miongozo miwili tofauti kwa tabia na mwenendo, bali inahusiana, kila mmoja ukiimarisha mwingine. Mtu wa kiroho pia ni mtu aliye mnyofu kimaadili na mtu mnyofu kimaadili anaonyesha mwenendo wa kiroho ambao wengine hawana budi kuiga.

## Elimu ya Maadili

Baraza la Dini Mbalimbali linahimiza mtazamo wa mkabala kwa watu wengine unaohusiana na mtu binafsi.




Mchoro huu unaonyesha mchakato wa kujifunza unavyoelezwa kama mzunguko. Ni kwa kujifunza, kukiwa na nafasi ya kutafakari ambako kila mtoto na kijana ataweza kujenga na kutenda *uhusiano chanya* na yeye mwenyewe, na watu wengine na mazingira na kile watu wanachoita 'Mungu' Uhalisia wa mwisho au Uwapo wa Mungu. Ujengaji huu wa uhusiano chanya utaimarisha mambo yao ya kiroho ya kuzaliwa, kufungua njia za ukuaji, kuelewana na kuheshimu watu wa dini na ustaarabu mbalimbali. Hii pia itawawezesha watoto na vijana kuwa wabia katika kujengwa kwa kushikamana na wengine ulimwenguni kwa msingi wa maadili na vitendo vinavyolinda hadhi ya binadamu na kuhimiza mshikamano, wajibu wa mtu binafsi na wa pamoja, na upatanisho. Kujifunza kunahusisha watoto na vijana katika kufundisha na kujizoeza mkabala wa maisha kwa msingi wa maadili na unyofu na kutoa nafasi ya tafakuri huru wakati huo huo kuendeleza mambo ya kiroho.

Baraza la Dini Mbalimbali linahimiza njia mpya na inayobadilika ya kufikiria kuhusu maadili katika jamii ya kimataifa na yenye mitazamo mbalimbali. Hili ni jambo ambalo dini na jamii zote zinaweza kufanya kwa kujitegemea, lililo la pekee kuhusu juhudi hii ni kwamba hufanyika kati ya dini mbalimbali. Baraza la Dini Mbalimbali halihimizi dini mpya lakini linakubali na kuthibitisha uanuwai. Si 'mafundisho' mapya bali njia mpya ya kusisitiza kujenga uhusiano chanya. Mkabala wake:

> Ni wa utamaduni mbalimbali.
> Ni wa dini mbalimbali.
> Unathibitisha uanuwai.
> Unathibitisha mazungumzo na mawasiliano ndani ya mtu na mwingine katika mchakato unaoendelea wa kujifunza mtu mmoja mmoja na kwa pamoja.

Katika mchakato wote wa kujifunza, nafasi inawekwa kwa ajili ya kubadilishana mawazo, mwingiliano na kuelewana. Kwa kuhimiza fikra tunduizi, kufikiri kitunduzi, kuelewa na kuwa tayari kusikiliza mawazo ya mwingine, mchakato huu unawezesha watoto, vijana na watu wazima kugundua mila na desturi zao, maadili yao na maadili na mila na desturi za wengine, mwingiliano na wengine na hivyo kujenga uwezekano wa kuimarishana na katika "kutoa na kupokea" kunakoendelea ambako ni sehemu ya ubinadamu wetu.

# Ubinadamu wetu

Katika takriban jamii zote, watu wana mila na desturi za dini mbalimbali, na jamii kwa upande wake hupata msukumo wa matendo ya kimaadili kutokana na ahadi na dhamiri za kidini zilizopo katika jamii ile. Kusema kweli mifumo bora ya uadilifu au kimaadili na maelezo mara nyingi yanahusiana kwa karibu sana na maadili ya dini. Kama tutamwuliza mtu kwa nini unajishughulisha na kazi ya kusaidia binadamu, anaweza kusema "Nampenda Mungu, kwa hiyo nampenda pia jirani yangu". Katika mila na desturi za Kikristo na Kiyahudi, kumpenda jirani yako, kuwatimizia mahitaji yao ya msingi, inaonekana kuwa ni kielelezo cha kweli cha imani ya mtu kwa Mungu. Katika mila na desturi za Kiislamu, kuwatimizia mahitaji yao wenye shida ni sehemu ya wajibu wa dini wa mtu anayehusika. Mkabala wa dini ya Kibudha kwa mazingira ya mtu unachochewa na huruma kwa viumbe vyote. Hali kadhalika, Mhindu, Singasinga au mtu wa Dini ya Jadi anaweza kupata msukumo wa namna wanavyohusisha na ulimwengu kutoka kwenye mafundisho ya mila na desturi yake. Siku hizi wengi pia wanapata msukumo kwa matendo ya kimaadili kutoka rasilimali ya kiroho zisizo na dini ya aina yoyote.

Kinachounganisha maelezo haya kwa matendo ni kiasi cha uadilifu au maadili kilichopo. Maadili ya msingi yanatuambia tunachotakiwa kufanya na kutofanya kuhusiana na wengine na kwa maumbile. Pia yanatusaidia kuunda mawazo na dira ya namna ulimwengu unavyotakiwa kuwa, ili fikra zetu zisiishie kwa ulimwengu kama ilivyo. Kwa hiyo maadili haya yanatusaidia kufanya kazi pamoja, kuufanya ulimwengu kuwa mahali bora.

## Maelezo thabiti kuhusu ubinadamu wetu

Imani kwamba tunaweza kuthibitisha ubinadamu wetu na kujitahidi kufikia mfano bora katika uhusiano kati ya mtu na mtu tayari imeonyeshwa katika maeneo mbalimbali.

Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu lilipitishwa mwaka 1948. Haki linazozitetea zinatafsiriwa kwa kina. Kwa mfano, wazo la mahitaji ya msingi halikomei katika chakula, maji, mavazi na malazi bali limepanuliwa kujumuisha mahitaji yetu ya kimwili, kiakili, kiutamaduni, na kiroho, haki ya utambulisho; na uwezo na uhuru wa kuchagua. Waraka mwingine wa hivi karibu zaidi ni Mkataba wa Ardhi unaohusu kulinda maumbile ya ulimwengu na kuongoza tabia na mwenendo wetu kwa mazingira.

Mahitaji ya kipekee ya mtoto hayakupata uzingativu wa kutosha tangu zamani ingawa hivi sasa yanazidi kutambuliwa. "Makubaliano ya Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Mtoto" (CRC) – sheria ya haki za binadamu kwa walio chini ya umri wa miaka 18 – ilipitishwa mwaka 1989 tu, lakini tangu wakati huo imeridhiwa na idadi kubwa ya nchi na mataifa yenye dini tofauti na imani za utamaduni na kuufanya kuwa mkataba wa haki za binadamu uliotiwa saini na nchi nyingi zaidi duniani. Dhamira ya kujenga ulimwengu bora kwa watoto inaweka haki za binadamu katika mstari wa mbele wa mapambano dhidi ya haki za binadamu kuhesabiwa kwamba ni wajibu wa kiuadilifu na kisheria. Kwa kipindi cha miaka tangu CRC ilipopitishwa, serikali nyingi zimetambua umuhimu wa maisha, maendeleo, ulinzi na ushiriki wa watoto.

Kwa maneno mengine, tuna uthibitisho ambapo watu wa jumuiya ya binadamu wanaweza kukusanyika, bila ya kujali tofauti zao, kufanya kazi ili kufikia malengo ya pamoja ya kimaadili na kiuadilifu yatakayoratibu, kuwezesha na kutia msukumo wa maisha yao kwa pamoja.

# Ulimwengu wenye dini mbalimbali

## Rasilimali za dini kwa maisha ya kiadilifu

Kwa karne nyingi, mila na desturi za kidini zimewafunza na kuwajengea maadili kwa wafuasi wao. Baadhi wanasema kwamba ni katika maisha ya kidini ndipo watoto wanapojifunza thamani ya maisha. Uelewa huu unamaanisha kwamba dini zenyewe na kama namna ya kuonyesha na kueleza utamaduni, ndizo zinazopitisha maadili na uadilifu, na kufundishwa kwa njia ya maandiko, hadithi za kidini zinazofundisha maadili, methali, mifano na vitendo. Ina maana pia kwamba bila ya mshikamano wa karibu wa msingi kwa familia na jumuiya, haitawezekana kuwa na maendeleo ya binadamu waadilifu yaliyojumuishwa katika kanuni za tabia na mwenendo wa binadamu.

Mtaalamu wa Sayansi ya Jamii, Michael Walzer alisema:

> *"Jamii ni muhimu kuwa mahususi kwa sababu zina watu na kumbukumbu, watu wenye kumbukumbu si zao wenyewe tu, bali pia za maisha yao ya pamoja. Ubinadamu, kinyume chake una watu lakini si kumbukumbu, kwa hiyo hauna historia wala utamaduni, hauna ada au kaida za kimila, wala aina za maisha yanayofahamika na wote, hauna sherehe na matamasha, hauna uelewa wa pamoja wa mambo mema ya kijamii. Ni ubinadamu kuwa na vitu hivi, lakini hakuna njia moja ya kuwa navyo."*[19]

Upekee uliokithiri unaweza kusababisha kujitenga na kujihisi bora isiyo na mantiki. Tusidharau hatari kubwa itakayotokea kwa amani na utulivu wa dunia kutokana na ukereketwa kupita kiasi wa watu wengi wanaodai kwamba wanatenda kwa ajili ya kudumisha maadili au kwa ajili ya dini yao. Tunaona mifano duniani kote ya watoto wanaoshawishiwa wawaone wengine kama maadui, wanaohimizwa kushiriki katika vitendo vya ugomvi kama sehemu za dhamiri za dini yao, au wamelelewa kutojali mahitaji na haki za watu wengine. Kwa hiyo michakato ya maisha ndani ya mila na desturi zote za kidini, hasa kuhusiana na watoto haina budi kuzingatia vipimo vinne vya dhima.



## Vipimo vinne vya dhima

**Kwanza:** Mila na desturi zote za kidini, wakati zinakuza imani na maadili ya jumuiya yao kwa watoto, hazina budi pia kuhakikisha kuwa maadili na imani vinafundishwa na kujifunza kwa namna inayowaheshimu wengine na 'utofauti' wa wengine. Mtoto asiyejifunza kuhusiana na wale wanaoamini na kutenda namna tofauti anakuwa na upungufu au kasoro ya kuishi katika ulimwengu wenye dini na utamaduni mbalimbali.

**Pili:** Mila na desturi zinatakiwa kufanya juhudi ya makusudi katika ufundishaji wao ili kuimarisha maadili ya kidini na kiutamaduni ya mila na desturi zao zinazohimiza uwazi, uaminifu na mtazamo wa huruma kwa binadamu wengine. Maadili haya hayana budi kuhimizwa kwa watoto tangu wakiwa na umri mdogo.

**Tatu:** Wakati tunatambua kwamba mila na desturi za kidini zinatofautiana, hatuna budi pia kuangalia maadili yanayofanana na yanayoingiliana yanayoweza kuleta misingi kwa watu kushirikiana kwa mambo yanayowahusu wote. Hatuna budi kufundisha na kutekeleza imani zetu kwa namna zinazoonyesha ubinadamu wetu wa kutegemeana.

**Nne:** Siku hizi tunasisitiza pia dhana ya elimu ya dini mbalimbali, kutojifunza kwa kujitenga bali kwa kuhusiana na wengine. Watoto hawana budi kujua na kuthamini si imani zao tu, bali pia wawe na uelewa wa kutosha wa wanachoamini wengine, na mambo yanayofanana kwetu sote kama jumuiya ya binadamu na kuhusiana na changamoto mahususi.

19 Michael Walzer, *Thick and Thin: Moral Argument at Home and Abroad*, Notre Dame, University of Notre Dame Press, 1994, uk. 8.

Maisha hayabaguliwi kwa imani. Bila ya kujali imani zetu, tuna uzoefu wa namna mmoja – kuzaliwa, kifo, furaha na maumivu. Sote tuna shauku ya kupata majibu kwa baadhi ya maswali yanayohusu maisha. Katika changamoto hizi mafundisho ya dini yanajitahidi kuhimiza kanuni za maadili zenye unyofu, na kila mila na desturi zinajitahidi kueneza unyofu wa maadili haya kupitia mafundisho ya dini yake, yanayotafsiriwa katika maisha ya kidini.

Katika Kikao Maalumu cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kuhusu Watoto, cha mwaka 2002, watoto walioshiriki walisema:

> *"Tunaahidi kumtendea kila mmoja kwa hadhi na heshima*
> *Tunaahidi kuwa wazi na kuzingatia tofauti zetu.*
>
> *Sisi ni watoto wa duniani na ingawa tunatofautiana asili zetu,*
> *tuna ukweli unaofanana.*
>
> *Tunaunganishwa na mapambano ya kufanya ulimwengu kuwa mahali pazuri kwa wote,*
> *Mnatuita kizazi kijacho, lakini pia sisi tupo sasa."*[20]

Vijana na watoto wengi siku hizi si kama wanaona ulimwengu huu wenye wingi kuwa ni uhalisia, bali pia wanapata rasilimali ya wote: Uelewa wao wa dunia, mwingiliano wao, michango yao na uzoefu wa maisha wa wote, utambulisho wao changamani na misingi yao ya kimaadili unaundwa na kuzingatia uanuwai huu mpya. Wanaungana katika mapambano yao ya kufanya mahali hapa kuwa ulimwengu bora zaidi na wako tayari kuangalia mila na desturi zao katika kutafuta kanuni za maadili zinazozingatia unyofu.

## Mchamungu na asiye na dini

Kuna uhusiano halisi kati ya elimu ya maadili na mafundisho ya dini; hata hivyo dhana mbili hizo si sawa. Elimu ya maadili inavuka mipaka ya imani za dini. 

Wilfred Gantwell Smith anasema:

> *"Kwa maoni yangu, imani ni ukubalifu wowote wa uzuri; juhudi zote za kutafuta ukweli, juhudi zote za kutafuta haki, utambuzi wowote kwamba baadhi ya mambo ni mazuri na baadhi ni mabaya. Na kwamba ina umuhimu; hisia yoyote au unyonyeshaji upendo kwa vitendo, upendo ambao waumini wanaita 'Mungu', mifano yote hii na minginemingi ni ya imani ya mtu binafsi na ya jumuiya."*[21]

Wilfred Gantwell Smith anasema kwamba sehemu ya kuwa mtu wa imani ni uwezo wa kutofautisha kati ya jambo zuri, linalokubalika au baya, na kuamini kuwa tofauti hizo ni muhimu. Watu wanaoamini hivyo si lazima wawe na bango la dini, bali wamekumbatia mambo ya kiroho yanayozingatia umuhimu wa uhusiano chanya kwa maisha ya jumuiya. Kusema kweli, kuna wabia muhimu wanaoweza kushiriki katika kujenga ulimwengu unaofaa kwa watoto wetu.

## Kujifunza Kuhusiana baina yetu

Imani na maisha ya kimaadili vinaweza kuwa na msingi katika mila na desturi ya dini, lakini pia vimevuka mipaka ya upekee wa dini yoyote. Maadili ambayo Baraza la Dini Mbalimbali linataka kuhimiza yana muktadha wa dini mbalimbali na yanahusika zaidi na uhusiano na wengine. Maadili ni suala la mtazamo na siyo seti ya mfumo wa imani unaofundishwa na kanisa au mafundisho – ni mkabala kwa jirani wa mtu, kwa maumbile na kwa maisha yenyewe. Ni kutokana na mtazamo huo, na desturi ambayo hutokana nayo, na si kupitia nadharia, kwamba tunaelewa mila na desturi zetu na za majirani wetu.

20 UNICEF, *A World Fit for Children*, September 2005, uk. 12.

21 Wilfred Cantwell Smith, *Patterns of Faith Around the World*, Oneworld, Oxford, 1962.

Hatuwezi kuishi kama kwamba kila dini ni kisiwa. Katika ulimwengu wa siku hizi, watu wa dini tofauti na watu wasio na dini, wanalazimika kukabiliana. Jamii zetu na jumuiya zimekuwa na utamaduni na dini nyingi na imani ya mtu mwingine ni muhimu. Uhusiano wa dini mbalimbali na mkabala wa maisha ya dini umekuwa sehemu muhimu ya kuwa Mchamungu.

Kujifunza dini mbalimbali lazima kueleweke katika muktadha wa elimu bora, kama inavyoelezwa katika lengo la 6 la Azimio la Elimu kwa Wote na ndani ya nguzo nne za UNESCO kwa elimu: kujifunza kujua, kujifunza kufanya, kujifunza kuishi pamoja na kujifunza kuwa. Kwa mujibu wa UNESCO, elimu ya ubora wa hali ya juu inahusu utayarishaji wa zana za maisha ambazo wanafunzi wanahisi kujiamini na kushawishika kutumia. Pia inahusu utayarishaji wa tabia na mwenendo kwa msingi wa maadili yanayofaa – uelewa na heshima kwa watu wa aina zote, kwa haki zao, kwa ulimwengu asilia, kwa siku zilizopita na zijazo.

Kwa UNICEF, elimu bora inawaandaa watu kuishi maisha yenye mafanikio na kujenga jamii bora kwa kuendeleza stadi, maarifa, mitazamo na maadili yanayohitajiwa kuleta mabadiliko ya tabia yatakayowawezesha watoto, vijana na watu wazima kuzuia migogoro na ugomvi, ambayo ni ya wazi na ya kimuundo; kutanzua migogoro kwa amani na kuweka masharti yanayofaa kwa amani, iwe kwa ngazi ya ndani ya mtu baina ya watu, kati ya vikundi, kitaifa au kimataifa. UNICEF inaunga mkono stadi za maisha kwa msingi wa kuzuia ugomvi na kujenga amani, kuhimiza kujifunza kufikiri, kihemko na kijamii kulingana na nguzo nne.

## Kusali Pamoja au Kuja Pamoja Kusali

Katika Siku ya Kimataifa ya Ibada kwa ajili ya Amani iliyofanywa, Assisi mwaka 1986, tofauti ya wazi ilifanywa: Washiriki hawakuja kusali pamoja , walikuja pamoja kusali. Hii inaleta hoja ya kusali pamoja.



Siku hizi watu wa dini tofauti wanakutana bila kutegemea, wanafahamiana na kufanya kazi pamoja. Watu wanaoishi na kuzungumza na majirani wa dini tofauti, na kuelewa mambo ya kiroho ya watu wengine, wagependa mchakato huu wa kukua pamoja uonekane pia katika sala na ibada. Kuna wale wanaojiuliza kama sala, ibada na kutaamali, kusema kweli visiwe mwanzo wa hija ya kiroho ya dini mbalimbali. Kwamba huo utafiti wa pamoja utaweza kuwa zaidi ya maneno, kuhimiza mazungumzo na kuelekea kwenye ushirikiano katika jamii zenye uanuwai.

Mara nyingi kutaka kushirikiana katika ibada na sala hutokana na wasiwasi wa pamoja wa jumuiya, au kama majibu ya mgogoro au maangamizi. Mashambulizi ya kigaidi ya tarehe 11, Septemba, 2001 na mafuriko ya tsunami Asia ya Kusini yalikuwa matukio ambapo watu wa dini tofauti walikutana pamoja kwa ibada na sala ya papo kwa hapo. Vita vya kwanza vya Ghuba viliwakutanisha Wayahudi, Waislamu na Wakristo katika sehemu mbalimbali duniani kukusanyika kwa ajili ya kile tunachokiita ibada ya dini mbalimbali. Katika baadhi ya sehemu za dunia, ibada za dini mbalimbali inaweza kuwa ishara ya mshikamano wa taifa, kama vile wakati wa sikukuu ya taifa na sherehe za jumuiya. Hii ni mifano ya umoja unaofikia kwenye tofauti za dini. Matukio kama haya yanaweza kuwa ya ghafla na yasiyofuata utaratibu na yasiyo ya binafsi, lakini matukio mengine ya ibada ya dini mbalimbali ni ya makusudi zaidi: sherehe za harusi, maadhimisho na matukio ya kifamilia.

Kuwahusisha na kuwashirikisha watoto katika ibada za dini mbalimbali lazima kufanywe kwa uzingativu zaidi na heshima kwa kila mila na desturi ya dini. Ibada na sala ni taratibu na mwelekeo wa kiroho wa kila mila na desturi inayokuwa kwenye kiini chenyewe hasa. Kujifunza dini mbalimbali zinazohimizwa na Baraza la Dini Mbalimbali kuhusu Elimu ya Maadili kwa Watoto ni safari ya uangalifu na ya kuheshimika ambayo lazima ichukuliwe kwa pamoja na uelewa kamili kwamba tunazuru maeneo matakatifu katika kila mila na desturi.

# Mambo ya Kiroho

Watoto wana uwezo mkubwa wa mambo ya kiroho. Kwanza, watoto wana hisia maalumu ya muda. Mtoto anaweza kutulia tuli kwa muda mrefu, kuinama kwenye mstari wa siafu, wakishangaa safari yao. Kutokana na mtazamo wa mambo ya kiroho, mtoto ana uwezo wa kutekwa na tukio, ambapo watu wazima wengi wanatumia muda mwingi kutafuta kujifunza tena. Uwezo huu ni pamoja na uelewa kamili wa uhalisia uliopo na hisia ya muda usio na kiwango.

Tunu nyingine ya mambo ya kiroho kwa watoto wadogo ni mshangao, na si ndoto za ajabu, au ndoto zinazokatikakatika kutoka uhalisi, lakini uzoefu wa ukamilifu wake. Inahusisha mwili na hisia kama ilivyo akili. Mtoto anaweza kutaka kusikia harufu ya kinyunya tena na tena wakati mkate unapotayarishwa, au kusikia matone ya mvua yakidondoka kwenye paa, au kukaa kimya akiangalia mshumaa ukiwaka. Mshangao unasababisha furaha, unahifadhi msisimko na shauku, na kujaza nguvu na matumaini.

Upendo ni sifa bainifu ya tatu ya uwezo wa mambo ya kiroho ya watoto wadogo. Kutoa na kupokea kuko kwenye kila moyo wa mtoto mdogo. Je, hatujawahi kuwa na wakati huo maalumu ambapo mtoto anatusogelea na mwanasesere anayempenda, akiamini kwamba hatutamchukua bali tutacheza na kumrudishia. Lakini pia tunajua ni mapema kiasi gani mtoto anaweza kujifunza kutomwamini mtu.

Akiwa amedhamiria kuunda mtandao wa watu wanaohusika na watoto, Mchungaji Takeyasu Miyamoto alianzisha Baraza la Dini Mbalimbali kuhusu Elimu ya Maadili kwa Watoto, akisema:

> *"Ni imani yangu ya dhati kwamba kuanguka kwa mambo ya kiroho na kukosekana kwa uzingativu kwa maadili ya msingi vipo kwenye kiini cha kuongezeka kwa ugomvi na udhalimu tunaouona siku hizi duniani kote. Hatua muhimu katika barabara ya kuelekea katika amani ni kuhakikisha kuwa kila mtoto anapata fursa ya kufikia kamilifu uwezo wake wa kuzaliwa wa kukua kiroho, na ndiyo maana utekelezaji wa elimu maadili ya dini mbalimbali – shuleni na kwenye maeneo mengine ya kielimu – ni muhimu katika kukamilisha lengo la kujenga ulimwengu wenye amani ya hadhi ya utu, ulimwengu unaofaa kwa watoto kwa uhalisia wake wote".*

Kauli inayofanyia kazi inazungumzia uwezeshaji wa watoto kufikia "uwezo wao wa kuzaliwa wa kukua kiroho". Hii ina maana kwamba mambo ya kiroho sio kitu cha kumbwagia au hata kumpa mtoto. Elimu maadili kwa upande mwingine inakusudia kumpa mtoto uwezo wa kushiriki kwa kikamilifu katika mambo ya kiroho kwa ustawi wake na jamii yote. Ni muhimu kutambua kuwa, wakati mtoto ana uwezo wa kuzaliwa na kukua kiroho, ni lazima kustawishwa na kuendelezwa. Kwa watoto wanaotuonyesha uzingatiaji usio na kikomo ya muda, mshangao na upendo, tunaweza kutoa maneno na taswira tulizotokea kujua kwamba ndiyo wenye upendo wa kudumu, wa kustaajabisha na usio na ukomo. Ni muhimu kwamba hali hii ya kiroho inastawishwa ndani ya mila na desturi mahususi za kidini au kiroho ili muundo na msingi thabiti vitolewe kwa ukuaji na maendeleo. Ukuaji huu unatokea kupitia mchakato unaohusisha ufundishaji, tafakuri tunduwizi, mjumuiko na kujenga na kuwa na desturi ya uhusiano mzuri.

Mambo ya kiroho na dini si sawa, na wakati mwingine yanasigana. Msisitizo unaowekwa na baadhi ya watu kuhusu mambo ya kiroho unaweza kutokana na hamu ya kuwa wazi zaidi ili si kila kitu kimo ndani ya mipaka ya dini iliyopo. Hata hivyo kuna mambo ya kiroho ambayo si ya kweli yanayowasababisha watu kujihusisha zaidi na ubinafsi wao wenyewe au kukengeuka hali halisi ya dunia wanamoishi. Kuna wale wanaofikiria kwamba mambo ya kiroho yanahusiana na hisia na mihemko. Lakini mambo ya kiroho ni njia ya kupitishia mihemko, hisia na huruma katika kujishugulisha. Kujishughulisha kwa upande mwingine ni msukumo wa ukombozi na uwezeshaji.

Mambo ya kiroho ni msimamo, namna ya kuishi, namna ya kumweka mtu kwenye ulimwengu. Ni jambo linalotuweka zaidi ya vile tulivyo, zaidi ya vile ambavyo kwa kawaida tumezoea.

Kwanza mambo ya kiroho yanayokwenda zaidi ya hapa tulipo yanatafuta hatima na siyo hali ya sasa. Kwa mfano, kama tunaangalia hali ambapo watu wazima wanatumia nguvu dhidi ya watoto, ni kwa sababu pengine wameathiriwa na matokeo ya sasa – hawaendi kwenye baadaye. Mara nyingi ni kujihusisha zaidi huku na mambo ya sasa ndiyo yanayosababisha watu wazima kuwa wakali na kutumia nguvu. Kuwaadhibu watoto kunaonyesha kero kuhusu mambo ya sasa, hatua ya kumnyamazisha mtoto kama matakwa ya sasa, bila ya kuuliza kuwa adhabu hii itakuwa na maana gani kwa mtoto huyu baada ya muda fulani. Mambo ya kiroho yanayokwenda mbali zaidi – mambo ya kiroho yanayopita uwezo wa binadamu – hayaridhishwi na mambo ya sasa, bali yanataka kukumbatia zaidi ya baadaye.

Pili, mambo ya kiroho yanayokwenda mbali zaidi – hayaridhishwi na majibu. Kwenda mbali zaidi ni kuhoji. Watu wengi wanahitaji majibu ya haraka. Kadiri watu wanavyouliza maswali mengi zaidi, ndivyo wanavyosogelea zaidi kile wanachotafuta. Wakati mwingine tuna hakika ya kuwa tuna majibu na hivyo tunashindwa kuuliza maswali. Msimamo wa mambo ya kiroho hauwezi kuridhishwa na majibu peke yake.

Tatu, mambo ya kiroho yanakwenda mbali zaidi, hayazuiwi na mipaka. Badala yake yanazingatia zaidi mambo yanayowezekana. Inawezekana kwa watu kuishi na kufanya kazi pamoja kwa manufaa ya jumuiya. Wito wa kumpenda jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe, ni changamoto ya kwenda mbali zaidi, kujaribu kuishi inavyoelekea kuwa mgongano. Je inawezekana kumpenda adui wako? Katika kuuliza kama ni kweli, tunajiweka wazi kwa uwezekano wenyewe.

Mambo ya kiroho ni wito wa kwenda mbali zaidi ya mahali ambapo mtu yupo – kutoka mambo ya sasa hadi ya baadaye, kutoka majibu hadi maswali, kutoka mipaka hadi kwenye yanayowezekana. Kuendeleza uwezo wa kuzaliwa kwa mambo ya kiroho kunaimarisha juhudi ya kujenga ulimwengu unaofaa kwa watoto.



**Sehemu zinazofuata za *Kujifunza Kuishi Pamoja* inatoa mwongozo wa vitendo kwa ajili ya programu ya utamaduni na dini mbalimbali kwa elimu ya maadili.**

**Mchakato huo umegawanywa katika Moduli mbili za Kujifunza zinazopendekeza mawazo kwa shughuli na zinasaidiwa na rasilimali kutoka mila na desturi tofauti na kanda zinazofaa kwa mchakato wa kujifunza.**

Ni matarajio yetu kwamba utaona kuwa ni kitabu kinachofaa.

# Sehemu ya 1

# Mwongozo wa Mtumiaji

## Upeo na Madhumuni

Kujifunza utamaduni na dini mbalimbali katika elimu ya maadili kunasimamia uanuwai na kuhimiza mazungumzo na mawasiliano na wengine, pamoja na mtu mwenyewe. Ni mchakato unaoendelea kwa kujifunza peke yako na kwa pamoja unaohimiza nja bora zaidi ya kuishi pamoja katika ulimwengu wa kimataifa na wenye dini mbalimbali. Kunahusu kutetea, kuendeleza na kuwezesha ukuaji wa unyofu wa pamoja kwa watoto na vijana.

Kanuni na misingi ya kimaadili na unyofu vinavyohimizwa na *Kujifunza Kuishi Pamoja* vinabainishwa katika dhamira ya Bazara la Dini Mbalimbali kuhusu Elimu ya Maadili kwa Watoto; yenye shabaha ya kukuza heshima kwa watu wa dini na ustaarabu tofauti miongoni mwa watoto kwa:

> Kuhimiza mifumo ya unyofu inayosisitiza kuishi kwa pamoja kwa heshima na mwafaka na mshikamano miongoni mwa watu wenye asili ya tabaka, mbari, dini, utamaduni na itikadi tofauti.

> Kuhimiza desturi ya unyofu chanya wa kimataifa kama vile dhamiri ya dhati ya kutekeleza haki za binadamu zilizoandikwa na kuridhiwa na jumuiya ya kimataifa.

> Kukuza mambo ya kiroho yatakayoleta kuheshimu dini nyingine na kuendelea na maelewano ya pamoja na mwingiliano miongoni mwa imani tofauti, kusababisha utajirishaji wa utamaduni wa dini iliyomo kwenye kila mila na desturi ya imani.

> Kujenga utamaduni wa amani unaowawezesha watoto na vijana kuwa chachu ya mabadiliko na wajenzi wa amani.

## Moduli za Kujifunza

*Kujifunza Kuishi Pamoja ina* Moduli Mbili za Kujifunza: ***Kujielewa Binafsi na Wengine*** na ***Kuubadili Ulimwengu Pamoja*** utakazozisoma kwenye Sehemu ya 2. Moduli hizi zinahusiana na zinakamilishana.

Moduli hizi zina **vibanda** vingi vilivyotayarishwa ili kuwawezesha washiriki kuona safari ya kujifunza, ambapo njia mbalimbali huwawezesha kukabili changamoto za kimaadili na kuwasaidia kugundua namna wanavyoweza kuwa chachu ya mabadiliko. Moduli hizi zina mbinu mbalimbali za tathmini zilizoko kwenye Sehemu ya 3, zitakazokusaidia wewe na washiriki kupima maendeleo. Sehemu ya 4, ina shughuli mbalimbali unazoweza kuzitumia wakati wa kubuni njia yako mahususi kwenye moduli. Mapendekezo ya shughuli zinazofaa yanatolewa kwenye kila moduli.

Moduli mbili hizo zimeonyeshwa katika ramani ya kijiji. Hakuna njia moja ya kufuata – unaweza kuamua njia yako mwenyewe pamoja na washiriki wako. Ili kuonyesha kila moduli, kuna bango la mchoro.

Kibanda ni sehemu yenye kivuli, iliyolindwa ambamo unaweza kusimama kwa ajili ya motisha, ugunduzi, kukabili hali, kutafakari na mazungumzo kupitia vibanda mbalimbali kutawapitisha washiriki kwenye safari ya ugunduzi binafsi.

Neno "kibanda" ni lenye asili ya Kiajemi na linamaanisha kitu kinachokuwa kama kivuli au kinachotoa kivuli. Asili yake ni usanifu majengo wa Kiislamu, kibanda cha wazi cha duara chenye paa lenye mihimili ya nguzo, mahali wazi lakini pamelindwa. Vibanda vilikuwa maarufu sana Uajemi, India, Pakistani na katika Ufalme wa Uturuki, kuanzia Karne ya 13 na kuendelea.

Neno hili hupatikana katika Kiajemi, Kiarabu, Kituruki, Kifaransa, Kijerumani, Kipolishi, Kireno, Kiramania na Kihispania.

Hakuna ukomo wa muda. Badala yake programu zinaweza kubadilishwa kulingana na mahitaji mahususi ya kikundi, kutoa muda wa kutosha kwa washiriki, kutafakari na kutafuta uhusiano ndani na baina ya kila kibanda. Moduli hizi zinaweza pia kurekebishwa kulingana na hali na miktadha tofauti. Ramani za kijiji zinaonyesha eneo au vituo vya kupumzikia, ambapo unaweza kusimama kupima mchakato wa kujifunza wa washiriki. Kwa maelezo zaidi unaweza kurejea alama za vituo vya kupumzika katika sehemu ya Ufuatiliaji wa Maendeleo.

Njia ya kujifunza utakayochagua haina budi kuwawezesha washiriki kufanya uhusiano baina ya vibanda vya mfululizo. Mkabala huu utawasaidia washiriki kuendeleza unyofu uliohimizwa katika kila moduli na kuhusisha zoezi hili na maisha yao wenyewe. Njia ya kujifunzia haina budi pia kuruhusu mchakato wa ugunduzi unaohimiza mitazamo chanya na tabia na mienendo inayofaa kwa kuishi pamoja, kuheshimu utamaduni na dini tofauti, na kwa pamoja kubadili ulimwengu wetu wenye dini nyingi.

## Unyofu wa Aina nne



*Kujifunza Kuishi Pamoja* kinahimiza unyofu wa kimaadili wa aina nne kuu:

> Heshima.
> Ushirikali.
> Uwajibikaji.
> Upatanisho.

Unyofu huu umechanganywa kwenye moduli mbili na kutumiwa katika miktadha na hali tofauti kwa lengo la kuwezesha mchakato wa kujifunza dini mbalimbali na kujenga amani.

Kupitia moduli hizo, washiriki wanahimizwa kujifunza:


> Namna ya kuheshimu na kujielewa wewe na kuwaelewa wengine.
> Namna ya kutenda kwa mtazamo wa usuluhishi kwa mtu mwenyewe na kwa wengine.
> Namna ya kukabili mahitaji ya dunia na kulinda haki za binadamu.

**Kuwaheshimu** watu wa dini, ustaarabu na utamaduni tofauti hukuzwa na kuimarishwa na kufikia kuwa mtu fulani – kujifunza maana ya **ushirikali**. Heshima na ushirikali huleta uelewa mkubwa na matendo kwa msingi **wajibu,** wa mtu na wa pamoja ambao matokeo yake ni kuwa tayari kwa **upatanishi**. Hadhi ya binadamu inalindwa na kukubaliwa wakati tunapoelewa uzoefu mbalimbali na uhalisia, historia na kumbukumbu walizonazo binadamu, na tunapotafuta amani, haki, usawa, na haki za binadamu na kuishi pamoja kwa mwafaka.

## Moduli

### Moduli ya 1: Kujielewa Binafsi na Wengine

Katika moduli hii, washiriki wanajifunza kuhusu wao wenyewe na kuhusiana na wengine. Wanajifunza kukubali tofauti na kufanana, kusikiliza na kukubali hoja na maoni ya watu wengine, na kuelewa na kuwaheshimu wale walio tofauti na wenye fikira tofauti.




### Moduli ya 2: Kuubadili Ulimwengu Kwa Pamoja

Katika moduli hii washiriki wanagundua kuwa ulimwengu unahitaji mabadiliko ya kijamii. Shughuli zinawaongoza kuwa tayari kwa upatanishi na kukuza uwezo wao wa kijamii wa kushirikiana na wengine. Moduli hii imetayarishwa kuwapa mbinu za kuwawezesha wafanyakazi na watu wa utamaduni na dini mbalimbali kuwasaidia kubadili jamii zao wenyewe na ulimwengu mpana, kwa pamoja na ndani ya uwezo wao wenyewe wa kushawishi.



## Kulea vijana wajenge mambo yao ya kiroho waliyozaliwa nayo

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kilitayarishwa kuwatambulisha vijana na watoto kwenye mielekeo ya maisha ya kiroho. Kinajaribu kuchangia kuelekea haki yao ya maendeleo kamili na ya afya kamili, kiakili, kiroho, kiuadilifu na kijamii kama ilivyoelezwa kwenye Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto. Lengo ni kumsaidia kila mshiriki kujenga taswira binafsi iliyo bora na uhusiano chanya kwa watu wengine, mazingira na ule ambao watu wanaiita kuwa ni Mungu, Ukweli wa Mwisho au Uwepo wa Mungu na hivyo kupanua ubora wa maisha kama mshiriki wa jamii ya taifa au jumuiya ya kimataifa. Watoto na vijana wakiwa na uelewa na kina, akili iliyojengwa kimaadili na kufikiria kitunduizi watakuwa na uwezo mkubwa wa kubadili changamoto ya kufanya uchaguzi bora zaidi katika ulimwengu wenye ushawishi na uteuzi wa aina mbalimbali.

## Waelimishaji wa Wawezeshaji – kiini cha mchakato wa kujifunza

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kinahitaji mtindo wa uwezeshaji wa kidemokrasia na shirikishi. Wazo si kwamba watu wazima/walimu wanajua kuhusu maadili na unyofu na kwamba watoto au vijana hawajui. Mwelimishaji/mwezeshaji haamuru bali anaelekeza na kuunda mchakato wa kujifunza kwa kupanga shughuli za kujifunza, ambazo mchakato wake unamsaidia kila mtu, wanafunzi na walimu kukuza pamoja na kuhoji maarifa yao, mitazamo na mienendo na tabia.


'Ubora' wa mwelimishaji/mwezeshaji hubadili kila kitu katika uzoefu wa kujifunza. Washiriki wanakutegemea wewe kama mwezeshaji kuwaongoza kwa usalama kwenye safari yao. Wanatakiwa waweze kukuamini na si kuwadharau bali kuwasaidia nyakati za matatizo au shida. Wawezeshaji wanaojionyesha kuwa wamejiandaa vizuri, wasio na upendeleo, waaminifu watajenga imani kwa washiriki na kusaidia kuhakikisha kuwa washiriki watafurahi kuwa sehemu ya safari uliyoianzisha kwa ajili yao.



Mambo machache muhimu ya kumwongoza mwezeshaji:

1. Jiandae kwa kila somo, lipitie kwa makini mapema na kufikiria kuhusu majadiliano na mawazo yatakayopatikana kwa kila hatua. Jiandae kwa matatizo au ugumu na maswali. Hakikisha kwamba una vifaa vyote unavyovihitaji na tafuta njia rahisi za kuanza na kumaliza shughuli zilizochaguliwa.
2. Kufuata muda ni muhimu sana. Panga shughuli zako kulingana na muda uliopo. Kama muda hautoshi, amua wapi utafupisha shughuli au kumalizia ipasavyo mpaka wakati ujao.
3. Daima uwe na vichangamsho ulivyoviandaa kukusaidia kuanzia somo, kuwarudisha washiriki katika somo(baada ya muda wa mapumziko), na agana nao wakifurahia somo.
4. Fanya somo lifurahishe – washiriki watakuwa tayari zaidi kuchangia, kushiriki na kujumuika kwenye somo kama wataweza kufurahi pamoja.
5. Usitetee tabia au mitazamo yoyote mibaya miongoni mwa washiriki. Weka wazi kwamba aina yoyote ya ubaguzi wa rangi au chuki au upendeleo wa aina yoyote hauna nafasi darasani. Kama hili huenda likawa ni tatizo toka mwanzo, litakuwa pia swala la kwanza kujadili na washiriki.
6. Wakati wote waheshimu washiriki, kwa kuwa kuwaheshimu wengine hutokana na mifano ya kuigwa.

# Mchakato wa Kujifunza na Maelekezo






Mchakato wa kujifunza uliyoonyeshwa hapa ni mwongozo utakaowasaidia wawezeshaji wa elimu maadili kuhakikisha kuwa washiriki wanashirikishwa kwa ukamilifu katika uzoefu. Mzunguko unawachukua washiriki katika mchakato wa ugunduzi, matokeo yake yanasababisha fikra mpya na kujifunza kwa mfululizo. Mchakato wa kujifunza unakuwa kama mfano wa kutayarisha masomo na kuwafanya washiriki waelewe zaidi uzoefu wao wa kujifunza dini mbalimbali.



## Motisha

Anza somo hili kwa kutumia hadithi, nyimbo, mashairi au katuni zinazochochea udadisi wa washiriki kuhusu mada, huwapa changamoto juu ya maono yao na kuwamotisha watafiti zaidi masuala ya kimaadili. Hakikisha kuwauliza washiriki kuhusu muziki na vyombo vya habari vitakavyofaa au kulingana na shughuli zitakazoongezwa kwenye rasilimali, zilizoko kwenye sehemu ya 5.



## Utafutaji

Mara baada ya washiriki kupata picha ya mada itakavyokuwa, watataka kupeleleza taarifa inayofaa. Hatua hii si ya kuwasilisha hoja nyingi, bali ni wakati wa washiriki kupeleleza mawazo na kupata uzoefu mpya kwa njia ya mazoezi kwa vitendo. Huu ni wakati unaofaa kujenga mazingira ambapo washiriki wanaweza kujua zaidi, kueleza mawazo, hisia na kile ambacho hisia ya nafsi inavyowaambia.



## Mazungumzo

Mazungumzo ni muhimu kwa mchakato wowote wa kujifunza, hasa mchakato wa kujifunza dini mbalimbali. Mazungumzo hutoa fursa ya kubadilishana mawazo, kushirikishana uzoefu, kugundua mengine na huwapa fursa washiriki kupima maono yao wenyewe. Nafasi inayofaa inahitaji kutafutwa ambapo washiriki watajihisi huru zaidi kushiriki kwa ukamilifu bila ya kufanyiwa uamuzi.



## Ugunduzi

Kupitia mchakato wa mazungumzo, washiriki watagundua maelewano mapya na mawazo. Hata hivyo ugunduzi hauji haraka au wote kwa wakati mmoja. Kunahitajika muda wa kushirikiana matokeo makuu ya majadiliano ya kikundi. Hii inawawezesha washiriki kupata uzoefu wa "Kumbe"! na kufurahia matokeo, ambapo wanaunganisha mawazo na kupata utambuzi mpya.



## Tafakuri

Huu ni wakati wa kutafuta uhusiano wa mtu mwenyewe. Unaweza kuwapa muda kwa kila mshiriki kutafakari kwa kutumia Utaratibu wa Kujifunza (angalia uk. 53), ambapo washiriki wanaweza kupitia waliyojifunza wao wenyewe kuhusiana na hali halisi na kupima unyofu na mitazamo yao.





## Tendo

Tendo mara nyingi sio lazima kiwe sehemu ya somo, lakini daima linatakiwa kuwa matokeo ya kujifunza. Kila somo lazima lihitimishe na washiriki kuhusisha kujifunza kwao na uhalisia wao ambao unaweza kuwachochea wabainishe kitendo kinachofaa. Somo linahitaji kuwawezesha washiriki kuwa chachu ya mabadiliko, kuimarisha uwezo wao wa kukabili hali inayohitaji uelewa wa pande zote.

Elimu ya Maadili kupitia kujifunza dini na tamaduni mbalimbali, si mwisho bali ni mwanzo wa kuwezesha elimu. Mchakato wa kujifunza, ukiwa umetayarishwa kutokana na mtazamo wa dini na tamaduni mbalimbali unawaruhusu washiriki watafakari tamaduni mbalimbali, mila na desturi za imani, mawazo na namna ya kufikiria. Pia umetayarishwa kuwasaidia washiriki kuwa wazi kwa wenzao, kukuza mawazo ya ndani na kushughulikia ipasavyo mahitaji ya mazingira yao ya karibu.

# Mbinu za ufundishaji

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kinashirikisha mbinu za kisasa na za jadi. Shughuli zimepangwa katika makundi kulingana na mbinu zake za kufundishia, kwenye uk 63-64, Sehemu ya 5 kuhusu Rasilimali, zinatoa vifaa vya kufundishia vya kutosha kwa shughuli hizi, lakini unaweza pia kubuni vya kwako kukusaidia kutoa uwiano unaofaa wakati wa programu yako.

Msukumo wa jumla ulianzishwa katika maandiko ya Janusz Korczak, mwandishi na mwelimishaji wa watoto wa kabila la Kiyahudi na Kipolandi aliyetoa mchango mkubwa katika kutoa utambuzi mpya katika saikolojia ya mtoto. Kutoka kwenye shajara yake na maandishi mengine mtu anaweza kuona mtazamo na mkabala ufuatao:

> Kushawishi kila mtoto kujenga hisia bora ya kujistahi. Lazima ajifurahie bila ya kuwapaka matope wengine, hili ni sharti la awali kwa mtu kuwa mwadilifu. Kila mtoto hana budi kuhimizwa kujenga hisia ya ufahari kwa familia yake, jumuiya, utamaduni na dini, wakati huohuo kuthamini familia nyingine, jumuiya, utamaduni na dini.

> Jadili na tafakari hali halisi kwa kutumia uchunguzi kifani, ama hadithi za kweli za watu wengine, au hali zilizochukuliwa kutoka kwenye uzoefu wa washiriki wengine, ambapo uamuzi wa kimaadili na uchaguzi vilikuwa muhimu. Majadiliano hayana budi kuzingatia zaidi uchaguzi uliofanywa na katika mchakato wa yaliyotangulia uchaguzi huo: Mambo gani yazingatiwe na kwanini? Je, matokeo yangekuwa nini kama uchaguzi mwingine ungefanywa?

> Tumia hadithi za kale za mapokeo, hadithi za mafumbo, methali na misemo na nyimbo kutoa muundo wa kuongoza majadiliano ya mwenendo wa kimaadili.

> Wawezeshaji wakati wote hawana budi kuonyesha tabia wa kimaadili kwa wanafunzi wao na kwa kila mmoja. Vijana huiga kwa haraka mivutano na ujeuri kati ya watu wazima na wanaweza kutumia hali hiyo kama kisingizio cha tabia yao wenyewe.

> Tayarisha kanuni za mwenendo wa kikundi na, kama utahitajika, fanya majadiliano ya kimaadili wakati kanuni hizi zikikiukwa.[1]

Mikabala hii huleta mbinu za kufundishia zinazotoa nafasi ya kubadilishana mawazo, mwingiliano, makabiliano, ugunduzi, kufikiria kitunduizi, tafakuri na kutenda. Mbinu hii ya *Kujifunza Kuishi Pamoja* humweka mtu katika mchakato wa kujifunza kwa kujituma, unaoendeshwa kuhusiana na wengine. Pia husaidia kukuza stadi, kuimarisha maarifa ya washiriki na kuendeleza mitazamo inayowawezesha kujifunza na kuishi na kutenda katika jamii yenye mitazamo, mawazo na dini mbalimbali.

Ni wajibu wako kama mwezeshaji kuchagua mbinu inayofaa zaidi kwa kikundi. Zingatia kwamba mbinu zilizopendekezwa zinaweza kutumiwa kwa kuchanganywa, kurekebishwa kwa mujibu wa muktadha na umri wa washiriki na kutumiwa kwenye shughuli nyingi. Njia hizo zimekusudiwa kuhimiza ushiriki mkubwa, ushirikishaji na uhusiano na wengine.

1 Janusz Korczak (1878-1742), Myahudi – Mpolandi bingwa wa watoto na maradhi yao, mwandishi wa watoto na mwalimu wa watoto. Alikataa kupewa misaada kwa usalama wake mwenyewe, alifuatana na wanafunzi wa kituo chake cha mayatima hadi Auschwitz na inasemekana alisema “Huwezi kumtelekeza mtoto mgonjwa usiku na huwezi kuwaacha watoto nyakati kama hizi”. Mkabala wa Korczak katika kuwafundisha ni kumthamini mtoto kama mtendaji wa sasa, kwamba watoto wana haki zao. Alifafanua mawazo ya “mahakama” katika nyumba ya mayatima, ambapo kila mmoja – watoto na watu wazima kwa pamoja – walizawadiwa na kurekebishwa kwa usawa (angalia UNESCO Prospects, Quartely Review of Education, volume XVII, 1987).

## Njia zilizopendekezwa

### Kujifunza kwa misingi ya uzoefu

Kujifunza kwa misingi ya uzoefu hutumia uzoefu na tafakuri iliyojengwa kuongeza maarifa, kujenga stadi na kufafanua unyofu[2]. Uzoefu unaweza kuhusisha matukio ya awali katika maisha ya mshiriki, matukio ya sasa au yale yanayotokana na ushiriki katika shughuli za vitendo vinavyotekelezwa na walimu na wawezeshaji. Wanafunzi hutatafakari, hutathmini na huchambua binafsi au kwa pamoja.

Kujifunza kwa misingi ya uzoefu kuna sifa bainifu tatu:

> Ushiriki wa watu kwa ukamilifu – akili, hisia na hisi.

> Uhusiano wa kujifunza na uzoefu binafsi.

> Tafakari ya mfululizo kwa ajili ya mabadiliko kuwa uelewa wa kina.

Mbinu zinazotegemea uzoefu zinaweza kutayarishwa kupitia mbinu nyingi, zikiwemo uigaji, michezo, igizo dhima, kujifunza huduma na safari za ugani.

### Kujifunza kwa misingi ya ushirika

Wanafunzi wanagawanywa katika vikundi vidogo vinavyofanya kazi kwa uhuru ili kufikia lengo la pamoja. Washiriki wanajitahidi kupata msaada wa pamoja ili wanakikundi wote wanufaike kutokana na juhudi za kila mmoja. Katika kujifunza kwa mujibu wa ushirika kuna kutegemeana chanya miongoni mwa juhudi za wanafunzi kujifunza, washiriki wanatambua kwamba wanaweza kufikia lengo iwapo tu wanakikundi wote wanachangia kwenye jukumu waliliopewa. Njia hii inawezesha kujifunza kupitia mwingiliano.



Kujifunza kwa ushirika kunaimarisha uwezo wa watoto kufanya kazi na watu tofauti. Wakati wa mwingiliano wa vikundi vidogo wanaweza kutafuta fursa nyingi kutafakari na kujibu hoja mbalimbali ambazo wanakikundi wengine wanaleta mezani. Vikundi vidogo pia vinawapa fursa watoto na vijana kuongeza maoni yao kwenye suala linalohusu tofauti zao za kiutamaduni. Ubadilishanaji huu wa mawazo unawasaidia washiriki kuelewa utamaduni mwingine na mawazo.

Kujifunza kwa mujibu wa ushirika pia kunaimarisha stadi za mawasiliano ya washiriki na kuimarisha kujistahi kwao. Shughuli zinazohusisha kujifunza kwa ushirika zinahimiza mafanikio ya washiriki wote katika kikundi na hivyo kuchangia katika hisia za kila mshiriki kuhusu umahiri na kufaa kwake. Mifano ya kujifunza kwa mujibu wa mbinu za ushirika ni miradi ya pamoja, michezo na igizo dhima.

### Kujifunza kwa misingi ya tatizo

Katika njia hii, tatizo linatumika kusaidia kukuza ubunifu wa watoto, kufikiria kwao kitunduizi, uwezo wa kuchambua na kutafakari kuhusu unyofu wa kimaadili. Njia zinazotumia tatizo kuwa msingi zinawashawishi washiriki kuuliza na kujibu maswali, wakitumia udadisi wao wa kimaumbile. Watoto na vijana wanakabiliwa na matatizo yasiyokuwa na majibu kamili na yanayoonyesha utata wa hali za ulimwengu halisi.

Kujifunza kwa misingi ya tatizo kunawasaidia washiriki kuchukua mkabala wa bidii, unaozingatia kazi, na kujidhibiti katika kujifunza kwao.

2 David Kolb, *Experiential Learing: Experience as the Source of Learinig and Development*, Englewood Clifs, NJ, Prentice Hall, 1984. Association for Experiential Education. http//www.aee.org

Njia hii inaweza kutumiwa pamoja na uigizaji dhima, uchambuzi wa uchunguzi kifani, mitazamo na masuala ya kijamii au pamoja na mbinu zinazohusisha kujifunza kwa mujibu wa uzoefu.

## Kujifunza kwa misingi ya majadiliano

Majadiliano ni mwingiliano wa mazungumzo miongoni mwa washiriki yanayochochea ubadilishanaji wa mawazo. Yanasaidia kukuza stadi za mawasiliano na kusikiliza na kuhimiza uelewa wa masuala mbalimbali ya maoni. Majadiliano yanaweza kufanywa kwa namna mbalimbali, ikiwemo midahalo, mazungumzo, na vikundi maalumu. Yanaweza kuhusu uchunguzi kifani, matukio halisi ya maisha na mitanziko au kuhusu filamu muhimu, picha na nyimbo.

Mara nyingi majadiliano yatanufaika kutokana na mwelekeo wa mwezeshaji. Inapendekezwa kuwa utumie mbinu shirikishi kutoa muhtasari wa mwanzo wa kutafuta uhusiano kati yao. Mbinu hizi zinajumuisha mbinu za ramani za akili, michoro ya dhana, mpango unaohusisha mingine au mbinu ya kadi.

## Kujifunza kwa misingi ya kujipima na kujichunguza

Kutafakari inaweza kufikiriwa kuwa ni sehemu ya njia zote zilizotajwa hapo juu. Zinahusisha maoni ya mtu binafsi na ya pamoja katika hatua mbalimbali. Hata hivyo kuna aina nyingine ya tafakuri inayokwenda zaidi ya akili na huwasaidia watoto kutathmini mawazo yao na kuzingatia zaidi kujifunza. Aina hii ya tafakuri inahusisha njia za kupijima na kujichunguza inayosaidia kuendeleza kiwango cha nafsi na kiroho kwa watoto.

Kujipima na kujichunguza kunawapa washiriki fursa ya kubainisha na kutathmini fikra zao za ndani, hisia na matamanio. Ni muhimu zaidi kwa program za utamaduni na dini mbalimbali kwa ajili ya elimu maadili kwa sababu inawaruhusu watoto kutafakari kuhusu maadili na mitazamo yao. Pia inafaa wakati wa kutathmini mabadiliko binafsi na misimamo.

Kujipima na kujichunguza kunaweza kufanyika kwa mtu au vikundi. Mbinu kama vile taamuli, kukaa kimya kwa muda au desturi nyingine za kutafakari zinasaidia washiriki kujenga uzoefu wa kujitafakari.

### Mbinu zilizopendekezwa

> **Sanaa:** Sanaa ni chombo kizuri kwa ajili ya kujifunza. Inachochea ubunifu na kuimarisha uwezo wa kufasiri mawazo kuwa maneno, taswira na sauti. Sanaa hujalizia taaluma na kuwasaidia watoto kutafakari halafu kueleza mawazo yao na fikra kiubunifu. Sanaa zinaweza kujumuisha kutunga nyimbo, utengenezaji wa picha za kugandisha vipandevipande, kuchora fulana, mchoro, kutengeneza filamu, kupiga picha na kuandika mashairi na hadithi. Pia inawezekana kugundua utamaduni au jamii kwa njia ya sanaa.

> **Uchunguzi Thaminifu:**[3] Hii ni mbinu iliyofafanuliwa zaidi inayokazia kwamba kwa kawaida matatizo ni matokeo ya maoni na mitazamo yetu wenyewe. Unazingatia zaidi kutafuta njia au namna ya kubadilisha hali kwa kutambua kilicho bora zaidi kwa watu na kutafuta kilicho thaminiwa katika uhusiano wa binadamu na mifumo. Unahusisha milinganisho kutoka kale kuchambua nini kilichofanikiwa zaidi wakati ule, na kupendekeza kinachotakiwa kwa siku zijazo. Unahitaji kuangalia uwezo wa watu na kutegemea zaidi nguvu yao kutafuta njia za kubadili hali halisi.

3 Kwa maelezo kuhusu njia hii angalia http://appreciativeinquiry.case.edu

> **Midahalo:** Hii ni njiaya kawaida ya mabishano kati ya timu mbili au watu. Zaidi ya kuwa stadi ya mazungumzo au matendo, mdahalo unajumuisha ukamilifu wa ubishi wa busara, stahamila kwa hoja na maoni yanayotofautiana, na kujipima zaidi. Mdahalo ni njia kwa wale wenye mawazo yanayopinga kujadili masuala yenye ubishani bila ya kuishia kutukanana, kupandisha na hasira au kuonyesha upendeleo.[4]

> **Kushirikishana Uzoefu:** Mbinu hii inaimarisha uwezo wa watoto na vijana kusikiliza, kueleza mawazo yao na hisia na kuhusisha na wengine na kuyafanya kuwa uzoefu wa kutafakari utakaowasaidia kushughulikia maoni yao. Matumizi ya kutamba hadithi, miduara ya ngoma, hadithi za maisha halisi, filamu, nyimbo, taarifa za habari hujenga mazingira ya mtu kushirikiana uzoefu.

> **Safari za Ugani:** Mbinu hii inapanua zaidi kujifunza kwa watoto nje ya kuta za darasa hadi kwenye jumuiya. Huwapa wanafunzi uzoefu mpya na mgeni ambao hauwezi kupatikana katika mazingira ya shule. Safari za ugani hutoa fursa ya kuimarisha kujichanganya katika jamii na uraia na kuongeza maarifa na uelewa wa somo mahususi.

> **Vikundi muhimu:** Katika mbinu hii majadiliano yanafanywa kwenye vikundi vya watu 5 hadi 10 ili kupata taarifa na maoni kuhusu mada fulani. Vikundi maalumu vinaendeshwa na msimamizi anayeandaa mwongozo wa majadiliano unaofaa vikundi hivyo na kuhakikisha kuwa kila mtu anapata fursa ya kuzungumza. Mwingiliano kati ya washiriki unaweza kuchochea majadiliano na utambuzi wenye manufaa na kupata data zenye ubora kuhusu athari na kufaa kwa programu. Vinaweza kutumiwa kuchunguza aina ya dhana na maadili waliyonayo watoto na watu wazima kuhusu amani, mawazo kuhusu namna ya kushughulikia ugomvi na kupendekeza namna bora ya kuhimiza amani kwenye shule na jumuiya.

> **Michezo:** Kwa kutumia michezo ya ushirika, washiriki wanashirikiana kukamilisha seti ya kazi au kufikia lengo. Michezo inayoimarisha uwezo wa washiriki kushirikiana na wengine, kujenga kujiamini, kugundua mawazo mapya na kukabili maoni yao inafaa kwa elimu maadili kupitia kujifunza dini mbalimbali. Hata hivyo unahitaji kujenga mazingira ya michezo isiyo na upendeleo na ya kuheshimika na kuepuka michezo inayoonyesha 'washindwa' na 'washindi'. Michezo inaweza kutumiwa kama kichocheo na kuhimiza ushiriki na kujenga ushirikiano.

> **Juhudi za pamoja:** Mbinu hii inazingatia zaidi kufanya kazi kwa pamoja, kushirikiana kwa kikundi chenye watu mbalimbali, kukabili hali au tukio mahususi. Inahimiza maelewano na kusaidia kujenga stadi za mawasiliano na za kusikiliza, pamoja na kufikiri kwa ubunifu kuhusu namna ya kuleta mabadiliko katika jamii. Juhudi za pamoja zinaweza kujumuisha kampeni za kuhimiza haki za watoto, mabadilishano baina ya shule, wiki za matukio maalumu, kutayarisha video na miradi ya kuhimiza maelewano na heshima.

> **Taamuli:** Mbinu ya taamuli inaweza kuwasaidia watoto kutulia, kuboresha uwezo wao kuzingatia jambo, na kuimarisha ustawi wa mwili na akili. Mbinu za taamuli zinajumuisha desturi za kufikiri zinazojenga uelewa mkubwa wa fikra, matamanio na misisimko, kutembea au taamuli inayofikirisha sana. Kupitia taamuli, watoto wanaweza kujifunza namna ya kudhibiti hasira, mfadhaiko na kuvunjika moyo.

> **Kutatua tatizo:** Hii ni mbinu ya kawaida ambapo washiriki wanatanzua matatizo kwa pamoja na kujadili uzoefu wao. Mbinu hii inapendekeza kufuata hatua za mfululizo: kufafanua tatizo, kuchambua nyenzo, kubainisha ufumbuzi mbadala, kutathmini kila mbadala, kuchagua mmoja, kuutekeleza na kutathmini kama tatizo limetanzuliwa au hapana. Shughuli zilizopendekezwa katika mbinu hii si lazima zifuate mtiririko wa hatua bali kuleta tatizo litakalochambuliwa na halafu kutanzuliwa au kurekebishwa.

4 Kwa maelezo zaidi juu ya mjadala nenda http://www.idebate.org/debate/what.php

> **Kujiweka nafsi ya mwingine:** Ni namna ya kuingia katika uzoefu wa watu wengine na kuchunguza matatizo ya washiriki bila mhusika kujulikana. Washiriki wanachukua nafsi za wahusika na kwa pamoja wanaunda hali itakayotokana na uhalisia wao. Washiriki wanaweza kuamua matendo ya wahusika wao kulingana na miongozo iliyowekwa na wawezeshaji. Kujiweka nafsi ya mwingine pia inaweza kusaidia kuondoa ukimya au kuanzisha jambo miongoni mwa washiriki kushawishi ubunifu na kujenga kufanya kazi kwa pamoja katika kikundi. Ni mbinu inayofaa sana kuimarisha kuelewa hali mahususi. Kujiweka nafsi ya mwingine inaweza kutayarishwa kwa msingi wa uchunguzi kifani au hali nyingine ndogo.

> **Majadiliano yasiyo na mwenyekiti:** Mbinu hii ni kwa ajili ya majadiliano na kubadilishana mawazo inayohimiza usawa na heshima. Hakuna hata mmoja aliyekaa kwenye meza ya majadiliano atakayechukua nafasi ya upendeleo na washiriki wote wanachukuliwa kuwa sawa. Katika majadiliano yasiyo na mwenyekiti, mwezeshaji haongozi, washiriki wote wanachangia.

> **Kujifunza Huduma:**[5] Mbinu hii inahusisha huduma za jumuiya na tafakuri ya huduma ile. Inaendeleza uwajibikaji wa washiriki katika jamii na mitazamo ya ubinadamu kwa jumuiya. Kujifunza huduma kunaweza kutumia pia maarifa na stadi kwa masuala mahususi au kujifunza namna ya kubadili hali mahususi. Mifano ya shughuli za kujifunza huduma ni pamoja na: kampeni za urelejeleji au programu za mazingira; au kuwafundisha kompyuta watoto katika maeneo ya hali ngumu ya maisha.

> **Kujifanya mtu mwingine:** Washiriki wanajifanya kuwa mtu fulani katika kikundi cha jamii cha kufikiria na hali na kupata uzoefu wa utata wa kutekeleza kazi mpya na kufanya kwa mujibu wa nafsi mpya. Mbinu hii inaweza kuwasaidia kuchambua njia mbalimbali za kuchukua hatua au kukabili hali, kutafakari kuhusu hali za kimaadili na kufikiria kuwa mtu fulani. Majaribio ya mwigo wa usaili na kufikirika ni sehemu za mbinu hii.

> **Michezo:** Michezo inaweza kuhimiza usawa, ushirika na upamoja na kuimarisha maadili ya kijamii na malengo ya watu binafsi, kama vile kufanya kazi kwa bidii, kutenda bila upendeleo, kujenga tabia na kufanyakazi kwa pamoja. Kushiriki katika michezo kumeonyesha kujenga ongezeko la kujituma kwa jumuiya, uhusiano na watu ulio bora zaidi na mwelekeo mkubwa zaidi wa kuchukua dhima za uongozi.[6] Kwa kuwa michezo pia huhimiza mshikamano wa kijamii na maelewano na heshima, pia inaweza kutumiwa kuwasilisha ujumbe wa amani na kusaidia kutafuta hali isiyotumia nguvu na ugomvi kwa kutanzua matatizo

> **Kutamba hadithi:** Mbinu hii inatumia sanaa ya kale ya kueleza matukio kwa maneno na sauti mara nyingi kwa kutunga papo hapo. Hadithi pia huwawezesha watoto kuingia katika ulimwengu mwingine, ambao wakati huo huo unafahamika sana au haufahamiki kwao. Kuna ushirikiano na jumuiya katika kusikiliza kwa pamoja hadithi. Hadithi si visa vya uongo bali ni hisia za kila ngazi za kinachomaanishwa hasa kuwa binadamu. Kwa njia ya kutamba hadithi, watoto wanaweza kukuza stadi zao za kusikiliza na uwezo wao wa kujiweka katika nafsi ya mtu mwingine. Wanaweza kukuza ubunifu wao na uwezo wa kufikiria kuhusu tabia na mienendo kwa kuingia kwenye ulimwengu uliyoelezwa kwenye hadithi.

Mchakato wa kujifunza na njia zilizopendekezwa zinakusudiwa kuwashawishi washiriki kudadisi, kufikiria na kuongeza uwezo wao wa kutoa uamuzi uliotokana na maadili. *Kujifunza Kuishi Pamoja* kinakusudia kuhimiza ubadilishaji na kufanya watoto na vijana waone na kujifunza kutokana na uzoefu wao wenyewe.

5 Kwa maelezo zaidi kuhusu kujifunza huduma unaweza kurejea kwenye Service Learning Lessons, Plans and Projects, Human Rights Education Program, Ammesty International and Human Rights Education Associates, HREA, Machi: 2007

6 Unaweza kusoma zaidi namna ya kutumia michezo kama njia ya amani tazama http://www.toolkitsportdevelopment.org

# Kujenga Mazingira Yanayofaa

Programu inahitaji mazingira yanayofaa kwa ajili kushirikiana mawazo, kueleza maoni, hoja na imani, kabla na wakati wa somo.

> Hakikisha kwamba mahali palipochaguliwa panawezesha shughuli zinazotumia uzoefu na shughuli za vitendo.

> Hakikisha kwamba vyumba vitakavyotumika havikubandikwa wala kuonyesha vitu vya dini kutoka madhehebu fulani mahususi. Mahali hapo hapana budi kuwa huru na kukaribisha imani zote na fikra tofauti.

> Waarifu washiriki angalau wiki moja kabla kuhusu warsha na shughuli zake. Wape kijitabu kilichoelezwa uk .63, kinachoeleza madhumuni ya programu, ratiba na taarifa nyingine muhimu wanayotakiwa kujua. Kijitabu hicho kitawasaidia kujiandaa kwa ajili ya programu na kupanga matarajio yao.Tumia muda mwanzoni mwa programu yako kufahamiana. Tumia vichangamsho kujenga kuaminiana kati ya washiriki.

> Waambie washiriki wa warsha wabuni kanuni zao za kuwaongoza. Haya ni makubaliano kuhusu taratibu za kufanyia warsha, matumizi ya muda au namna ya kuwasiliana yanayoruhusu kikundi kuingiliana kama timu. Ubunifu wa kanuni hizi unaweza kujenga ushirikiano katika kikundi na hisia ya umiliki kuhusu programu. Buni kanuni kwa kushawishi ubunguaji bongo miongoni mwa washiriki.

> Tathmini kwa mfululizo motisha ya kikundi chako na daima kuwa tayari na vichangamsho ili kurejesha na kudumisha umakinifu na nguvu za washiriki.

> Himiza ushiriki wa watu wa makabila madogo na tayarisha shughuli zinazohimiza ushirikishaji na mwingiliano wa mara kwa mara.

> Tumia mapumziko ya wakati wa chai au kahawa, chakula na jioni baada ya masomo rasmi kukuza nafasi ya mwingiliano wa washiriki. Nyakati hizi zitaimarisha mchakato wa maelewano na uvumbuzi.

> Hakikisha kwamba mawazo, hoja, maoni na mapendekezo ya washiriki yanazingatiwa na kwamba yanaonekana kwenye matokeo na shughuli za programu. Hii itawezesha kujenga maarifa pamoja na kuwafanya washiriki wajihisi kuthaminiwa na kutambuliwa.

> Hitimisha programu yako na shughuli zinazohimiza motisha na kuwa kama hitimisho linalofaa. Tumia shairi au sala ya dini mbalimbali kwa ajili ya kufungia na kutayarisha onyesho la muziki na picha kutoka kwenye warsha.

> Himiza uanzishaji wa mtandao wa mawasiliano na marafiki miongoni mwa washiriki na waambie waendelee na mazungumzo baada ya kumalizika kwa programu.

## Kuwa Mfano wa Kuigwa

Ni muhimu kuwa mfano mzuri wa kuigwa. Namna unavyowatendea washiriki wako itakuwa ni ishara nzuri ya namna watakavyotendeana. Kwa hiyo watendee kwa heshima na uwazi daima. Watoto na vijana huwa wanamwangalia sana mtu waliye na uhusiano wa karibu sana nao na kwa wale ambao matendo yao na maneno ni thabiti na waaminifu. Kwa hiyo unatakiwa kuonyesha mwelekeo mzuri na namna ya kufikiri na kufanya kwa namna iliyo wazi, inayokubalika na wote.

Mifano mizuri ya kuigwa inawachochea wengine watafakari kuhusu *Mimi ni Nani na Natakiwa Niwe Nani* na kuwavutia watu watafute ufumbuzi wa hali ngumu. Hii ni muhimu zaidi kwa watoto na vijana na zaidi kabisa katika elimu ya maadili inayotaka kukuza utamaduni wa amani. Mifano mizuri ya kuigwa inaweza kuzidisha manufaa ya *Kujifunza Kuishi Pamoja*.

# Namna ya Kuanza Moduli za Kujifunza

Kupanga na kutayarisha ni muhimu sana. Kabla ya kuanza Moduli za Kujifunza, timu ya kufundisha haina budi kushughulikia mchakao wa mipango kwa jumla kwa kutumia hoja zilizoelezwa hapa chini.

## Fahamu Maudhui ya Moduli

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kimetayarishwa kwa kuzingatia maadili ya msingi: heshima, ushirikali, dhima na upatanisho. Maadili haya ya msingi yamejumuishwa kwenye Moduli za Kujifunza: **Kujielewa Binafsi na Wengine na Kuubadili Ulimwengu.**

Pitia moduli na andika sentensi mbili au tatu kuhusu maadili na dhana zilizoelezwa zina maana gani kwako na namna unavyoweza kurekebisha programu kwenye muktadha wako**.** Hii inasaidia kufafanua uelewa wako mwenyewe na unachotaka kuwasilisha. Halafu:

1. Kwa kutumia ramani za vijiji, **tayarisha njia yako ya kujifunza** kuchagua vibanda vya moduli, au moduli nyingi utakazozifanyia kazi.
2. **Chagua shughuli** zitakazofaa zaidi kwenye muundo wa programu yako na hakikisha kwamba njia zilizoelezwa zinafaa kwa ajili ya mazingira na kikundi.
3. Fahamu mchakato wa kujifunza na tafakari kuhusu namna itakavyokusaidia **kufikia madhumuni ya moduli** kupitia shughuli ulizochagua.

## Mazingira na washiriki

Bainisha mazingira ya kielimu utakayofanyia kazi, kwa jumla na kimahususi zaidi. Je, ni kambi ya majira ya joto, warsha, somo moja, programu ya muda mrefu ya masomo ya kila wiki, au semina? Mazingira ya kielimu yataamua namna utakavyoendelea na mchakato wa kupanga. Fikiria maswali yafuatayo:

> Je, ni nani atashiriki?
> Je, kikundi ni cha watu wa tabaka moja au tabaka nyingi? Fikiria historia ya kidini na kiutamaduni.
> Je, mazingira na hadhira yataathiri vipi programu na masomo yako?

## Madhumuni

Bainisha madhumuni ya kila somo katika programu. Madhumuni hayana budi kuwa ('SMART') na yenye sifa zifuatazo:

> Mahususi (S)
> Yanayopimika (M)
> Yanayotekelezeka (A)
> Halisia (R)
> Yanayokwenda na wakati (T)

Madhumuni hayana budi pia kujadiliwa na washiriki na kubadilika kama ni lazima.

## Njia za Kufundishia

Jizoeze njia za kufundishia kwenye ukurasa wa 28-29. Tumia njia mbalimbali za kufundishia zitakazofaa kwenye mazingira ya somo lako na washiriki wako. Bainisha changamoto zinazoweza kuwapo. Njia za kufundishia zilizopendekezwa zote ni shirikishi, jumuishi na zinahimiza mchakato wa kujibidisha kujifunza.

## Rasilimali

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kinatoa benki ya rasilimali kwa ajili ya shughuli zinazoweza kuimarisha kufikiri kitunduwizi kwa washiriki. Rasilimali hizo ni pamoja na hadithi, mashairi, uchunguzi kifani, nyimbo, filamu, mitanziko, kadi za kujiweka nafasi ya mtu mwingine na sala za amani.

Angalia rasilimali na jiulize maswali yafuatayo:

> Je, ni wapi tena nitakapopata vifaa vya kusaidia kufundishia?

> Je, katika kikundi, kuna vifaa gani vilivyo tayari kusaidia kufundisha?

> Je, ni kifaa gani cha kufundishia kitakachotumiwa na shughuli gani? Je ni njia gani itakayofaa zaidi hasa kwa kuzingatia mazingira ya somo na washiriki?

> Je, kuna vifaa mbalimbali k.m muziki, sanaa, fasihi simulizi, hadithi?

> Je, ni njia bora ipi ya kutumia au kutambulisha vifaa vya kusaidia?

## Panga Muhtasari

Katika kila kibanda, angalia shughuli zilizopendekezwa na chagua zile zinazofaa zaidi kwa kikundi chako na mahali.

Sanifu mtiririko wa mchakato wa kujifunza utakaofuata wakati wa masomo, wenye mwanzo unaoeleweka na mwisho unaoeleweka – na kuruhusu marekebisho makubwa kati ya masomo. Rejea kwenye mzunguko wa mchakato wa kujifunza uliopendekezwa katika ukurasa wa 25, unaoweza kukusaidia kuleta washiriki kwenye mchakato wa kujifunza ambao ni shirikishi na unaofikirisha zaidi.

Hakikisha kwamba mchakato wa kujifunza kwa ajili ya somo lako unavutia, unatoa fursa kwa ajili ya maswali na kuwasaidia washiriki kuvumbua na kutoa muda wa kutosha kwa ajili yao kuhusisha zoezi na maisha yao wenyewe.

## Elekeza Kwenye Kuchukua Hatua

Kila somo halina budi kuhitimisha kwa washiriki kuhusisha walichojifunza na maisha yao wenyewe na majadiliano ya hatua gani itakayofaa kuchukuliwa katika muktadha huo. Hatua hiyo inahitaji kufuata muktadha na kitafaa tu kama kinatokana na washiriki wenyewe na kumilikiwa na kikundi. Kutegemea muktadha, hatua inaweza kuchukuliwa na mtu binafsi, kuchukuliwa kupitia shuleni au kuhusiana na jumuiya.

## Tathmini

Katika sehemu ya 3, usimamizi wa maendeleo utaona njia mbalimbali kwa ajili ya maendeleo yako na washiriki kupima kujifunza kwao. Njia mojawapo ni Logu ya Kujifunza ambayo kila mshiriki anatakiwa kuwa nayo. Maelezo ya njia tano za tathmini unazoweza kutumia na baadhi ya njia za papo kwa hapo kwa ajili ya "kupima joto", pia zimetolewa.

Kila kibanda kina alama ya kituo cha kupumzikia inayokukumbusha kuwataka washiriki waandike kwenye Logu ya Kujifunza na kupima maendeleo yao. Tathmini hizi zinafanywa na washiriki na si mwezeshaji. Tathmini ya maendeleo inatokana na kujipima na kujitafakari mwenyewe; washiriki hawana budi kuhusisha kujifunza kwao na miktadha yao. Kwa hiyo washiriki wanakuwa wasimamizi wa kujifunza kwao, jambo ambalo lenyewe ni wezeshi.

Wewe, kama mwezeshaji unahimizwa kufanya tathmini ya athari kwa washiriki ili kupima mabadiliko ya mitazamo, maarifa na stadi katika ngazi ya mtu mmoja baina ya watu na kijamii. Tathmini hii haina budi kuzingatia kuhusisha maadili na uhusiano kati ya kujifunza na hali halisi ya kila mshiriki. Kuhusu mfano wa tathmini ya athari, angalia ukurasa wa 61.

Ni muhimu kwa timu ya wawezeshaji nayo kupita katika mchakato wa kujitathmini mwenyewe baada ya kila somo, kupima kujifunza kwao na matokeo ya jumla ya zoezi.

Tumia muundo wa tathmini kupima maoni ya papo kwa papo moja ya washiriki kuhusu vifaa, maudhui ya program na kujifunza (angalia ukurasa wa 228).

# Je, *Kujifunza Kuishi Pamoja* kitumiwe pamoja na nani?

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kimetayarishwa kitumiwe na watoto na vijana wenye umri wa zaidi ya miaka 12. Unaweza kuchagua njia ya shughuli zinazofaa zaidi kulingana na rika. Njia na shughuli zimesanifiwa kuweza kutumiwa na kurekebishwa kwa miktadha tofauti ya kiutamaduni na kijamii.

Mchakato wa kujifunza na njia za kufundishia vinasaidia kujenga dhamira ya dhati na kupanga kwa pamoja, vinavyotokana na uwezo wa washiriki, ili watoto na vijana waweze kuleta mabadiliko katika jamii zao.

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kimesanifiwa kitumiwe hasa na vikundi vya dini mbalimbali, na kimsingi lazima viwe na wawakilishi kutoka angalau dini mbili zilizopo. Hii inaweza isitokee mara zote, kwa hali yoyote ile, ni muhimi zaidi kuhakikisha uwazi na heshima kwa dini, mila na desturi na tamaduni zingine.

# Je, *Kujifunza Kuishi Pamoja* kitumiwe wapi?

Kitabu hiki kinaweza kutumiwa kwa madhumuni tofauti na katika mazingira tofauti:

1. Moduli za kujifunza zinaweza kutekelezwa wakati wa **warsha**, **mikutano** au **semina**. Fuata vibanda vyenye dhamira ya kila moduli na vitumie kulingana na muda, hadhira na mazingira.
2. Moduli za Kujifunza, zinaweza kurekebishwa kwa matumizi kwenye **muhtasari wa shule**. Shughuli zinaweza kuingizwa kama sehemu ya mafunzo ya dini au maadili. Kwa mfano, unaweza kuchagua njia ya kujifunzia kwa kila moduli na kuendesha shughuli moja au zaidi kutoka kila kibanda chenye dhamira kwa kipindi cha miezi kadha. Vibanda vyenye dhamira moja vinaweza pia kutumika kujalizia masomo mahususi ya shule.
3. Moduli zinaweza kutumika katika kambi za **majira ya joto** kwa watoto na vijana. Moduli zinaweza kuchangia katika uzoefu mpana zaidi wa kujifunza kati ya watu kutoka dini na utamaduni tofauti. Vibanda vya kila moduli vinaweza pia kuwa kama mada za kambi za majira ya joto.

# Je, ni nani anaweza kutumia *Kujifunza Kuishi Pamoja*?

Watumiaji wa msingi wa kitabu hiki ni wale wanaoshughulika na watoto na vijana katika mazingira ya kielimu iliyo rasmi, isiyo rasmi na mahali pasipo rasmi.[7] Hii ni pamoja na wanachama wa GNRC, pamoja na jumuiya ya dini na utamaduni, waelimishaji wa kidini, walimu na taasisi za mafunzo.

## Mazingira rasmi

Shule zinaweza kuwawezesha watoto na vijana kwa kujumuisha *Kujifunza Kuishi Pamoja* kwenye mitaala yao, na kwa kutoa njia na shughuli mpya zinazoimarisha uwezo wa mwanafunzi kufikiri kitunduizi.

Kutumia *Kujifunza Kuishi Pamoja* shuleni kunaleta manufaa kwenye jumuiya pana. Shule imekuwa, na katika baadhi ya sehemu za duniani bado ni kituo cha maendeleo ambako watu wanakusanyika kwa ajili ya shughuli, mikutano na kubadilishana mawazo. Kwa hiyo shule zinaweza kuwa mahali panapofaa kwa jumuiya kujenga na kujifunza kuwezesha kuheshimu na kuelewana vizuri zaidi.

## Maeneo yasiyo rasmi

Mahali pa kujifunzia nje ya mfumo rasmi wa shule panapotoa elimu ya kukuza stadi kwa watoto walio nje ya shule na vijana na wengine wasio bahatika na walio hatarini (kama vile wakimbizi, wahamiaji na mayatima), yanaweza kuwa chachu ya namna mpya ya kupata maarifa, mitazamo chanya, ustahimilivu na uelewa, pamoja na kuhimiza mabadiliko ya tabia.

Mashirika ya dini, vikundi vya vijana, klabu za amani pamoja na aina za asasi kama hizo za elimu ni muhimu katika kuhimiza maadili kupitia kujifunza dini na tamaduni mbalimbali. Mara nyingi vijana wanahudhuria vikundi hivi kwa hiari kutoa na kujadili masuala ya kijamii katika mazingira ya wazi. Vipengele hivi hufanya mahali panapofaa pa kuchangamsha uwezo wa vijana kukidhi mahitaji ya jamii zao.

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kinaweza kutumiwa kwa urahisi katika programu ya amani na elimu ya haki za binadamu, hususani zile zinazosisitiza kujifunza tamaduni na dini mbalimbali na uhimizaji wa hadhi ya mtu. Midahalo, mijadala ya wazi, mikahawa ya dini mbalimbali majadiliano ya pamoja na juhudi za pamoja vinaweza kufanyika kwa urahisi katika mazingira yasiyo rasmi, kutoa fursa ya kuhimiza kufikiri kitunduizi na mazungumzo baina ya dini mbalimbali.

Katika mahali ambako muingiliano rasmi wa dini mbalimbali ni vigumu kupangwa ama uwe kutokana na ubaguzi au kutokana na migogoro ya kidini, mahali pasipo rasmi panahitajika kuhimiza maelewano na kutoa fursa ya mwingiliano na mazungumzo.

7 Elimu rasmi:hutolewa shuleni na kwenye taasisi za mafunzo;Elimu isiyo rasmi hutolewa kupitia vikundi vya kijamii, jamii za kidini na mashirika mengineyo; Elimu isiyo rasmi hufunika mambo yaliyosalia kutoka elimu rasmi, mfano; kuchangamana na marafiki, familia na watenda kazi. Tofauti ni kwamba kwa sehemu kubwa ni ya kiutawala lakini inatumika kuziba vipengele vyote vilivyoachwa na elimu rasmi vya kujifunza maishani.

## Mahali pasipo rasmi

Nafasi ya nyumbani na familia katika kuhimiza heshima na maelewano kati ya vikundi mbalimbali ni muhimu. Kuweka thamani iliyo dhahiri kuhusu wingi wa dini na utamaduni ni namna moja ya kuwavutia watoto na vijana kutafuta na kujitahidi kutafuta njia nzuri zaidi ya 'kuishi pamoja'. Familia ni majukwaa yanayoweza kuhimiza kukubali tofauti na ukuzaji wa utambulisho wa mtu. Kwa hali hiyo, wazazi ni wasaidizi muhimu na wenye nguvu kubwa katika kuwapa uwezo wanafunzi na vijana.

# Kijitabu cha Washiriki

Tayarisha kijitabu kidogo cha washiriki kinachotoa taarifa kuhusu maudhui ya programu, kinachotarajiwa kutoka kwao, watakachojionea na namna bora watavyojiandaa kwa safari ya kujifunza.

Kuwapa washiriki kijitabu mapema kutawawezesha kujitayarisha, kuchochea shauku yao na kuwawezesha kueleza matarajio yao.

Je, kijitabu kijumuishe nini?

1. Ujumbe wa utangulinzi: Wakaribishe washiriki kwenye programu, eleza muda, nani anayeendesha programu, washiriki wangapi, wanatoka nchi zipi na imani gani za dini, na eleza umuhimu wa ushiriki wao kwa ufanisi wa programu.
2. Madhumuni: Eleza kinachotarajiwa kupatikana mwisho wa programu. Tumia madhumuni ya SMART.
3. Ratiba: Panga muda kwa kila somo. Hakikisha kwamba kuna muda wa mapunziko, chakula, burudani na matembezi ya jioni.
4. Maelezo ya masomo: Eleza masomo yanahusu nini, namna yanavyotayarishwa kwa aijili yao, na taarifa zingine zozote za matayarisho, vifaa, nyenzo kwa kila somo.
5. Utaratibu wa Kujifunza: Waeleze washiriki kwamba, kama sehemu ya safari hii ya kujifunza, watatakiwa wawaambie watunze shajara au daftari la kumbukumbu za kila siku – Logu ya Kujifunza kuhusu uzoefu wao wakati wa kujifunza.
6. Taarifa ua Utendaji: Kama ni kambi ya majira ya joto au warsha, hakikisha kwamba unawaarifu kuhusu mahali, hali ya hewa, aina ya nguo wanazohitaji kuja nazo, na huduma watakazopata mahali pa mkutano, kwa mfano simu ya umma, maeneo ya kutembelea, utumiaji wa Intaneti. Iwapo ni programu ya shule, hakikisha kwamba unatoa taarifa kuhusu uwezekano wa ziara za ugani na aina ya shughuli za nje utakazofanya, kama zipo.

Hakikisha kwamba kijitabu chako kinavutia washiriki na kwamba taarifa unayowapa ni fupi na inaelewaka.

# Je, Naweza kufanya nini kama...

Katika sehemu hii kuna mapendekezo ya nini cha kufanya unapokabiliwa na changamoto mahususi katika utekelezaji wa programu ya elimu ya maadili. Mifano ya kinadharia ifuatayo hapa chini na mapendekezo yamechukuliwa kutokana na uzoefu wetu wakati wa warsha za majaribio na changamoto zilizokabiliwa wakati *Kujifunza Kuishi Pamoja* kilipokuwa kinatayarishwa.

Hali zenye changamoto huenda zikatokea. Watahitaji matayarisho kuhusu upande wa wawezeshaji na kwake kuchukua hatua ya utetezi na wakati huo huo ikiwa ya kiakili, kihemko. Tunakuomba upitie mifano ifuatayo na kutafakari namna hali hizi zinavyoweza kuathiri utendaji wako kama mwezeshaji.

## Je, Naweza kufanya nini kama...

### Sina kikundi chenye dini mbalimbali.

> Nataka kuleta uelewa kuhusu dini mbalimbali na kuhimiza maadili yanayofaa kwa kuishi pamoja na watu kutoka dini mbalimbali; hata hivyo, sina kikundi chenye dini mbalimbali na hakuna dini mbalimbali nyingi jijini kwangu.

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kimetayarishwa ili kitumike na washiriki kutoka dini mbalimbali. Hata hivyo kama unakosa kikundi chenye dini mbalimbali, bado unaweza kukitumia kitabu hiki kuleta uelewa kuhusu dini nyingine au kushughulikia masuala ya kiutamaduni. Fikiria mapendekezo haya muhimu, na yenye manufaa:



- Hakikisha kwamba unaelewa imani za dini nyingine kwa kutumia shughuli zinazotokana na uzoefu. Unaweza kutumia Ziara ya Dini Mbalimbali kwenye ukurasa wa 127 kuwafahamisha imani nyingine na kutafakari uelewa wao na mawazo.
- Waalike wageni kutoka dini nyingine kwenye mkahawa wa dini mbalimbali au kujadili wapi watakapozungumza na washiriki hao na kujifunza.
- Tumia filamu zinazoonyesha haki ya kueleza imani za dini. Jadiliana na washiriki mawazo yao na mawazo baada ya filamu.
- Kama sehemu ya kujitathmini, waambie washiriki wakutane na mtu mwenye imani tofauti za dini kuliko zao wenyewe na kujifunza kuhusu dini hizo.
- Tumia taswira za mila na desturi za dini nyingine na chunguza kazi yao na maana
- Unda kikundi cha wawezeshaji kutoka dini mbalimbali.
- Chunguza tofauti na kufanana kokote ndani ya kikundi cha dini kinachowakilishwa – je kuna zaidi ya madhehebu moja au kabila? Jadili namna tofauti hizi zinavyounda utambulisho wa dini wa washiriki.

### Nataka kutatua masuala ya kijamii badala ya masuala ya kidini.

> Napenda kutumia *Kujifunza Kuishi Pamoja* lakini sitaki kuzungumzia masuala ya kidini; ningependa kujadili matatizo ya kijamii yenye umuhimu mkubwa kwa eneo langu.

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kimesanifiwa kuwahusisha vijana katika kubadili migogoro ya udhalimu na ugomvi, na msisitizo uko kwenye migogoro inayochochewa na tofauti za kidini.

Mkabala huu unakusudia kuelewa uanuwai kutoka mitazamo mingi, lakini mkazo upo hasa kwenye tofauti za kidini.

Hii isikuzuie kutumia kitabu hiki kama mfano wa kushughulikia aina nyingine za migogoro na tofauti. Bila ya shaka, *Kujifunza Kuishi Pamoja* kitatumiwa kukabili suala lolote linalohusiana na kukosa heshima na maelewano miongoni mwa watu. Hata hivyo tunapendekeza wewe utumie kitabu hiki kwa vikundi vya dini mbalimbali, hata kama mada kuu si maelewano ya kidini, kwa sababu hii itasaidia kujenga mshikamano miongoni mwa washiriki na kuhimiza ushirikiano wa dini mbalimbali.

Yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo yanayofaa:

> Chagua mada ya kijamii ya kushughulikia (km. ugomvi miongoni mwa vikundi vya vijana, masuala ya uhamishwaji makazi, uhamiaji, migogoro ya rasilimali na ubaguzi kwa msingi wa kijinsia).

> Tutumia moduli ya kwanza, *Kujielewa Binafsi na Wengine*, kusisitiza utamaduni mbalimbali au tofauti wa namna ya kufikiri, maoni na kujirudia kwa vikundi vya kiutamaduni na kijamii, na umuhimu wa kuwathamini wengine, bila ya kujali ni kina nani.

> Tumia moduli ya pili, *Kuubadili Ulimwengu Pamoja* kwa mada uliyochagua na sisitiza namna suala hilo linavyoathiri uhusiano miongoni mwa watu na dhima zao binafsi na za pamoja kutenda. Waache washiriki wagundue kuwa wanaweza kuwa sehemu ya ufumbuzi kuliko kuwa sehemu ya tatizo.

Kuona namna *Kujifunza Kuishi Pamoja* ilivyotumiwa kushughulikia uhamishwaji makazi na hali za ugomvi, rejea kwenye “Warsha nchini Ecuador” katika ukurasa wa 210, “Warsha nchini El Salvador” katika ukurasa wa 213 na “ Warsha nchini Panama” katika ukurasa wa 216.

## Nina mivutano kwenye kikundi kwa sababu ya tofauti za kidini.



Nataka kutambulisha *Kujifunza Kuishi Pamoja* kwenye kikundi chenye dini mbalimbali, hata hivyo baadhi ya vikundi vya dini vina historia ya ugomvi, na kumekuwa na makabiliano miongoni mwa washiriki.

*Kujifunza Kuishi Pam*oja kinasaidia kujenga uelewa kuhusu haja, maelewano na kuwapa fursa wengine waliotofauti. Kina shabaha ya kujenga daraja ya imani na kuendeleza mitazamo ya washiriki kuhusu upatanishi. Kwa hiyo *Kujifunza Kuishi Pamoja* hakina budi kukabili aina ya changamoto iliyoelezwa hapo juu.

Yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo yanayofaa:

> Tumia muda zaidi kwenye moduli ya kwanza, *Kujielewa Binafsi na Wengine*, kujenga mazingira salama kwa ajili mwingiliano miongoni mwa washiriki.

> Sisitiza umuhimu wa ubinadamu wetu na utajiri wa uanuwai. Hii itakuruhusu kujenga hisia ya kuungana miongoni mwa washiriki.

> Kabili mazoea potofu na maoni ya washiriki kwa kutumia njia ya uzoefu zinazowezesha kupata uzoefu wa namna wengine wanavyoishi na kufikiria.

> Tenga nafasi ya mazungumzo na kushirikiana. Sisitiza umuhimu wa kuwa wazi kwa maoni ya watu wengine.

> Tumia shughuli zitakazowafanya washiriki kujiweka katika nafasi ya watu wengine na uwape fursa ya kutafakari kuhusu hisia zao na hisia za watu wengine.

> Bainisha migogoro miongoni mwa vikundi vya dini pamoja na washiriki kwa kusikiliza maoni na mawazo yote nakutafuta utaratibu na historia ya migogoro, watu waliohusika nayo, uhusiano ulioathiriwa na hatima ya mgogoro. Waambie watafakari mgogoro ulivyo katika kushindwa kwetu kuhusisha na wengine na kushindwa kwetu kuelewa na kuheshu wengine. Kama washiriki watajionyesha kutoelewa vizuri kuhusu historia na sababu za mgogoro, tumia hali hii na kuhoji chuki waliyonayo.

> Tumia uchunguzi kifani, makala, filamu na nyimbo kuhusu ubadilishaji wa migogoro katika eneo jingine na ruhusu majadiliano ambapo tofauti zinabainishwa katika muktadha wa washiriki.

> Wasilisha matukio ya watu wanaoshughulikia uelewa wa pamoja miongoni mwa vikundi vya dini tofauti na waruhusu washiriki wajadili na kutafakari kuhusu kazi hii.

> Waruhusu washiriki watafakari kuhusu migogoro yao binafsi na wale walioko katikia kikundi cha dini tofauti na wape muda kwa ajili ya shughuli kwenye kibanda. *Amani inaanza na mimi*, ipo kwenye moduli ya *Kuubadili Ulimwengu Pamoja*.

> Unda kikundi cha wawezeshaji kinachowakilisha aina mbalimbali za dini kwenye kikundi ili kuunda hali ya uwiano na ukinzani katika majadiliano na uwezeshaji.

Kama unataka kupata baadhi ya mawazo ya kutumia kitabu cha *Kujifunza Kuishi Pamoja* kwa muktadha wa ugomvi na mgogoro wa kidini, unaweza kusoma taarifa ya warsha ya Uyahudi, *Massa – Massar (Safari – Njia)* katika http://www.arigatou.ch/mm/file/massa – massarreport.pdf

## Washiriki wamekabiliwa na hali za vurugu



| |
|---|
| Kikundi changu cha washiriki kinakabiliwa na vurugu kila siku na ni sehemu ya vikundi vidogo vinavyotengwa kutoka katika jamii. |

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kinaweza kutumiwa na vikundi kutoka historia tofauti za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni. Watoto na vijana ambao wamekuwa au wanaendelea kuathiriwa na vurugu wanahitaji fursa za kuimarisha kujistahi na kuwa na uwezo wa kujiimarisha ili waweze kuepuka vizuri hali hiyo na kuchangia kwa ukamilifu kwenye hitimisho la amani.

Yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo yanayofaa:

> Sisitiza kibanda cha *Kujikubali Mwenyewe Kuhusiana na wengine* katika moduli ya *Kujielewa Binafsi na Wengine*.

> Weka nafasi kwa washiriki kuimarisha kujiamini na kujistahi kwao kupitia shughuli zinazowahimiza wao kutumia ubunifu wao, kushiriki na mwingiliano bila ya kuhukumiwa. Hakikisha kuwa vikundi vidogo vinasikilizwa na kwamba wao pia wanahisi kwamba nao wanasikilizwa.

> Tayarisha shughuli zinazowasaidia washiriki kujenga taswira ya vyanzo vya uonevu katika jamii zao na haja ya uwezeshaji kusaidia kutafuta ufumbuzi wa amani kwa hali hiyo. Tumia shughuli zinazoimarisha uwezo wa kufikiri kiuhakiki na uwezo wa kutanzua tatizo.

> Wasaidie washiriki kugundua mibadala isiyotumia ugomvi kwa kushughulikia migogoro ya kijamii na uonevu na kuwajengaea uwezo wa kushughulikia kwa amani hali zao wenyewe. Unaweza kutumia filamu zinazoonyesha mapambano ya kutafuta haki yanayoongozwa na viongozi tofauti wa kidini na wa kijamii, au alika asasi au watu wanaofanya kazi na vyama vinavyopinga kutokuwa na ugomvi.[8]

8 Kwa maelezo ya kiundani kuhusu rasilimali, michezo na vyombo vya habari kuhusu migogoro isiyo ya vurugu, ona kikosi nguvu zaidi http://www.aforcemorepowerful.org

> Wasaidie washiriki kutafakari migogoro yao binafsi au hali za ugomvi na wape muda zaidi kwa shughuli kwenye kibanda cha Matembezi ya Upatanisho katika Moduli ya Kuubadili Ulimwengu Pamoja.

Kwa maoni zaidi kuhusu namna ya kutumia *Kujifunza Kuishi Pamoja* katika hali ya namna hii, rejea "Warsha ya nchini Tanzania" kwenye ukurasa 207 na "Warsha ya nchini El Salvador" kwenye ukurasa 213.

## Mada za Warsha zinasababisha jazba za hatari kwa Washiriki

Mada, masomo na shughuli za warsha zinawafanya washiriki kuwa wepesi kuhisi hisia zao wenyewe na kuwazuia kushiriki kwa ukamilifu.

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kimesanifiwa kuhusiana na masuala binafsi mno: utambulisho, maadili na utamaduni. Kwa hiyo programu hii itawalazimisha washiriki kutafakari kuhusu maoni ya mtu binafsi, upendeleo na uzoefu – kuangalia mioyo yao na jazba. Inatarajiwa kwamba mchakato huu utasababisha kufanya mitazamo chanya kuzoeleka.

Yafuatayo ni badhi ya mapendekezo muhimu:

> Toa nafasi ya kusikiliza hisia za washiriki kama wanataka au wanahitaji kushirikiana hisia hizo na wengine.

> Zungumza faragha na washiriki waliowahi kupata jazba la hatari na wafahamishe kwamba ni sawa kuwa na mhemuko kuhusu muda. Waulize washiriki kinachowasababishia uchungu na kwa nini unawasononesha.

> Kama mshiriki anaonyesha hali mbaya inayoathiri maisha, hakikisha kwamba unazungumza nae baada ya warsha au shughuli na saidia kutafuta msaada au ufumbuzi wa tatizo.

> Kama mshiriki anaonyesha jazba za hatari katikati ya somo, onyesha msisitizo. Uliza kuna nini, mruhusu mshiriki kueleza hisia zake na waambie washiriki wengine wasikilize na kujaribu kuelewa hemko za mtu huyo.

> Waambie washiriki watulie kwa kupumua kwa kuvuta pumzi kubwa, kuimba kwa kurudiarudia, kuimba, au kwa kuwaachia walale tu.

> Tayarisha baadhi ya shughuli zinazowawezesha wafanye jambo la ubunifu kujieleza, kama vile kuchora au kupaka picha rangi.

> Kama washiriki wanakueleza mambo kwa siri, hakikisha kwamba unaheshimu utunzaji siri huo.

# Sehemu ya 2

# Moduli za Kujifunzia

**Moduli ya 1:** Kujielewa Binafsi na Wengine
**Moduli ya 2:** Kuubadili Ulimwengu kwa Pamoja

**Dira ya Baraza la Dini Mbalimbali kuhusu Elimu ya Maadili**
Tunatarajia kuwa na ulimwengu ambao watoto wote wanapewa uwezo wa kuendeleza mambo yao ya kiroho, kukumbatia maadili, kujifunza kuishi kwa mshikamano na watu wa dini na ustaarabu mbalimbali na kujenga imani ambapo watu wanamwona Mungu, Ukweli wa Mwisho au Uwepo wa Mungu.

## Kuwawezesha vijana kuubadili ulimwengu

Vibanda katika Moduli Mbili za Kujifunza vitawachukua washiriki katika safari ya dini na tamaduni mbalimbali inayowawezesha kujenga madaraja ya kuaminiana ili kuubadili ulimwengu.

Kupitia shughuli za programu, washiriki watajifunza thamani ya kuendeleza uhusiano na watu wanaotofautiana nao. Wataelewa umuhimu wa kujiendeleza wao wenyewe na kwa uhusiano wao na watu wengine na kuimarisha maadili yao katika maisha yao. Katika safari hii, washiriki watakabiliwa na changamoto katika kuelewa ulimwengu na watu wanaowazunguka, changamoto zitakazowasaidia kuelewa wajibu wao binafsi na wa pamoja kama raia wa kimataifa. Washiriki watatafakari kuhusu uzoefu wao, kuhusisha maadili mbalimbali na watakuwa na uwezo zaidi wa kujibadili wao wenyewe na mazingira yao ya karibu. Kwa kujifurahisha na ukamilishaji wa kufanya kazi pamoja, watatafuta njia za amani za kuubadili ulimwengu wao.

Moduli ya kwanza, **Kujielewa Binafsi na Wengine**, inamlenga zaidi mtu binafsi na utambulisho wake. Inawasaidia washiriki kugundua kufanana, pamoja na tofauti kati ya wao wenyewe na watu wa dini na utamaduni tofauti. Watajiona kutoka mitazamo ya wengine na kujifunza kuwatambua wengine kwa ushirikali, kuelewa na kuheshimu hisia zao, itikadi na namna ya kuishi. Ifikapo mwisho wa moduli ya kwanza, washiriki watakuwa wameweza kutafakari kuhusu wajibu wa kila mtu kutenda kwa njia ya amani na huruma. Hii itawasaidia kuendeleza masuala yao ya kiroho.

Moduli ya pili, **Kuubadili Ulimwengu kwa Pamoja** inazingatia zaidi umuhimu wa kuunganishwa na wengine katika kuleta mabadiliko. Inawachukua washiriki kwenye safari ambayo watachambua chanzo cha migogoro ya kijamii, matukio ya ugomvi na uonevu, kupata stadi za kutafuta ufumbuzi wa amani kwa matatizo haya. Watagundua kwamba, kwa kupata amani ya nafsi, watajenga mtazamo wa upatanishi utakaosaidia kujenga madaraja ya kuaminiana na wengine. Ifikapo mwisho wa moduli ya pili, watoto na vijana watashawishika kushirikiana na wengine kukabili kiuadilifu haja ya kuwa na mabadiliko katika jamii zao.

Katika kila moduli, wawezeshaji hawana budi kuchagua ni vibanda gani vya kuzingatia na utaratibu waliozoea.

# Moduli ya 1
# Kujielewa Binafsi na Wengine

## NENO MUHIMU: KUHESHIMIANA

Kuheshimiana kunakua pamoja na kuelewana zaidi na kukubali tofauti na mifanano.




Kupitia vibanda vya Moduli ya 1, washiriki watajifunza kuhusu wao wenyewe kuhusiana na wengine. Watajifunza kukubali tofauti zao na wengine na kugundua mambo ya kawaida yanayofanana ambayo sote tunashirikiana. Kwa kupita kwenye njia tofauti, washiriki wataweza kuona namna utambulisho wao unavyotayarishwa na chimbuko lao, uhusiano wao na familia, marafiki na watu wanaowazunguka. Safari hii itawasaidia kukubali uanuwai, kukabili maoni yao na kukubali haja ya kuelewa na kuheshimu watu wengine.

**Kama mwezeshaji, chagua vibanda unavyotaka kutembelea na panga safari ya kikundi chako kwa Kujielewa Binafsi na Wengine!**

## Kukubali uanuwai

Shughuli ndani ya kibanda hiki zinawasaidia washiriki kuangalia ulimwengu tunamoishi . Washiriki watajifunza zaidi kuhusu watu wengine na kugundua uanuwai na utajiri kwa watu wengine. Njia hii itawawezesha kubaini kile kinachotutofautisha na kukubali uanuwai huu bila ya kukimbilia chuki.



## Shughuli zinazopendekezwa

> Kushirikiana picha, uk. 70.
> Uchoraji ramani, uk. 76.
> Kufikia nyota, uk. 77.
> Ziara za dini mbalimbali, uk. 80.
> Linganisha, uk. 82.
> Shughuli za Utamaduni za jioni, uk. 83.
> Chemsha bongo – je, ninaelewa nini kuhusu dini nyingine? Uk. 112.

**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**



## Kujitambua mwenyewe kuhusiana na wengine

Shughuli ndani ya kibanda hiki zinawasaidia washiriki kujiangalia kwa undani na namna wanavyohusiana na wengine. Washiriki watakubali utambulisho wao na kujifunza namna ya kuheshimu haki za kila mtu kuwa na utambulisho. Washiriki watagundua kuhusiana kwao na wengine na namna utambulisho wao unavyoundwa kupitia uhusiano na uzoefu wa wengine.



## Shughuli zinazopendekezwa

> Historia ya maisha yangu, uk. 65.
> Kubadilishana uzoefu binafsi, uk. 67.
> Kufikia nyota, uk. 77.
> Linganisha, uk. 82.
> Shughuli za utamaduni za jioni, uk. 83.
> Hadithi ya Bobby, uk. 103.
> Kuchora kwenye fulana, uk. 109.

**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**

## Ubinadamu wetu

Kupitia shughuli ndani ya kibanda hiki, washiriki watagundua kwamba zaidi ya tofauti zetu, ubinadamu wetu unalingana. Washiriki watatafuta kilichopo ndani ya nafsi zao, na kusikiliza hadithi za watu wengine kuwasaidia kuhusiana na kushirikiana. Watagundua haja ya kuwa na wajibu wa pamoja kama binadamu.



## Shuguli zinazopendekezwa

> Kutamba hadithi, uk. 74.
> Kufikia nyota, uk. 77.
> Miduara ya kupiga ngoma, uk. 79.
> Nderemo za kuridhika, uk. 105.

**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**



## Je, tunaweza kupatana?

Shughuli ndani ya kibanda hiki zitasaidia washiriki kujifunza na kutathmini maana ya kuwaheshimu wengine. Washiriki watahoji mitazamo yao, namna wanavyofikiri na tabia na mienendo yao ya kujifunza kuona zaidi ya tofauti, maamuzi bila tafakuri na mawazo yaliyozoeleka.



## Shuguli zinazopendekezwa

> Hadithi kwa ajili ya nafsi uk. 73.
> Ninachotetea, uk. 78.
> Benki ya kimaadili, uk. 87.
> Vikundi lengwa kuhusu heshima, uk. 95.
> Migahawa ya mazungumzo ya dini mbalimbali, uk. 96.
> Hadithi ya Bobby, uk. 103.
> Mazungumzo baina ya dini mbalimbali, uk. 122.

**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**

## Kujiweka katika nafasi ya mtu mwingine

Shughuli ndani ya kibanda hiki zitawasaidia washiriki kutambua na kushughulikia chuki zao ili kuelewana vizuri zaidi na wengine. Kibanda hiki kinasaidia mchakato wa kujifikiria wa mwamsho wa kiroho kwa mahitaji na hisia za wengine. Kibanda kitasaidia kuimarisha mambo yao ya kiroho na uwezo wa kushiriki hali ya watu wengine.



### Shuguli zinazopendekezwa


> Taswira ya umbo lako ni yangu, uk. 69.
> Ziara za dini mbalimbali, uk. 80.
> Kujiweka katika nafasi ya mwingine, uk. 85.
> Kutumia uchunguzi kifani, uk. 86.


**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**



## Kushughulikia mahitaji ya kuelewana

Ndani ya kibanda hiki, washiriki wanashughulikia maoni yao ya kuwa wenye heshima zaidi na kujaribu kuwaelewa wengine. Kibanda kinategemea zaidi uvumbuzi uliofanywa wakati wa safari na kufanya mwanzo wa safari mpya ya kushirikiana kuubadili ulimwengu.



### Shuguli zinazopendekezwa



> Migahawa ya mazungumzo ya dini mbalimbali, uk. 96.
> Kutengeneza filamu, uk. 110.
> Kampeni za kujifunza dini mbalimbali, uk. 117.
> Kubadilishana ziara za shule, uk. 118.
> Wiki yenye dhamira maalumu, uk. 119.
> Kampeni za Haki za Watoto, uk. 120.
> Mazungumzo ya dini mbalimbali, uk. 122.


**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**

# Moduli ya 2
# Kuubadili Ulimwengu Pamoja

## NENO MUHIMU: USULUHISHI

Upatanishi si aina ya uponyaji tu wakati mambo yanapoharibika; ni njia pia ya kujizatiti kushughulikia matatizo yasiyoepukika, tofauti na migogoro ya maisha ya jamii.




Kuendelea kutoka **Kujielewa Binafsi na Wengine**, safari hii inawashawishi washiriki kujenga madaraja ya kuaminiana na kushirikiana ili kila mmoja aweze kuchangia katika kuleta amani kwenye mazingira yake. Washiriki watagundua kwamba uonevu na ugomvi hutokea wakati tunaposhindwa kuheshimiana, na kwamba mara nyingi kuna haja ya kuwa na mtazamo wa usuluhishi wakati wa kushirikiana na wengine. Mtazamo wa usuluhishi unahimiza na kuwasaidia washiriki kurudisha uhusiano uliovurugika, kutafuta amani ndani na kutimiza dhima yao binafsi na ya pamoja.

**Kama mwezeshaji, chagua vibanda unavyotaka kutembelea na panga safari ya kikundi chako kubadili ulimwengu pamoja!**

## Inakuwaje wakati tunaposhindwa kuheshimiana?

Kibanda hiki kinaonyesha kuwa migogoro ni ya kawaida ndani ya uhusiano wa kibinadamu, lakini pia inaweza kutanzuliwa kwa amani kupitia mabadiliko yanayosaidia. Washiriki watachunguza namna kushindwa kuelewana na kuheshimiana kunaweza kuleta ugomvi, uonevu na ukiukaji wa hadhi ya mtu.



### Shuguli zinazopendekezwa


> Wakati wa kuangalia sinema, uk. 71.
> Kujifunza kutokana na hadithi za maisha halisi, uk. 72.
> Hali ya uonevu, uk. 75.
> Je, ulimwengu utakuwaje kama…, uk. 104.
> Korongo elfu moja wa karatasi, uk. 107.
> Visiwa vinavyotoweka, uk. 114.


**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**



## Kuelewa migogoro, ugomvi na uonevu vinavyonizunguka

Kibanda hiki kinawasaidia washiriki kuelewa kiini na matokeo ya migogoro, uonevu na hali za ugomvi zinazowazunguka. Washiriki watachunguza tabia na mienendo ya kibinadamu na matendo na watajifunza kuhusu uwezo wa binadamu kujenga, kuharibu na kubadili.



### Shuguli zinazopendekezwa


> Wakati wa kuangalia sinema, uk. 71.
> Kujiweka katika nafasi ya mwingine, uk. 85.
> Kutumia uchunguzi kifani, uk. 86.
> Mitanziko, uk. 89.
> Mikutano ya majadiliano, uk. 97.
> Midahalo, uk. 98.
> Korongo elfu moja wa karatasi, uk. 107.


**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**

## Amani inaanzia kwangu

Kibanda hiki kinawasaidia washiriki kutafakari kuhusu namna mitazamo yao mara nyingi inavyoweza kuchangia ugomvi na uonevu. Wakati huo huo watazidi kuelewa wajibu wao wa kubadili mitazamo hii. Washiriki watajitazama wao wenyewe na kutafakari kuhusu uhusiano wao na wengine. Wataweza kukuza nafsi zao wakati wanapoimarisha uwezo wao wa kuubadili ulimwengu.



## Shuguli zinazopendekezwa

> Miduara ya kupiga ngoma, uk. 79.
> Kutafakari kuhusu mimi mwenyewe – safari ya kimyakimya, uk. 99.
> Nderemo za kuridhika, uk. 105.
> Mandalas, uk. 106.
> Korongo elfu moja wa karatasi, uk. 107.
> Kuchora kwenye fulana, uk. 109.

**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**



## Mibadala isiyo na ugomvi

Ndani ya kibanda hiki, washiriki watatiwa msukumo na kuwezeshwa kushughulikia kwa amani hali zinazoathiri utambulisho na haki zao. Washiriki watagundua mibadala isiyo na ugomvi na kujifunza kuhusu harakati za kupinga matumizi ya ugomvi zilizoshughulikia hali ya uonevu na ugomvi. Watatafakari kuhusu umuhimu wa kujenga amani ili kubadili jamii, jumuiya na dunia.



## Shuguli zinazopendekezwa

> Ziara za ugani, uk. 84.
> Benki ya kimaadili, uk. 87.
> Kutatua tatizo kwa hatua sita, uk. 91.
> Habari za amani, uk. 93.
> Viongozi wa kidini na kijamii, uk. 101.

**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**

## Matembezi ya usuluhishi

Kibanda hiki kitawasaidia washiriki kutathmini usuluhishi kama namna ya kurekebisha uhusiano uliovunjika. Wataendeleza nafsi zao na kujifunza kusikiliza wengine, kusamehe, kuponya na kurudisha uhusiano. Nija hii itawaruhusu washiriki kuona ubinadamu wa wengine, kukubali maumivu yanayosababishwa kwa wengine na haja ya kutafuta na kutoa msamaha.



### Shuguli zinazopendekezwa

> Hadithi kwa ajili ya nafsi, uk. 73.
> Kutamba hadithi, uk. 74.
> Kutatua tatizo kwa hatua sita, uk. 91.
> Viongozi wa kidini na wa kijamii, uk. 101.
> Kwa nini inaniumiza?, uk. 102.

**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**



## Kujenga madaraja ya kuaminiana

Katika kibanda hiki, washiriki watashirikiana na wengine kujenga madaraja ya kuaminiana na kusuluhisha tofauti zilizopo. Mazoezi yatasaidia pia kuimarisha stadi za mawasiliano na za kusikiliza. Washiriki watashirikiana wenyewe kwa wenyewe na wengine, kutimiza malengo ya pamoja wakati huo huo kutathmini na kuchunguza uwezo wao wa kubadili jamii zao.



### Shuguli zinazopendekezwa

> Kujiweka katika nafasi ya mwingine, uk. 85.
> Kutatua tatizo kwa hatua sita, uk. 91.
> Migahawa ya mazungumzo ya dini mbalimbali, uk. 96.
> Kutengeneza filamu, uk. 110.
> Mpira hewani, uk. 115.
> Utayarishaji wa miradi, uk. 121.
> Mazungumzo baina ya dini mbalimbali, uk. 122.

**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**

## Kushirikiana kuubadili ulimwengu

Baada ya kupitia vibanda vyote vya moduli hii, washiriki watavutiwa na kupata uwezo wa kuanza kuubadili ulimwengu wao wa karibu. Watakuwa tayari zaidi kushirikiana na wengine kubadili hali zilizowazunguka, kuleta amani na mabadiliko kwa jamii zao, na kuanzia hapo, hadi kwenye ulimwengu.



## Shuguli zinazopendekezwa


> Kujifunza kutoa huduma, uk. 116.

> Kampeni za kujifunza dini mbalimbali, uk. 117.

> Wiki yenye dhamira maalumu, uk. 119.

> Kampeni za haki za mtoto, uk. 120.

> Utayarishaji wa mradi, uk. 121.



**Kabla ya kuendelea, pima walichojifunza washiriki kwa kutumia mfano mmoja au zaidi wa tathmini. Angalia Sehemu ya 3, Kusimamia maendeleo.**

# Sehemu ya 3

# Usimamizi wa maendeleo

*Kujifunza Kuishi Pamoja* kina madhumuni na malengo yaliyo dhahiri. Kinakusaidia kuwashawishi vijana kuleta mabadiliko ya kijamii. Kufikia madhumuni haya ni muhimu kusiamamia na kupima athari ya programu yako. Njia muhimu zaidi miongoni mwa njia za tathmini zilizopendekezwa katika sehemu hii ni utaratibu wa kujifunza.

## Logu ya Kujifunza



"Kijitabu kwa Washiriki", kilichoelezwa kwenye ukurasa wa 37, kinawezesha washiriki tarajali kujua kuwa watatarajiwa kutunza Logu ya Kujifunza. Kwa hali hiyo kila mshiriki anapewa au lazima alete daftari watakazotumia kwenye shughuli zao na moduli. Logu hiyo ni ya binafsi na haina budi kutumiwa katika kila kipindi na kila mshiriki kuandika uzoefu wake na hisia zake. Logu ya kujifunza inakusudiwa kuimarisha mchakato wa kujitafakari. Lazima ijazwe baada ya kipindi, wakati washiriki wako peke yao na wana muda wa kutafakari.

Kutunza Logu ya kujifunza binafsi ni kipengele muhimu zaidi cha *Kujifunza Kuishi Pamoja* na haina budi, kama inawezekana itumiwe mwisho wa kila shughuli. Katika mchakato wa kujifunza utamaduni na dini mbalimbali, Logu ya Kujifunza inaweza kuwasaidia washiriki kuona zaidi ya hali ya kufikia uamuzi bila tafakuri na kukuza uelewa wao kuhusu uanuwai. Wakati mwingine mchakato huu unahitaji "kutojifunza" au kujitenga na walichojifunza kabla na kujiondoa katika kile walichoona mwanzoani kuwa ni sahihi. Kwa hiyo, Logu ya Kujifunza ni za binafsi na zinaweza kujadiliwa kwa hiari tu.

Kuwapa watoto fursa ya kujumuika na wenzao, kujiuliza kwa nini na kwa namna gani mambo yanavyotokea, na kukiri wanayoyajua, kutambua na kuzoea ni muhimu kwa kujenga kujifunza kujihakiki mwenyewe. Maswali ya kutafakari yanayowasaidia vijana kwenda zaidi ya uelewa wao wenyewe, wanahoji maoni yao kuhusu ulimwengu na kuwashawishi kufikiria upya hoja zao na tabia na mwenendo wao.

Ifuatayo ni baadhi ya mifumo ya maswali ya kutafakari na maelezo yatakayojumuishwa kwenye Logu ya Kujifunza:

- Je, nimejifunza nini kutokana na uzoefu huu?
- Je, mawazo yangu yamebadilika? Kama yamebadilika, kwa nini?
- Je, kuna kilichokosewa? Kwa nini? Je, naweza kukirekebishaje? Je, hali hiyo naweza kuikabilije?
- Jambo moja nililojifunza leo kuhusu mimi ni ______
- Leo nimekuwa na tatizo la kujaribu ______ Kesho nitatanzua tatizo hilo kwa____
- Sehemu bora zaidi kuhusu ______
- Nilizoea kufikiri ______ na sasa nafikiri ______
- Leo nimebadili namna ninavyo ______ kwa sababu ______

Mifano ya maswali au shughuli unayoweza kupendekeza kwa ajili ya Shajara za Kujifunza baada ya shughuli ni pamoja na:

> Je, heshima ina maana gani kwako? Andika nyakati ulipowaheshimu wengine shuleni kwako, katika familia au jamii.
> Pia fikiria nyakati ambapo hukuwaheshimu, wengine.
> Andika kwenye Logu yako ya Kujifunza kuhusu nyakati watu wengine hawakukuheshimu.
> Andika kwenye Logu yako ya Kujifunza ahadi mbili ambazo uko tayari kuzitimiza ili kuwa na heshima zaidi kwa wengine.
> Andika kwenye Logu yako ya Kujifunza mabadiliko unayotaka kufanya maishani mwako ili kuwa mshirikali zaidi.
> Andika kwenye Logu yako ya Kujifunza jambo moja unaloweza kufanya sasa kusaidia kutanzua hali iliyokuzunguka ambalo linaathiri maelewano yako.

# Njia za Kupima Kujifunza kwa Washiriki

**Mifano mitano ya Tathmini iliyopendekezwa hapa imebuniwa kuwasaidia watoto na vijana:**

> Kujiangalia na kutafakari namna walivyobadilika wakati wa programu.
> Kuangalia uhusiano wao na wengine na namna uhusiano huo ulivyobadilika kwa kujumuika na wengine.
> Kutafakari kuhusu wao ni kina nani na wanataka wawe nani.
> Kuwaangalia wenyewe na uhusiano wao na kujumuika na ulimwengu.



# Pima kujifunza kwa Washiriki!

**Tumia *Njia ya Rika kwa Rika kama* namna ya kuwasaidia washiriki kupima kujifunza kwao wenyewe**

## Njia ya Rika kwa Rika

Jozi za vijana wanajifunza kutoka kwa wenzao kwa kushirikiana uzoefu wao na kile walichojifunza. Njia hii inaleta uzoefu wa kujifunza pamoja na kuhoji mawazo ya awali ya kila mtu kuhusu historia tofauti za tamaduni, kijamii na kidini.

Jozi za rika zinaweza kuwa, ama kwa kujichagua wenyewe au zilizopangwa na wewe. Kimsingi, upangaji jozi huo hauna budi kujumuisha washiriki kutoka dini na tamaduni tofauti.

## Mifano ya Maswali au shughuli za kutumia

Unaweza kujifunza mengi miongoni mwenu. Tumia dakika 20 na rika lako kufahamiana vizuri zaidi.

> Jadili familia zenu, utamaduni, dini, nchi na mada nyingine.
> Elezaneni kuhusu namna mnavyoishi, imani za dini zenu ni zipi na namna mnavyozifuata, na namna unavyofikiri maisha yako yatakavyoboreshwa.
> Je, una maswali ambayo ungependa kuulizana?
> Elezaneni hisia zenu kuhusu programu.

Mwisho, andika kujifunza kwako na uzoefu uliopata kwenye Logu yako ya Kujifunza.



# Pima Kujifunza kwa Washiriki!

**Tumia *Njia ya Kushirikiana kwa Kikundi* kama namna ya kuwasaidia washiriki kupima kujifunza kwao wenyewe**

## Njia ya Kushirikiana kwa Kikundi

Njia hii inawapa washiriki fursa ya kushirikiana kile wanachojifunza kuhusu wao wenyewe miongoni mwao na dunia na kikundi. Wanaweza pia kushirikiana walichojifunza kuhusu heshima, haki na wajibu. Muundo hauna budi kuwahimiza washiriki kufanya uhusiano kati ya uzoefu wao unaohusika.

Waambie washiriki watafute wakati katika wiki kushirikiana na kikundi namna wanavyoimarisha uhusiano wao na wengine na namna wanavyojifunza kuwaelewa na kuwaheshimu wengine.



## Mifano ya maswali au shughuli za kutumia

> Tuambie kile tulichodhani kuwa ni sehemu yenye thamani sana katika somo lililopita au ya programu?
> Kwa nini ulifurahia wakati huu hasa?
> Je, unadhani wakati huu ulikuwa na umuhimu gani hasa?
> Fikiria kuhusu hali katika familia yako, shule au ujirani ambayo ni ukiukaji wa haki za binadamu na hadhi ya utu. Fikiria kuhusu watu wanaohusishwa katika hali hiyo na fikiria kuwa wewe ni miongoni mwao.
> Tuambie ambavyo ungehisi. Utaipokeaje hali hiyo.
> Je, unadhani kifanyike nini kusaidia kutanzua hali hii?

Mwisho, andika ulichojifunza na uzoefu uliopata kwenye Logu yako ya Kujifunza.



# Pima Kujifunza kwa Washiriki!

**Tumia *Njia ya Mimi na Ulimwengu* kama namna ya kuwasaidia washiriki kupima kujifunza kwao wenyewe**

## Njia ya Mimi na Ulimwengu

Njia hii inawasaidia washiriki kuelewa namna kujifunza kwao kunavyoathiri maoni yao kuhusu ulimwengu na kuhusu haja ya ubadilishaji wa kijamii. Kwa kutafakari matatizo ya maisha halisi na kwa kuchambua michango ya mtu kwa ufumbuzi kwa jumla, njia hii ya kujipima inaweza kusaidia kuleta kuchukua hatua halisi.

Washiriki wanaweza kuona haja ya kuwa na mageuzi kieneo na kimataifa kwa kushirikali na wale walioathiriwa wakati huo kujadili pia ufumbuzi na michango inayoweza kutolewa. Njia hii inasaidia washiriki kuingiza hali yao ya 'kieneo' kwenye muktadha wa 'Kimataifa' na kujiona kuwa raia wa kimataifa.

## Mifano ya Maswali au shughuli za kutumia

> Tayarisha ramani ya dunia (kubwa kadiri iwezekanavyo) ining'inize mahali pa kuonekana. Washiriki wachague mahali pawili (majiji, nchi au kanda) wasipopaelewa au wanapopapenda kujifunza. Chomeka pini kila mahali na waambie washiriki waandike kile wanachotaka kufahamu kuhusu mahali hapo.

> Kwa mwezi mmoja, tafuta taarifa zaidi kuhusu mahali palipochaguliwa. Washiriki hawana budi kusoma magazeti, taarifa ya habari ya TV na Intaneti na waulize taarifa zaidi wazazi na marafiki. Kila kitu ni muhimu. siasa, matukio, utamaduni, uanuwai wa watu, desturi zao za dini. Kila wiki washiriki wanashirikiana taarifa walizokusanya na ongeza zaidi taarifa waliyopata kwenye ramani.

> Wakishafahamu zaidi kuhusu mahali, bainisha kile kinachoonekana kuwa hali muhimu katika jamii ile mahususi, kitu kinachotakiwa kubadilishwa au jambo linaloleta huzuni kwa watu wake. Andika na bandika kwenye ramani.

> Wahimize washiriki watafakari kuhusu namna tatizo lililobainishwa litakavyoweza kutanzuliwa. Je nani atalitanzua? Je, tunaweza kusaidia kutanzua?

Mwisho, andika ulichojifunza na uzoefu uliopata kwenye Logu yako ya Kujifunza.



# Pima kujifunza kwa Washiriki!

**Tumia *Njia ya Ushauri* kama namna ya kuwasaidia washiriki kupima kujifunza kwao wenyewe**

## Njia ya Ushauri

Washiriki wanajadili mawazo yao, hofu, juhudi na malengo maishani pamoja na mifano yao ya kuigwa. Hii ni dhana kwa ajili ya kushirikiana uzoefu na kuhimiza kila mshiriki alete mabadiliko katika mazingira yake ya karibu. Pia inamsaidia kutafakari kuhusu uzoefu wa wengine na inaweza kusaidia kama kichocheo cha kupata udhibiti mzuri zaidi kuhusu maisha yake. Njia hii pia inaruhusu mifano ya kuigwa ya watu wazima kusaidia kujifunza kwa washiriki kwa kuonyesha mienendo ya kiuadilifu.

Katika Mithiolojia ya Kigiriki washauri walikuwa marafiki wa kuaminika na waelekezi. Katika utenzi uliotungwa na Homer, mtoto wa Odysseus, Telemachus, alilewa na Mshauri aliyesaidia katika kumwendeleza Telemachus kwa upande wa uwajibikaji katika maisha.



## Mifano ya Maswali au shughuli za kutumia

- Bainisha angalau mtu mmoja ambaye unadhani ni mfano wa kuigwa kwa baadhi ya vijana katika kikundi chako au waeleze washiriki wako mfano wa kuigwa ni nini na waambie wateuwe watu kwenye jumuiya zao. Watu ambao ni mifano ya kuigwa lazima wawe ni watu wanaoheshimika na wanaojistahi lakini pia wanaoweza kuzungumza na kuwasikiliza watoto na vijana.
- Mwalike mtu ambaye ni mfano wa kuigwa atembelee kikundi na kushirikishana nao baadhi ya uzoefu kuhusu maisha yake, uhusiano na wengine na maisha yake ya kiroho na imani zake.
- Washiriki kwa upande wao wanaweza kushirikishana kuhusu baadhi ya uzoefu wao na mtu huyu, hali ngumu wanazokabiliana nazo, mafanikio yao na changamoto za kiuadilifu. Je kuna jambo lililowatokea katika kipindi cha miezi mitatu ya mwisho wanayotaka kushirikishana na mtu huyo aliye mfano wa kuigwa?
- Kama imani imejengwa kwa mtu huyo na iwapo anakionea huruma kikundi, umwombe atembelee kikundi mara kwa mara.
- Washawishi washiriki watafute nje ya program watu wao binafsi ambao ni mfano wa kuigwa, sifa iwe mtu anayeweza kutoa utambuzi, busara, na maarifa na ambaye mshiriki anahisi kuaminiwa, kuendelezwa na kuhimizwa kutimiza wajibu wake kuwa sehemu ya kujenga ulimwengu bora zaidi na unaozingatia haki zaidi.



# Pima kujifunza kwa Washiriki!

**Tumia *Njia ya Ushauri* kama namna ya kuwasaidia washiriki kupima kujifunza kwao wenyewe**

## Njia ya Chati ya Kuhakiki

Hii ni seti ya maswali kwa ajili ya kupima kujifunza mtu. Inawezesha washiriki kutafakari kuhusu nafsi zao na kwa mujibu wa kujifunza, kutafuta namna ya kutenda kwa kuwajibika ili kubadili mazingira yao.

## Mifano ya maswali au shughuli za kutumia

Chora Chati ya Kuhakiki kwenye Logu yako ya Kujifunzia

**CHATI YANGU YA KUHAKIKI**

| Hali ninayotaka kuiboresha | Kwa nini ninataka kuiboresha zaidi? | Je, kuna jambo linalonikwaza nisiboreshe? | Je, inahusisha watu wengine? | Je, naweza kushirikiana na watu wengine kuboresha hali hii? |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

# Njia za Kupima ya 'Kipima Joto'

Njia tano zilizoelezwa hapo juu zilikuwa kama tathmini binafsi au za kikundi kwa washiriki, zitakazotumika katika njia ya kujifunza. Kama mwezeshaji ungependa kujua namna mambo yanavyokwenda kwa kutumia njia ya papo kwa hapo. Baadhi ya njia chache zinazofaa ni pamoja na:

> **Mikono Juu:** Kama washiriki wanaulizwa swali linalowataka wainue mikono (kuzungumza au kama kunyoosha mikono), wanaweza kujifunza mambo mengi kuhusu furaha yao na kiwango cha kuridhika kwa namna wanavyonyoosha mikono yao. Je, mikono yao iko juu, iko nusu juu au haikuinuliwa kabisa? Njia hii inaweza kutumiwa pia kupima iwapo taarifa imeeleweka kwa ukamilifu.

> **Utafiti:** Wape washiriki utafiti na waambie wazungushie vivumishi vitatu ambavyo kwao vinaonyesha kuridhika kwao na somo. Jaribu kujumuisha maneno ambayo washiriki wanaweza kuyatumia kujieleza:

adhimu   a kustaajabisha   safi sana   safi, nzuri   OK   a kufurahisha   a kushangaza

kazi ngumu   ngumu   fikra   chokozi   ndefu mno   inachosha   a kuchusha

> **Kitu nilichopenda na ambacho sikukipenda:** Washiriki waweke mikono yao kwenye mduara na wataje kitu kimoja walichokipenda na ambacho hawakukipenda kuhusiana na somo lililopita.

# Tathmini ya Athari

**Madhumuni ya *Kujifunza Kuishi Pamoja* (angalia ukurasa x) yanaweza kutafsiriwa katika mitazamo na uwezo ufuatao:**


- Dhima ya kufanya uamuzi wa busara zaidi
- Kuathiriwa haraka na tofauti za watu wengine
- Kuwa tayari kusuluhisha tofauti na watu wengine
- Kuheshimu tamaduni na imani za wengine
- Uwezo wa kushirikali na wengine
- Uwezo wa kushughulikia hali ngumu ukitumia mibadala isiyotumia nguvu

Majedwali ya kipimo cha athari kwenye viambatisho vya ukurasa 230 hadi 232 yanatokana na madhumuni ya *Kujifunza Kuishi Pamoja*. Majedwali hayo yatakusaidia kupima kama programu imefanikiwa kuleta maarifa, tabia na mienendo ya kiuadilifu, mitazamo na uwezo wa washiriki au hapana.

Ni vigumu kupima mabadiliko ya mitazamo na tabia kutokana na aina za data zinazohitajika katika kutathmini hali za nafsi. Majedwali haya yatakupa fursa tu ya kuelewa kama washiriki wamebadili maono yao na wako tayari kuenenda kwa njia ya amani na heshima kwa wengine.

Maswali katika majedwali yametayarishwa chini ya vichwa vitatu vifuatavyo: maarifa, mitazamo na stadi. Maarifa kuhusu mtu mwenyewe, wengine na kuhusu ukweli wa dunia unavyoathiri mitazamo na mienendo na tabia ya watoto waliyonayo kwao wenyewe na kwa watu wengine. Hatimaye hii husababisha namna ya utendaji ambao ni jumuishi, wenye huruma na unaojali au unaobagua na wenye uchoyo. Namna watoto wanavyojiheshimu na kutenda vinaathiriwa sana na uendelezaji wa maadili na nafasi wanazopewa kujumuika na wengine.

Baadhi ya maswali yanahusiana na mambo ya kuchagiza upendeleo na ubaguzi dhidi ya wengine. Chagizo inahusu ujumuishaji wa sifa bainifu za watu katika vikundi. Upendeleo ni mitazamo kwa watu kwenye kikundi kwa msingi hasa wa kuwamo kwao kwenye kikundi kile (yanaweza kuwa hasi au chanya), na ubaguzi ni matendo hasi au chanya kwa dhamira ya upendeleo. Aina hizi za maswali zitakupa uwezo wa kutathmini mitazamo kuhusu wao wenyewe na wengine na uhusiano na matendo yao.




## Maelekezo ya namna ya kutumia majedwali



Majedwali kwenye Viambatisho vya ukurasa 230 na 232 yametayarishwa kutumika kabla na baada ya Programu ya *Kujifunza Kuishi Pamoja*.

Mpe kila mshiriki nakala ya majedwali (A,B,C) mwanzo wa programu na eleza kwamba madhumuni ya zoezi ni kujaribu kujielewa vizuri zaidi. Sisitiza kwamba si lazima waandike majina yao kwenye karatasi kama hawataki. Waambie kwa sasa waweke karatasi kwenye majalada yao au Logu ya Kujifunza.

Gawa seti nyingine ya pili ya majedwali inayofanana mwisho wa programu na waambie washiriki wajaze. Waambie kwamba madhumuni ya kujaza karatasi hizi ni kutathmini kama kumekuwa na mabadiliko yoyote katika maono, mawazo na hoja baada ya programu.

Waambie washiriki wabane seti mbili za karatasi pamoja baada ya kumaliza kujaza karatasi hizo. Wape muda wa kuandika kwenye Logu yao ya Kujifunza kilichobadilika kwenye majibu yao kutoka karatasi ya kwanza na ya pili

Waambie washiriki wakukabidhi seti mbili za karatasi zilizobanwa pamoja baada ya kumaliza.

Linganisha majibu kutoka kwenye seti ya kwanza ya majibu na seti ya pili kwa kila mshiriki (bana pamoja karatasi za majibu) na tathmini athari za programu kwa washirki kwa kuangalia mabadiliko katika:

1. Maono yao na ya wengine.
2. Maarifa waliyonayo kuhusu utamaduni na imani za watu wengine.
3. Maarifa waliyonayo kuhusu ukweli wao wa kijamii.
4. Maoni yao kuhusu maelezo kwenye jedwali.
5. Namna watakavyotenda katika hali mahusus Kujadiliana picha Kujadiliana picha.

# Sehemu ya 4

# Shughuli

## Jedwali la Shughuli

### MODULI YA 1 Kujielewa Binafsi na Wengine

| Kibanda | Shughuli | Njia | UK |
|---|---|---|---|
| Kukubali Uanuai | Kujadiliana picha | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 70 |
| | Kuchora ramani | Kujifunza kwa msingi wa Majadiliano | 76 |
| | Kufikia nyota | Kujifunza kwa msingi wa Majadiliano | 77 |
| | Ziara za dini mbalimbali | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 80 |
| | Linganisha | Kujifunza kwa msingi wa Majadiliano | 82 |
| | Shughuli za utamaduni za jioni | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 83 |
| | Chemsha Bongo, Je, najua nini kuhusu dini nyingine? | Kujifunza kwa msingi wa ushirika | 112 |
| Kujikubali mwenyewe kuhusiana na wengine | Mti wa Historia ya Maisha yangu | Kujifunza kwa msingi wa kujipima na kujichunguza | 65 |
| | Kubadilishana uzoefu binafsi | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 67 |
| | Kufikia nyota | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 77 |
| | Linganisha | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 82 |
| | Shughuli za utamaduni za jioni | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 83 |
| | Hadithi ya Bobby | Kujifunza kwa msingi wa Kujipima na Kujichunguza | 103 |
| | Kuchora kwenye fulana | Kujifunza kwa msingi wa kujipima na kujichunguza | 109 |
| Ubinadamu wetu wa pamoja | Kutamba hadithi | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 77 |
| | Kufikia nyota | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu na Kujipima na Kujichunguza | 79 |
| | Miduara ya Kupiga Ngoma | Kujifunza kwa msingi wa Kujipima na Kujichunguza | 74 |
| | Nderemo za kuridhika | Kujifunza kwa msingi wa Kujipima na Kujichunguza | 105 |
| Je, tunaweza kupatana? | Hadithi kwa ajili ya nafsi | Kujifunza kwa kwa msingi wa mawasiliano | 73 |
| | Ninachotetea | Kujifunza kwa msingi wa Majadiliano | 78 |
| | Benki ya Kimaadili | Kujifunza kwa msingi wa Tatizo | 87 |
| | Vikundi lengwa kuhusu heshima | Kujifunza kwa msingi wa Majadiliano | 95 |
| | Migahawa ya mazungumzo ya Dini mbalimbali | Kujifunza kwa msingi wa Majadiliano | 96 |
| | Hadithi ya Bobby | Kujifunza kwa msingi wa Kujipima na Kujichunguza | 103 |
| | Mazungumzo baina ya dini Mbalimbali | Kujifunza kwa msingi wa Majadiliano | 122 |
| Kujifikiria kuwa katika nafasi ya mtu fulani | Taswira ya umbo lako ni yangu | Kujifunza kwa msingi wa Kujipima na Kujifunza | 69 |
| | Ziara za Dini Mbalimbali | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 80 |
| | Kutumia njia ya kujiweka katika nafasi ya mwingine | Kujifunza kwa msingi wa Uzoefu na Tatizo | 85 |
| | Kutumia uchunguzi Kifani | Kujifunza kwa msingi wa Uzoefu na Tatizo | 86 |
| Kushughulikia mahitaji ya kuelewana | Migahawa ya mazungumzo ya dini mbalimbali | Kujifunza kwa msingi wa majadiliano | 96 |
| | Kutengeneza filamu | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 110 |
| | Kampeni za kujifunza dini mbalimbali | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 117 |
| | Mabadilishano ya shule | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 118 |
| | Wiki maalumu yenye dhamira | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 119 |
| | Kampeni za haki za watoto | Kujifunza kwa msingi wa uzoefu | 120 |
| | Mazungumzo baina ya dini mbalimbali | Kujifunza kwa msingi wa majadiliano | 122 |

## MODULI YA 2 Kuubadili Ulimwengu Pamoja

| Kibanda | Shughuli | Njia | UK |
|---|---|---|---|
| Je, itatokea nini kama tutashindwa kuheshimiana? | Wakati wa filamu | Kujifunza kwa Msingi wa Majadiliano | 71 |
| | Kujifunza kutokana na hadithi za maisha halisi | Kujifunza kwa Msingi wa Majadiliano | 72 |
| | Hali ya Uonevu | Kujifunza kwa Msingi wa uzoefu | 75 |
| | Je, ulimwengu ungekuwaje kama… | Kujifunza kwa Msingi wa kujipima na kujichunguza | 104 |
| | Korongo elfu moja wa karatasi | Kujifunza kwa Msingi wa kujipima na kujichunguza | 107 |
| | Visiwa vinavyotoweka | Kujifunza kwa Msingi wa uzoefu | 114 |
| Kuelewa migogoro, ugomvi na uonevu unaonizunguka | Wakati wa filamu | Kujifunza kwa Msingi wa Majadiliano | 71 |
| | Kujiweka katika nafasi ya mwingine | Kujifunza kwa Msingi wa uzoefu na tatizo | 85 |
| | Kutumia uchunguzi kifani | Kujifunza kwa Msingi wa uzoefu na tatizo | 86 |
| | Mitanziko | Kujifunza kwa Msingi wa Majadiliano | 89 |
| | Mikutano ya Majadiliano | Kujifunza kwa Msingi wa Majadiliano na tatizo | 97 |
| | Midahalo | Kujifunza kwa Msingi wa Majadiliano | 98 |
| | Korongo elfu moja wa Karatasi | Kujifunza kwa Msingi wa kujipima na kujichunguza | 107 |
| Amani inaanzia kwangu | Miduara ya kupiga ngoma | Kujifunza kwa Msingi wa kujipima na kujichunguza | 79 |
| | Tafakari kuhusu mimi mwenyewe – safari ya kimya kimya | Kujifunza kwa Msingi wa kujipima na kujichunguza | 99 |
| | Nderemo za kuridhika | Kujifunza kwa Msingi wa kujipima na kujichunguza | 105 |
| | Mandalas | Kujifunza kwa Msingi wa kujipima na kujichunguza | 106 |
| | Korongo elfu moja wa Karatasi | Kujifunza kwa Msingi wa kujipima na kujichunguza | 107 |
| | Kuchora kwenye fulana | Kujifunza kwa Msingi wa kujipima na kujichunguza | 109 |
| Mibadala isiyo na Ugomvi | Ziara za Ugani | Kujifunza kwa Msingi wa uzoefu | 84 |
| | Benki ya Kimaadili | Kujifunza kwa Msingi wa tatizo | 87 |
| | Kutatua tatizo kwa hatua sita | Kujifunza kwa Msingi wa tatizo | 91 |
| | Habari za Amani | Kujifunza kwa Msingi wa tatizo na uzoefu | 93 |
| | Viongozi wa kidini na Kijamii | Kujifunza kwa Msingi wa kujipima na kujichunguza na majadiliano | 101 |
| Njia ya Upatanishi | Hadithi kwa ajili ya Nafsi | Kujifunza kwa Msingi wa majadiliano | 73 |
| | Kutamba Hadithi | Kujifunza kwa Msingi wa kujipima na kujichunguza | 74 |
| | Kutatua tatizo kwa hatua sita | Kujifunza kwa Msingi wa tatizo | 91 |
| | Viongozi wa kidini na kijamii | Kujifunza kwa Msingi wa kujipima na kujichunguza na majadiliano | 101 |
| | Kwa nini inaniumiza mimi? | Kujifunza kwa Msingi wa majadiliano | 102 |
| Kujenga Madaraja ya kuaminiana | Kujiweka katika nafasi ya mwingine | Kujifunza kwa Msingi wa tatizo | 85 |
| | Kutatua tatizo kwa hatua sita | Kujifunza kwa Msingi wa tatizo | 91 |
| | Migahawa ya mazungumzo baina ya dini mbalimbali | Kujifunza kwa Msingi wa majadiliano | 96 |
| | Kutengeneza filamu | Kujifunza kwa Msingi wa uzoefu | 110 |
| | Mpira hewani | Kujifunza kwa Msingi wa ushirika | 115 |
| | Utayarishaji wa mradi | Kujifunza kwa Msingi wa ushirika | 121 |
| | Mazungumzo baina ya dini mbalimbali | Kujifunza kwa Msingi wa majadiliano | 122 |
| Kushirikiana kuubadili ulimwengu | Kujifunza kutoa huduma | Kujifunza kwa Msingi wa uzoefu | 116 |
| | Kampeni za kujifunza Dini Mbalimbali | Kujifunza kwa Msingi wa uzoefu | 117 |
| | Wiki yenye dhamira maalumu | Kujifunza kwa Msingi wa uzoefu | 119 |
| | Kampeni za haki za mtoto | Kujifunza kwa Msingi wa uzoefu | 120 |
| | Maendeleo ya miradi | Kujifunza kwa Msingi wa ushirika | 121 |

# Mti wa Historia ya Maisha Yangu

**Madhumuni:** Kuwahimiza washiriki watafakari kuhusu maisha yao wenyewe na utambulisho na kukubali utambulisho wa kipekee wa watu wengine.


**Matokeo:** Washiriki wanajielewa zaidi na utambulisho wao. Kwa kushirikishana historia ya maisha yao, wanajielewa pia kuhusu maisha na utambulisho wa wengine, hata kama vilionekana kufanana au kutofautiana hapo awali.

**Vifaa vya Kufundishia:** Karatasi isiyoandikwa chochote kwa ajili ya kuchorea, kalamu za rangi au kalamu za kuchorea.

## Shughuli

Mpe kila mshiriki karatasi nyeusi ya kuchorea na baadhi ya kalamu za rangi na waambie wachore mti, kujiwakilisha mwenyewe. Wakimaliza waambie wafikirie taarifa kuhusu wao wenyewe ambazo wangependa kuandika kwenye mti huo. Tayarisha orodha ya mapendekezo ya washiriki ubaoni au karatasi kubwa ambayo wanaweza kurejea. Vifuatavyo ni baadhi ya vitu ambavyo wanaweza kupendekeza:

- Ninakoishi.
- Mahali nilikokuwa naishi zamani.
- Wanafamilia.
- Marafiki.
- Shule, ikiwemo jina na ngazi ya darasa.
- Kitu ninachokiweza zaidi.
- Hiki ndicho ninachopenda kufanya.
- Hili ndilo linalonifurahisha.
- Hili linanihuzunisha.
- Hili ndilo ninaloamini.
- Nitakapokua, nataka kuwa…



Kabla ya washiriki kuanza kuandika, zungumza nao kuhusu mti. Nini madhumuni ya mizizi yake? Je, kukua kunafanyika wapi? Je, kwenye mizizi, kwenye ncha za matawi, na juu ya kilele cha mti waweke nini? Baadhi ya washiriki wanaweza kuhitaji msaada katika kufikiria kuhusu wao wenyewe na matarajio yao.

Shughuli inahitaji muda wa kujipima na kujichunguza na kushirikiana isivyo rasmi na wengine. Baada ya washiriki wote kumaliza kuongeza taarifa kwenye mti wao, omba washiriki wa kujitolea kuwaarifu kikundi chote kuhusu historia ya maisha yao. Baada ya uwasilishaji kiasi pendekeza kuwa washiriki wazunguke kwenye kikundi na wajaribu kutafuta:

> Angalau mtu mmoja mwingine aliyekulia mahali hapo pia – na mtu mwingine anayetoka mahali tofauti kabisa.
> Mtu aliyehuzunishwa na kitu hicho hicho na mtu aliyehuzunishwa na kitu kingine tofauti kabisa.
> Mtu anayeweza vitu hivyo hivyo – na mtu anayeweza kitu tofauti kabisa.

Haya ni mapendekezo tu, uwe huru kuleta mada mpya.

Hitimisha somo kwa majadiliano kuhusu kufanana na kutofautina na namna ambavyo haya yanaunda sehemu ya utambulisho wetu. Je, washiriki watafanya hitimisho gani? Tafakari kuhusu upekee wa kila mtu na wa kuheshimu tofauti za kila mmoja.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza



### Maelezo yangu

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

.................................................................................................................................

# Kushirikishana uzoefu binafsi

**Madhumuni:** Kunawezesha washiriki kujifunza kutokana na mambo ya kiroho ya wengine na kutafakari kuhusu imani zao wenyewe.

**Matokeo:** Washiriki wamechunguza na kushirikishana uzoefu wao wa kiroho na kila mmoja na kutafakari pamoja.

**Vifaa vya kufundishia:** Karatasi na kalamu za kuchorea kwa washiriki. Tayarisha maswali machache – angalia mifano hapo chini – kuhusu namna washiriki wanavyohusiana na watu wengine, wanachofanya wanapojisikia huzuni au furaha, wanapotaka kutafakari au kuwa peke yao.

**Maswali ya sampuli:**

Nini kinachokufanya utabasamu, nini kinachokufanya uchangamke, jambo gani linalokugusa?

Nini kinachokufanya ukose raha, kinachokufanya ukasirike na kutokuwa tayari kuwasiliana na mtu mwingine yeyote?

Je, unaweza kueleza baadhi ya vitu vinavyotokea kwako wakati unapohisi huna matatizo?

Je, unaweza kueleza nini kinakosekana wakati unahisi kuvunjika moyo?

Je, unadhani kuna uhusiano wowote kati ya namna unavyohisi moyoni na namna unavyowasiliana na wengine?

Je, uhusiano wako na wengine unakusaidia kujihisi vizuri zaidi ndani ya nafsi yako?

## Shughuli

1. Kiweke kikundi chako mahali ambako ni patulivu na kila mmoja anaweza kukaa na kufikiria bila ya usumbufu, inaweza kuwa bustani, bustani kubwa au chumba chenye muziki mwororo.
2. Waambie washiriki kwamba shughuli hii inawataka wafikirie kuhusu nafsi zao, hisia zao na imani, matukio yaliyopita na uhusiano wao na wengine. Waambie kwamba umetayarisha baadhi ya maswali kuwaongoza katika kufikiri kwao na kila mshiriki mpe nakala au weka maswali kwa kila mmoja kuona. Wahakikishie washiriki kuwa kwa vyovyote vile si jaribio bali ni zoezi la kuwasaidia kutafakari. Pia wahakikishie kwamba hakuna ulazima wowote wa kushirikiana mawazo yao, kama hawataki kufanya hivyo na kwamba wanachokiandika kwenye karatasi yao ni kwa ajili yao tu.
3. Wape nakala ya maswali ya papo kwa hapo au yabandike mahali yanapoweza kuonekana. Wambie washiriki watafute mahali kimya na patulivu ambapo wao peke yao wanaweza kuandika majibu ya maswali ama iwe kwenye karatasi ya maswali yenyewe au kwenye karatasi mpya.
4. Wape angalau dakika 30 kwa kutafakari binafsi halafu wakusanye washiriki pamoja kwenye mduara ili waweze kuzungumza miongoni mwao kwa urahisi. Anzisha majadiliano kwa kuwauliza kwa ujumla walijihisi vipi wakati wa kujibu maswali. Waalike washiriki wa kujitolea wakieleze kikundi kuhusu majibu yao kwa kila swali. Fanya hali kuwa tulivu, salama na yenye uelewano – kama mtu hataki kuchangia hoja, asilazimishwe kufanya hivyo.
5. Mwishowe unaweza kuzingatia swali la mwisho na kushirikiana kaida zao za dini, nyakati zao za kutafakari na hisia na imani zao. Zungumzia namna wanavyoweza kuimarisha uhusiano wao na wengine, bila ya kujali imani au dini zao.

Kuhitimisha somo, unaweza kuwasomea shairi washiriki, “Chumvi ya Nafsi” unaloweza kulipata kwenye sehemu ya Nyenzo /Mashairi kwenye ukurasa wa 160.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

**Maelezo yangu**

# Taswira Yako ni Yangu

**Madhumuni**: Kuwasaidia washiriki kuelewa na kufurahia maono ya watu wengine kupitia matumizi ya taswira.

**Matokeo:** Washiriki wawe wamejifunza kuhusu watu 'wengine' kwa kuelewa hisia zake. Washiriki wawe wametafakari kuhusu namna watu 'wengine' wanavyotenda au kwa nini watu 'wengine' wanafikiria kwa namna mahususi.

**Vifaa vya kufundishia**: Karatasi pana ukubwa wa mwili (tumia karatasi nyingi kutoka kwenye chati pindu, karatasi ya nyuma ya karatasi za ukutani au zinazolingana) kalamu za rangi au kalamu za kuchorea, muziki mwororo.

## Shughuli

Wagawe washiriki katika jozi – waeleze kwamba katika shughuli hii watafanya kazi kama washirika. Mpe kila mshiriki karatasi yenye ukubwa wa mwili. Waambie watandaze karatasi sakafuni na kupeana zamu ya kuchora taswira ya umbo ya mshiriki mwenza.

Wakishamaliza kuchora taswira za maumbo ya washirika, waambie kila mshiriki aandike taarifa ifuatayo kwenye taswira ya umbo lake mwenyewe:

| | |
|---|---|
| Kwenye kichwa: | wazo |
| Kwenye titi (moyo): | hisia |
| Kwenye tumbo: | mahitaji |
| Kwenye mikono: | haja ya kufanya jambo |
| Kwenye miguu: | shughuli unayoipenda au kuifurahia |

Kila mmoja akikamilisha kazi hiyo, waambie washiriki washirikishane taarifa na washirika wenza wao na kueleza kila wazo, hisia, mahitaji, haja au shughuli wanayoipenda bila ya kueleza sababu ya kufanya hivyo.

Baada ya kushirikishana kilichoandikwa kwenye taswira za maumbo yao, waambie washiriki walale kwenye taswira ya umbo la mwenzake, wafumbe macho na wafikirie kuwa wao ni wenzao. Unaweza kupiga muziki mwororo na kuanzisha tafakuri kwa kuwaambia washiriki kuwa "waache fikra zao na waingie kwenye fikra za mshiriki mwenza wako", ili kujaribu kufikiria mawazo ya mtu mwingine, kuhisi mahitaji ya mtu mwingine na kufikiria kufanya shughuli ambazo washiriki wenza wao wanafurahia.

Mwishoni bakisha dakika chache kwa tafakuri binafsi kuhusu maana ya kufikiria kuwa mtu fulani. Unaweza kumaliza shughuli kwa kuwauliza washiriki kukumbatiana kama namna ya kuonyesha kuelewana.

## Waambie washiriki waandike kuhusu Shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Kushirikishana Picha

**Madhumuni:** Kuwavutia washiriki wajifunze zaidi kuhusu uhalisia wa dunia kwa kuwataka waeleze wasifu wa dunia.

**Matokeo:** Washiriki wawe wametafakari uelewa wao wa dunia na itakuwaje watu watakaposhindwa kuelewana.

**Vifaa vya kufundishia:** Magazeti na majarida mbalimbali ya zamani, mikasi na gundi ya maji, kiasi cha meta mbili au zaidi za karatasi au kitambaa (upande wa nyuma wa gombo la karatasi ya ukutani au karatasi nyingi kubwa na pana zilizoungwa pamoja), kalamu za rangi au kalamu za kuchorea, rangi za kunyunyizia zisizo na sumu.

## Shughuli

Bandika karatasi au kitambaa kirefu ukutani. Kwa kutumia kalamu nyeusi ya kuchorea, chora matofali na kuweka vitu vingine muhimu kwenye karatasi ionekane kama ukuta wa mtaa.

Wape magazeti na majarida ya zamani washiriki na waambie watengeneze picha iliyotengenezwa kwa kugandishwa vipande vya karatasi kuhusu dunia wanayoiona. Wanaweza kuandika maneno, taswira, kuchora picha zao wenyewe, michoro au maneno ya mikwaruzo ukutani – kila kitu wanachoona kuwa kinaonyesha au kuwakilisha uhalisi wa dunia. Wape dakikia 45 hadi 60 kukamilisha zoezi hilo halafu waache huru wafanye peke yao, kwa pamoja, kwa jozi nk.

Watakapokamilisha picha ya kugandisha vipande vya karatasi, wakusanyike kuizunguka na kuiangalia kwa dakika chache.



Halafu waulize washiriki maswali ya kutafakari kama ifuatavyo:

> Je, huu ni ulimwengu unaotaka kuishi?
> Je, huu ni ulimwengu unaotaka kuwarithisha watoto wako?
> Je, ni nani aliyeufanya ulimwengu kuwa namna hii?
> Je, nini sababu za matukio yaliyoonyeshwa kwenye ukuta?
> Je, tunaweza kuchukua au kuiga matendo mazuri yaliyoonyeshwa kwenye ukuta mahali penye ugomvi au uonevu?
> Je, sisi tunawajibika kwa kile kinachotokea duniani?

Ruhusu majadiliano yaingie katika ushirikianaji wa uzoefu binafsi, ambapo washiriki wanaeleza zaidi kuhusu uhalisi wanaokabiliana nao katika jamii zao wenyewe.

Waambie kwamba hii ni sehemu tu ya safari yao na kwamba hawana budi kufikiria kama kuna hatua zozote watakazochukua kusaidia kuboresha hali hiyo.

Unaweza kumaliza shughuli kama inafaa kwa kuwasha mshumaa na kuongoza sala ya kudumisha amani duniani, au kwa kuimba wimbo wa amani.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Wakati wa Filamu

**Madhumuni:** Kuongeza uelewa wa washiriki kuhusu hali za migogoro, uonevu na ugomvi duniani kote, na namna matendo japo machache yanavyoweza kuleta tofauti kubwa.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wamejifunza kuhusu watu wapya, mahali papya na historia. Ujasiri na kujituma kwa wale ambao matendo yao yamejitokeza katika filamu, kutawafanya washiriki kuhoji sababu za umaskini, ugomvi na mgogoro, na haja ya ustahimilivu kwa watu kubadili hali hizo kuwa kitu kingne bora zaidi.

**Vifaa vya kufundishia:** Nakala nzuri ya filamu ya video au DVD, mahali patulivu pa kuangalia filamu hiyo. Kama una ziara ya kikundi ya kuangalia filamu kwenye nyumba ya sinema, jaribu kupanga muda wako wa kupata mahali au fursa ya kujadili filamu hiyo kabla kikundi hakijatawanyika.

## Shughuli

Filamu ni njia ya mawasiliano inayoweza kuwasaidia washiriki kuingia katika ulimwengu mwingine au maisha mengine na kuangalia namna mambo yalivyokuwa au bado yako hivyo, kwa ajili ya watu wengine. Kutegemea ustadi wa mtengenezaji filamu, washiriki wataweza pia kufikiria hoja za maoni tofauti, sababu za kuchukua hatua na utata wa hali tunazokabiliana nazo.

Baadhi ya filamu zinazofaa, zimeorodheshwa kwenye Sehemu ya Nyenzo, ukurasa 149, lakini filamu nyingine zaidi zinaweza kuongezwa kwenye orodha hii.

Andaa "ziara ya kwenye nyumba za sinema" kwa kuwapa washiriki muhtasari wa mtiririko wa kisa cha filamu na kipindi ambacho kisa hicho kinatokea. Waulize kwanini kuangalia filamu hii wanadhani ni muhimu sana kwa kazi yao kuhusu maadili.

Baada ya kuangalia filamu, waulize washiriki maswali mengi yanayodadisi uelewa wao kuhusu filamu hiyo na matukio na wahusika waliowakilishwa. Waulize kuhusu mvuto wa wahusika: namna ambavyo baadhi wanatii amri na namna ambavyo wengine wanavyotumia dhamiri yao na juhudi kuchukua hatua binafsi kwa niaba ya wengine. Unaweza kuuliza kama filamu ina uhusiano wowote na maisha halisi ya jamii au wanachoelewa kuhusu matukio ya sasa duniani. Panua majadiliano kwa kufikiria sababu za migogoro na uonevu duniani. Pia unaweza kuuliza kuwa washiriki wanadhani watachukua nafasi gani wakati watakapokabiliwa na hali kama hiyo ilivyo kwenye filamu.

Mwisho, waambie washiriki wapitie matukio ya filamu kupitia mitazamo ya haki, ya heshima na uwajibikaji. Je, ni haki za nani zinavujwa au kukiukwa? Haki za nani zinatimizwa? Je watu wanaheshimiana? Je, watu wanatimiza wajibu kwao wenyewe na wengine? Je, wanalinda haki za wengine?

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Kujifunza kutokana na hadithi za maisha halisi

**Madhumuni:** Kuwasaidia washiriki kuchunguza hali za uonevu, migogoro na kudharauliana kupitia hadithi za maisha halisi.

**Matokeo:** Washiriki wawe wametambua kuwa kila mmoja ana wajibu wa kuheshimu haki na hadhi ya utu, ambayo ni ya kiulimwengu na haiwezi kutenganishwa.

**Vifaa vya kufundishia:** Kusanya maandishi mbalimbali kuhusu ukiukaji wa hivi karibuni wa haki za binadamu kutoka kwenye magazeti, majarida au kutoka miongoni mwa uchunguzi kifani (ukurasa wa 139, Nyenzo/Uchunguzi Kifani). Unaweza kuamua kutumia hadithi moja au mbili au nyingi. Jaribu kuchagua hadithi zenye urefu unaolingana na unaweza kutaka kila mtu ajadili dhamira ya aina moja au kuwasilisha hadithi zenye dhamira nyingi tofauti. Shughuli hii inahitaji chatipindu na kalamu za kuchorea kwa mwezeshaji.

## Shughuli

1. Wagawe washiriki katika vikundi vidogo vya watu watatu hadi watano na wape kila kikundi nakala ya hadithi.
2. Kiambie kila kikundi kisome hadithi yao, kijadili sababu ipi ya hali iliyoonyeshwa kwenye hadithi, ni kanuni gani za kimaadili au haki za binadamu zimekiukwa na matokeo yake ni yapi.
3. Kama una muda, viambie vikundi vitayarishe igizo dhima kuwakilisha hali waliyokwisha isoma. Igizo dhima hilo si lazima liwe ni uigizaji wa moja kwa moja wa hadithi yao bali tafsiri ya hadithi hiyo. Kama utaamua kuruka hatua hii, nenda moja kwa moja kwenye hoja ya 5 ya majadiliano.
4. Mara baada ya vikundi kujadili na kutayarisha maigizo dhima yao, kusanya vikundi vyote pamoja kuonyesha kazi zao na jadili uwasilishaji wao.
5. Tumia maswali yaliyopo hapa chini kuhusu hadithi. Wakati wa kupitia maswali, toa muhtasari wa majibu ya maswali ya washiriki na andika kwenye chatipindu ili washiriki wapate taswira ya kujifunza kwao. Unaweza pia kutumia mbinu za kadi au ramani za akili kuwasilisha hitimisho za vikundi na ili waweze pia kujifunza kutoka miongoni mwao.
   - Je, ni nani wahusika wakuu na uhusiano wao ulikuwaje?
   - Je, tukio kuu lilikuwa nini au hali katika hadithi? Nini kimesababisha hali hiyo?
   - Je, ni haki za nani zinazokiukwa? Je, haki za nani zinatimizwa? Je, watu wanaheshimiana? Je, watu wanachukua wajibu wao wenyewe na wa wengine? Je, wanalinda haki za watu wengine?
   - Je, hali za sasa zinaweza kutanzuliwa kimaadili?
   - Je, hadithi ilifunza nini na inaweza kuhusiana vipi na maisha yetu wenyewe?

Washawishi washiriki wajitolee kueleza uzoefu binafsi kuongeza kwenye majadiliano.

Hitimisha shughuli kwa kutafakari namna matendo yetu na mitazamo inavyoweza kuathiri watu wengine, ama kwa uzuri au ubaya.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Hadithi kwa ajili ya nafsi

**Madhumuni:** Kuwasaidia washiriki kuchunguza mitazamo na unyofu unaohitajika kubadili hali ngumu.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wametafakari kuhusu mitazamo na unyofu unaohitajika kuleta heshima, uelewano na amani kwa jamii zao.

**Vifaa vya kufundishia**: Chagua hadithi zinazofaa kuhusu heshima, kuwasaidia wengine, upatanishi, msamaha n.k. kutoka ukurasa 123 wa Nyenzo/Hadithi. Unaweza kuchagua kutumia hadithi moja tu au hadithi mbili au nyingi. Jaribu kuchagua hadithi zenye urefu unaolingana lakini zenye dhamira tofauti. Chatipindu na kalamu za kuchorea vinahitajiwa na mwezeshaji.

## Shughuli

1. Wagawe washiriki katika vikundi vidogo vya watu watatu hadi watano na wape kila kikundi nakala ya hadithi.
2. Waambie kila kikundi wasome hadithi yao, wajadili ujumbe wake na mafunzo ya kiuadilifu.
3. Halafu ama tayarisha maigizo dhima yatakayowakilisha hadithi bila ya kulazimika kurudia kuigiza, au endelea hadi hoja ya 5.
4. Vikusanye vikundi vyote kwa ajili ya maigizo dhima yatakayoigizwa. Hitimisha kwa majadiliano.
5. Tumia maswali yaliyoandikwa hapa chini kuhimiza majadiliano kuhusu hadithi. Wakati wa kupitia maswali, toa muhtasari wa majibu ya maswali ya washiriki na andika kwenye chatipindu ili washiriki wapate taswira ya kujifunza kwao. Unaweza pia kutumia mbinu za kadi au ramani za akili kuwakilisha hitimisho za vikundi na ili pia waweze kujifunza kwa kutoka miongoni mwao.
   > Je, hadithi imewafundisha nini na itakuwa na maana gani kwa maisha yetu?
   > Je, ni aina gani za unyofu zilizoonyeshwa kwenye hadithi?
   > Je, tunaweza kuhusisha hadithi hii na hali ya maisha halisi? Toa baadhi ya mifano.

Washawishi washiriki wajitolee kueleza uzoefu binafsi kuongeza kwenye majadiliano.

Hitimisha shughuli kwa kutafakari namna mafundisho kutoka kwenye hadithi au maandiko matakatifu yanavyoweza kuwa muhimu kwa maisha yetu. Washawishi washiriki wafikirie kuhusu namna matendo yetu na mitazamo inavyoweza kuathiri watu wengine, ama kwa uzuri au ubaya.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Kutamba Hadithi

**Madhumuni:** Kukuza stadi za kusikiliza na kuhusisha kila mmoja kwa kuingia kwa pamoja kwenye ulimwengu wa hadithi.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wamekuza hisia ya kukaribisha ubunifu na kukuza uwezo wao wa kusikiliza. Watakuwa wamefurahia urithi wa utamaduni uliofikishwa kupitia hadithi.

**Vifaa vya kufundishia:** Chagua hadithi zinazofaa kutoka kwenye Nyenzo/Hadithi, uk 123. Pia unaweza kuchagua hadithi za jadi kutoka kwenye utamaduni wako au kutoka mila na desturi za dini. Weka hali na mazingira ya furaha na burudani.

Miongozo ifuatayo imechukuliwa kutoka *Kiongozi kwa ajili ya Watamba Hadithi.*[1]

## Shughuli

Weka mazingira yanayofaa kwa ajili ya kutamba hadithi. Inaweza kuwa kuzunguka moto mkubwa, bustani au hifadhi karibu na maumbile asilia au mahali patulivu. Unaweza kutumia mishumaa, udi, vifaa kama vile gitaa na ngoma, au muziki mwororo kuanzisha kutamba hadithi.

Wakati mwingine muhtasari mfupi wa taarifa ya historia ni muhimu kuelewa hadithi. Daima eleza chanzo cha hadithi yako: mtambaji hadithi mwingine; kitabu, n.k.

Unaweza kuwa na kifungu cha kutambulisha au kufunga hadithi. Kwa mfano, kutambulisha hadithi, onyesho linatayarishwa kwa ajili ya kutambwa kwa mila na desturi ya Wenyeji wa Karibea:



Mtambaji: Paukwa

Hadhira inajibu: Pakawa ( tunataka kusikia hadithi yako).

Mwisho waweza kuwa: Hadithi yangu inaishia hapo. Huu ndio mwisho wa hadithi.

Hadithi pia inaweza kuanza kwa maneno ya mvuto. "Hapo zamani za kale." Kwa Kiarabu utambaji wa hadithi mara nyingi unaanza kwa kusema: *Ken ye me ken*, "ilikuwa na haikuwa" na kila mtu anajua kwamba wakati wa hadithi umewadia. Au wakati baadhi ya watu wa Irani wanapotamba hadithi, wanaanza kwa kusema, *Yeki bud, yeki nabud,* "Kulikuwapo na mtu, hapakuwa na mtu".

Hakikisha unaangalia hadhira yako. Kuwa makini kama watoto si watulivu. Kama hadithi haivutii sana utakuwa umekosea aina ya hadithi kulingana na kikundi. Kama itatokea hivyo, fikiria kuhitimisha hadithi na kuimaliza haraka. Unaweza kutafuta pia mahali pazuri pa kusimama na kupendekeza kuwa watoto wangependa kujua namna hadithi ilivyoishia kwa kusoma kitabu.

Kama watoto hawana uhakika na maana ya baadhi ya maneno, jaribu kuingiza maana kwa muhtasari kwenye hadithi. Kama kikundi chote si kitulivu, usikasirishwe nao. Epuka hali kwamba muda wa utambaji hadithi sasa unabadilika kuwa uzoefu usiopendeza kwa wote. Chambua tatizo. Inawezekana hadithi yako haifai kwa hadhira au hadithi inaweza kuwa ndefu mno na inayochosha. Mazingira ya nje yanaweza kuingilia uwezo wa watoto kumakinika.

Kimori au vazi maalumu la kutambia hadithi linaweza kuwafurahisha watoto wadogo. Kimori au vazi la seremala lenye mifuko litafaa. Katika kila mfuko kunawekwa kitu kimoja kinachowakilisha hadithi, kama kokwa kwenye Supu ya Kokwa. Mtoto anachagua mfuko na hadithi inatambwa. Nguzo chache rahisi zinaweza kutumika. Hata hivyo usiruhusu nguzo hizo kukengeusha hadithi.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

1 Inez Ramsey, Profesa Emeritus James Madison.University http://falcon.jmu.edu/- ramsey /storyhandbook.htm

# Hali ya uonevu

**Madhumuni:** Kuwavutia washiriki kujifunza zaidi na kutafakari kuhusu uonevu duniani.

**Matokeo:** Washiriki kuhoji sababu za uonevu duniani na watakavyoweza kufanya kusaidia.

**Vifaa vya Kufundishia:** Taswira za aina nyingi za hali za uonevu duniani (tabia za kutoheshimu watu, mateso ya watu, taswira za umaskini, taswira za migogoro zilizochukuliwa kutoka kwenye magazeti, majarida, mabango, n.k. Uwasilishaji mada kwa projekta (Power Point) unaweza pia kutumika. Tovuti za AZISE kwa kawaida huwa na picha nyingi zinazofaa zinazoweza kupakuliwa.

## Shughuli

Bandika baadhi ya taswira mbalimbali ukutani au sakafuni halafu waambie washiriki wazunguke kwenye chumba kuangalia taswira hizo. Halafu warudi kukaa kwa mduara ili picha ziweze kuendelea kuonekana.

Waambie washiriki wajadili walichohisi wakati walipoangalia taswira.

> Waulize ni taswira ipi iliyovuta uzingativu wao zaidi na kwa nini.

> Waambie baadhi yao kuzungumzia kile wanachodhani kuwa kinatokea kwenye taswira waliyochagua:

  > Kungeweza kutokea nini?

  > Ni nani aliyefanya hivyo?

  > Kwa nini ilitokea?

  > Kwa nini watu hao wanaonyesha hali hiyo nyusoni kwao?

  > Wanaweza kuwa wanafikiria na kuhisi nini?

  > Hivi sasa wanaweza kupatwa na nani?

Washiriki wanaweza kuwa na maswali mengi na hoja kuhusu baadhi ya hali zilizoonyeshwa kwenye picha na ni muhimu kwamba hawaondoki kwenye kipindi kwa kuhisi hawana msaada na mamlaka na hata kufadhaishwa.

Fanya kipindi kielekee mwisho kwa kuwauliza maswali washiriki yatakayowasaidia kuwaelewa wengine:

> Kwa nini watu wanasononeshana?

> Kwa nini watu hawaheshimu maisha, imani na mawazo ya watu wengine?

> Ni nini kinachosababisha chuki, uonevu na ugomvi duniani?

> Je, mashirika ya kidini na kiserikali yana nafasi gani katika matukio ya ugomvi au uonevu?

> Je, dini zinachangia nini katika amani?

> Je, washiriki watafanya nini hapa mjini/kijijini kwao, kuwasaidia wengine na kujaribu kufanya ulimwengu kuwa mahali pazuri zaidi?

Inawezekana kukawa na mapendekezo mengi ya aina mbalimbali kwa swali hili la mwisho kutaka kuwasaidia wanaotafuta hifadhi au wale ambao wako “nje” ya kitovu cha watu hadi kuombea dunia, kuiongeza uelewa au kuandika barua kwa bunge lao, waziri mkuu waon n.k. Ni muhimu kuwahimiza washiriki wafikirie kuhusu hatua watakazochukua.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Kuchora Ramani

**Madhumuni:** Kuwafanya watu wapende ulimwengu na utajiri wake kwa kuwaonyesha utamaduni na dini zinazofuatwa katika sehemu mbalimbali za dunia.

**Matokeo:** Washiriki kuwa na uelewa mzuri zaidi kuhusu dini na utamaduni mbalimbali na umuhimu wa kujifunza kuhusu uanuwai.

**Vifaa vya kufundishia:** Ramani kubwa ya dunia, tufe, au ukishindwa kuvipata, mchoro wa ramani ya dunia. Mahali pa kuning'inizia, lebo ndogo, pini za kubandikia, vyote vinaweza kuwa muhimu kubandikia maoni na maelezo kwenye ramani.

## Shughuli

Wagawe washiriki katika vikundi vya watu 3 au 4 na waambie kila kikundi waonyeshe kwenye ramani angalau nchi nane zinazowakilisha angalau dini tofauti.

Wape washiriki dakika 15 kujadili kwenye vikundi vyao na dakika 5 zaidi kuandika majibu yao kwenye ramani.

Mwache kila mtu aangalie ramani na washiriki kushirikiana maarifa yao.

Dadisi majibu yao kwa kuwauliza washiriki kuhusu makabila madogo yanayofuata dini tofauti kwenye nchi walizochagua.

Unaweza kuhitimisha kipindi kwa kuwauliza maswali baadhi au maswali haya yote ya jumla:



> Je duniani kuna dini gani? Tayarisha orodha na kuangalia ni dini ngapi zimetajwa.
> Kwa kuwianisha, ni watu wangapi wanafuata kila moja ya dini ulizoorodhesha ?
> Je, ni dini gani imeenea zaidi nchini kwako? Jijini kwako? Shuleni kwako? Je, kuna dini nyingine zinazofuatwa huko pia? Je, una uzoefu gani kwa wale wanaofuata dini zingine?
> Je, wale wanaofuata dini tofauti nchini kwako, jijini, shuleni, wanakabiliwa na matatizo kutokana na imani zao? Je, kuna chuki au ubaguzi? Kama ni hivyo, kwa nini unadhani ni hivyo? Je, kuna jambo lolote tunaloweza kufanya ili kupunguza kutovumiliana na kukosekana kwa kuheshimiana?
> Je, wale wasio na dini au wasiofuata dini yoyote inakuwaje? Je, kuna chuki au ubaguzi dhidi yao? Jadili.
> Washiriki wanaweza kutoa mapendekezo thabiti – ziara ya baina ya dini mbalimbali, usiku wa shughuli za utamaduni au ziara ya ugani – ambayo yanaweza kufuatiliwa.

Kama majibu ya maswali mengi hayafahamiki, zingatia maswali makuu yanayojitokeza, ili kila mmoja, wakiwemo washiriki, anaweza kufanya utafiti kwenye maktaba au katika Intaneti, na kuarifu kikundi kuhusu matokeo ya utafiti wakati wa kipindi kifuatacho.

Itafaa zaidi kama utaonyesha video/DVD inayohusu dini tofauti, au wasilisha mada inayoonyesha majina ya dini tofauti, waasisi wao, imani zao kuu na mila na desturi (kwa mfano, mavazi, ibada na maandiko matakatifu).

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Kufikia Nyota

**Madhumuni:** Kuwawezesha washiriki kugundua wengine ni kina nani, je wanafanana au kutofautianaje na wao wenyewe?

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wamefahamu namna watu wengine walio tofauti wanavyoweza pia kufanana sana. Washiriki watajikubali na kuwakubali wengine kwa kuona upande wao wa ndani na nje.

**Vifaa vya Kufundishia:** Kalamu na karatasi, vireli au mabunda mengi ya nyuzi za rangi, gundi ya nailoni, mikasi mingi.

## Shughuli

1. Kila mshiriki achore nyota yenye ncha tano – wape mfano au nakala wanakili ili nyota zote zifanane. Waulize washiriki ni taarifa ya aina gani ni muhimu kwa utambulisho wao na chagua maswali matano kutoka kwenye orodha. Waambie waandike kwenye kila ncha majibu ya maswali hayo. Kwa mfano, dini yao, muziki waupendao, mahali penye umuhimu zaidi kwao, mtu muhimu zaidi kwao, shughuli waipendayo zaidi. Unaweza kuchagua maswali ya aina nyingine kulingana na muundo wa kikundi.
2. Wakimaliza kuandika kwenye nyota yao, wakae kwenye mduara na kila mmoja aeleze chaguo lake. Waambie washiriki wabandike nyota yao ukutani. Mpe kila mshiriki bunda la uzi wa rangi watakalotumia kuhusisha ncha za nyota zao na ncha za nyota za wengine zinazoeleza uchaguzi unaofanana.
3. Kila mtu hana budi kujaribu kutafuta angalau mfanano wa aina moja ama na mtu aliyewasilisha mwanzo au mtu mwingine yeyote aliyetangulia. Wewe au mwezeshaji mwenza hana budi kuanza ili kila mwezeshaji aweze kutafuta angalau mfanano mmoja.
4. Baada ya uhusishaji wote kukamilika, waambie washiriki waende kutafuta taarifa zaidi kuhusu wachoraji wa nyota zinazohusishwa. Kwa kufanya mazungumzo ya muda mfupi wanaweza kugundua mifano zaidi na watu hawa, lakini wanaweza kugundua pia baadhi ya tofauti. Kwa mfano, sote tunapenda chakula cha Kihindi, napenda kucheza kandanda lakini yeye hapendi, anapenda kupika lakini, mimi sipendi, sote tunatoka sehemu moja ya jiji, n.k.
5. Angalia ni ncha ngapi za nyota zisizohusishwa – je, shauku au mapenzi haya ni ya pekee kwa watu mahususi? Onyesha namna inavyostaajabisha kuona kuwa kuna uanuwai mkubwa na utajiri duniani. Kama ilivyo kwamba, nyota zinaweza kufanana, tunajua pia kuwa zote zinatofautiana, ni ajabu iliyoje!
6. Waambie washiriki wazungumzie kuhusu mtu waliyekutana naye wakieleza ni mambo gani yanayolingana na walichoona ni tofauti.
7. Mwisho, fanya majadiliano ya kina kuhusu jambo linalotufanya kila mmoja wetu awe wa pekee. Sisitiza kuwa watu wote wana mambo yanayofanana, lakini wanatofautiana katika mambo muhimu. Hitimisha kipindi kwa kuzungumzia umuhimu wa kuwaona watu wengine kutoka ndani kuliko nje tu.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Ninachotetea

**Madhumuni:** Kuwawezesha washiriki kutetea kile wanachokiamini. Kuwawezesha washiriki kutafakari kuhusu imani zao wenyewe na kugundua imani za watu wengine.

**Matokeo:** Washiriki wawe wamegundua namna imani na mawazo yao yanavyotofautiana na yale ya watu wengine.

**Vifaa vya Kufundishia**: Vifaa vya kufundishia vinavyofaa ndivyo vinavyotakiwa kugawa chumba au kiwanja cha michezo katikati, kwa mstari, k.m chaki, gundi ya nailoni, jora la kitambaa. Mabango mawili makubwa yaliyoandikwa. “Nakubaliana” na “Sikubaliani”.

## Shughuli

Chora mstari katikati ya chumba na weka mabango hayo mawili kila upande wa chumba. Waambie washiriki wajipange kwenye mstari wa katikati wakikuelekea wewe. Waambie wajibu mfululizo wa maswali kwa kwenda kwenye bango wanalochagua.

Soma kauli chache – ifuatayo ni baadhi ya mifano:

> Watoto wote hawana budi kwenda shule.
> Ni wale werevu zaidi ndio wenye haki ya kupata elimu baada ya umri wa miaka 14.
> Kumwua mtu kwa sababu yoyote ile ni kosa.
> Watu wana haki kutetea wanachokiamini.
> Kila mmoja ana haki ya kuishi kwa amani.
> Hakuna atakayeishi chini ya uvamizi wa nchi nyingine.
> Kila mtu ana haki ya kuheshimiwa.
> Nawaheshimu wale tu wanaoniheshimu.
> Uchafuzi wa mazingira ni wajibu wa Serikali.
> Kwa kawaida hakuna haja ya kutupa taka kwenye pipa wakati watu wengine hawafanyi hivyo.
> Kila mtu anayo haki ya kufuata dini yake.
> Dini ndiyo kiini kikubwa cha migogoro duniani.

Maswali haya yametayarishwa ili kuwafanya washiriki wajikute wamebabaika na kukosa msimamo, hali hiyo inahimiza majadiliano. Baada ya kushughulikia kauli zako, waambie washiriki wakae katika mduara na waambie baadhi yao wazungumzie kuhusu majibu yao. Jadili baadhi ya masuala ambayo wameyaona yana makabiliano na hali hiyo imewafanya wahisi vipi.

Kama washiriki walipata tabu sana katika kujibu maswali hayo, waulize kwa nini walihisi hivyo. Hoja muhimu itakayotokana na majadiliano ni kwamba ulimwengu si kitu rahisi na kwa kawaida si rahisi kuamua tu cha kuamini na wakati gani wa kuchukua msimamo.

Waulize washiriki kuhusu walivyojihisi wakati watu wengine wanaposimama upande wa pili wa mstari. Je, walijihisi vipi kuhusu watu hao na imani zao?

Hitimisha zoezi hili kwa kusisitiza namna imani na maoni ya watu yanavyotofautiana na namna imani na maoni ya watu yanavyotakiwa yaheshimiwe, hata kama hayafanani na yetu.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Miduara ya Kupiga Ngoma

**Madhumuni**: Kuunda nafasi na fursa ya uhusiano kati ya washiriki kupitia uzoefu wa pamoja katika mazingira tofauti.

**Matokeo:** Washiriki wawe wamehusiana miongoni mwao kwa njia tofauti na kwa urafiki wa ndani zaidi, na wamejifunza zaidi kuhusu maisha ya kila mmoja wao.

**Vifaa vya Kufundishia:** Ngoma nyingi mbalimbali, kuni, vibiriti na vitu vya kuwaka. Unaweza kupata maelekezo ya namna ya kuwasha moto kwa kambi kwenye http://www.luontoon.h/page.asp sehemu= 8497

## Shughuli

Tayarisha moto wa kambi na panga baadhi ya ngoma. Wakusanye washiriki kuzunguka moto halafu gawa ngoma. Kama tayari kuna washiriki wanaojua kupiga ngoma, waruhusu waanze kupiga. Jaribu kupanga shughuli ya kupiga ngoma itakayomwezesha kila mtu au watu wengi kadiri iwezekanavyo kujiunga. Lengo ni kuwawezesha washiriki waone na kuzoea msisimko wa kupata mdundo wa ngoma pamoja. Kila mtu akishapata muda wa kufurahi na kujipumzisha, weka mazingira ya kuzungumza.

Wahimize washiriki wazungumze kila kitu kinachowajia akilini mwao. Fanya hii kuwa nafasi ya kujifunza miongoni mwao na kugundua undani wa kila mmoja.

Toa maana ya muziki, moto, usiku ule na kwa kila anayeshiriki katika shughuli hiyo. Jadili vipengele vinavyofanya wakati huu kuwa wa pekee. Jadili zaidi dhamira hiyo kwa kufikiria watu wote wasio wa kawaida ambao ni sehemu ya binadamu na wanaishi katika ulimwengu wa wote.

Miduara ya kupiga ngoma inaweza kuwa nafasi ya upendo na kama muda wa kutafakari, kwa binafsi na kwa wengi, kuhusu namna watu wanavyoweza kushirikiana kwa ajili ya amani. Washiriki wanashirikiana kwa pamoja na kujifunza zaidi kuhusu wao wenyewe na miongoni mwao na kuunda mifungamano itakayofaa kwa kufanya kazi pamoja.

Kama ikiwezekana, fanya mduara wa kupiga ngoma kwa tukio maalumu kila mwezi.

Miduara ya kupiga ngoma inaweza kutumika pamoja na shughuli zifuatazo:

- Kutamba hadithi.
- Kuimba na kucheza.
- Kutaamali na kutafakari.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Ziara za Dini Mbalimbali

**Madhumuni:** Kupata uzoefu wa vyanzo vingine vya mambo ya kiroho na kujifunza kuhusu dini nyingine kupitia ziara ya mafunzo kwenye maeneo mbalimbali ya dini, kama vile: mahekalu, misikiti, masinagogi, makanisa na misikiti ya singasinga.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wamepanua uelewa wao kuhusu imani, ibada na hisia za kiroho za dini zingine.

**Vifaa vya Kufundishia:** Wagawie washiriki karatasi kubwa za taarifa kuhusu dini watakazojifunza. Hawana budi pia kuandika maelezo yanayohusu mahali walikotembelea.

## Shughuli

Washiriki wanatembelea mahali mbalimbali pa ibada. Ziara hizo hazina budi kupangwa katika makundi ya safari ya siku chache, wiki au hata muda mrefu zaidi. Bila ya kujali aina ya dini ya washiriki ama kama hawaamini dini yoyote, kila mtu anaweza kunufaika kutokana na uzoefu mpya na pengine wa pekee wa kujifikiria kuwa katika nafasi ya mtu mwingine.

Maeneo ya ibada yanaweza kutembelewa ama wakati yanapokuwa wazi kwa watu wote au wakati ibada inapofanyika. Kwa hali yoyote iwayo, ni bora kupanga ziara yako kwa kuwasiliana na mhudumu wa mahali pa ibada. Ni muhimu kukutana na mtu atakayepanga ziara ili uweze kueleza programu ya dini mbalimbali na madhumuni ya ziara. Mwarifu mwenyeji wako kwamba, kulingana na kusudi la ziara, programu haina budi kutoa taarifa ya ufafanuzi zaidi kuliko ile ambayo ni ya uhimizaji au linganishi. Kwa mfano, ziara hiyo inaweza kujumuisha:



> Mazungumzo yanayofanywa na mmojawapo wa mahali pa ibada kuhusu imani ya msingi ya dini hiyo.
> Maelezo ya ibada mbalimbali mahali hapo pa ibada na umuhimu wa ibada hizo.
> Fursa ya kikundi chako kuuliza maswali.
> Fursa ya kuzungumza na vijana wanaosali mahali hapo pa ibada.
> Fursa, kama ikiwezekana kuona jinsi ibada inavyoendeshwa.
> Kama inafaa, mwombe mmojawapo wa wenyeji wako kuendesha sala kwa utaratibu wa dini yake.

Kabla ya ziara, waarifu washiriki madhumuni ya ziara: kujifunza kuhusu dini nyingine. Pia sisitiza haja ya kuheshimu kanuni ya mavazi yanayofaa mahali patakapotembelewa na kutii inavyopasa.

Toa muda wa majadiliano na washiriki baada ya kila ziara na kuendelea. Wahimize wote wazungumzie kuhusu walichojifunza na namna kujifunza huko kunavyolinganishwa na dini yao au na dini nyingine waliyojifunza. Jadili kuhusu walichokiona walipokuwa mahali hapo pa ibada na namna walivyohisi.

Logu ya Kujifunza ya washiriki haina budi kuandika kwa mfano:

> Mahali pa ibada, ikiwemo jina la mahali.
> Waliyekutana naye na walichojifunza.
> Hisia zao kuu kuhusu jengo na namna ya kuabudu.
> Imani kuu ya watu wa dini ile.
> Mfanano na tofauti za kile mtu anachoamini – kama mtu anafuata taratibu za kidini au hapana.

## Mwongozo wa Kuandaa Ziara za dini mbalimbali

1. Pata taarifa kuhusu mahali pa ibada unakotaka washiriki watembelee. Zingatia imani za dini za washiriki, kwa hiyo unawajumuisha kwenye ziara. Jadili chaguo lako la mahali pamoja na washiriki.
2. Tayarisha orodha ya mahali pa ibada na panga namna inavyowezekana kutembelea maeneo hayo yote wakati unapoamua kufanya shughuli hiyo. Kumbuka kutenga muda wa kutosha kwa ajili ya kutembelea kila mahali pa ibada na panga kwa wakati utakavyotoka sehemu moja kwenda nyingine.
3. Wasiliana na mhusika wa kila mahali pa ibada unapotaka kutembelea. Eleza madhumuni ya ziara yenu na umuhimu wa kujua na kujifunza kuhusu imani za watu wengine. Hakikisha kwamba taarifa wanayopewa washiriki kila mahali inaeleweka na inatolewa katika mazingira ya kuheshimu dini nyingine.
4. Eleza hali ya dini mbalimbali ya kikundi, bila ya kujali kikundi kinajumuisha vijana kutoka dini mbalimbali au kikundi cha dini moja katika mchakato wa kujifunza na kuheshimu dini nyigine.
5. Kubaliana kuhusu siku na muda wa ziara na mtu atakayewapokea washiriki. Panga na mtu huyo kuhusu aina ya ziara, kama itakuwa wakati wa ibada, namna washiriki watakiwavyo kuvaa na kama watatoa vinywaji vyovyote. Uliza kama inawezekana kupanga ushiriki wa watoto wengine au vijana wa mahali pa ibada.
6. Kama inawezekana, tayarisha brosha kwa ajili ya washiriki kuhusu dini utakazojifunza wakati wa ziara.
7. Waarifu washiriki kuhusu namna wanavyotakiwa kuvaa.
8. Fanya mkutano wa maandalizi na washiriki kabla ya ziara. Waambie waandae maswali na kuiona hiyo sehemu na kila kitu nje na ndani. Katika mkutano wa maandalizi, fanya majadiliano kuhusu dini na waambie baadhi ya washiriki waeleze washiriki wengine kuhusu dini yao wenyewe. Waambie washiriki kuhusu umuhimu wa kuwa mwenye heshima na kuwa tayari kupokea ushauri.
9. Wakati wa ziara, waambie washiriki wavinjari hiyo sehemu na wapange muda wa kuuliza maswali kabla ya kuondoka.
10. Baada ya ziara waambie washiriki waandike uzoefu wao na hisia zao na wapate muda wa pamoja wa kupeana muhtasari. Sisitiza umuhimu wa kujifunza kuhusu imani za watu wengine pamoja na zetu wenyewe.

# Linganisha

**Madhumuni:** Kutafuta tofauti na mfanano kati ya sehemu mbalimbali, dini, utamaduni na imani. Shughuli hii inaweza kutumiwa kwa manufaa zaidi kabla (au kama ni lazima, badala ya ) ziara ya Dini mbalimbali.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wameimarisha maarifa yao kuhusu uanuwai duniani na kushawishi kujifunza zaidi kuhusu imani na ibada za dini za watu wengine.

**Vifaa vya Kufundishia:** Vifaa vinavyoeleza dini mbalimbali na ibada za dini.

## Shughuli

> Kama haiwezekani kupanga ziara ya dini mbalimbali – au pengine katika matayarisho ya ziara mbalimbali – tayarisha maonyesho na uwasilishaji wa dini nyingine. Jumuisha picha, taswira, maneno au vitu halisi (sanaa) vinavyoweza kueleza dini mbalimbali na ibada za dini duniani. Kama unaweza, changanya shughuli hii na video kuhusu dini mbalimbali.
Hakikisha kuwa taarifa yako inatoa maelezo ya namna watu wanavyovaa, wanachofanya, wanakokwenda, nani wanamwabudu, na wasichofanya.

> Baada ya uwasilishaji, wagawe washiriki katika vikundi vidogo na waambie wabainishe angalau tofauti tano na mifanano mitano miongoni mwa mila na desturi walizojifunza.

> Malizia shughuli kwa kutafakari kuhusu namna ulimwengu ulivyo tofauti na ulivyo na mambo anuwai, namna watu wanaoishi duniani wanavyotofautiana na walivyo anuwai na jinsi ilivyo muhimu na lazima kujifunza kuhusu imani za watu wengine na kuweza kuzielewa.

Zingatia: Hakikisha kwamba wakati wote wa shughuli heshima kwa ibada za dini mbalimbali inadumishwa.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

## Maelezo yangu

# Shughuli za Utamaduni za jioni

**Madhumuni:** Kuweka fursa kwa washiriki kushirikiana utamaduni na desturi zao mbalimbali.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wanaelewa utamaduni mbalimbali na hivyo kugundua mambo mengi zaidi kuhusu wao wenyewe kuhusiana na wengine.

**Vifaa vya Kufundishia**: Mahali panapofaa kwa uwasilishaji wa utamaduni mbalimbali, panapoweza kuwekwa maonyesho ya vielelezo, uwasilishaji wa mada, muziki na kucheza ngoma, vinywaji na vitu vingine.

## Shughuli

Usiku wa shughuli za Utamaduni ni fursa nzuri ya kushirikishana na kuelewa mila na desturi au dini ya nchi nyingine. Usiku huo unaweza kujumuisha vyakula vya asili, mavazi, muziki na kucheza ngoma pamoja na maonyesho yanayoonyesha taarifa za kijiografia, kiutamaduni, kidini na kiuchumi za nchi. Unaweza ama kupanga usiku wa namna hiyo mara nyingi na kujifunza utamaduni mmoja kwa tukio au kuwa na usiku mmoja tu ambapo vikundi vyote vya utamaduni vinawasilishwa. Fikiria kama unaweza kujumuisha tukio maalumu la utamaduni kama vile wanamuziki au wacheza ngoma maarufu kwa nchi hiyo au dini inayowasilishwa.

Hii ni fursa itakayowawezesha washiriki wako vijana kuchukua wajibu wa kupanga na kuendesha tukio, maadamu tukio hili liwe linahusu utamaduni na maisha yao. Hawana budi kuamua na kupanga vipengele vyote vya programu. Hakikisha mahudhurio mazuri kwa kupeleka mialiko mapema zaidi kwa familia na marafiki na viongozi wa maeneo.

Kama washiriki watakabiliwa na matatizo katika kupata vifaa vinavyohitajika kwa usiku huo, washauri wawasiliane na ofisi za ubalozi na hoteli, zinazoweza kudhamini usiku huo. Ofisi za ubalozi zinaweza kutoa taarifa, ramani na brosha wakati hoteli zinaweza kutoa vyakula vya kiasili kama lengo la shughuli za utamaduni za usiku huo zitaelezwa mapema.

Kama unasheherekea tamaduni za aina mbalimbali katika usiku mmoja, pendekeza wazo la kuwa na "maduka ya vikorokoro" ambapo kila nchi inawakilishwa na kibanda. Wageni wataweza kutembea kutoka kibanda kimoja hadi kingine na kuona vitu vya sanaa na vitu vingine vinavyoonyeshwa, wakati huo wakifurahia viburudisho na kusikiliza muziki wa tamaduni mbalimbali.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Ziara za Ugani

**Madhumuni:** Kuweka fursa kwa washiriki kutembelea mahali ambapo hawajawahi kutembelea kabla, kukutana na watu ambao wasingeweza kukutana nao. Wanachokiona na kujifunza kitakuwa na athari muhimu sana kwa wanavyouelewa ulimwengu.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wameelewa jumuiya iliyo tofauti na ile yao. Watakuwa wameelewa namna jumuiya hiyo inavyofanya kazi ya kuboresha maisha ya wakazi. Pia watakuwa wamebainisha namna haja ya kufanya mabadiliko katika jumuiya hii, kuhusu aina ya msaada utakaohitajika, msaada huo utatoka wapi na jinsi wao wenyewe watakavyokuwa chachu ya mabadiliko.

**Vifaa vya kufundishia**: Panga ziara kwenye jumuiya ambayo ni tofauti na haifahamiki kwa washiriki wengi katika kikundi. Pengine mahali hapo ni tofauti kijamii na kiuchumi, panakaliwa na kabila tofauti kabisa au ni mbali sana, na hata katika nchi tofauti. Ziara hiyo inaweza kuhitaji saa chache, siku nzima, usiku mmoja au kukaa na kulala siku moja.

Ni muhimu kupanga na kuandaa vizuri ziara hiyo, hasa kushirikiana na asasi ya eneo husika. Ama liwe ni tukio la kijamii, "onyesho" au mkusanyiko wa vijana kushiriki kwenye shughuli, usilenge tu katika maisha ya sasa ya jumuiya bali pia kwenye uzoefu uliopita na mabadiliko yaliyofanywa na watu wake kuboresha maisha yao.

## Shughuli

Watayarishe washiriki kwa ziara kwa kuwahusisha katika maandalizi yake. Jadiliana nao mahali pa kwenda, watakutana na nani na watakachofanya pale.

Kama programu ni jumuishi, hakikisha kwamba washiriki wanajiandaa. Pengine washiriki wanaweza kufanya igizo, kupiga muziki au kuimba nyimbo au kuandaa michezo ya kucheza na watoto watakaowatembelea, kama itakuwa hivyo. Itakuwa rahisi zaidi kwa washiriki kushirikiana na jumuiya kama watafanya jambo fulani pamoja. Kama vijana wengine watakuwa kikundi mwenyeji na hivyo kuwa pamoja, pengine kufanya shughuli pamoja, halafu pande zote mbili wanaweza kujifunza mambo mapya kuhusu kila upande.

Kama ziara yako inawahusu watu walioleta mabadiliko na mageuzi kwa jumuiya, andaa jopo la majadiliano au mikutano ya majadiliano kuruhusu maswali na majibu.

Kama mwezeshaji, uwe mwangalifu kwa mitazamo inayojirudia miongoni mwa washiriki kwa jumuiya itakayotembelewa na kujaribu kuhakikisha kuwa programu hiyo inashughulikia mitazamo hiyo kwa njia nzuri.

Programu haina budi kupangwa kwa ukamilifu na mwezeshaji mwenza na kama ikiwezekana ziara ya maandalizi lazima iwe imefanywa ili uelewe madhumuni na programu ya ziara.

Baada ya ziara ya ugani, fanya majadiliano na washiriki yatakayowawezesha kutoa hisia zao, na mijibizo na namna zilivyobadilika kutokana na ziara hiyo.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Kujiweka Katika nafasi ya Mwingine

**Madhumuni:** Kujifunza chanzo cha migogoro na namna inavyoweza kutanzua hali za ugomvi. Shughuli inawasaidia washiriki kuchukua madhila ya watu wengine na kutafakari hali zao.

**Matokeo:** Washiriki wameelewa kwa nini watu wanafanya wanavyotenda katika hali mahususi na kutafuta chanzo cha upendeleo, chuki na migogoro. Washiriki wamechambua namna matendo yasiyo ya kimaadili yanavyoathiri vibaya jamii na kujadili namna wanavyoweza kubadili au kupunguza kiwango cha ugomvi kwenye mgogoro.

**Vifaa vya kufundishia:** Waruhusu washiriki kutoa hali zao wenyewe na kutumia kadi za kuchukua madhila ya mwingine zilizoko kwenye ukurasa 175 katika Nyenzo/Kujiweka katika nafasi ya mwingine. Pia unaweza kutayarisha hali zako mwenyewe kutokana na masuala ya matukio ya sasa. Tumia ama kadi moja ya kujiweka katika nafasi ya mwingine kwa washiriki wote au matukio mengine kwa msingi wa dhamira hiyo hiyo.

## Shughuli

Wagawe washiriki katika vikundi na waambie kila kikundi wafikirie kuhusu hali ya mgogoro au ugomvi waliowahi kuona au uliowahi kutokea shuleni kwao au jirani au miongoni mwa familia zao au marafiki. Himiza ubunifu wa washiriki kwa kuwapa mifano ya migogoro inayoweza kutokea kama vile ubaguzi shuleni, hali za ugomvi jirani kwao, matatizo kati ya wanafamilia au matatizo ya mshikamano wa jumuiya.

Waambie washiriki waigize mgogoro huo ili wawakilishe wakati ambapo umepamba moto hadi usababishe ugomvi. Wape muda wa kusoma na kufanya mazoezi ya michezo yao ya kuigiza kabla ya kuwasilisha mbele ya vikundi vingine.

Waambie washiriki pia wanatakiwa kutafuta ufumbuzi au namna ya kupunguza kiwango cha ugomvi katika hali zilizowasilishwa na vikundi vingine.

Baada ya kila hali kuigizwa na mgogoro kuongezeka, simamisha igizo kwa kusema "Poza" wakati huu waambie washiriki kutoka vikundi vingine wafikirie haraka namna ya kubadili hali hiyo au kupunguza kiwango cha ugomvi. Kama kuna mshiriki mwenye wazo, waambie wachukue nafasi ya mmojawapo wa waigizaji wanaodhani ataweza kusaidia kupunguza kiwango cha ugomvi kwenye mchezo wa kuigiza au kuigiza mwigizaji mpya. Rudia igizo dhima pamoja na ufumbuzi unaowezekana na himiza mawazo zaidi kutoka kwa washiriki wengine. Rudia mara mbili au tatu.

Fanya majadiliano mafupi baada ya kila ufumbuzi unaowezekana na kuwauliza washiriki:

- Je, huu ulikuwa ufumbuzi mzuri?
- Je, wale wote walioshiriki wameridhishwa kwamba haki imetolewa na italindwa?
- Je, inawezekana katika hali halisi?
- Je, ufumbuzi wa upande mmoja unawezekana au mwafaka ni muhimu (kiini cha igizo)?
- Je, kungetokea nini kama… (igiza mchochea mjadala kwa kuonyesha ila au kasoro ya kitu kuwahimiza wawe na fikira tunduizi).

Baada ya kuwasilisha maigizo dhima yote, tafakari namna matendo yasiyo ya kimaadili yanavyoharibu jamii na kuvunja uhusiano miongoni mwa watu. Jadili maana ya ushirikali na umuhimu wake; ushirikali unahusiana vipi na heshima na kuwaelewa wengine kunasaidiaje kuunda uhusiano mzuri?

**Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza kuhusiana na desturi, tabia na mienendo wanayoweza kufuata na kuleta haki zaidi na heshima kwa jamii zao.**

# Kutumia uchunguzi kifani

**Madhumuni:** Kuwawezesha washiriki kuchukua madhila ya mtu mwingine na kutafakari kuhusu hali yao.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wameelewa kwa nini watu wanatenda kama wanavyofanya katika hali mahususi. Washiriki wamechambua namna desturi zisizo za kimaadili zinavyokuwa na madhara kwa jamii. Washiriki watakuwa wameelewa kuhusu sababu za migogoro ya ugomvi na uonevu.

**Vifaa vya Kufundishia:** Tumia uchunguzi kifani katika ukurasa wa 138, Nyenzo/Uchunguzi Kifani au tayarisha wako mwenyewe kwa kutumia masuala ya matukio ya sasa. Tumia ama uchunguzi kifani mmoja kwa washiriki wote au uchunguzi kifani mwingi unaohusu dhamira moja.

Zingatia: Uchunguzi kifani wote umezingatia hali zinazoathiri makundi madogo au kuchochea desturi zisizo za kimaadili miongoni mwa vijana. Uchunguzi kifani unahitaji kuonyesha dhamira hii.

## Shughuli

Wagawe washiriki katika vikundi vya watu wanne hadi sita na wapatie kila kikundi uchunguzi kifani na maswali machache yatakayosaidia majadiliano yao:

- Kunatokea nini katika uchunguzi kifani?
- Waathirika ni kina nani?
- Je, kifanyike nini kuwasaidia?

Vipe muda vikundi kusoma uchunguzi kifani.

Fanya majadiliano ya wote pamoja. Zungumza kuhusu uchunguzi kifani. Je, matokeo mabaya ya uchunguzi kifani yanaweza kuepukwaje?

- Kama ningekuwa katika hali hiyo ningehisi namna gani?
- Je, ningefanya nini?
- Je, watu walipungukiwa na nini?

Baada ya kumalizika majadiliano, tafakari kuhusu namna desturi zisizo za kimaadili zinavyoharibu jamii na kuvunja uhusiano miongoni mwa watu.

Tambulisha maana ya ushirikali na jadili umuhimu wake. Je, ushirikali unahusianaje na heshima na kuwaelewa watu wengine kunasaidiaje watu wengine kuunda uhusiano bora zaidi?

**Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza kuhusiana na desturi, tabia na mienendo wanayoweza kufuata na kuleta haki zaidi na heshima kwa jamii yao.**

# Benki ya Kimaadili

**Madhumuni:** Kuwasaidia washiriki kutafuta ufumbuzi wa chuki, kukosa uvumilivu na uonevu, kwa kutumia "benki" kama sitiari.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wametafuta namna ya kuhimiza heshima katika jamii zao na kuelewa namna maelewano ya pande mbili yanavyosaidia kukuza mtaji wa kijamii.

**Vifaa vya Kufundishia:** Boksi kuwakilisha benki. Benki pia inaweza kuwakilishwa na "ubao wa waraka mizania" – karatasi kubwa inayoonyesha uchukuaji na uingizaji wa fedha (mapato na matumizi). Tayarisha karatasi yenye rangi moja kuwakilisha "Kutoa" na karatasi ya rangi nyingine kwa ajili ya "Hundi".

## Istilahi

Kutoa – haya ni 'matatizo' yaliyobainishwa.

Hundi – ufumbuzi wa 'matatizo' yanayoweza kuwekwa benki.

Ubao wa waraka mizania – ubao wa matangazo ambapo 'kutoa' kunaorodheshwa upande wa kushoto na 'hundi' zinawekwa upande wa kulia, mpaka ubao utengeneze mizania.

## Shughuli

Benki ya kimaadili ni benki ya kubuni inayoanza shughuli zake kwa madeni (kuchukua zaidi ya akiba) kutokana na baadhi ya matatizo kama vile kutoelewana na kukosa heshima katika mazingira fulani (k.m, shule, klabu, katika familia, na marafiki, mjini/jijini au serikalini). Kazi ya washiriki ni kujaribu kuifanya benki iingize kwa kuweka ufumbuzi na hatua za kutanzua matatizo.

Shughuli hii inaweza kufanyika kwa wiki nyingi, na kikundi kukubaliana kabla kuhusu muda ambao inatarajiwa kuwa benki itakuwa katika hali nzuri kifedha.

## Awamu ya Kwanza: Kukusanya "Kutoa"

Kwa kipindi kimoja au zaidi, washiriki wanabainisha 'matatizo' yanayoifanya benki iwe na madeni. Washiriki wabainishe matatizo kwa kufanya kazi kwa vikundi na kujadili matatizo katika mazingira tofauti, familia, jirani, shule, jiji au nchi.

Wakumbushe washiriki kuhusu mikataba ya haki za binadamu na heshima na dhima inayoendana na haki. Waulize washiriki ambao haki zao zinakiukwa na kama watu wanawajibika kwao wenyewe na kwingine, na kama wanaheshimu haki za watu wengine. Je, uchambuzi huu unaweza kusaidia kubainisha kiini cha matatizo pamoja na ufumbuzi wao unaoweza kutolewa?

Vikundi vinajumuika kujadili 'kutoa' walikokubainisha na majibu kuandikwa kwenye karatasi ya rangi inayohusika. Halafu kutoa "kunawekwa benki": Kunaorodheshwa kwenye ubao wa waraka mizania kwenye akaunti mbalimbali kama vile, "familia" 'jirani', 'shule' na 'nchi'.

## Awamu ya Pili: Benki Inafanya Kazi

Washiriki ndiyo wahusika wa kubainisha ufumbuzi na kutayarisha hatua za kushughulikia 'kutoa' kwenye benki. Benki itaendelea kuwa na deni mpaka washiriki wachukue hatua ambayo angalao itachangia katika ufumbuzi wa akaunti mahususi ya kutoa. Hatua kama hizo au ufumbuzi zinaandikwa kwenye karatasi ya "hundi" katika kipindi mahususi, michango hii inasomwa, kuchunguzwa na kujadiliwa na baada ya muda ubao wa waraka mizania unarekebishwa.

Wahimize washiriki wachangie mawazo na wajadili namna wanavyotanzua baadhi ya matatizo.

### Waambie washiriki waandike kumbukumbu za shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

#### Maelezo yangu

# Mitanziko

**Madhumuni:** Kujifunza umuhimu wa kufanya uamuzi kwa msingi wa kanuni za kimaadili.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wameendeleza uwezo wao wenyewe wa kufanya uamuzi wa kimaadili wao wenyewe.

**Mtanziko wa Kimaadili** ni hali ambayo mara nyingi itahusisha mgongano dhahiri kati ya uadilifu wa lazima, ambapo utekelezaji wa mmoja anaelekea kukiuka mwingine.

**Vifaa vya kufundishia:** Nakala za Mtanziko wa Uadilifu mmoja au wa aina mbalimbali – angaliza Nyenzo/Mitanziko ya Uadilifu kwenye ukurasa wa 143 au andika mitanziko yako mwenyewe (angalia hapo chini), Miongozo ya Utoaji Uamuzi (angalia uk. 90).

## Andika mitanziko yako ya uadilifu

1. Wasilisha hali ambapo washiriki wanatakiwa waamue kilicho sahihi na kilichokosewa.
2. Pendekeza mtanziko ambapo ufumbuzi bora zaidi unaelekea kuwa ni ule unaowanufaisha washiriki wenyewe lakini wenye madhara kwa wengine.
3. Eleza hali inayohusisha fursa za kukwepa sheria na kanuni.
4. Hakikisha kuwa mtanziko unahusisha hali ambapo washiriki watatakiwa kufanya uamuzi wao wenyewe.

## Shughuli

Washiriki wawe katika vikundi vya watu watatu hadi watano na wapewe mtanziko wa kiuadilifu.

Wape dakika 30 kujadili mtanziko na kufikia ufumbuzi wa mwafaka wa pamoja. Halafu wape fursa ya kushirikiana uamuzi wao na vikundi vingine.

Watambulishe washiriki kwenye Miongozo ya Utoaji Uamuzi wa Kimaadili (ukurasa ufuatao). Kwanza washiriki wajadili miongozo hiyo halafu waitumie kupitia uamuzi wao.

Jadili kama kutambulishwa kwa miongozo hiyo kumebadili uamuzi wa kikundi au hapana. Je, uelewa wao wa haki za binadamu umeathiri uamuzi wao? Je, wangependa kupitia Miongozo ya Utoaji Uamuzi wa Kimaadili?

Ongeza muda wa kutafakari kuhusu ukweli kwamba suala fulani linaweza kusababisha hoja nyingi za mawazo na zinazotofautiana. Jadili haja ya kuangalia mambo kwa mitazamo tofauti ya mawazo na kuzingatia kila hoja kwa uzito wake.

## Mwongozo wa Utoaji Uamuzi wa kimaadili – mkabala wa dini mbalimbali

Wakati wanapokabiliwa na hali fulani ambapo watalazimika kufanya uamuzi, jaribu kutumia maswali yafuatayo kukusaidia kufanya uteuzi mzuri.

> Je, uamuzi huu unawaathiri watu wengine? Ni kina nani?
> Je, uamuzi wako unaathiri imani yako?
> Je, uamuzi wako unaathiri imani za wengine?
> Je, uamuzi wako utawafanya watu wengine watende kinyume na utashi wao au imani zao?
> Je, uamuzi wako unaheshimu mawazo ya watu wa dini au imani tofauti?
> Je, uamuzi wako unaonyesha taswira mbaya ya watu wanaotofautiana na wewe (kwa jinsia, dini au hadhi tofauti)?
> Je, uamuzi wako unashusha hadhi ya utu?
> Je, unaweza kushirikiana uamuzi wako na familia yako, marafiki au walimu?
> Je, uamuzi wako unashughulikia tatizo au unalificha tu?
> Je, kuna matokeo yoyote mabaya ya baadaye kutokana na uamuzi wako?

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza



### Maelezo yangu

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

# Kutatua Tatizo kwa Hatua Sita

**Madhumuni:** Kuwatambulisha washiriki namna iliyopangwa ya kutatua migogoro aliyo nayo mtu.

**Matokeo:** Washiriki wawe wamejifunza njia mbadala zisizo za ugomvi kwa kutatua tatizo. Watakuwa wamegundua kuwa wanaweza kufanya kazi kutafuta ufumbuzi kwa kujibadili wao wenyewe na kwamba mtazamo wa upatanishi mara nyingi unaweza kusaidia.

## Shughuli

Wachague washiriki wawili wa kujitolea waigize mgogoro, kama vile mabishano kuhusu kitabu au kifaa shuleni, utani kuhusu mwonekano au mavazi, kudhalilishwa kwa ajili ya fedha, kurudishiwa kitu kikiwa katika hali mbaya zaidi ya kilipoazimwa au kukodiwa, au kushurutishwa kufanya kitendo usichotaka.

Washiriki wa wanajiweka katika nafasi ya mwingine kwenye kikundi cha wote. Ni vizuri mabishano yawe makali na kwamba wasifikie ufumbuzi.

Halafu watambulishe washiriki kwa mchakato wa kutatua tatizo kwa hatua sita.

## 1. Bainisha mahitaji

*"Je, unahitaji nini (au unataka nini)?"*

Kila mmoja aliye kwenye mgogoro hana budi kujibu swali hili bila ya kulaumu au kushutumu mtu mwingine.

## 2. Fafanua Tatizo

*"Je, unalionaje tatizo?"*

Kikundi kinaweza kusaidia kutayarisha jibu linalojumuisha mahitaji ya watu lakini si kugawa lawama. Watu waliyo kwenye mgogoro hawana budi kukubaliana na ufumbuzi wa tatizo.

## 3. Bungua bongo kuhusu masuluhisho mbalimbali yanayowezekana

*"Je, ni nani mwenye wazo la namna ya kutatua tatizo hili?"*

Mshiriki yeyote kwenye kikundi anaweza kupendekeza jibu. Mapendekezo yote yaandikwe bila ya maoni, uamuzi au tathmini. Lengo la hatua hii ni kupata masuluhisho mengi kadiri iwezekanavyo.

## 4. Tathmini utatuzi

*"Je, utaridhika na suluhisho hili?"*

Kila upande unaohusika na migogoro unapitia orodha ya masuluhisho yanayowezekana, ukieleza ni utatuzi gani utakubaliwa au utakataliwa.

## 5. Amua kuhusu suluhisho bora zaidi

*"Je, wote mnakubaliana na utatuzi huu? Je, tatizo limetatuliwa?"*

Hakikisha kwamba pande zote zinakubali na kuidhinisha juhudi zao katika kushughulikia ufumbuzi.

## 6. Hakikisha kuona namna suluhisho hili linavyofanya kazi

*"Tuzungumze miongoni mwetu kwa dakika 10 kuhakikisha kwamba matatizo yametatuliwa kabisa"*

Hatua hii ni muhimu sana. Kwa madhumuni ya tatizo la kubuni kwenye kujiweka katika nafasi ya mwingine, tathmini halisi haitawezekana kufanywa. Hata hivyo unaweza kutaka kupitia upya na kujadili utatuzi uliofikiwa baada ya kipindi cha muda kilichowekwa kuanzia dakika chache au saa moja, hadi siku ya pili au juma linalofuata, kutegemea hali ya migogoro na umri wa watoto.

Washiriki watajigawa katika vikundi vya watu wanne wafanye kwa vitendo suluhisho katika hali mbalimbali za igizo dhima

Hitimisha shughuli kwa kutafakari maoni miongoni mwetu pale kwenye tofauti kati yetu na umuhimu wa kutafuta utatuzi badala ya kuwalaumu wengine.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza



## Maelezo yangu

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

# Habari za Amani

**Madhumuni:** Kuwawezesha washiriki kutafuta utatuzi pale panapokosekana heshima na uelewano.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wametafuta utatuzi mzuri kwa hali zinazohusisha kukosekana kwa heshima na kutumia njia hii kwa migogoro ndani ya maisha yao wenyewe.

**Vifaa vya Kufundishia:** Kadi za habari za amani. Angalia Nyenzo/Kadi za habari za amani, uk. 177.

## Shughuli

Waambie washiriki wajigawe kwenye vikundi vya watu wanne au watano. Kila kikundi wapatie Kadi ya habari za Amani. Waambie kwamba lazima watafute utatuzi na kuutolea taarifa kama vile ilikuwa habari kuu kwenye taarifa ya habari ya TV.

Kila kikundi kinapewa dakika thelathini kutafuta utatuzi na kutayarisha taarifa yao ya habari. Waambie waigize hali hiyo au wahoji watu wanaohusika na watoe taarifa ya utatuzi.

Fanya majadiliano baada ya kila taarifa za habari. Baadhi ya maswali yanaweza kuwa:

- Je, kuna utatuzi mwengine unawezekana kwa hali hiyo?
- Ingekuwaje kama hali hiyo ingechochewa zaidi kwa …?
- Je, utatuzi uliopendekezwa haukiuki haki za watu wengine?
- Je, ungefanya nini kama ungekuwa katika hali hii?
- Je, watu watapatana vipi?
- Je, upatanisho ni muhimu kuleta amani ulimwenguni?

Wape nafasi washiriki kuchemsha bongo na kufikiri bila kulazimishwa kuhusu utatuzi wa kuhimiza mawazo yenye ubunifu na ubishani. Wahimize wafikirie kuhusu upatanisho wa amani usiowaathiri watu wengine.

Waambie washiriki waangalie matukio kupitia mtazamo wa haki, heshima na uwajibikaji. Je, ni haki za nani zinazokiukwa? Ni haki za nani zinazofuatwa? Je, watu wanaheshimiana? Je, utatuzi unawaona watu wakichukua wajibu kwa ajili yao na wengine? Je, wanalinda haki za watu wengine?

Hitimisha kipindi kwa kutumia Jedwali la Stadi 12 za Ubadilishaji wa Migogoro kwenye ukurasa unaofuata, kutafakari na washiriki kuhusu njia zinazowezekana kubadili migogoro. Kwa mfano, waeleze washiriki namna upatanishi unavyoweza kuleta maelewano miongoni mwa pande mbili zinazohusika katika migogoro. Waulize kama wamewahi kuwa wapatanishi katika mgogoro au kama wamewahi kuona hali ambapo wengine wanalazimika kupatanisha. Jadiliana nao, kwa mfano, namna ya kueleza haki zao watakazopata katika hali za uwiano au kwa kuwa mpole kwa watu na kutokuwa tayari kubadilika kwa tatizo, mazungumzo ya kuleta amani kunavyoweza kufikiwa.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Stadi 12 za Ubadilishaji wa migogoro

| UWIANO | MAJIBU YA UBUNIFU | KUELEWA |
|---|---|---|
| **Kurejea mahitaji**<br>> Tafuta fursa za manufaa ya pande zote | **Mgogoro kama fursa**<br>> Umuhimu wa mabadiliko<br>> Utayarishaji wa fursa | **Je, inaonekanaje kutoka upande wa pili?**<br>> Sikiliza nia, mahitaji na maslahi |
| **Upiganiaji haki**<br>> Jua haki zangu<br>> Eleza haki zangu kwa usahihi | **Uwezo wa kubuni**<br>> Tunafanya vizuri kwa pamoja<br>> Tofauti kati ya madaraka juu ya madaraka | **Kushughulikia mihemko**<br>> Hakuna upendeleo<br>> Usikatae<br>> Weka uhusiano unaostawisha |
| **Kuwa tayari kutanzua matatizo**<br>> Nimevaa miwani gani<br>> Kuelewa sababu za kufanya jambo | **Elewa mgogoro**<br>> Mahitaji ni yapi?<br>> Maslahi ni yapi?<br>> Kuelewa muktadha | **Tayarisha mibadala**<br>> Mibadala mipya kwa utatuzi mzuri zaidi<br>> Andaa mawazo mengi |
| **Stadi za mazungumzo ya mapatano**<br>> Kutokuwa tayari kubadilika kwa matatizo, kuwa mpole kwa watu<br>> Tayarisha makubaliano | **Mtazamo mpana na ustahamilivu**<br>> Tatuzi zinazoonyesha hoja zote za maoni<br>> Uwiano wa ubunifu<br>> Makubaliano mapana | **Taamuli**<br>> Kuza mazingira salama ya kujifunza<br>> Tafuta na tumia wakala asiyeegemea upande wowote |

## Maelezo yangu

# Vikundi lengwa kuhusu heshima

**Madhumuni:** Kuanzisha majadiliano kuhusu dhana ya 'heshima' ina maana gani, na kukosekana kwa heshima kunavyoweza kuathiri jamii.

**Matokeo:** Washiriki wamegundua namna kutambua haki za kila mtu kuheshimiwa kunavyoweza kuboresha uhusiano – kutoka kwa wapenzi zaidi wa ndani hadi kimataifa.

**Vifaa vya Kufundishia:** Nakala za Tamko la Haki za Binadamu na Makubaliano kuhusu Haki za watoto (angalia Nyenzo).

## Shughuli

Waambie washiriki kuwa wanatakiwa kuunda vikundi lengwa kuzungumzia kuhusu heshima.

Vikundi lengwa ni sawa na mahojiano, lakini vinaendeshwa na vikundi vya watu watano hadi kumi, kuliko kwa msingi wa mtu. Vinaendeshwa na msimamizi anayetayarisha mfumo ambao kila mtu ana nafasi ya kuzungumza. Mawasiliano kati ya washiriki unaweza kuchochea majadiliano yenye hoja na utambuzi, kupata data bora kuhusu athari za kufaa kwa programu. Vikundi lengwa vinaweza kuendeshwa kwa haraka zaidi kuliko mahojiano ya kina. Vimekuwa vikitumika kuchunguza aina ya dhana na imani ambayo watoto na watu wazima wanayo kuhusu amani, mawazo kuhusu namna ya kushughulikia ugomvi, na mapendekezo ya namna bora zaidi ya kuhimiza amani kwenye shule na jumuiya.

Muhtasari kwa majadiliano kuhusu heshima unaweza kuwa kama ifuatavyo:

## Muhtasari wa Msimamizi wa Kikundi Lengwa kwa majadiliano kuhusu heshima

Tunataka kutafuta namna watu katika Kikundi Lengwa wanavyohisi kuhusu heshima. Tumia maswali haya kuchochea majadiliano. Si lazima uyatumie kwa utaratibu huu.

> Je, ni nani anayekuheshimu?
> Je, ni nani ambaye mara nyingi hakuheshimu?
> Je, utajuaje kama watu wanaonyesha heshima kwako?
> Je, watu wengine unawaonyesha heshima kiasi gani? Ni nani hasa unaowaheshimu?
> Lini na kwa nini huwaheshimu watu wengine?
> Je, kuna mabishano gani kwa kumheshimu kila mtu?
> Je, kuna mabishano gani kwa kuwaheshimu baadhi ya watu tu?

Kama ikibidi unaweza kuvitaka vikundi vyako kuzingatia mojawapo ya mada zifuatazo:

| | |
|---|---|
| Heshima shuleni | – Je, kuna matukio mahususi yanayoonyesha kukosa heshima? |
| Heshima jijini | – Je, kuna makundi yanayokabiliwa na ukosefu wa heshima, kama vile wahamiaji na makabila madogo? |
| Heshima katika familia | – Je, kuna heshima kiasi gani inayoonyeshwa kati ya wanafamilia? Je, ni nani anayeheshimiwa zaidi? Nani anayeheshimiwa kidogo zaidi? |
| Heshima ya Kidini | – Je, tunaheshimu imani za watu wengine? Kama hapana kwa nini? |

Hitimisha shughuli kwa kushirikishana hitimisho la kila kikundi lengwa. Unaweza kutaka kutumia ramani ya fikra kukumbuka namna washiriki wanavyoelewa maana ya heshima na namna inavyotumika.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Migahawa ya Mazungumzo ya Dini Mbalimbali

**Madhumuni:** Kuwawezesha washiriki kujadili masuala yanayozungumzwa sana na kujenga maelewano ya pande mbili na kujifunza.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wamemiliki kupanga na kuendesha shughuli ambapo watu wanakusanyika kujadili na kutafakari mada zenye maslahi na kupendekeza utatuzi unaowezekana kwa matatizo ya kijamii.

**Vifaa vya Kufundishia:** Mahali kama vile shule, ujirani, mahali pa ibada, nyumba za washiriki ambapo watu hukutana, pengine mara kwa mara kujadili matukio ya kila siku na masuala ya kidini kutoka mielekeo mbalimbali.

## Shughuli

Tambulisha wazo la Mikahawa ya Mazungumzo ya Dini Mbalimbali kwa washiriki wako, kama ni mahali ambapo watu bila ya shaka wa dini mbalimbali, wanakutana kujadili masuala yanayozungumzwa kila siku, na kama ilivyo kwenye mkahawa, hufurahia viburudisho.

Waambie washiriki wako kwamba kupanga Migahawa ya Mazungumzo ya Dini Mbalimbali mara moja au zaidi inaweza kuwa sehemu ya dhamira zao za kuhimiza maelewano ya pande mbili. Kikundi kidogo cha watu wanaojitolea kinaweza kuunda 'kamati' kuhakikisha kuwa mikutano hii isiyo rasmi ni mahali ambapo washiriki wanajiona huru zaidi kuzungumza na kujifunza miongoni mwao na kwamba pia wanashirikisha watu ambao vinginevyo wasingeweza kukutana.

Kuandaa Mgahawa wa Mazungumzo ya Dini Mbalimbali, Kamati haina budi:



- Kuchagua mada.
- Kuamua kuhusu njia ya kuwasilisha taarifa, k.m. makala fupi, uwasilishaji kwa njia ya Projekta, (PowerPoint), msemaji wa nje au maonyesho ya picha na habari fupi fupi.
- Andaa programu itakayomaliza saa kadhaa. Programu haina budi kutarajia muda wa watu kuanza kuwasili, vinywaji, uwezekano wa kuhitaji kufungua mazungumzo au kuvunja ukimya, uwasilishaji wa mada na haja ya kuwa na kipindi cha maswali na majibu na/au majadiliano ya kawaida ambapo hadhira yote inaalikwa kushiriki.
- Amua ni aina gani ya vinywaji vitakavyogawiwa, mahali vitakakotoka au nani atatoa, na vitapatikana wakati gani wa kipindi.
- Mtu mmoja (si lazima awe mtu mzima) atakuwa mwenyekiti wa mgahawa usio rasmi, kutambulisha uwasilishaji/mzungumzaji, n.k, kusimamia mazungumzo, kupokea maswali na kuwezesha kubadilishana mawazo kutoka kwa 'hadhira'.
- Mwenyekiti hana budi kuhakikisha kuwa majadiliano yanaendelea kwa kuuliza maswali kwa washiriki au wazungumzaji, pengine kuhusu kifanyike nini kuhusu hali na namna inavyoweza kubadilishwa.
- Mwenyekiti hana budi kuhakikisha kwamba mchango wa mawazo wa kila mtu unaheshimiwa.
- Mwenyekiti atafunga kipindi kwa kukaa kimya kwa muda, kwa ajili ya amani. Kama ni muhimu kuwa na Migahawa ya Mazungumzo ya Dini Mbalimbali zaidi ya mmoja, wape waliohudhuria tarehe na mahali kabla hawajaondoka. Pia watu wataweza kuombwa wapendekeze mada za kujadiliwa.
- Kamati haina budi kutangaza Migahawa ya Mazungumzo ya Dini Mbalimbali kwa njia ya mabango, n.k, hasa mahali pa ibada, hata katika vyombo vya habari. Hawana budi pia kuwashirikisha wazazi wao ili kuhakikisha mchanganyiko mkubwa wa umri.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Mikutano ya Majadiliano

**Madhumuni:** Kujadili na kujifunza zaidi kuhusu masuala muhimu ya kidini na migogoro kwa kukaa katika mkutano ambapo washiriki wote ni sawa.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wamepata taarifa kuhusu migogoro mbalimbali ya kidini, namna ilivyoathiri dunia na haja ya kuwaheshimu watu wa dini, utamaduni na mila na desturi mbalimbali.

**Vifaa vya Kufundishia:** Meza ya mduara au kitu kinachokaribia kufanana nayo, ambayo kila mshiriki atakaa kwenye mduara na kuwaona wote, taarifa kuhusu mgogoro au mada inayojadiliwa, chatipindu na kalamu za kuchorea.

## Shughuli

1. Waeleze kwa muhtasari washiriki wako kuhusu njia ya Mikutano ya Majadiliano kwa kujadili masuala. Meza ya mduara haina "kichwa" "pande" wala "miguu" na kwa hiyo hakuna hata mtu mmoja anayekaa kwenye meza hiyo atakayejiona yuko kwenye nafasi ya upendeleo na wote wanahesabiwa kuwa ni sawa. Wazo lilianzia kwa hekaya ya Kiathuri ya Kiingereza kuhusu mashujaa wa Meza ya Duara katika Camelot (British Arthurian Legend about the Knights of Round Table in Camelot).
2. Kwa kushirikiana na washiriki wako, chagueni suala la kidini au mgogoro ambao watazungumza katika meza ya mduara. Pangeni tarehe ya majadiliano ili washiriki wapate muda wa kujiandaa. Waambie kuwa mkutano huo umekusudiwa kuwezesha uchambuzi kutoka pande zote (kiuchumi, kisiasa, kijamii na kidini). Waambie walenge hasa kuhusu uwezo wa binadamu kuumba, kuharibu, lakini pia kubadili.
3. Wapatie mapema washiriki taarifa kuhusu mada, hata hivyo wahimize wafanye utafiti wao wenyewe na kuleta jambo jipya kwenye meza ya majadiliano.
4. Kwenye meza ya duara, mwambie mmoja wa washiriki awe mwenyekiti. Hakikisha kila mtu anachangia kwa kuwashirikisha wale walioleta taarifa au wape maswali na kwa kuwashirikisha wale ambao wasiozungumza kwa hiari.
5. Unaweza kutaka kutumia chatipindu kwa ajili ya kutaka kuchorea picha na kutaka kuwasilisha taarifa kuhusu mgogoro. Mtu wa kujitolea anaweza kufanya kazi hii.
6. Kama mwezeshaji, shiriki kama mshiriki miongoni mwa watu sawa lakini usitoe maarifa; huo ni wajibu wa washiriki. Usisahihishe mawazo yao au kuyafasiri bali fafanua kama kuna upotoshaji wa dhana.
7. Hitimisha majadiliano kwa kuuliza maswali kama:
   - Kwa nini dini zinachochea migogoro?
   - Je, watu wanataka kupigana na wale wasio wa dini yao au wasioshirikiana imani zao?
   - Je, haiwezekani kwa watu kutoka dini tofauti kuishi na kufanya kazi kwa pamoja.
   - Je, tunaweza kufanya nini kuhakikisha kuwa wale watu wa dini tofauti au wasio na dini, wanaishi pamoja kwa amani na utulivu?

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Midahalo

**Madhumuni:** Kuwawezesha washiriki kuelewa migogoro na uonevu kutoka mitazamo tofauti na kubishana kwa kujenga katika mazingira yaliyodhibitiwa.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wametafakari hali, tabia na mienendo na mitazamo inayoathiri hadhi ya utu na mifumo yao ya unyofu.

Midahalo ni malumbano rasmi ya mdomo kati ya watu wawili, timu au vikundi wanaowasilisha mabishano ya kuunga mkono pande zinazopingana kuhusu swali fulani, kwa kawaida kulingana na utaratibu au muundo uliokubaliwa. Midahalo ina kanuni zinazowawezesha watu kujadili na kuamua kuhusu tofauti, ndani ya mfumo wa mawasiliano uliokubaliwa.

Kanuni zilizotolewa hapa zimechukuliwa kutoka kwenye "World School Debating Championships"[2] (Mashindano ya Midahalo ya Shule Duniani). Washiriki watanufaika kwa kufanya midahalo ya mara kwa mara ili wote wapate fursa ya kuwa mzungumzaji na kujenga nidhamu inayotakiwa kuchangia kwenye midahalo.

## Shughuli

Washiriki wachague suala linalojadiliwa siku hizi na lililoko kwenye habari, au lililo muhimu kwa washiriki. Kwa kawaida huendeshwa kwa njia ya "pendekezo la hoja" linalosema : mkutano huu unaamini kwamba… upande mmoja au timu ya wazungumzaji inapendekeza hoja, upande mwingine unapinga. Lazima pia kuwe na Mwenyekiti anayedhibiti nidhamu na muda.

1. Kila upande una wazungumzaji watatu.
2. Kila timu haina budi kuamua kuhusu utaratibu ambao mzungumzaji wao atasema. Kabla ya kuanza mdahalo kila timu lazima umwarifu mwenyekiti kuhusu majina ya wazungumzaji wao watatu, na watakavyofuatana katika kuzungumza.
3. Wazungumzaji wakuu kutoka kila timu watasema kwanza, na kwa urefu. Upande unaopendekeza hoja unaanza kuzungumza kwanza, na kufuatwa na upande unaopinga.
4. Wazungumzaji wa kwanza wanafuatiwa na wazungumzaji wa pili kutoka kila upande, wanaojibu mazungumzo ya kwanza, huku upande unaopinga ukianza kuzungumza ukifuatwa na timu inayopendekeza hoja.
5. Mzungumzaji wa tatu kutoka kila upande anachukua zamu. Hapa pia upande unaopinga unajibu kwanza, na upande unaopendekeza hoja unafuata.
6. Muda wa mazungumzo ya kwanza ni dakika 8 na kwa mazungumzo yanayojibu mdahalo ni dakika 4.
7. Watu pekee wanaoweza kuzungumza kwenye mdahalo ni wazungumzaji watatu kwa kila timu, kama ilivyotangazwa na mwenyekiti mwanzoni mwa mdahalo.
8. Wakati wa mdahalo, wazungumzaji hawaruhusiwi kuwasiliana na mtu yeyote kwenye hadhira.
9. Unaweza kuhitimisha mdahalo wako kwa kuitaka hadhira kupiga kura kwa mabishano yaliyovutia zaidi.
10. Kama mjadala wa kuhitimisha, waulize washiriki iwapo na kwa namna gani imani za dini zao zinakuwa kama miongozo kwa maoni yao, hoja na tabia na mwenendo.

Ubora wa mdahalo utakuwa mzuri zaidi kama mada na wazungumzaji wamejulikana mapema na hivyo kuwapa muda wa kutosha wa matayarisho.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

2 http://www.schoolsdebate.com/guides.asp

# Taamuli kuhusu mimi mwenyewe – Safari ya Kimya

**Madhumuni:** Kuweka fursa kwa washiriki kutafakari kuhusu maisha yao, wao ni kina nani, na kuhusu uhusiano wao na wengine na mazingira yao.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wametambua haja ya kujithamini wao wenyewe ili waweze kuhusisha na wengine kwa namna nzuri zaidi.

**Vifaa vya Kufundishia:** Chumba chenye mwanga mdogo sana au maeneo sita ya faragha; karatasi ya rangi au kadibodi (njano, nyekundu, kijani, nyeusi, nyeupe, bluu). Weka mazingira tulivu sana yenye muziki mwororo, ubani, mishumaa, picha za mandhari tulivu au aya za maandiko matakatifu au mashairi ukutani. Wawezeshaji sita pia wanahitajika.

## Shughuli

Ondoa samani na weka maeneo sita kwenye sakafu au kwenye nyumba tofauti kwa kutumia karatasi za rangi tofauti au kadibodi kwenye sakafu. Kunahitajika wawezeshaji sita, mmoja kwa kila rangi. Kwa kila rangi, mwezeshaji atatoa baadhi ya maswali kwa ajili ya kutafakari ( angalia mapendekezo hapa chini).

Waambie washiriki kuwa wataenda kwenye safari ya kimya kujifunza zaidi kuhusu wao wenyewe. Watapita katika maeneo sita tofauti, na katika kila eneo watataamali kuhusu maisha yao na uhusiano wao na wengine. Wagawe washiriki katika vikundi sita visivyozidi watu watano kila kimoja. Kwa kuanzia waelekeze kila kikundi kwenye moja ya maeneo sita. Wahamishe vikundi baada ya dakika 15 katika kila eneo.

Wakiwa kwenye eneo washiriki wanaweza ama kukaa ama kulala chini. Wanaweza kufumba macho yao kama wanataka na kujaribu kupumzika. Mwezeshaji atauliza maswali lakini hawatakiwi kujibu kwa mdomo au kuingia katika majadiliano. Lengo hapa ni kufikiria maswali yote kimyakimya, wakihusisha na maisha yao.

Kipindi kinaweza kuwafadhaisha baadhi ya washiriki, hali ambayo huna budi kujiandaa nayo. Pia wape muda wa muhtasari wa jumla kuhusu namna washiriki walivyohisi kuhusu kipindi hicho; walichopenda zaidi na wasichopenda, wanachokumbuka kwa dhahiri zaidi na watajifunza nini kutokana na uzoefu.

## Mapendekezo kwa Wawezeshaji (maswali ni fasaha na si ya kudodosa):

> Njano – kutafakari kuhusu kutafuta mwanga ndani ya nyoyo zetu. Je, unahusiana kwa amani kiasi gani na wengine? Je, wakati mwingine wewe ni mwanga kwa wengine? Fikiria namna unavyoweza kuleta mwanga katika hali ngumu. Je, unawezaje kutafuta amani ndani na kuleta amani kwa wengine?

> Kijani – rangi ya maumbile. Sote tuna wajibu kwa mazingira. Pia hatuna budi kuwa na matumaini kwamba hata katikati ya matatizo kuna kitu ndani yetu kinachotuambia kwamba mambo yatakuwa mazuri.

> Nyekundu – rangi ya mapenzi. Je, ni nani unayempenda zaidi? Sikiliza moyo wako unavyodunda, lini moyo wako unapodunda zaidi – kwa nguvu kiasi cha wewe kuhisi? Tunatoa mapenzi yetu kwa ajili ya watu bure, lakini tunawanyima wengine ambao wangehitaji. Je, tutajifunzaje kuwajali wale ambao si rahisi kuwapenda?

> Nyeusi – rangi ya ubadilishaji na nguvu ya ndani. Ina maana ya uwezekano na kuwa na nguvu zilizojificha. Hapa ndipo washiriki wapo na tafakari kuhusu namna tunavyowahukumu watu wengine. Je, unawahukumu watu kiuhakiki zaidi? Je, wewe unakuwa mkosaji mahususi kama watu wanapotofautiana sana na wewe? Je, unaona vigumu kuelewa na kumpenda mtu unayemwona kuwa ni tofauti na wewe?

> Nyeupe – hapa ndipo washiriki wanapotafakari namna wanavyojipenda na kujiheshimu wao wenyewe. Inasemekana kuwa huwezi kuwapenda wengine mpaka ujipende wewe mwenyewe – je, usemi huu una ukweli gani kwako?

> Bluu – hapa ndipo washiriki wanapotafakari kuhusu ubora wao na vipaji. Nini kinachokuvutia? Je, nini kinachokufanya uwe wa pekee? Je, ubora wako na vipaji vinawaathirije wengine? Je, unatumiaje sifa hizi kuwasaidia au kuwahudumia wengine? Ni muhimu kuishi kwa amani na wengine na kuchangia kwenye amani ulimwenguni.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

### Maelezo yangu

...........................................................................

...........................................................................

...........................................................................

...........................................................................

...........................................................................

...........................................................................

...........................................................................

...........................................................................

...........................................................................

...........................................................................

...........................................................................

# Viongozi wa Kidini na wa Kijamii

**Madhumuni:** Kujifunza kuhusu viongozi wa kidini na kijamii walioleta amani duniani na kutokana na matendo ya kiroho yanayoweza kuleta amani kwa maisha ya washiriki na maisha ya wengine.

**Matokeo:** Washiriki wawe wamechunguza kuhusu tabia na mienendo na mitazamo ya mifano ya kuigwa na wametafakari kuhusu namna ya kujenga mtazamo wa usuluhishi kwa wengine.

**Vifaa vya Kufundishia:** Filamu (zikiwemo filamu za matukio za TV, video na filamu za makala) za maisha ya mmojawapo au zaidi ya mifano ya kuigwa ifuatayo: Aung San Suu Kyi, Dalai Lama, Mohandas Gandhi, Martin Luther, King, Jr, Pope John Paul II, Iman W. Deen Mohamed, Mother Teresa, Nelson Mandela, Cat Stevens (Yusulf Islam), Rabbi Abraham, Joshua Heschel, Moses Maimonides, Thich Hanh, Shirin Ebadi, Swami Vivekanada, mtu mwingine yeyote unayedhani amekuwa na taathira na ameshughulikia amani na ubora wa binadamu.

## Shughuli

Tayarisha uwasilishaji au onyesha filamu kuhusu kiongozi mmoja au zaidi wa kidini na wa kijamii walioleta amani duniani. Baada ya filamu (angalia Nyenzo/Filamu kwenye ukurasa 149) au uwasilishaji, waambie washiriki wajadili mhusika mkuu.

> Je, ni sifa gani alizokuwa nazo zilizomfanya kuwa mashuhuri kiasi hicho?
> Je, ni imani gani zilizovutia kazi yake?
> Je, mtu huyu alifanya nini na walitenda nini kubadili hali ya uonevu?
> Je, mtu huyu alishughulikiaje msamaha na kuleta upatanishi katika jamii?

Unaweza kutaka kujadiliana na washiriki maana ya upatanishi kwao, je, mtu anawezaje kupatana na wengine, na kwa nini ni muhimu.

Fanya majadiliano kuwa ya binafsi zaidi kwa kuwauliza washiriki namna wanavyoshughulikia msamaha na upatanishi. Unaweza kuuliza maswali mahususi kama vile:

> Je, nini kinachotuzuia kuwasamehe wengine?
> Je, inagharimu nini kuwa mpatanishi zaidi, k.v. je, tunatahitajika tuwe na nini ili kutenda katika hali ya amani?
> Je, mafundisho kutoka kwenye mifano ya kuigwa yatawezaje kutumiwa kwenye maisha yetu?
> Je, upatanishi unawezaje kuwa zana ya kuubadili ulimwengu?

Hitimisha somo kwa kumwambia kila mshiriki kuzingatia ni mitazamo na tabia na mienendo gani wanayotaka kuendeleza ili kupata amani ya ndani ya nafsi.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Kwa nini inaniumiza?

**Madhumuni:** Kuweka nafasi ya 'kuponya' mioyo ya washiriki na kujaza mioyo iliyowazi na faraja ya kiroho na amani ya ndani ya nafsi kwa kuondoa majonzi na maumivu yao.

**Matokeo:** Washiriki wawe wametafakari kuhusu hisia zinazojaza mioyo yao na maumivu na majonzi na kukubali mahitaji ya upatanishi na amani ya nafsi.

## Shughuli

Waambie washiriki kuwa hii ni shughuli ya tafakuri kuhusu vitu vinavyowasababishia maumivu, na kuhusu maumivu waliyowahi kuwasababishia wengine. Utajaribu kuwasaidia kutafuta upatanishi na amani ya ndani ya nafsi.

Anza kwa kutafakari madhara tunayoweza kuwasababishia wengine kwa maneno yetu, mienendo yetu na mitazamo na tabia zetu. Ulinganisho unaofaa ni madhara yaliyofanywa ukutani wakati tunapoubomoa kwa nyundo na kufanya matundu ambayo si rahisi kuyaziba na ni kwa namna gani ni vigumu kuyaziba matundu hayo ili ukuta uwe tena safi na imara. Au kunja kunja karatasi katika kiganja chako na mpe mshiriki mmoja ajaribu kuinyosha tena kuondoa mikunjamano.

Waeleze jinsi mitazamo, mienendo na maneno yanavyoweza kutengeneza matundu katika uhusiano wetu na watu, matundu ambayo hayawezi kuzibika kwa urahisi. Hali kadhalika watu wanaweza kufanya matundu kwenye mioyo yetu ambayo si rahisi kuyaziba. Mioyo yetu inakuwa mitupu wakati inapokuwa na matundu na mioyo mitupu hii inahitaji kujazwa na msamaha na usuluhishi.

Baada ya tafakuri yako, ama uwe tayari na maswali yafuatayo kwenye chatipindu, au yaliyoandikwa kwenye karatasi na kusambazwa kwa washiriki. Maswali yanakusudiwa kusaidia washiriki kutafakari kuhusu kinachowasababishia majonzi na maumivu.



### Kwa nini inaniumiza?

Je, kuna jambo lililotokea hivi karibuni maishani mwako linalosababisha maumivu moyoni mwako? Ni jambo gani hilo?

Je, unahisi nini ndani ya nafsi? Ni hisia gani zinazokusababishia maumivu na uchungu moyoni?

Je, hisia hizo ni za kimwili? Mchomo wa moyo? Eleza hisia hizo.

Je, unataka kuendelea kuhisi namna hii? Je, hisia hizo zinakuathiri wewe peke yako na bila ya mtu mwingine? Je, unataka kuendelea kupoteza nguvu zako katika kulea hisia hizo za maumivu?

Je, unaweza kufikiria utakuwa na furaha kiasi gani kama ungeweza kuziba matundu hayo moyoni mwako? Unaweza kufikiria namna maisha yako yatakavyokuwa kama utaondoa maumivu? Je, unaweza kufanya hivyo sasa hivi?

Fumba macho yako na fikiria kuhusu maisha yako bila ya hisia hizo na mawazo. Jifikirie mwenyewe katika mahali pa amani na utulivu. Sasa acha hisia hizo zinazokutia uchungu ziondoke.

Wewe ndiye unayeweza 'kuponya' moyo wako na ndiye pekee anayeweza kuleta amani katika nafsi yako. Jisamehe. Msamaha haina maana ya upatanishi bali unakuandaa kukabiliana na hali hii kwa mtazamo wa upatanishi.

Hitimisha shughuli kwa kumpa mshumaa kila mshiriki awashe. Inawakilisha kutafuta amani na kuwa tayari kupatana na wale waliowasababishia maumivu na majonzi. Waambie washiriki wakusanyike katika kukaa kimya kwa muda kujaza mioyo yao mitupu na msamaha na upatanishi.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Hadithi ya Bobby

**Madhumuni:** Kugundua unyofu wa kila mtu kwa kuwaangalia wengine na ndani ya nafsi yako.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wamegundua kuwa wanaweza kuwa ndiwo walioamua. Washiriki watakuwa wametafakari kuhusu chuki zao na namna wao wenyewe wanaweza kuwa waathirika wa chuki.

## Shughuli

Ungana na washiriki wengine na waambie hadithi ya Bobby.

### Hadithi ya Bobby

Wote mnajua Bobby. Hasemekani kuwa ni mtu mzuri zaidi shuleni na mwonekano wake unamfanya aonekane dhahiri. Bobby ana uzito wa takriban kilo 12 zaidi ya wanafunzi wenzake na mara nyingi anaonekana kituko. Mavazi yake yamepitwa na wakati mwingine yananuka, meno yake machafu, na ana chunusi nyingi usoni mwake.

Je, unamwona Bobby? Ni mwanafunzi ambaye watu wanakwepa kuonana naye kwenye njia na vichochoro vya shule. Yeye daima yuko peke yake kafteria au wakati wa mapumziko. Wakati mwingine, watu wenye huruma wanapenda kukaa karibu yake lakini wana wasiwasi kwamba wengine watamfanyia mzaha. Hata hivyo nilikaa karibu yake mara moja tu na kuzungumza naye na kugundua kwamba Bobby ni kama mimi au wewe tu.

Waulize washiriki:

- Je, ni nini kinachowavutia watu kwako?
- Je, ni nini kinachowafanya baadhi ya watu wakukimbie?
- Je, mambo yote mabaya tuliyosema kuhusu Bobby yatakusaidiaje?
- Je, kumkwepa Bobby kutakusaidiaje kuondokana na ulimwengu wake mwenyewe?
- Je, Bobby atakuwa na mambo gani mazuri?
- Je, tutakuwa na mambo gani ya pamoja na Bobby?

Baada ya washiriki kumaliza majadiliano, mtambulishe Bobby kwao. Bobby anawakilishwa na tufe. Waambie washiriki wapilizane tufe kwa mikono kwa makini. Bobby ana hisia kali na tunaweza kumwathiri. Baada ya tufe kupitizwa darasani kote, waambie washiriki wakutane katika vikundi vidogo kujadili namna wanavyowafanya wengine au kuchangia katika kufanya maamuzi kuhukumu bila kutafakari.

Rudia katika mkusanyiko wa wote na tafakari na washiriki kuhusu haja ya kujithamini wao wenyewe na kuwathamini wengine, bila ya kujali uwezo au udhaifu. Tafakari kuhusu umuhimu wa kuangalia nafsi za watu wengine na si kulenga mwonekano wao wa nje.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Je, ulimwengu ungekuwaje kama...

**Madhumuni:** Kuweka fursa kwa washiriki kufikiria kuhusu taarifa ya mgogoro katika ulimwengu na unyofu gani unahitajika na kila mtu kusaidia kujenga ulimwengu bora zaidi.

**Matokeo:** Washiriki wawe wametafakari kuhusu vyanzo na matokeo ya mgogoro na umuhimu wa maelewano ya wote. Watakuwa wametafakari namna wanavyoweza kuchangia kwenye kuleta maelewano.

**Vifaa vya Kufundishia:** Chatipindu, kalamu, postikadi, majarida, magazeti, gundi ya maji; kusanya vifaa vingi kadiri unavyodhani kuwa vinahitajika.

## Shughuli

1. Waambie washiriki waunde jozi na watumie vifaa walivyopewa kuchora au kutoa picha ya ulimwengu ungekuwaje kama:
   > Kusingekuwa na migogoro ya ugomvi
   > Ningebadili _____ au kufanya____.
   > Au maelezo yako kutokana na kile ambacho majadiliano yako ungetaka yasisitize.
2. Wakusanye washiriki na waambie kila jozi waeleze mchoro wao.
3. Ongoza majadiliano kwa msingi wa masuala yaliyoakisiwa kwenye michoro. Pia fikiria:
   > Tunaweza kufanya nini kuhimiza maelewano miongoni mwa watu kutoka imani na dini mbalimbali?
   > Tunawezaje kuhimiza usuluhishi miongoni mwa watu kutoka imani, dini na tamaduni tofauti?
   > Je, ni sifa na unyofu gani unaohitajika kueleweka zaidi?
   > Je, unadhani dini inatoa mchango gani kuwasaidia watu kuelewa hisia za wengine na kuwa wenye heshima zaidi?
   > Je, utawezaje kusaidia katika kujenga ulimwengu ambao watu wanaheshimiana?

Shughuli inaweza kuwa kampeni ya shule ambapo michoro inabandikwa kwenye maonyesho.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

## Maelezo yangu

# Nderemo za kuridhika

**Madhumuni:** Kujenga kujiheshimu na kusherehekea shukurani yenye furaha.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wameongeza kujiamini kwao na kujiheshimu na kupata msaada wa uadilifu na shukurani yenye furaha miongoni mwa watu kwenye kikundi.

**Vifaa vya kufundishia:** Vikombe viwili vya plastiki na maharage makavu kwa kila mshiriki (mbegu za maharage makubwa zinafaa zaidi).

## Shughuli

1. Washiriki wakae katika mduara. Waambie washiriki wafumbe macho na kuvuta pumzi kubwa, na kusahau uzoefu wa siku na pirikapirika zao za kutwa.
2. Wape kila mtu kwenye kikundi vikombe viwili vidogo vya plastiki. Kimoja chenye mbegu za maharage makubwa na kingine kitupu.
3. Waambie washiriki kufikiria kuhusu matendo bora waliyofanya wiki iliyopita; hii itajumuisha tabia na mienendo bora, kuzungumza vizuri kwa watu au kuhusu watu, kumsaidia mtu, n.k.
4. Kwa kila kitendo kizuri mshiriki anaweza kuchukua harage moja kutoka kwenye kikombe kilichojaa na kuingiza kwenye kikombe kitupu. Haya yote yafanyike kimya kimya na mwezeshaji naye ashiriki. Ruhusu dakika tano kwa sehemu hii ya zoezi.
5. Zungukia mduara na mwambie kila mshiriki aeleze hadithi za mambo mema (wema) kwa washiriki wote, wakati wengine wakisikiliza "kwa kina" – kusikiliza kwa ushirikali na bila ya hukumu pasipo tafakuri.
6. Kwa kuwa sehemu ya mduara iliyojaa wema na furaha na shukurani yenye furaha, mshiriki anajiamini zaidi.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

### Maelezo yangu

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

# Mandalas

**Madhumuni:** Kuwa patia washiriki fursa ya kutafuta nafsi yao ya ndani na kutafuta amani ndani yao.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wametafakari kuhusu maisha yao wakati fulani mahususi na kuwa wametafakari maana ya mabadiliko na ubadilikaji ndani yao.

**Vifaa vya kufundishia**: Penseli za rangi, kalamu za kugandamiza, nta ya rangi, kalamu za kuchorea, muziki mwororo, ubani.

## Shughuli

Neno 'mandala' lina asili ya lugha ya asili ya kihindi ya Sanskrit. Hutafsiriwa juu juu kama mduara, mandala inakaribiana zaidi na umbo rahisi. Inawakilisha ukamilifu na inaweza kuonekana kama mfano kwa ajili ya muundo wa maisha yenyewe – mchoro wa ulimwengu unaotukumbusha uhusiano wetu na ukubwa usio na kikomo, ulimwengu unaokwenda kwa upana zaidi kwenye upeo na ndani ya miili yetu na akili. Kwa maelezo zaidi na mifano ya mandalas tafadhali fungua http://www.mandalaproject.org/index.html.

Mandalas hutumika kuangalia ulimwengu kutoka ndani na kubaini umoja na ulimwengu na uumbaji. Bailey Cunningham, Mkurugenzi Mtendaji na mwasisi wa mradi wa Mandala, shirika lisilo la kibiashara linalojihusisha na uhimizaji wa amani, kwa njia ya sanaa na elimu, anasema "Kuelewa kuhusu mandala kunaweza kuwa na uwezekano mkubwa wa kubadili namna tunavyojiona wenyewe, sayari yetu, na pengine hata madhumuni ya maisha yetu wenyewe".[3]



> Tafuta mahali pa kimya na patulivu ambapo washiriki hawatasumbuliwa na ambako wanaweza kutafakari. Waambie washiriki watafute hali yao ya akili ili kuamsha sehemu ya ubongo inayohusika, ambako ubunifu na kipawa cha kujua bila kufikiri kinapatikana. Hii itawasaidia kuingia katika hali ya kujipima na kujichunguza itakayosababisha kutafakari namna wanavyohisi wakati ule, na kuchora mambo yanayowakilisha hali yao ya akili.

> Wapigie muziki mwororo au choma ubani kuchochea hisia zao. Waambie washiriki wachore mduara kutumia sahani au bikari, na onyesha kitovu cha mduara kwa nukta. Kuanzia kwenye kitovu watajaza mduara kwa 'michoro' – inayowakilisha au ya dhahania, alama, maneno, maumbo ya kijiometri, n.k., vyovyote wanavyopenda.

> Washiriki wakimaliza kuchora, ongoza tafakuri ya namna sasa wanavyohisi. Waongoze wafikirie kuhusu kila rangi na umbo wanadhani vinawakilisha nini kwao na wamefahamu nini wakati walipofanya zoezi hilo. Waeleze kwamba Mandalas ni uwakilishi wa namna wanavyohisi ndani ya nafsi. Wahimize washiriki wachukue mandalas zao nyumbani na waweke mahali wanapoweza kuichunguza mara kwa mara.

> Unaweza kufanya tena shughuli hii baada ya wiki kadhaa ili kuwapa washiriki fursa ya kulinganisha mandala zao kwa kipindi kirefu na kuchunguza mabadiliko ndani yao wenyewe.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

3 Mandala; Journey to the centre, Bailey Cunningham, DK Publishing. 2002

# Korongo elfu moja wa Karatasi

**Madhumuni:** Kutafakari kuhusu taathira ya dunia kwa kukosa maelewano na kwa washiriki kufanya alama halisi za amani.

**Matokeo:** Washiriki kuwa sehemu ya mtandao wa dunia wa watu wanaofanya kumbukumbu ya shambulio la bomu la atomiki huko Hiroshima kwa kutengeneza korongo wa karatasi. Watakuwa wametafakari namna wanavyoweza kuwa chachu ya mabadiliko na watunzaji wa amani.

**Vifaa vya Kufundishia:** Karatasi ya Origami au karatasi zilizokatwa maumbo ya mraba ya 20cm × 20cm. Maelekezo kuhusu namna ya kutengeneza korongo yapo kwenye uk.183, Nyenzo/Namna ya kukunja korongo wa katarasi. Pia unaweza kusoma kuhusu Mradi wa Amani Duniani kwa Watoto katika www.sadako.org

## Shughuli

> Waambie washiriki hadithi ya Sadoko.

### Hadithi ya Sadako

Korongo wa Karatasi imekuwa alama ya amani ya kimataifa kutokana na hadithi ya msichana wa Kijapani anayeitwa Sadako Sasaki, aliyezaliwa mwaka 1943.

Sadako alikuwa na umri wa miaka miwili wakati bomu la nyuklia lilipodondoshwa Hiroshima, Japani tarehe 6 Agosti 1945. Wakati alipoendelea kukua, Sadako alikuwa msichana jasiri, mwenye nguvu na shupavu wa mwili. Hata hivyo, mwaka 1955 alipokuwa na umri wa miaka 11, wakati akifanya mazoezi ya mashindano ya mbio, alipata kizunguzungu na kuanguka chini. Sadako baada ya kupimwa alionekana kuwa na saratani ya damu (kikemia), saratani ambayo kwa kawaida inaitwa saratani ya "bomu la nyuklia".

Rafiki mpendwa wa Sadako alimwambia hekaya ya zamani ya Kijapani kwamba mtu yeyote aliyekunja korongo elfu moja wa karatasi atapewa matamanio. Sadako alitaraji kwamba miungu itampa matamanio ya kupona ili aweze tena kukimbia. Alianza kutengeneza korongo wa karatasi na kumaliza zaidi ya 1000 kabla ya kufariki tarehe 25 Oktoba, 1955 akiwa na umri wa miaka 12 tu.

Wakiwa wametiwa moyo na ujasiri na nguvu zake, marafiki na wanafunzi wenza wa Sadako walitunga kitabu kilichokusanya barua zake na kukichapisha. Wameanza kuwa na ndoto za kujenga mnara kwa ukumbusho wa Sadako na watoto wote waliouliwa na bomu la nyuklia. Vijana wote wa nchini Japani walisaidia kukusanya fedha kwa ajili ya mradi.

Mwaka 1958, sanamu ya Sadako ikishika korongo wa dhahabu ilizinduliwa katika Bustani ya Wananchi ya Amani ya Hiroshima (Hiroshima Peace Park). Watoto pia wamefanya matamanio yaliyochangwa kwenye kitako cha sanamu yaliyosomeka; **"Hiki ndicho kilio chetu, hii ndiyo sala yetu, Amani Duniani"**

Leo watu duniani kote wanakunja korongo wa karatasi na kupeleka kwenye sanamu ya kumbukumbu ya Sadako, Hiroshima.

> Fanya majadiliano kuhusu namna ugomvi na migogoro kati ya watu na nchi vinavyoathiri watu wasio na hatia. Toa hitimisho kuhusu umuhimu wa kuhimiza amani na maelewano. Jadili namna hadithi ya Sadako inavyosaidia kujenga uelewa wa umuhimu wa kujifunza namna ya kuishi pamoja kwa heshima na utu.

> Wagawie karatasi washiriki na wafundishe namna ya kutengeneza korogo wao wenyewe. Wape muda waandike sala yao ya amani kwenye karatasi kabla ya kutengeneza korongo. Wahimize wafikirie kuhusu hadithi ya Sadako na madhara ya maafa ya nyuklia huko Hiroshima.

> Hitimisha shughuli yako kwa kukaa kimya kwa dakika moja kwa kuombea amani duniani kwa wathirika wa vita na kukosekana maelewano kati ya watu na mataifa.

Hata kama shughuli hii inaweza kuendeshwa wakati wowote, inafaa zaidi kufanyika tarehe 6 Agosti, kuambatana na kumbukumbu za mwaka kwa waathirika wa mashambulio ya mabomu ya nyuklia ya Hiroshima na Nagasaki.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logo yao ya Kujifunza

### Maelezo yangu

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

# Kuchora kwenye Fulana

**Madhumuni**: Kuwashirikisha washiriki katika shughuli itakayowasaidia kutafakari kuhusu utambulisho wao.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wametafakari kuhusu utambulisho wao na namna wanavyotaka kujidhihirisha kwa dunia. Pia wanaunda kitu kinachovutia na chenye thamani wanachoweza kukitunza na kukivaa.

**Vifaa vya Kufundishia:** Washiriki ama wanapewa au wanaleta fulana zao nyeupe. Vifaa vya kuchorea kwenye nguo, rangi inayofaa, brashi za ukubwa tofauti, stensili, n.k. karatasi zisizo na mistari na kalamu za rangi za kusawidi ubunifu wao.

## Shughuli

Ni muhimu kwa washiriki kupata muda wa kutafakari na kujadili kile watakachochora kwenye fulana.

Waambie watafakari kuhusu kile wanachotaka kuchora kwenye fulana kama tamko lao na mambo wanayothamini. Wakumbushe washiriki kuwa fulana zao zitaonekana na watu wengine wanaoweza kufanya mahitimisho ya haraka kuhusu wao kutokana na kile ambacho nguo zao zinaonyesha. Itasaidia sana kama tayari wamemaliza shughuli **Kubadilishana uzoefu** ili washiriki wajisikie vizuri kuzungumzia mambo ya maana kuhusu utambulisho wao.

Wape washiriki karatasi na kalamu za rangi kwa ajili ya kusawidi ubunifu wao – wakumbushe kwamba ubunifu wao hauna budi hatimaye kuenea kwenye fulana zao.

Wakisharidhika na usanifu wao, warudufu kwenye fulana zao.

Washiriki wavae fulana zao na washirikiane kile walichochora pamoja na kikundi chote.

Karibu mwisho wa kipindi, wape muda wa kutafakari kuhusu kile ambacho washiriki wamechora na ujumbe wa kwenye fulana zao unaohusu utambulisho wao na umuhimu wa kuthamini sisi ni kina nani na wengine nao ni kina nani.

Pia kama fulana zinaweza kuchukua ujumbe, unaweza pia kuzungumzia kuhusu kile ambacho watu wengine wanaweza kuandika kwenye fulana, zao kama vile, wale wanaoishi kwenye maeneo ya migogoro.

Unaweza kupiga picha ya kila mshiriki akiwa na ubunifu wake au fulana yake na kuwapa kama ukumbusho wa warsha.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Shajara yao ya Kujifunza

# Kutengeneza Filamu

**Madhumuni:** Kuwahimiza washiriki watafakari kuhusu mada wanayoipenda na kujenga uelewa kuhusu mada hiyo kwa njia ya filamu.

**Matokeo:** Washiriki wawe wametengeneza filamu watakayoionyesha kuongeza uelewa kuhusu suala watakalochagua.

**Vifaa vya Kufundishia**: Kamera ya video, kanda za video na kompyuta ya kuhariria.

## Shughuli

Anza kuwafundisha mada ya kutengeneza filamu kama njia ya kuongeza uelewa kuhusu mada mahususi. Waambie washiriki kuwa kuna fursa kwao ya kutengeneza filamu fupi. Eleza kuwa utatafuta mahali ambako washiriki wataonyesha filamu yao, kwa marika yao, kwa hadhara au kwa viongozi wa ngazi za juu.

Kwa kutumia njia mbalimbali – bungua bongo, majadiliano au mikutano ya majadiliano – washiriki watachagua mada yao. Uwashawishi washiriki kuchagua mada inayohusiana na matatizo ya kijamii au itakayowasaidia kujifunza zaidi kuhusu uanuwai, ama kitaifa au kidunia.

Kuna rasilimali za kitaalamu zitakazowasaidia washiriki wako kutengeneza filamu (jaribu kuangalia http://www.filmyourissue.com/making/index.shtml) na itasaidia sana kama utamleta pia mtu mwenye utaalamu na ataweza kusaidia. Washiriki lazima wawe na udhibiti mkubwa wa kutoa uamuzi kadiri iwezekanavyo na kufanya kazi kwa ushirika – ambao ni mwelekeo mkuu wa shughuli hii.



## Kabla ya Kuanza

1. Bainisha madhumuni ya video yako.
2. Bainisha walengwa wanaokusudiwa.
3. Angalia vipingamizi ikiwemo, muda, fursa za upigaji filamu, uwezekano wa kuhariri.
4. Chora ubao wa hadithi (mfuatano wa video).
5. Jadili kile ambacho washiriki wangependa kuona kwenye video (mahojiano, michoro, vibonzo, taswira, nyimbo).
6. Gawa majukumu miongoni mwa washiriki. Baadhi yao watafanya mahojiano, wengine watafanya utafiti, ikiwezekana kuendesha taftishi, baadhi watatengeneza sanaa, kutafuta taswira na muziki, wengine watapiga video na wengine watahariri.

## Baada ya kutengeneza filamu

Jadili mchakato wa uhariri na washiriki ili kila mmoja aweze kuchangia kwenye sehemu ya mwisho itakayokatwa, Baada ya kukamilika kwa filamu na kuiangalia, hakikisha kuwa washiriki nao wanatafakari kuhusu uvumbuzi waliofanya wakati wakifanya filamu.

Hii ni kazi inayoweza kuchukua miezi kadhaa, kwa hiyo hakikisha unadumisha hamasa ya washiriki wote. Fanya mikutano ya mara kwa mara na mapitio na panga tarehe ya uzinduzi wa mwisho.

Unaweza kuwa na uangaliaji wa filamu wa faragha kwanza na wazazi na washiriki. Kulingana na tukio hili unaweza kujadili namna bora ya kuonyesha filamu kwa walengwa.

Video zinaweza kuingizwa kwenye Intaneti na kupelekwa kwenye matamasha ya filamu au kwenye mitandao ya Web. 2.0, kama vile YouTube. Siku ya Kimataifa ya Utangazaji ya Watoto inasheherekewa kila jumapili ya mwezi Desemba, siku hiyo watangazaji wa vipindi vya TV duniani kote wanatenga muda wa matangazo yao kwa filamu zilizotengenezwa na vijana kama sehemu ya Ibara ya 12 – haki yao ya kusikika.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

### Maelezo yangu

# Chemsha Bongo –
# Je, ninaelewa nini kuhusu dini nyingine?

**Madhumuni:** Kujifunza kuhusu imani za watu wengine na tofauti za kidini kwa njia ya mzaha.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wamejifunza kuhusu desturi za dini mbalimbali na mila zao.

**Vifaa vya Kufundishia:** Maswali, vipande vya karatasi, picha au vitu vya dini mbalimbali.

## Shughuli

Kwa kawaida vijana huwa wanafurahia sana chemsha bongo. Chemsha bongo hii haikusudiwi kuwa tathmini bali mchakato wa uvumbuzi anaoufanya mtu. Tumia chemsha bongo kwa namna ya ubunifu na ushirikianaji.

Tayarisha maswali mengi kuhusu dini mbalimbali. Kwa kupata mifano michache, rejea kwenye maswali ya Mfano wa Chemsha Bongo kuhusu dini nyingine kwenye ukurasa wa 113. Inafaa zaidi vilevile kuwaambia washiriki wako watayarishe maswali ya chemsha bongo kuhusu dini za ulimwengu. Unaweza kuyakusanya maswali haya na kuwa kama hazina ya chemsha bongo au washiriki wanaweza kugawanywa kwenye timu na kuulizana maswali. Kila mmoja atalazimika kuuliza maswali mengi kwa kuwa baadhi wanaweza kuuliza mara nyingi.

Njia nyingine ni kuandika maswali na halafu kuyapa namba kila moja kwenye karatasi. Bandika karatasi ukutani na ambatisha na majibu, chini – juu (pindu) ili yasiweze kusomwa kutoka mbali.

Gawa washiriki katika vikundi vya watu watatu au wane halafu wapeane zamu ya kujibu maswali hayo. Mchague mshiriki kutoka kikundi kimoja na mwambie ajibu kila swali. Anaweza kuchagua maswali kutoka ukutani, lakini kikundi kinaweza kumsaidia kujibu. Kadiri mchezo unavyoendelea, ndivyo idadi ya maswali itakavyopungua.

Kama inawezekana, fafanua zaidi maswali kwa kuonyesha picha, taswira au vitu halisi, kama vile Bendera ya Kibuddha, Msalaba, biblia, Picha ya Torah, Picha za Buddha au Picha za Msikiti.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

## Maelezo yangu

# Maswali ya Mfano na Chemshabongo kuhusu dini nyingine

1. Je, Mohammed alikuwa nani?
2. Je, Buddha alikuwa nani?
3. Je, neno "Kristo" lina maana gani?
4. Je, Yesu alikuwa nani?
5. Kippa ni nani?
6. Je, imani ya roho ya mfu kuingia kwa mtu mwingine, ni nini?
7. Je, Tirthankara ni nini kwa wafuasi wa Jaini?
8. Hija ni nini?
9. Je, jina la Mungu kwa Waislamu na Wayahudi linaitwaje?
10. Je, Yesu alikuwa na wanafunzi wangapi?
11. Je, Mtume Mohamed alizaliwa lini?
12. Je, kwa dini ya Hindu, Brahman lina maana gani?
13. Veda ni nini?
14. Je, kitabu kitukufu cha Waislamu kinaitwaje?
15. Je, mahali wanaposali Wayahudi panaitwaje?
16. Guru ni nini?
17. Siddhartha Gautama alikuwa nani?
18. Je, neno 'Buddha' lina maana gani?
19. Je, Yesu alizungumza lugha gani?
20. Je, neno Tripitaka kwa lugha ya Sanskrit lina maana gani?
21. Je, bendera ya Kibuddha ina rangi gani?
22. Taamuli ni nini?
23. Je, kitabu kitukufu cha Wayahudi kinaitwaje?
24. Je, Baha 'u' llah alikuwa nani?
25. Kwa maana gani na kwa nini Wahindu wanasheherekea Divali?
26. Je, Hamukkah ni nini na inatekelezwaje?
27. Je, Ramadhan ni nini na inatekelezwaje?
28. Katika dini ya Kihindu, Shiva ni nani?
29. Maandiko matakatifu ya Singasinga yanaitwaje?
30. Je, nguzo kuu tano za Kiislamu ni zipi?

# Visiwa Vinavyotoweka

**Madhumuni:** Kutambulisha mada ya ubadilishaji wa mgogoro na mibadala isiyotumia nguvu au ugomvi.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wametafakari kuhusu migogoro na vyanzo vyao. Washiriki watakuwa wametafuta umuhimu wa kujenga hali ya kuridhiana.

**Vifaa vya Kufundishia:** Kurasa za magazeti na muziki uliorikodiwa.

## Shughuli

Tandaza kurasa za magazeti kweye sakafu huku kukiwa na nafasi kati yao. Anza na kurasa nyingi za magazeti. Kila ukurasa unawakilisha Kisiwa kimoja. Piga muziki na waambie washiriki watembee visiwani bila ya kuvikanyaga. Waambie wakanyage kwenye kisiwa wakati muziki unaposimama. Simamisha muziki kila baada ya muda.

Ondoa kisiwa kimoja kila unapoanzisha tena muziki, kwa hiyo idadi ya visiwa itapungua hatua kwa hatua na kila kimoja kinakuwa na msongamano wa watu. Hatimaye hakutakuwa na nafasi kwa washiriki wote, wale watakaoshindwa kufika kisiwani watatoka kwenye mchezo. Endelea na mchezo mpaka kibaki kisiwa kimoja tu na washiriki wengi wametolewa mchezoni.

## Tathmini baada ya shughuli kumalizika

Baada ya mchezo kumalizika, jadiliana na washiriki kuhusu kilichotokea. Unaweza kuuliza baadhi ya maswali yafuatayo:

> Kulitokea nini baada ya kuwa na visiwa vichache zaidi?
> Je, watu walikuwa na hoja gani?
> Je, ulihisi vipi wakati uliposhindwa kufika kisiwani na kuwa nje ya mchezo?
> Je, ulilindaje nafasi yako mwenyewe?
> Je, uliwasaidia wenzako?
> Je, hii ni sawa na kinachotokea katika maisha halisi?

Husisha mchezo huu na hali halisi na fanya majadiliano na washiriki kuhusu rasilimali na sababu za migogoro. Waambie washiriki kuwa migogoro ni ya kawaida lakini wakati mwingine inaweza kuwa ugomvi iwapo watu wanashindwa kushirikiana, kugawana na kuwa katika mshikamano na wengine. Tunaelekea kutatua migogoro kwa kujifikiria sisi wenyewe tu; lakini kwa nini tusishirikiane kubadili hali ili kusiwe na wanaokosa?

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Mpira Hewani

**Madhumuni:** Kukuza stadi za timu kuweza kufanya kazi pamoja na kujenga daraja za kuaminiana miongoni mwa washiriki.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wamejifunza namna ya kuwasiliana vizuri na watu wengine na kukuza stadi za kufanya kazi pamoja kwa kufikia lengo la pamoja.

**Vifaa vya Kufundishia**: Mpira mmoja mdogo na mwingine mkubwa.

## Shughuli

Wafahamishe washiriki kuwa watacheza mchezo wa mpira ambapo mpira itabidi uwe hewani kwa muda mrefu kadiri iwezekanavyo. Katika kikundi cha watu wasiopungua 10 na wasiozidi 40, wanatakiwa wapige mpira kwa mikono yao na kuzuia usidondoke. Lengo ni kuhakikisha kubakia mpira juu mara nyingi iwezekanavyo na kupigwa kwa mfululizo kadiri iwezekanavyo.

Anza mchezo kwa kutumia mpira mdogo. Utagundua kwamba mwanzoni washiriki wengi wanapiga mpira bila ya kuzingatia mawasiliano ya watu wengine kwenye timu au hoja ya kujifunza namna ya kufikia lengo pamoja. Kama mpira unaanguka chini, wahimize washiriki wafikie idadi kubwa ya upigaji na kila mara jitahidi kufikia lengo kubwa zaidi.

Mara baada ya washiriki kugundua namna ya kupata kupiga kwa mfululizo, badili mpira mdogo na chukua mpira mkubwa. Kwa kuwa mpira ni mkubwa itakuwa ni vigumu zaidi kuupiga bila ya kuacha uanguke. Himiza ushiriki wa watu wote na kuwa makini kupata alama za juu zaidi.

Baada ya washiriki kupata idadi kubwa na kuhisi kuridhika na matokeo, tafakari pamoja nao walichojifunza kutokana na mchezo huo. Baadhi ya maswali utakayowauliza ni pamoja na:

1. Je, ulijisikiaje kucheza mchezo huu?
2. Je, nini lengo la mchezo huu?
3. Je, ni vipengele gani vilivyochangia kupatikana kwa matokeo mazuri?
4. Kwa nini mwanzoni walishindwa kupata idadi kubwa ya upigaji?
5. Je, mchango wa kila mshiriki wa timu ulikuwa nini?
6. Je, kwa nini kila mtu alikuwa muhimu katika kufikia lengo?
7. Je, timu ilitumia mbinu gani?
8. Je, ushirikiano ulikuwa muhimu katika kufikia lengo?

Shawishi kila mshiriki kueleza uzoefu wake na kuonyesha umuhimu wa kukuza stadi za mawasiliano ili kuweza kufanya kazi vizuri zaidi na wengine. Hitimisha kipindi kwa kuwauliza washiriki namna wanavyoshirikishana na wenzao na kwa nini ushirikiano ni muhimu katika jamii yenye watu tofauti.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Kujifunza kutoa Huduma

**Madhumuni:** Kujenga fursa kwa washiriki kupata mvuto wa kuwasaidia watu wengine ambao ni tofauti na wao na ambao wamenyimwa haki zao.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wamepata uelewa kuhusu umuhimu wa watu wengine na wametafakari namna kukosa heshima kunavyosababisha ukiukaji wa hadhi ya utu.

## Shughuli

Wahimize vijana waanzishe shughuli za kujitolea na zinazowahusu watu ambao wamenyimwa haki zao au haki zao zimekiukwa. Shughuli hizo zinaweza kujumuisha:

> Wakimbizi.
> Watu waliohamishwa makazi.
> Watu wenye mahitaji maalumu.
> Watu wasiobahatika – yaani ambao hawakupewa umuhimu.
> Wahamiaji wanaoishi katika hali duni.
> Watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri.

Shughuli hizo zinaweza kuwa sehemu ya darasa lako au kufanya sehemu ya shughuli za shule kama namna ya kuhimiza huduma kwa jamii na huduma za kiroho.

## Mwongozo wa utayarishaji na uendelezaji wa shughuli ya kujifunza kutoa huduma



> Kusanya taarifa kuhusu hali jijini kwako ambako hadhi ya utu imekiukwa.
> Tayarisha orodha ya mashirika jijini kwako yanayowahudumia watu wasiobahatika – yaani ambao hawakupewa umuhimu au ambao haki zao za binadamu zimekiukwa.
> Wasiliana na shirika moja au mawili ambayo unadhani vijana wako wanaweza kufanya shughuli za kujitolea.
> Pata makubaliano na shirika/mashirikia kutayarisha programu ya kujitolea inayowashirikisha vijana wako.
> Mwombe mkurugenzi wa shirika au mratibu kuzungumza na washiriki kuhusu kazi yao na watu wanaohudumiwa.
> Amua kuhusu aina ya msaada unaohitajika na shughuli zipi wanazoweza kufanya washiriki wako: shughuli za burudani, kupiga muziki, kutayarisha mchezo wa kuigiza, mafunzo (k.m. kuchora, kushona, muziki, hisabati, kusoma na kuandika) au msaada wa jumla (k.m. kusaidia kununua vitu, kuandika barua).
> Pamoja na washiriki wako, bainisha lengo moja au mawili ambayo watajaribu kufikia ifikapo mwisho wa programu au katika kipindi Fulani.
> Tayarisha vipindi vya kutafakari pamoja na washiriki kugundua uzoefu wao:
- Walichojifunza wakati wa shughuli ya kujitolea.
- Wanavyojihisi wakati wanapowahudumia au kuwasaidia watu wengine.
- mambo tofauti na ya kufanana wanayoshirikiana na watu hao.
- Namna watakavyoepuka kumvunjia mtu haki zake za binadamu.
- Kwa nini wanadhani makabila madogo wanakabiliwa na ubaguzi.
- Linganisha ubaguzi huo na ubaguzi wa kidini na madhara yake.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Kampeni za Kujifunza Dini Mbalimbali

**Madhumuni:** Kutoa nafasi kwa washiriki kutayarisha kampeni za ubunifu na kuhimiza kujifunza dini mbalimbali.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wametayarisha shughuli za dini mbalimbali kama njia ya kuhimiza kuheshimu imani za watu wengine. Washiriki watakuwa na dhamira ya kuchukua hatua kusaidia kujemga maelewano baina ya watu.

## Shughuli

Kuhimiza washiriki kuanzisha kampeni shuleni kwao na kwenye mashirika kwa kutia mkazo umuhimu wa kuheshimu dini na imani mbalimbali.

Kampeni za namna hiyo zinaweza kuwa za aina mbalimbali; ifuatayo ni baadhi ya mifano:

## Kampeni za Mawasiliano na kujifunza

### Mbao za matangazo

Tayarisha ubao wa matangazo unaotoa maelezo kuhusu imani za watu wengine, sherehe, matamasha na habari: Kikundi cha wanafunzi kinakusanya taarifa mara kwa mara na kutoa habari mpya na kutunza ubao huo.

### Redio ya dini Mbalimbali

Himiza programu ya redio shuleni ambao wanafunzi wanaweza kuhojiwa kuhusu imani zao.

### Maduka ya Dini Mbalimbali

Tayarisha maduka kwa ajili ya kujifunza dini mbalimbali. Maduka hayo yanaweza kuwa na vibanda vyenye taarifa kuhusu dini nyingine, chumba cha filamu kinachoonyesha filamu zinazohusika, vibanda vyenye muziki wa dini, na mikutano ya majadiliano na watu kutoka dini mbalimbali. Maduka hayo pia yanaweza kuwa ni fursa ya kuonyesha maandiko na michoro ya washiriki kuhusu masuala ya dini mbalimbali.

### Majadiliano ya kila mwezi ya dini mbalimbali/migahawa ya dini mbalimbali

Alika wanafunzi kutoka dini mbalimbali wafike shuleni kwako na jadiliana nao imani zao na fanya majadiliano kuhusu mada zenye manufaa.

Wasilisha kampeni kama namna ya kuwafanya vijana wavutike: nia ya kujifunza, kupata maarifa zaidi kuhusu watu wengine na kujua imani za watu wengine.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Kubadilishana ziara za Shule

**Madhumuni:** Kuwapa fursa washiriki kuelewa shughuli za shule kwenye shule tofauti na shule yao na watu wa dini tofauti.

**Matokeo:** Washiriki wanahimiza na kupata uzoefu wa maelewano na kuheshimu imani za watu wengine.

## Shughuli

Wanafunzi wawili, wa darasa sawa lakini kutoka shule mbili tofauti na kutoka dini tofauti wanabadilishana mahali kwa kipindi maalumu kilichopangwa.

Kama shughuli hii itatekelezwa kati ya shule, itahitaji ridhaa ya bodi za shule husika na walimu. Kubadilishana huku kunaweza kufanywa pia kwa mashirika mbalimbali ya dini na vikundi vya vijana. Kufahamiana kati ya wanafunzi kutoka shule na dini mbalimbali kunaweza pia kukuzwa kwa kuwaalika wanafunzi shuleni kwako kila panapotokea tukio au shughuli maalumu.

Kubadilishana ziara za wanafunzi si kama zinazochangia maelewano baina ya watu wa dini mbalimbali tu, bali pia zinasaidia kujenga uhusiano wa kudumu kati ya jumuiya tofauti utakaochangia kuwapo kwa amani zaidi ya baadaye.

Kubadilishana ziara kati ya vikundi mbalimbali vya vijana kunaweza kuhusisha mradi unaohitaji ushirikiano wa vikundi viwili au zaidi, huku washiriki wa kila kikundi wakiwa na wajibu mahususi. Kwa mfano, mradi kama huo unaweza kuhitaji ushiriki wa mwezi mmoja wa watu kutoka dini mbalimbali.

Unaweza kutayarisha programu maalumu ya kubadilishana itakayohusisha kazi mahususi: kushiriki katika Kamati ya Dini Mbalimbali, ushiriki kwenye madarasa ya shule nyingine, midahalo au uendeshaji wa shughuli za dini mbalimbali.

Kama sehemu ya Programu ya Kubadilishana, tenga muda wa kuchunguza mila, dini au utamaduni wa aina mbili ulioletwa pamoja kutokana na kubadilishana. Uchunguzi huu unaweza kuhusisha uwasilishaji wa aina mbalimbali, kuandika makala, au michoro.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

### Maelezo yangu

..........

..........

..........

..........

..........

..........

..........

# Wiki zenye dhamira Maalumu

**Madhumuni:** Kuhimiza uelewa kuhusu desturi za kimaadili ili kusaidia kubadili ulimwengu.

**Matokeo:** Washiriki wawe wamezindua juhudi za kuhimiza uelewa kuhusu desturi za kimaadili katika jumuiya zao, ili kuimarisha maelewano na heshima.

## Shughuli

Wiki zenye dhamira maalumu zinazohimiza desturi za kimaadili zinaweza kushawishi uelewa miongoni mwa watu na kusaidia kuleta amani kwenye jamii zao.

Wiki zenye dhamira maalumu zinaweza kuzingatia mada kama vile 'usuluhishi' 'kusameheana', 'huruma' au "uaminifu", n.k. Nia ni kuhimiza desturi za kimaadili kwa kuonyesha namna maelewano na heshima vinavyonufaisha jamii na kusaidia kubadili ulimwengu kuwa mahali bora zaidi.

Waambie vijana waongoze uandaaji wa Wiki Maalumu. Kama ni lazima wanaweza kupanga wiki maalumu nyingi, zitakazotokea mara kwa mara. Watu wa kujitolea wanaunda kamati ya maandalizi kwa kila wiki.

Wahimize watayarishaji hao vijana kupanga shughuli nyingi za aina mbalimbali, lakini kumbuka kupata idhini ya mamlaka za shule. Yafuatayo ni baadhi ya mawazo:

- Majopo yanayohusu mada, ambapo dhamira ya wiki hiyo inajadiliwa na wageni maalumu au na watu kutoka shuleni hapo.
- Kikao cha Filamu: onyesha na jadili filamu zinazohusiana na mada.
- Maigizo Dhima yaliyotayarishwa na wanafunzi.
- Mbao za matangazo, zinazozingatia matukio yaliyopita yanayoonyesha mfano wa dhamira.
- Maonyesho ya muziki, yenye muziki au nyimbo zinazohusika.
- Mashindano: toa zawadi kwa michoro bora, mashairi au insha kuhusu mada.
- Ibada ya amani.

Fanya Wiki yenye dhamira Maalumu kuwa rasmi katika shule yako au kikundi na himiza wiki kama hizo katika jiji lako.

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

### Maelezo yangu

......................................................................

......................................................................

......................................................................

......................................................................

......................................................................

......................................................................

# Kampeni za Haki za Mtoto

**Madhumuni:** Kuongeza uelewa wa Mkataba kuhusu Haki za Mtoto.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wamejifunza kuhusu haki zao na namna ya kuzihimiza. Watakuwa wameelewa umuhimu wa kuhimiza haki hizo kwa watoto wote, bila ya kujali dini au utamaduni wao.

## Shughuli

Shughuli hii inasaidia kueneza uelewa wa Mkataba kuhusu Haki za Mtoto (CRC), sheria ya haki za binadamu ya kimataifa iliyoridhiwa na nchi 193 kati ya 195 duniani.

Vijana watakuwa na sheria ya kuwafungamanisha na wenzao duniani kote kwa kujua kwamba wote wana haki zinazotambuliwa na kuelezwa vizuri duniani kote.

Kuendesha kampeni za uelewa za mara kwa mara kwenye shule na vikundi vya vijana kunasaidia kueneza maarifa ya haki hizo na nafasi yao katika kuwalinda watoto wote, bila ya kujali rangi yao, utamaduni au imani yao ya dini. Kampeni hizi zinaweza kuwa za aina mbalimbali. Unaweza kulenga haki mahususi au seti ya haki au kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi. Ushirikiano na shule nyingine, mashirika au vikundi vya dini tofauti unahimizwa.

## Baadhi ya mifano ya matukio ya kila mwezi:

**Mwezi wa ushirikishwaji wa watoto (kwa mujibu wa ibara ya 12)**

Watoto wanaweza kushiriki kwenye midahalo, majopo na mikutano iliyoandaliwa na shule au mashirika mengine kuhimiza demokrasia na maelewano. Ni muhimu kuwapo kwa watoa uamuzi na kusikiliza watoto hao.



**Mwezi wa maoni na imani za watoto (kwa mujibu wa ibara ya 13 na 14)**

Watoto wanaeleza mawazo yao, imani zao za dini na utamaduni wao.

**Mwezi wa mambo anuwai (kwa mujibu wa ibara ya 30)**

Watoto wanatayarisha shughuli za kuhimiza ujumuikaji na makundi ya dini ndogo, vikundi vya wenyeji wa asili na wahamiaji kwa lengo la kujifunza kutoka kila upande.

Ujumla na umataifa wa Mkataba kuhusu Haki za Mtoto lazima utiliwe msisitizo. Washiriki hawana budi pia kuelewa kuwa utimizaji wa haki zao za ulinzi, utoaji huduma (chakula, elimu), maendeleo na ushirikishwaji zinafuatiliwa kwa karibu na Kamati ya Haki za Mtoto, ambako kila nchi haina budi kuwasilisha ripoti.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Utayarishaji wa Miradi

**Madhumuni:** Kuwawezesha washiriki kuhusishwa katika ubadilishaji wa hali inayowahusu.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wameshawishiwa kuchangia katika uhimizaji wa amani na haki duniani.

## Shughuli

Waambie washiriki wabuni mradi utakaosaidia kubadili jamii zao. Mradi hauna budi kukamilishwa kwa tarehe watakayokubaliana.

Washiriki waunde vikundi visivyozidi watu kumi kila kimoja na wanatakiwa wabuni mradi wa kubadili tatizo au hali kwenye jamii iwe shuleni kwao, jijini au nchini kwao – utakaofanikishwa ndani ya miezi michache.

Baadhi ya miradi itahitaji kuungwa mkono na wakurugenzi wa shule au viongozi wa shirika lako na kuzinduliwa kama programu ya kawaida. Miradi hii itawezesha kuwahusisha watu wengi zaidi. Itakuwa muhimu pia kupata misaada ya fedha za mradi.

Miradi haina budi kukidhi vipengele mahususi, vitakavyoamuliwa na washiriki. Kwa mfano hauna budi:

- Kuwa na mwelekeo wa dini mbalimbali.
- Kuwa thabiti na unaoeleweka.
- Kuzingatia desturi za kimaadili.
- Kusaidia kubadili hali mahususi.
- Kuwa wa ubunifu.
- Kuwa na lengo la kutatua tatizo.

Programu ya utayarishaji wa mradi inaweza kufanywa kwa wanafunzi wa vidato vya juu na ikipewa utaratibu mzuri na unaofaa, inaweza kuhesabiwa kama alama ya kufaulu kwa baadhi ya masomo.

Tayarisha sherehe maalumu, waalike wazazi na wageni maalumu, na wape fursa washiriki wawasilishe miradi yao.

Filamu zinaweza kuwa njia inayofaa sana kuwamotisha wanafunzi na kuchochea fikra zao. Filamu zilizopendekezwa ni: *Pay it Forward* na *Schindler's list.*

## Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Mazungumzo baina ya Dini Mbalimbali

**Madhumuni:** Kuhimiza maelewano kwa kuwakusanya pamoja watu kutoka dini mbalimbali katika mazungumzo kuhusu namna ya kusaidia kubadili ulimwengu.

**Matokeo:** Washiriki watakuwa wamechangia katika kuongezeka kwa maelewano kati ya watu kutoka dini mbalimbali. Washiriki watakuwa wametafuta uwezekano wa kuleta mabadiliko duniani kupitia mtazamo wa upatanishi.

**Vifaa vya kufundishia:** Vifaa vya Utangazaji, vipande vya karatasi na kalamu.

## Shughuli

Mazungumzo baina ya dini Mbalimbali yamekusudiwa kujenga maelewano na namna ya ushirikiano kati ya watu wa dini tofauti. Majadiliano kati ya dini mbalimbali yanatayarishwa kwa kuzingatia mada maalumu, kwa mfano: kutoheshimiana, imani kali, uhusiano kati ya dini, upatanishi na kusameheana, namna kila dini inavyoelewa na kushughulikia amani, na kulinda haki za watoto.

Washiriki katika kazi yako ya dini mbalimbali watasaidia kutayarisha mazungumzo mengi ya dini mbalimbali.

## Kutayarisha mazungumzo ya dini mbalimbali

- Chagua mada inayohusika.
- Tangaza mazungumzo ya dini mbalimbali katika maeneno tofauti, kama vile shuleni, mahali pa ibada au vikundi vya vijana, kutegemea ni kwa kiasi gani iwe au isiwe rasmi unataka tukio hilo liwe.
- Hakikisha kwamba una wawakilishi kutoka dini tofauti.
- Tayarisha maswali mapana na ya wazi kusaidia majadiliano kuleta matokeo mazuri.
- Chagua mwenyekiti wa majadiliano na mwambie atambulishe mada kwa kutoa sehemu ya taarifa na kuibua maswali ya msingi. Mwenyekiti huyo pia anaweza kutaka kutambulisha wazungumzaji.
- Waambie washiriki wakae kwenye mduara, kwa hiyo kila mmoja ni sawa na anaweza kumwona na kumsikia kila mmoja.
- Hitimisha mazungumzo ya dini mbalimbali kwa kuuliza, Je, sasa tunaweza kufanya nini kwa pamoja?

Hitimisha mkutano kwa sala ya amani na kuelewana. Unaweza kuwaambia washiriki kuandika sala zao na kuzisoma kwa sauti, kama wanataka.

### Waambie washiriki waandike kuhusu shughuli kwenye Logu yao ya Kujifunza

# Sehemu ya 5

# Nyenzo

## Hadithi

*Watu wangu, naomba msikilize mafundisho yangu;*
*tegeni masikio yenu kwa maneno yanayotoka mdomoni mwangu.*
*Nitafumbua mdomo wangu kwa hadithi yenye maadili;*
*Nitasema misemo ya kale kutoka kwa wahenga,*
*mambo ambayo tumeyasikia na kuyajua,*
*ambayo wahenga wetu walituambia.*
*Hatutayaficha kwa watoto wao;*
*tutakiarifu kizazi kijacho*
*matendo adhimu ya Mungu, na uwezo wake,*
*na maajabu ambayo ameyafanya.*

Aya hizi kutoka Biblia ya Kiyahudi (Ps 78:1-4) inatoa mwanga upande mmoja wa maana ya kuwa binadamu: Ili kufikia ndani ya keto za nafsi za kila mmoja wetu, hadithi hii zaidi ya kitu kingine chochote, inavuka kizingiti na kutuingia kwenye nafsi zetu. Mungu au Mwisho au Ukweli au Busara au mpita uwezo wa binadamu au asiyefahamika vizuri au anayepita wote, maneno yote haya – yanapatanishwa kwenye hadithi hizi. Hadithi inatoa mwangi wa misemo kutoka katika mila na desturi za zamani, tuliyoyasikia na walichotuambia wahenga wetu. Hadithi zinaridhishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Zinadumu kwa kumbukumbu na ndiyo mamlaka yao. Hivi ndivyo zinavyotoa utambuzi kwa kizazi kipya. Hazidai kwamba ni ukweli usiopingika, na hazina haja ya kufanya hivyo, kwa sababu zinakubalika kama aina nyingine tofauti ya ukweli kuliko ule ambao hufundishwa na ni nadharia. Kusema kweli kutakuwa na ukweli zaidi katika hadithi ya kubuni, na uwongo mwingi katika hadithi inayotumia hoja. Kutamba hadithi anasema Hannah Arendt, kunafichua maana bila ya kufanya kosa la kueleza maana yake.[1] Hii ndiyo nguvu na uwezo wa hadithi. Maana inadokezwa tu na haidhihirishwi kwetu kama jalada. Inatambuliwa lakini haiingii akilini. Ipo lakini haionekani.

Hadithi zinaunganisha mbingu na ardhi, ukweli halisi na ambao ni mgumu zaidi kueleza kwa ufasaha au kuelewa. Hadithi zinaweza kufungulia mambo ya zamani, zinaifanya leo irindime, katika ukomo usio na mwisho na zina maana kwa siku zijazo. Mshairi na mwandishi wa riwaya wa Nigeria Ben Okri anasema; "Hadithi zinaweza kushinda hofu kama ujuavyo. Zinaweza kukuza mioyo."

Sote tunapenda kusikiliza hadithi. Mtoto aliye kitandani kabla ya kulala, watu waliojikusanya kumzunguka mtamba hadithi karibu na mahali pa kuotea moto, wakifurahia maneno, wakitikisa vichwa, wakitabasamu, wakicheka na wakidukuana kwa kiwiko kwa furaha. Kuna umoja na ushirikiano katika kusikiliza pamoja hadithi. Ingawa pengine ni kweli kwamba teknolojia, vyombo vya habari shirikishi, michezo ya kompyuta ya tamaduni mbalimbali hutoa hadithi za kiwango kikubwa, matukio ya kuvutia sana, maelezo ya kusisimua mwili, mvuto wa hadithi ni sehemu ya kuwa binadamu. Katika mila na utamaduni wa Wayahudi, inasemekana kuwa binadamu hayuko peke yake katika kufurahia utambaji wa hadithi. Swali linaulizwa, "Kwa nini Mungu amemuumba binadamu?." Na jibu linatolewa "Kwa sababu Mungu anapenda kusikiliza hadithi nzuri."

1 Hannah Arendt ( 1976-1975), mnadharia na mwana falsafa, *Origins of storytelling*, Bartlett's Book of Quotations.

Hadithi inawawezesha watoto kuingia katika ulimwengu mwingine, ambao wakati huo huo unafahamika vizuri au kutofahamika. Hadithi inaanza kwa maneno ya mvuto, “Hapo zamani za kale”. Kwa kiarabu utambaji wa hadithi unaanza kwa kusema: *Ken ye me ken*, “ilikuwa na haikuwa” na kila mtu anaelewa kwamba muda wa hadithi umewadia. Au wakati baadhi ya watu nchini Iran wanatamba hadithi, wanaanza kwa kusema: *Yeki bud, yeki nabud*, “Alikuwapo mtu, hakuwapo mtu yeyote.” Na kila mtu anatulia na kusikiliza na kuingia kwenye ulimwengu, ambao haya yote yanawezekana. Hadithi si hadithi na masimulizi tu, bali ni hisia kwenye kila kiwango ambacho ina maana kuwa binadamu. Hakuna atakayeota kufanya imani isiyo na hoja au mapendekezo ya kinadharia yanayotokana na hadithi. Hadithi zinatokea katika mazingira ambayo pana mtu na pale pasipo na mtu au pale inapotokea au pale ambapo haitokei.

Utambaji wa hadithi unatokea katika ulimwengu halisi, lakini hadithi yenyewe si ulimwengu halisi. Ni ulimwengu tofauti kabisa, ambao unahusiana zaidi na mwanga hafifu wa machweo. Aina mbili za mwanga zinakutana: mwanga wa mchana unakutana na mwanga wa jioni na hakuna anayeweza kusema mwanga mmoja unakoanzia na mwanga mwingine unakoishia. Mmoja uko kizingitini wakati mmoja hauko nje wala ndani. Ni kizingiti tu ndipo tunapoweza kuelewa kwamba aina mbili za ukweli unaosigana haukatazi kila mmoja bali unaweza kuwekwa pamoja kama mvutano wa ubunifu kutuleta karibu na ndani zaidi ya maisha yetu.



## Ngano ya Kichina

Hapo zamani za kale nchini China palikuwa na mvulana mmoja jina lake anaitwa Ping. Mvulana huyu alipenda sana maua na kila mbegu aliyopanda ilikua na kuzaa maua ya kupendeza sana. Mfalme wa zamani aliyetawala China alipenda sana maua pia. Kipindi chake cha kuchagua mrithi wake kilipowadia, aliyaachia maua yachague mrithi. Aliwaalika watoto wote kwenda kwenye Kasri kugawiwa mbegu maalumu za maua. Baada ya mwaka mmoja mtoto mwenye maua ya kuvutia zaidi atachaguliwa kuwa mfalme atakayerithi. Ping alikuja na kundi kubwa la watoto na kuwa na furaha kupita kiasi wakati mfalme alipompa mbegu.

Ping alijaza chungu cha kuotesha maua kwa udongo wenye rutuba sana na kupanda mbegu kwa makini. Alimwagilia maji kwa utiifu mkubwa lakini hakuna kilichomea. Alibadili chungu lakini hakuna kilichomea. Alibadili udongo lakini hakuna kilichoota. Mwaka ukapita.

Watoto wote walivalia nguo zao nzuri sana na kwenda kwenye Kasri na maua yao ya kupendeza. Ping aliona aibu watoto wengine wangemcheka. Baba yake alimshauri aende na mtungi mtupu kwa sababu Ping alijitahidi kila njia.

Wakati Ping alipofika kwenye Kasri ya Mfalme, Mfalme alikuwa akikagua maua yote ya kuvutia lakini alikuwa akikunja uso. Ping aliona aibu sana wakati mfalme alipomwuliza,

“Kwa nini umeniletea chungu kitupu?”

Huku akilia, Ping alijibu, ‘”Nilijaribu kila njia.”

Mfalme alitabasamu, “Nilichemsha mbegu zote!” aliwaambia watoto. “Haikuwa rahisi kwa mbegu hizo kuota! Mtoto huyu ndiye pekee anayestahili kuwa mfalme kwa sababu ameonyesha kuwa ni mwaminifu na mkweli na mwerevu kwa sababu leo amekuja kuniarifu kushindwa kuota kwa mbegu zake! Ana sifa inayofaa kuwa Mfalme wa China.”



*(Unseth, Benjamin (edit). Honesty, Little Books of Virtues, Series One. Garborg’s Inc. Bloomington, 1995, uk. 11 – 13)*

## Mtoto aliyepiga mayowe ya “Uongo”

Kulikuwa na kijana mchunga kondoo aliyechunga kundi la kondoo mbali kidogo na kijiji. Kuna wakati alifikiria kuwafanyia hila wanakijiji na kuwafanyia mzaha. Kwa hiyo alikimbilia kijijini akipiga kelele kwa sauti kubwa:

“Mbwamwitu! Mbwamwitu! Naomba msaada! Mbwamwitu anashambulia kondoo wangu!”

Wanakijiji wema waliacha kazi zao na kukimbilia kondeni alikokuwapo ili wamsaidie. Lakini walipofika pale aliwacheka kwa taabu waliyopata kwa sababu hapakuwa na mbwa mwitu yeyote pale.

Siku nyingine tena mtoto alifanya hila ileile, wanakijiji walikimbilia tena kutoa msaada na aliwacheka tena.

Halafu siku moja mbwamwitu aliingia kweli na kushambulia kundi la kondoo na kuwaua. Akiwa na hofu sana, mtoto huyo alikimbilia kijijini kuomba msaada. “Mbwamwitu! Mbwamwitu! Alipiga yowe. “Kuna mbwamwitu kwenye kundi! Naomba msaada!

Wanakijiji walimsikia lakini walidhani ilikuwa hila nyingine na wote walimdharau na hakuna aliyekwenda kumpa msaada. Na kijana mchunga kondoo akapoteza kondoo wake wote.

Hayo ndiyo yanayowakuta watu waongo, na hata kama wanasema kweli, hawataaminiwa.

*(Unseth, Benjamin (edit). Honesty, Little Books of Virtues, Series One. Garborg’s Inc. Bloomington, 1995, uk. 34 – 36)*

## Ujasiri unaotakiwa kuwa nao

Nilipokuwa mtoto, nilipendwa sana na familia yangu na majirani. Nilistarehe sana kwa kucheza michezo, Rama, Ontario, nilikozaliwa. Wakati nilipofika Darasa la Tatu, ilinibidi nipande basi kila siku kwenda shule kwenye mji wa karibu unaoitwa Orillia.

Siku moja nikiwa shule, mvulana mmoja alinisukuma na nilishindwa kujizuia kumwaga na kutapanya vitabu vyangu ardhini.

"Tafadhali viokote" Nilimwambia.

"Hapana", alijibu kwa ujeuri.

"Viokote", nilisisitiza kwa sauti kubwa.

"Siviokoti, mwanamke we!" Alisema kwa sauti. Mwanamke Mhindi mwekundu wee!

Nilicharuka.

"Okota vitabu vyangu! Ulisababisha nividondoshe."

Nilibwata.

"Jaribu uone, mwanamke wee!" alimdhihaki. Wewe si lolote zaidi ya kuwa mwanamke, Mhindi Mwekundu."

"Fimbo na mawe vinaweza kuvunja mifupa yangu lakini kamwe majina hayawezi kuniumiza" Nilimjibu.

Ghasia hizo zilimfanya mwalimu wetu aingilie kati na kutukaripia wote. Lakini hakuniambia samahani. Nilikasirika sana. Amenifanyia jambo ambalo si zuri.

Nilijisikia mpweke, mwenye hasira, mwenye fahari na mkorofi vyote kwa wakati mmoja. Nilikwenda nyumbani kumwambia mama yangu. Aliniambia niwe imara na kujiamini. Aliniambia Mungu yu pamoja nasi daima, na nisiogope chochote au mtu yeyote.

Ndani ya nafsi yangu nilijua ni mtu wa kabila la asili ya Australia lakini si Mwanamke, Mhindi Mwekundu. Mvulana yule amekosea. Na sasa naelewa kwamba ni lazima nijitetee na kujua kilicho sahihi.

*Imechukuliwa kutoka hadithi ya Peggy Monague, Christian Island, Ontario*
*(Wilson, Lois Miriam, Mary and Me. Wood Lake Books Inc. Winfield, 1992, uk. 62).*

## Hakuna kilicho juu zaidi

Katika mojawapo ya hafla kubwa kwenye kasri ya mfalme, kila mmoja ameketi kulingana na wadhifa akisubiri kuingia kwa Mfalme. Akaingia mtu aliyevaa nguo za kawaida za ovyo ovyo akakaa kwenye kiti kilicho juu kuliko wengine.

Ushupavu wake haukumfurahisha Waziri mkuu , aliyetaka mgeni ajitambulishe.

– Je, alikuwa waziri? – Hapana. Jaribu tena.
– Je, alikuwa Mfalme? – Hapana. Zaidi yake.
– Je, alikuwa Mtume? – Hapana. Jaribu tena
– Je, wewe ni Mungu? "Aliuliza Waziri Mkuu.
– Hapana, niko zaidi yake" alisema mtu maskini.
– "Hakuna kilicho zaidi ya Mungu" alijibu kwa ukali, Waziri Mkuu.
– "Kile ambacho siyo kitu" alijibu, "ni mimi!"

*(Keneth Cragg: The wisdom of the Sufis, London, 76. uk. 8).*

## Panya waliokula Chuma

Hapo zamani za kale kulikuwa na mfanyabiashara tajiri aliyeitwa Naduk. Lakini mambo hayakwenda vizuri na biashara yake ilikwenda vibaya. Aliamua kuhama mji na kwenda kujaribu bahati yake mahali pengine. Aliuza mali zake zote na kulipa madeni. Kilichobaki ni boriti nzito ya chuma. Naduk alikwenda kumuaga rafiki yake Lakshman na kumwomba amtunzie boriti hiyo ya chuma mpaka atakaporudi. Lakshman aliahidi kumtunzia.

Kwa miaka mingi, Naduk alisafiri masafa marefu sana na sehemu mbalimbali, akitafuta bahati yake. Bahati ilikuwa yake kwa sababu alitajirika tena. Alirudi nyumbani na kununua nyumba mpya na kuanza tena biashara yake. Alikwenda kumtembelea rafiki yake Lakshman aliyemkaribisha kwa moyo mkunjufu. Baada ya muda, Naduk alimwomba amrudishie boriti yake ya chuma. Lakshman alijua kwamba boriti hiyo ingempatia Naduk fedha nyingi kwa hiyo hakuwa tayari kumrudishia. Kwa hiyo alimwambia Naduk kuwa aliiweka boriti ile ghalani na panya wamekula.

Naduk hakujali. Alimwambia Lakshman amtume mtoto wake waongozane naye kwenda nyumbani akampe zawadi aliyomnunulia. Kwa hiyo Lakshman alimtuma mwanawe Ramu afuatane na Naduk.

Naduk alimfungia Ramu kwenye ghala ya chini ya ardhi nyumbani kwake. Ilipofika usiku Lakshman alikuwa na wasiwasi na hivyo alifika kuja kuuliza aliko mtoto wake. Naduk alijibu kuwa walipokuwa njiani kuelekea nyumbani kwake, mwewe alimbeba mtoto. Lakshman alimtuhumu Naduk kwa kusema uongo. Naduk alisisitiza kuwa mwewe hawezi kumchukua mtoto wa kiume wa umri wa miaka kumi na tano.

Ugomvi mkubwa ulitokea na suala hilo lilifikishwa mahakamani. Baada ya hakimu kusikiliza maelezo ya Lakshman, alimwamuru Naduk amrudishe mtoto kwa baba yake. Lakini Naduk alisisitiza kuwa mtoto amechukuliwa na mwewe. Hakimu aliuliza ingewezekanaje: Naduk alijibu kama boriti kubwa ya chuma inaweza kuliwa na panya, kwa hiyo mtoto naye bila ya shaka anaweza kuchukuliwa na mwewe.



Naduk alisimulia kisa chote. Kila mtu aliyehudhuria mahakamani alicheka sana halafu hakimu alimwamuru Lakshman amrudishie Naduk boriti yake ya chuma na kwamba Naduk amrudishie Lakshman mtoto wake.

*(Panchatantra – The mice tha ate Iron (1999).*
*(Inapatikana katika:http://www.indiaparenting.com/stores/panchatantra/panch009.shtml)*

## Pepo na Jehanamu

Ngano ya kale ya Kiyahudi inaeleza kisa cha mtu aliyetembelea jehanamu, na kushangazwa kuwakuta wakazi wake wote wameketi katika meza ndefu, zenye vitambaa vya mezani vya kuvutia, vyombo vizuri vya fedha, na vyakula vingi mbele yao. Hata hivyo hakuna aliyekuwa anakula, na wote walikuwa wakiomboleza. Alipoangalia kwa karibu zaidi, hakuna hata mmoja aliyeweza kukunja kiwiko; yaani ingawa waliweza kugusa chakula, hakuna hata mmoja aliyeweza kuingiza mdomoni.

Halafu mgeni huyo alikwenda Peponi, ambako mandhari yalikuwa kama ya Jehanamu, meza ndefu, vitambaa vya mezani vya kuvutia, vyombo vya fedha vizuri na chakula kingi mbele yao. Hapa pia watu hawawezi kukunja viwiko vyao, hata hivyo hakuna aliyekuwa akiomboleza, – kwa sababu kila mtu alikuwa akimhudumia jirani yake.

## Ombaomba

Nilikuwa napita mtaani wakati ombaomba kikongwe mmoja dhaifu aliponisimamisha. Macho yaliyovimba yanayotoka machozi, midomo ya rangi ya bluu, mavazi yaliyochanika mafupi, na vidonda vichafu…

Duuh, umaskini unamtafuna kiumbe yule asiye na furaha!

Alininyoshea mkono mchafu mwekundu…

Alipiga kite kwa sauti nzito ya kuomba msaada.

Nilianza kupapasa mifuko yangu yote… Hakukuwa na pochi, saa wala leso… sina kitu chochote.

Ombaomba kwa upande wake alikuwa bado anasubiri… akiwa amenyoosha mikono yake, ambayo ilikuwa ikitetemeka na kuyumba…

Nilikuwa nimechanganyikiwa, niliutikisa mkono wake mchafu kwa moyo wa upendo… "Usinilaumu ndugu yangu, sina kitu ndugu yangu."

Ombaomba aliendelea kunikodolea macho yake; midomo yake ya bluu ilitabasamu – na kwa upande wake alinibonyeza vidole vyangu kwa upendo.

"Usijali ndugu yangu." Alimunyamunya. "Asante kwa hili pia, ndugu yangu – Na hii pia ni sadaka kwa maskini, ndugu yangu."

Nilielewa kuwa nilikuwa nimepokea sadaka kutoka kwa kaka yangu.

*(Elbert Hubbard's Scrap Book, Wm. H. Wise & co. Roycroft Distributors, New York City, 1923, uk. 9)*



## Mbwamwitu wawili ndani yako

Jioni moja, Cherokee mmoja mzee alimwambia mjukuu wake kuhusu vita vilivyokuwa vinaendelea ndani ya nafsi yake.

Alisema, "Mwanangu, ni kati ya mbwamwitu wawili. Mmoja ni uovu: uliojaa hasira, husuda, huzuni, majuto, choyo, kiburi, kujihurumia, hatia, mfundo, uongo, fahari ya uongo, ubora na ubinafsi. Mwingine ni uzuri: uliojaa furaha, amani, utulivu, unyenyekevu, utu wema, hisani, ushirikali, ukarimu, ukweli, huruma na imani."

Mjukuu alifikiria kwa dakika moja halafu akamuuliza babu yake, "Je, mbwamwitu yupi anayeshinda?"

Cherokee mzee alijibu tu, "Yule ninayemlisha."

## Bado ni Farasi tu

Mtu mmoja kijana alikuja kwa Rabbi Israel wa Rizhyn, akijigamba kuwa alikunywa maji tu, alibingirika kwenye theluji, alivaa misumari kwenye viatu vyake, na aliruhusu achapwe viboko mara kwa mara. Rabbi Israel alimpeleka kijana huyo dirishani na kumwonyesha farasi kwenye uwanja:

"Naye pia anavaa misumari kwenye viatu vyake, anabiringika kwenye theluji, anakunywa maji tu na anachapwa viboko mara kwa mara. Hata hivyo bado yeye ni farasi tu!"

## Mwanasesere wa Chumvi

Baada ya hija ndefu kwenye nchi kavu, mwanasesere wa chumvi alikuja baharini na kugundua kitu ambacho hajawahi kukiona na pengine hawezi kuelewa.

Alisimama imara ardhini, mwanasesere mdogo mgumu wa chumvi, na kuona kwamba kuna ardhi nyingine inayotembea, isiyo salama, yenye kelele, ngeni na isiyofahamika.

Aliuliza bahari, “Lakini wewe ni nani?”

Bahari ikamjibu, “Mimi ni bahari.”

Mwanasesere akasema, “Bahari ni nini?”

Ambapo bahari ilimjibu, “Ni mimi.”

Halafu mwanasesere alisema, “Sielewi, lakini nataka, nitawezaje?”

Bahari ilijibu, “Niguse.”

Kwa hiyo mwanasesere kwa aibu aliingiza mguu na kuyagusa maji na alipata hisia isiyo ya kawaida kwamba ni kitu kilichoanza kueleweka. Alitoa mguu wake na kuona vidole vyake vimetoweka na aliogopa na kusema, “oh” lakini vidole vyangu viko wapi? Je, umenifanyia nini?

Na bahari ilisema, “Umetoa kitu fulani ili uelewe.”

Mwanasesere alizidi kuingia baharini na maji yalichukua chembechembe za chumvi ya mwanasesere na kila mara alikuwa na hisia ya kuelewa zaidi na zaidi na bado ameshindwa kusema kuwa bahari ilikuwa nini.

Wakati alipoendelea kwenye kina zaidi, aliyeyuka zaidi na zaidi, karudia kusema, “Lakini bahari ni nini?” Mwishowe wimbi liliyeyusha mwili wake wote na mwanasesere alisema, “Ni mimi!”

Alikuwa amegundua bahari ni nini lakini bado hakugundua maji yalikuwa nini.

*(Anthony Bloom: Living Power, Libra,London, 1966, uk. 105-106)*

## Amepotelea Msituni

Mtu mmoja amepotelea kwenye msitu mnene na mzito. Kadiri mwanga wa mchana ulivyofifia kwenye vivuli virefu utusitusi na kuongezeka kwa unene wa giza la usiku, ndivyo alivyozidi kuogopa. Baada ya siku tatu za mchana na usiku wa hisia hizi za maumivu ya kupotea bila ya matumaini, alizidi kukata tama.

Hatimaye siku ya nne ya kuhangaika, ilipoingia utusitusi aliona kitu alichodhani kuwa ni jinamizi akitokea mbali kumfuata. Alijaza mfuko wake mawe ya kulitupia na alitayarisha rungu kubwa na zito kutoka kwenye tawi kwa ajili ya kujihami. Kifuani mwake moyo ulimwenda mbio sana. Jasho la woga lilijaza mashavu yake kadiri jinamizi hilo lilipoonekana kubwa zaidi na zaidi wakati likizidi kukaribia. Lilikuwa refu kama binadamu. Alijificha nyuma ya vichaka. Alishika baadhi ya mawe yenye ncha zaidi na kuwa tayari kuendesha mashambulizi. Kadiri jinamizi lilivyokaribia zaidi na zaidi aliganda kwa woga.

Baadaye akabaini kwamba jinamizi lile la kutisha alikuwa binadamu. Aliyatupa mawe yake lakini aliendelea kushikilia rungu kwa tahadhari. Wakati mtu alipokuwa karibu naye alitupa hata rungu wakati alipomkumbatia mabegani. Kumbe alikuwa kaka yake mwenyewe!

Mtu huyo alimshikilia mabegani ndugu yake kwa upendo na shukurani.“Asante Mungu umekuja kunitafuta mimi. Tafadhali nionyeshe namna ya kutoka msituni!”

Kila mmoja wa ndugu hao alimtazama ndugu yake huku machozi yakimlengalenga wakati akijibu: “Hivi sasa hata mimi nimepotea ndugu yangu lakini nitakuonyesha ni njia gani TUSIPITE. Kwa pamoja tutatafuta njia ya kutokea.”

## Kula chakula pamoja na Jenerali



Siku moja Jenerali wa Kijeshi alimwalika Sufii wa Kibuddha I-hsiu (yenye maana ya “Pumziko moja”) kwenye makao makuu ya jeshi kwa chakula cha jioni. I-hsiu hakuzoea kuvaa nguo za fahari kwa hiyo alivalia joho lake la kawaida la zamani kwenda kwenye kituo cha kijeshi.

Wakati alipokaribia Makao Makuu ya ya Jeshi, walitokea wanajeshi, mbele yake na kupiga kelele, “Ombaomba huyu anatoka wapi? Jitambulishe! Huna kibali cha kuwapo hapa!”

“Jina langu ni I-hsui Dharma Master. Nimealikwa na Jenerali wenu kwa chakula cha mchana.”

Wanajeshi hao wawili walimchunguza Sufii huyo na kumwambia, “Mwongo wewe. Inawezekanaje Jenerali wangu amwalike kwa chakula cha jioni Sufii aliyevalia midabwada? Anamwalika kwa taadhima Mheshimiwa I-hsiu kwenye kituo chetu cha kijeshi kwa sherehe kubwa leo, lakini si wewe. Kwa hiyo ondoka!”

I-hsiu alishindwa kuwaridhisha wanajeshi wale kuwa kweli ndiye mgeni mwalika, kwa hiyo alirudi kwenye Hekalu na kubadili mavazi na kuvaa joho la heshima kwa ajili ya chakula cha jioni. Wakati aliporudi kwenye kituo cha jeshi, wanajeshi wakagundua kuwa huyu alikuwa Sufii mkuu wa Kibuddha, na kumruhusu kuingia kwa heshima.

Wakati wa chakula cha jioni, I-hsiu aliketi mbele ya meza iliyojaa vyakula, ingawa badala ya kuingiza chakula mdomoni mwake, alichukua chakula kwa vijiti vya kulia na kuingiza kwenye mikono ya joho.

Jenerali alikuwa na shauku kubwa na kumnong’oneza, “Hii inaaibisha sana. Je, unataka kupeleka kiasi cha chakula kwenye Hekalu? Nitamwamuru mpishi apike na kukuandalia mahitaji yako”.

“Hapana”, alijibu Sufii Yule. “Nilipokuja hapa sikuruhusiwa kuingia kwenye kituo chako na wanajeshi wako mpaka nilipovalia joho hili la sherehe. Hukunialika kwa chakula, umealika joho langu. Kwa hiyo joho langu ndilo linalokula na si mimi.”

*(Inapatikana kutoka http://www.geocities.com/Tokyo/Courtyard/1652/MilitaryDiner.html)*

## Zimwi

Hapo zamani kwenye kijiji kitulivu kilichozungukwa na miti ya matunda na kijisitu cha mizaituni, aliishi mvulana mmoja aliyeitwa Hasan. Karibu na kijiji kulikuwa na Mlima.

Mapema kila asubuhi, wanawake na wanaume walikuwa wakiharakishia mashambani, wasichana nao walikuwa wakijivuta wakitembea kwa uvivu kuteka maji kwenye chemchem kujaza madumu yao ya maji kwa matumizi ya siku wakati watoto nao walikuwa wakicheza kwenye uwanja. Maisha ya kijiji yalikuwa yakiridhisha. Hata hivyo kulikuwa na kitu kimoja kilichochafua furaha ya wanakijiji. Alikuwa Zimwi mla Maiti mkubwa wa kutisha ambaye watu waliamini kuwa anaishi juu ya kilele. Kila mtu alimwogopa Zimwi Mla Maiti. Wanakijiji walikuwa wanaharakisha kwenda mashambani kwao wakiangalia nyuma na maeneo yaliyowazunguka, na wakati mwingine wakitembelea ncha za vidole. Wanakijiji watawanyamazisha watoto wao kwa kusema, “Msipige kelele sana kama mtapiga kelele Zimwi atakasirika na makelele yote mnayopiga na atakuja kutushambulia.” Lakini wakati watoto walipokuwa watundu au kukataa kulala watawatishia Zimwi kwa kuwaambia, “Kama hamtatutii na kuendelea na utukutu wenu, Zimwi atakuja kuwatafuna.” Watoto kwa upande wao wataogopa na kuanza kutulia na kuwa na tabia nzuri.

Siku moja wakati wa msimu wa kuvuna mizaituni, Hasan alimwuliza shangazi yake Um Hamed, “Niambie Shangazi, kwa nini watu wa kijijini wanamwogopa sana Zimwi?”

Um Hamed alishusha pumzi na kusema, “Oho, Hasan! Umeuliza swali hili mara ngapi?”

Zimwi ni kiumbe mkubwa mwenye nywele nyingi. Ana jicho moja katikati ya paji la uso na kucha ndefu kali, meno makali yenye ncha. Wewe Hasan hasa ni lazima uwe mwangalifu kwa sababu chakula chake kikuu ni vijana kama wewe. Kwa hiyo acha kunisumbua na maswali yako yasiyokwisha na rudi kwenye kazi yako.”

Hasan hakuridhika na jibu la Um Hamed na alitaka kupata ufafanuzi zaidi kuhusu Zimwi, kwa hiyo Hasan alikwenda nyumbani na kumwuliza Baba yake, Yaha: Je, umewahi kumwona Zimwi?

Baba yake Hasan alifikiri kwa dakika moja na akajikohoza kusafisha koo na kusema, “Hapana, Hasan sijawahi kumwona lakini ninachojua ni kwamba anatisha na hatari sana.”

Halafu Hasan alimgeukia mama yake na kumwuuliza, Je wewe Yumma, Je, umewahi kusikia Zimwi.”

Mama yake Hasan alishtuka kidogo na kusema, “Hapana, sijawahi kusikia lakini najua kwamba mngurumo wake ni mkubwa kama simba. Iwe itakavyokuwa Hassan usijaribu kwenda kumchokoza Zimwi?”

Hasan alijisemea, “inaelekea kwamba watu wa vijijini wanamwogopa Zimwi ingawa hakuna aliyemwona wala kumsikia. Pengine hakuna Zimwi, au pengine yupo Zimwi lakini hatishi kama wanakijiji wanavyosema alivyo. Lazima nitafute ukweli mimi mwenyewe. Nimechoshwa kwa kutembea kwa ncha za vidole kijijini na kunyamazishwa kote. Nataka niruke na kupiga kelele na mayowe, na kucheka na kupanda mlima pia. Kesho mapema asubuhi nitaanza safari yangu ya kupanda mlima. Sitamruhusu mtu yeyote anikataze.”

Siku ya pili wanakijiji walipagawa kuhusu safari ya Hasan ya mlimani. Wengine walivutiwa na ujasiri wake na kusema, Ni kijana shujaa sana. Pengine atatuokoa dhidi ya Zimwi.

Hali ya kuwa wengine wanasema, Ni kijana kichwa maji, mpumbavu kiasi gani. Kubaliana nasi kwamba pengine ataliwa na Zimwi na atamkasirisha Zimwi na atatuonyesha ghadhabu yake sisi wanakijiji maskini.”

Asubuhi na mapema siku iliyofuata, Hasan alianza safari yake ya kupanda mlimani. Wanakijiji walimwangalia kwa karibu wakiwa wamejifungia nyumbani kwao. Hasan alihisi woga kidogo lakini hakutaka kuonyesha woga wake kwa hiyo alianza kusema kwa sauti kubwa:

"Simwogopi Zimwi Mkubwa mwenye nywele! Mimi ni shujaa Hasan nisiyeogopa! Siogopi! Siogopi Chochote!"

Hasan alitembea na kupanda mlima mpaka alipofika kileleni. Aliangalia huku na kule, lakini hakuona kitu chochote cha kutisha. Alishusha pumzi ya faraja na kupiga kelele sana akitarajia wanakijiji wangemsikia: "Simwogopi Zimwi mkubwa mwenye nywele. Mimi ni shujaa Hasan. Hasan asiye na woga. Niangalie ninavyoruka. Nisikie ninavyopiga kelele. Siogopi kitu."

Ghafla Hasan alisikia sauti nyuma yake. Alisikia sauti za kiumbe kikubwa na kizito. Aligeuka haraka na kujikuta uso kwa uso na Zimwi.

Zimwi alikuwa kama wanakijiji walivyoelezea. Alikuwa na nywele nene na kucha ndefu na jicho moja kali katikati ya paji la uso. Hasan aliganda kwa hofu. Alitamani angesikia walichosema wanakijiji na kutoacha usalama wa kijiji chake. Kwa upande wa Zimwi, alizidi kumsogelea kwa karibu zaidi na halafu alikwenda kumzunguka Hasan kwa hadhari zaidi na ghafla alikimbia akinguruma na kunung'unika.

Hasan alishusha pumzi ya faraja. Hakuamini kama Zimwi ambaye wanakijiji walikuwa wakimwogopa namna ile alimwogopa kijana mdogo kama yeye. Hasan alimfuata Zimwi Mla Maiti hadi kwenye pango lake na kumwita. "Zimwi! Zimwi! Uko wapi?"

Zimwi alijibu kwa sauti ya kutetemeka. "Nenda zako kijana, nenda, sikudhuru chochote."

Hasan alisema kwa furaha, "Lakini wewe ni Zimwi na watu wote wanakuogopa!"

Zimwi alikuna kichwa akionyesha kuchanganyikiwa kwa mshangao na kusema, "kuniogopa mimi! Kioja kilioje! Watu wananiogopa na mimi nawaogopa watu."



Hasan alicheka sana na kwa sauti kubwa alisema, "Kwanini unawaogopa watu wakati wewe ni Zimwi?"

Zimwi alitetemeka na kusema, "Watu wanaonekana wakutisha sana. Wana macho mawili badala ya jicho moja kama mimi. Hawana nywele nyingi kama mimi na wanasauti kali. Hofu kubwa ni kwamba wote wanapenda kula Mazimwi."

Hassan alicheka na kusema, "Haiwezekani! Hatuli Mazimwi. Ni nyie Mazimwi ndiyo mnaokula watu."

Zimwi alisema, "Kula watu? Akha futa wazo hilo! Sisi mazimwi tunakula mimea na wadudu."

Baada ya kusikia hivi, Hasan alisema, "Wanakijiji hapana shaka watafurahi na kuondokewa na hofu kwa kusikia haya."

Zimwi alimwangalia Hasan kwa muda mrefu halafu akaangua kicheko na kusema, "Hata kama unaonekana kichekesho na wakutisha kwangu, nadhani wewe ni mzuri."

Hasan na Zimwi alicheka na kukimbia kwenda kucheza.

Tangu siku hiyo Zimwi amekuwa rafiki mkubwa wa wanakijiji.

Amewalinda kutokana na hatari na kuwasaidia kazi zao za kila siku na kucheza na watoto wao.

*(Na Taghreed A. Najjar, Al-Salwa Publishing House, published 2002, Stand No.5.0 D953)*

## Hadithi ya Wanawake Wawili

Mwanamke alikwenda kuishi katika mji mpya, na wakati alipokuja getini, mlinzi wa geti alimwuliza, "Je, watu wanaoishi katika mji unaotoka wakoje?"

Alijibu, "Wana hasira, wagomvi, watetaji, na kwa kawaida wabaya sana."

Mlinda geti alisema, "Watu wa hapa ni wabaya kama huko kwa hiyo napendekeza wende zako."

Mwanamke wa pili alikuja, na mlinzi wa geti alimwuliza swali hilo hilo, ambapo alijibu, "Watu wa mjini nilikotoka walikuwa wakarimu na wanaojali. Walikuwa mashujaa wakati wa matatizo na walikuwa tayari kushirikiana nami na kukaribisha wageni."

Halafu mlinzi wa geti alisema, "karibu ndani utawaona watu wa hapa wakarimu na wenye msaada."

## Wanaume vipofu na tembo

Siku moja, wanaume watatu vipofu walikutana na kupiga gumzo kwa muda mrefu kuhusu mambo mbalimbali. Ghafla mmoja wao alikumbuka kuwa, "Nimesikia kuwa tembo ni mnyama wa ajabu. Ni bahati mbaya sisi ni vipofu na hatuwezi kumwona." "Ah, ndiyo ni bahati mbaya kweli, hatujapata bahati nzuri ya kumwona mnyama wa ajabu," mwingine alishusha pumzi.

Wa tatu, aliudhika sana, alijiunga na kusema, "Kuona?, Sahau habari hiyo! Kugusa tu itakuwa bora zaidi."

"Ndiyo ni vizuri kama kungekuwa tu na namna ya kumgusa tembo sote tutaweza kujua." Wote walikubali.

Ilitokea kwamba mfanyabiashara mmoja mwenye kundi la tembo alikuwa anapita, na kusikia mazungumzo yao. "Nyie jamaa mnataka kweli kumgusa tembo? Basi nifuateni, nitawaonyesha" alisema.

Mfanyabiashara huyo aliwaambia waketi chini na halafu alimkongoja mwanamume mmoja kipofu kwenda kumgusa tembo. Akiwa amepanua mikono kwanza, alimgusa mguu wa mbele wa kushoto na halafu wa kulia. Baada ya hapo, aligusa miguu yote miwili kutoka juu hadi chini, akiwa na uso wa tabasamu, aligeuka na kusema, "Kwa hiyo mnyama wa ajabu alikuwa namna ile" halafu akarudi kweye kikundi.

Baada ya hapo, kipofu wa pili alikongojwa hadi sehemu ya nyuma ya tembo. Aligusa mkia uliokuwa ukitikisika mara chache na alisema kwa kuridhika, "Ha! Mnyama wa ajabu alikuwa namna ile! Ni ajabu kweli! Sasa najua! Najua. Alijitenga kwa haraka.



Zamu ya kipofu wa tatu ilifuata, naye aligusa mkonga wa tembo, uliokwenda mbele na nyuma, ukigeuka na kuzunguka na alifikiria, "Ndiyo, Nimejua".

Vipofu hao watatu walimshukuru mfanyabiashara na kuondoka. Kila mmoja alifurahia kisirisiri kuhusu uzoefu na alikuwa na mengi ya kusema.

"Tukae na kufanya majadiliano kuhusu mnyama huyu wa ajabu." Kipofu wa pili alisema kwa kuuvunja ukimya.

"Wazo zuri sana. Vizuri sana." Vipofu wengine wawili walikubali. Bila ya kusubiri kila mmoja kukaa vizuri, kipofu wa pili aliropoka, "mnyama huyu wa ajabu ni kama pepeo zetu za mianzi zinazokwenda mbele na nyuma ili kutupa upepo mwanana. Hata hivyo si mkubwa wala kutengenezwa vizuri. Sehemu kuu ni kama kitita."

"Hapana, Hapana, Siyo!, kipofu wa kwanza alipiga kelele akikataa. Mnyama huyu wa ajabu anafanana na miti mikubwa miwili isiyo na matawi."

"Nyie wote mmekosea" mtu wa tatu alijibu, "Mnyama huyu wa ajabu anafanana na nyoka, ni mrefu na mviringo, na ana nguvu sana."

Ubishi ulikuwa mkubwa kiasi gani! Kila mmoja wao alisisitiza kuwa yeye ndiye aliyekuwa sahihi. Bila shaka hakukuwa na hitimisho kwa kuwa hakuna aliyechunguza kwa ukamilifu tembo mzima. Je, mtu atawezaje kueleza kwa ukamilifu mpaka awe amejifunza kila sehemu kwa ukamilifu?

*(Kutioka: Kuo, Louse and Kuo, yuan- His(1976) Chinese Folk tales, "Celestial Arts: 231 Andrian Road, Millbrae, CA94030, uk. 83-85)*

## Mpende jirani yako kama unavyojipenda mwenyewe

Mila ya Kihasidi ya Kiyahudi inaeleza hadithi ya Rabbi aliyedai kwamba amejifunza maana halisi ya kumpenda jirani yake kama unavyojipenda mwenyewe kutoka kwa wakulima wawili (Walawi 19: 18 "Usilipize kisasi au kuwa na kinyongo dhidi ya mtu yeyote anayekuhusu, bali umpende jirani yako kama unavyojipenda wewe mwenyewe").

Mmoja alimwambia mwenzake: Ivan, je, unanipenda?

Ivan alisema: Vladimir, bila ya shaka nakupenda.

Vladimir alisema: Ivan, unadhani nini kinachoniumiza?

Vladimir alimwambia Ivan: Ivan, kama hujui kinachoniumiza utawezaje kunipenda kwa dhati?

Kama tunadai kweli tunawajali watu wanaohusika na mgogoro, basi ni wajibu wetu, jukumu letu la dhati, kutafuta kuelewa nini kinachowaumiza wengine.

## Mbweha na Korongo

Mbweha mwenye choyo, siku moja alimwalika Korongo kwa chakula cha jioni nyumbani kwake kwenye mti wenye pango. Jioni ile, korongo aliruka hadi nyumbani kwa mbweha na kugonga mlango kwa mdomo wake mrefu. Mbweha alimfungulia mlango na kumwambia, "Tafadhali karibu na furahia chakula change."

Korongo aliombwa aketi mezani. Alikuwa na njaa sana na chakula kilinukia vizuri! Mbweha alipakua supu kwenye mabakuli yasiyo na kina na aliramba supu yote kwa haraka. Hata hivyo Korongo hakupata hata tone kwa sababu bakuli halikuwa na kina kwa ajili ya mdomo mrefu. Korongo alibaki akitabasamu polepole na kubaki na njaa.

Mbweha mwenye choyo aliuliza, "Korongo, kwa nini hukula supu yako? Je, huipendi?"

Korongo akajibu, "Nimefurahi sana kwa wema wako wa kunialika mimi kwa chakula cha jioni. Kesho jioni tafadhali karibu kwangu kwa chakula cha jioni."

Siku iliyofuata wakati mbweha alipofika nyumbani kwa Korongo, aliona pia kuwa wanakunywa supu kwa chakula cha jioni. Safari hii supu ilipakuliwa kwenye majagi marefu. Korongo alikunywa supu kwa urahisi sana lakini mbweha alishindwa kufikia ndani ya jagi ndefu. Safari hii ilikuwa zamu yake ya kuondoka na njaa.

## Jirani

Sayyed Jawad Ameli, Mujtahid maarufu, alikuwa akila chakula chake cha jioni wakati mtu mmoja alipogonga mlango wake. Alikuwa mtumishi aliyetumwa na mkubwa wake, Ayatullah Sayyed Mehdi Bahrul Uloom, aliyesema:

"Mkubwa wako amekwambia uje kwangu haraka. Amekaa kwa ajili ya chakula chake cha jioni lakini anakataa kula mpaka akuone."

Hakukuwa na muda wa kupoteza. Sayyed Jawad Ameli aliacha chakula chake cha jioni na kukimbilia nyumbani kwa Ayatullah Bahrul Uloom. Wakati alipoingia, mkubwa wake alimwangalia kwa kutoridhishwa na kusema:

"Sayyed Jawad! Humwogopi Allah! Huoni aibu mbele ya Allah?"

Hii ilikuja kama jambo la kumshangaza , kwa sababu hakumbuki kufanya chochote kustahili ghadhabu ya mkubwa wake.

Alisema: " Mkubwa wangu ataweza kuniongoza pale niliposhindwa."

Ayatollah Bahrul Uloom alijibu: "Sasa ni juma moja kwamba jirani yako na familia yake hawana ngano wala mchele. Alikuwa akijaribu kununua tende kutoka dukani kwa mkopo lakini muuza duka amekataa kumpa mkopo zaidi. Amerudi nyumbani mikono mitupu na familia haina hata chembe ya chakula."

Sayed Jawad alishtukizwa, "Na Allah," alisema, "Sijui lolote kuhusu hilo."

"Ndiyo maana nimechukia kila kitu. Itakuwaje usimjali jirani yako? Siku saba za matatizo zimepita na unaniambia hujui kuhusu hilo. Sawa, kama ulielewa na kumpuuza pamoja na kuelewa, basi huwezi kuwa Mwislamu," Ayatullah Uloom aliongeza.

Halafu alimwamuru aondoe vyakula vyote vilivyokuwa mbele yake na kumpelekea jirani yake.

"Kaa naye mle, ili asione aibu. Na chukua fedha hizi kwa ajili ya chakula chake cha siku zijazo. Kamwekee chini ya mto au zulia ili asidhalilishwe, niarifu wakati kazi hiyo inapokamilika, mpaka wakati huo ndiyo nitakapokula. Mtu Yule si kutoka kwangu anayelala kwa raha mustarehe wakati jirani yake analala na njaa."

Nabii Muhammad (Amani iwe juu yake)

*(Inapatikana kutoka: http://www.ezsoftech.com/stories/mis40asp)*

## Kiti cha Pweza

Hapo zamani za kale, kulikuwa na mtu mmoja mwerevu aliyezoea kwenda pwani kuandika. Alikuwa na tabia ya kutembea ufukweni kabla ya kuanza kazi yake. Siku moja alipokuwa akitembea ufukweni, aliangalia ufukweni na kuona mtu aliyekuwa akitembea kama mcheza dansi. Alijichekesha akifikiria mtu ambaye angecheza kufurahia siku hiyo, na hivyo alitembea haraka kumfikia.

Kadiri alivyokaribia, aliona kuwa huyu ni kijana ambaye hakuwa akicheza dansi, badala yake alikuwa akifikia ufukweni, akiokota kitu fulani na akakitupa polepole baharini.

Kadiri alivyokaribia, alimwambia, “Habari za Asubuhi! Unafanya nini?”

Kijana alitulia, akamwangalia na kujibu,

“Natupa kiti cha pweza baharini.”

“Nadhani, ningeuliza, Kwa nini unatupa kiti cha pweza baharini?”

“Jua ni mchana na maji yanakupwa, kama sikuwatupa sasa hivi watakufa.”

“Lakini kijana huoni kwamba kuna ufukwe wenye urefu wa maili nyingi na kwamba kuna viti vya pweza vingi vilivyoenea. Huwezi kamwe kufanya lolote!”

Kijana alisikiliza kwa upole, halafu aliinama akaokota kiti cha pweza mwingine na kutupa baharini, kupitia mawimbi yaliyokuwa yakifoka.

“Kwa huyu ameleta tofauti!”

Jibu lake lilimshangaza mtu huyo. Alimfadhaisha. Hakujua namna ya kujibu. Kwa hiyo badala yake aligeuka na kurudi kwenye nyumba yake ya mapumziko na kuanza kuandika.

Kutwa nzima alipokuwa akiandika, taswira ya kijana yule ilikuwa inamsumbua. Alijaribu kupuuza lakini sura yake iliendelea kubaki. Hatimaye baadaye alasiri, alitambua kuwa yeye kama mwanasayansi, mshauri amekosa sehemu muhimu sana ya hali ya matendo ya yule kijana. Kwa sababu alitambua kuwa alichokuwa akifanya yule kijana ni kuamua kutokuwa mtazamaji katika ulimwengu na kufanya mabadiliko. Alifadhaika sana.

Usiku ule alikwenda kulala usingizi wa mang’amung’amu. Kulipokucha aliamka akijua kwamba anatakiwa kufanya kitu fulani. Kwa hiyo aliamka, akavaa nguo zake, akaenda ufukweni na kumkuta kijana. Wakiwa pamoja walitumia muda wote wa asubuhi kuwatupa kiti cha pweza baharini.

*(Imechukuliwa kutoka: The Star Thrower by Loren Eiseley 1907-1977.)*

# Uchunguzi Kifani

Waelimishaji na wawezeshaji wanaweza kutumia uchunguzi kifani kwa msingi wa hali ya maisha halisi na watu hutoa vifaa kwa ajili ya majadiliano kuhusu masuala ya kimaadili na hali zinazoathiri hadhi ya watu na haki za binadamu. Uchunguzi kifani ulioandikwa vizuri, unaweza kuwafikisha watoto na vijana hadi ulimwengu mwingine unaowasilishwa kulingana na mtazamo wa mada. Uchunguzi kifani pia unaweza kuwasilisha masuala yanayofahamika sana, yanayoweza kuwasaidia washiriki kutafakari kuhusu hali zao wenyewe lakini bila ya kufanya kuwa mali yao.

Kupitia uchunguzi kifani, watoto na vijana wanaweza kuchanganua hali inayoweza ama kujulikana kwa kiasi fulani au kuwa ngeni kabisa kwao. Uchunguzi kifani inaweza kuwa dhana muhimu katika kuendeleza ushirikali kwa kuwa taarifa inawasilishwa kwa msingi wa mtazamo kuliko kuwa ni “ripoti yenye habari” tu. Kufikiria kuhusu uchunguzi kifani na mada zitakazowasilishwa kunaweza kusaidia kujenga utambulisho imara wenye mada.

Matumizi ya uchunguzi kifani yanahimiza stadi za ukamilifu na uchanganuzi na kukuza uwezo wa watoto na vijana kuuliza maswali na kujadili mibadala. Uchunguzi kifani pia unawasaidia watoto na vijana kuchunguza mitazamo yao wenyewe na tabia na mwenendo kupitia maisha ya wengine.

Uchunguzi kifani si lazima uhitaji ufumbuzi, wanaeleza hali ambayo tayari ina mwisho au hitimisho. Kwa kawaida huchukuliwa katika maisha halisi.

Kama unatumia uchunguzi kifani kuhusu unyanyasaji wa watoto, unaweza kutumia vifaa vinavyotayarishwa kuhusiana na Ripoti ya Dunia kuhusu Unyanyasaji dhidi ya Watoto.[1]



1 Utafiti wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa juu ya Ukatili dhidi ya Watoto. http://www.violencestudy.org/r236

## Uchunguzi Kifani 1 – Asubuhi mbaya ya Chris

Ilikuwa Jumatatu asubuhi na Chris hakutaka kuamka na kwenda shule. Kitanda kilikuwa na joto na chenye raha na nje kulikuwa na baridi. Pia alijua kuwa hajamaliza mazoezi ya kufanyia nyumbani na ilitakiwa akabidhi siku hiyo. Alifumbua macho polepole na kumwona mbwa wake, Prowler amelala kwenye sakafu akitafuna moja ya raba zake mpya.

"Prowler, ondoka hapa!" alifoka kwa hasira, akichechemea kutoka kitandani. Prowler alikimbia na kujibanza pembeni.

Kwa kuwa tayari alikwishaamka, alivaa polepole, kupiga mswaki na kushuka ngazi hadi sakafu ya chini. Alikuwa amekasirika sana kwa sababu mojawapo ya raba zake zimeharibiwa, pia lazima aende shule leo. "Kwa nini isingeendelea leo kuwa mwisho wa wiki?" alifikiria.

Chris alikunywa chai, akachukua begi la shule, na kwenda kituo cha basi. Watoto walikuwa wakicheza mchezo wa kupiga shuti. Wakati alipoinama kutua begi lake, mpira ulipita juu na kugonga kichwa chake. "Ouch! Alipiga kelele, "Nani amefanya hivi?" Shawn alikiri kufanya hivyo, "Kusema kweli sikukusudia kufanya hivyo" wakati watoto wengine wakicheka. Chris alihamaki.

"Ehe, ndiyo umenipiga mpumbavu we. Subiri uhisi inavyokuwa!" Baada ya kusema hivyo aliinua mpira na kumtupia Shawn, na kumpiga tumboni."

Shawn alipiga kelele, "Ala we! Haipendezi, Mpira ulikupiga kwa bahati mbaya lakini wewe umenirudishia kwa makusudi. Wewe mtu mgomvi.

Safari hii Shawn alirudisha kwa nguvu zaidi na kupiga mguu wa Chris. Chris alimkimbilia Shawn na kumpiga kikumbo. Kama marafiki wengine wasingeingilia kati, ungebadilika kuwa ugomvi kamili ambao ungesababisha mmoja wao kuumia.

- Je, unadhani ni kitu gani kinaeleza alichofanya Chris kwa kupigwa na mpira?
- Je, Chris angefanya tofauti?
- Je, hali hiyo ingeepukwaje?
- Je, Chris angefanya nini baadaye siku hiyo baada ya kupunguza hasira na kutulia?

## Uchunguzi Kifani 2 – Mkaa pweke au aliyetengwa na Jamii?

George ni mwanafunzi wa darasa la 8 katika shule yako. Unampenda kwa sababu daima amekuwa mtoto mwema na anapenda kusalimia. Kuwa mwema na anayependa wenzake namna hiyo, kunamfanya awe maarufu kwa takribani kila mtu na anaonekana kuwa na stadi nzuri za uongozi.

Hata hivyo umetambua kuwa George anaelekea kuwa na matatizo na mmoja wa wanafunzi wenzake darasani , Siffan. Siffan anatoka Jordan na baba yake amehamishia familia yake mjini kwake wakati anafanya kazi ya muda.

Siffan daima yuko peke yake na yaelekea hapendi kujifunza na wanafunzi wenzake. George anaelekea kudhani kwamba Siffan hataki kuwa na marafiki wanafunzi na kwamba anajiona kuwa bora zaidi ya wanafunzi wengine wa darasa lake.

Ni kweli kwamba Siffan amekuwa akigombana na George mara nyingi, hali hii imemfanya kuwa na maoni hasi kuhusu Siffan, mara nyingi akitaja rangi ya ngozi yake na tabia yake ya kitamaduni.

Hakuna watoto wengi kutoka nchi za Kiarabu shuleni kwao na baadhi ya watoto huwafanyia mzaha wote. Bila shaka, hii pia imetokea kwa Siffan mara nyingi.

Wiki iliyopita, baba yake Siffan ilimbidi aende Amman, Jordan kwa ajili ya mkutano wa kikazi. Wakati akiwa huko aliuawa kwa bomu kwenye mojawapo ya hoteli. Hali hii hivi sasa inafahamika shuleni kote na walimu wamempa Siffan na familia yake rambirambi zao.

Siffan amerudi shule, lakini hakuna hata mwanafunzi mwenzake mmoja aliyezungumza nae. Kwa kuwa anaelekea kutokuwa na marafiki shuleni, yuko pweke na huzuni yake.

- Je, unadhani Siffan alijihisi vipi?
- Je, unahisi nini kuhusu hali ya Siffan?
- Je, unadhani George itabidi afanye nini?
- Je, kama wewe ungekuwa Geore ungefanya nini?
- Je, nini wajibu wa George kama mwanafunzi wa darasa moja na Siffan na kama kiongozi shuleni?
- Je, unadhani Siffan anahitaji kuzungumza na mtu yeyote?
- Je, unadhani Siffan angefanya nini kama angekuwa George?
- Je, unadhani walimu na shule wanatakiwa kufanya nini kumsaidia Siffan?

## Uchunguzi Kifani 3 – Hadithi ya Anna

“Nilikuwa ninaishi Alto Bando nchini Colombia mpaka matukio ya mjini kwangu yaliponifanya niukimbie mji na kwenda uhamishoni Esmeraldas, Ecuador. Jina langu ni Ana”.

“Mkoa wetu umekabiliwa na kikundi cha askari wa msituni kwa miaka mingi. Baadhi ya miaka walituacha, na miaka mingine walifanya mashambulizi machache kwenye nyumba za wale wanaodhani kuwa wamewasaliti.

Siku moja waliwaita mkutanoni watu wote wa mjini. Walimtuhumu kaka yangu Andres kwa kushirikiana na upande wa pili, wanamgambo. Hawakutaka ajitetee bali walimpiga risasi ya kichwa, kwenye uwanja hadharani. Alikuwa na mke kijana na watoto watatu.

Kwa kuwa mimi ni dada yake, pia nilikuwa ninashukiwa, lakini niliambiwa nihame mji au watawauwa watoto wangu pia. Bila ya kuwa na muda wa kufunganya nguo zangu, niliondoka na watoto wangu sita, wifi yangu na watoto wake watatu.

Nina umri wa miaka 49 na nina watoto wanane. Mmoja alikuwa anasoma Quibdo’ lakini alijiunga na vikundi vya askari wa msituni, vikundi hivyo hivyo vilivyonitishia na kumwua Andres. Mmojawapo wa binti yangu amejiunga na wanamgambo. Je unaweza kufikiria ingekuwaje kama wangewahi kukutana?

Maisha huko Esmeraldas yamekuwa magumu kwa watoto wangu wadogo sita na kwangu mwenyewe. Nauza matunda na kupata kiasi cha kuweza kulipa kodi ya chumba kidogo kile ninakoishi na watoto wangu. Carlos mmoja wa watoto wangu, anafanya kazi posta ingawa hajalipwa fedha zozote kwa kipindi cha miezi mitatu iliyopita. Jorge mwenye umri wa miaka 16 alifungwa juma lililopita kwa sababu ya kutuhumiwa kwa kuiba saa. Hatukuwa na fedha za kula.

Watoto wangu wengine hawajapata ajira na sina uwezo wa kuwapeleka shule. Wakati mwingine majirani zetu wanatuita wauzaji dawa za kulevya (mihadarati), askari wa msituni na wanatufanya kama wahalifu. Hata hivyo maisha haya ni bora zaidi kuliko kurudi Colombia na kwenye vita. Sidhani kama matatizo yatatatuliwa. Kwa kuwa kuna vikundi vya watu wenye silaha katika eneo, siwezi kurudi kwenye mji wangu.

Tumepata hifadhi ya ukimbizi wa ovyoovyo kufika Esmeraldas. Lakini tutaishi vipi? Je, nina uchaguo gani? Nina wasiwasi kuhusu watoto wangu wadogo. Hawawezi kwenda shule kwa sababu sina uwezo wa kulipa ada ya shule, Je watafanya nini siku nzima? Nina wasiwasi wataishia kwenye makundi ya wahalifu na kusababisha matatizo na kuishia jela au mitaani. Maisha ni mateso matupu.

> Je, una hisia gani kuhusu Ana?
> Je, angefanya nini kufanya maisha kuwa mazuri zaidi kwake na kwa watoto wake?
> Je, angemfuata nani kumsaidia?
> Je, ungefanya nini kama ungekuwa katika hali kama ya Ana?
> Je, kuna watu kama Ana mjini kwako?
> Je, kuna njia yoyote ya kuwasaidia?

## Uchunguzi Kifani wa 4 – Hadithi ya Maria

Maria ambaye sasa ana umri wa miaka 16, ana baba wa kambo katili. Kabla ya kumpiga Maria, alimsikia akimpiga mama yake. Alipokuwa na umri wa miaka minane, alimwuliza ilikuwa ni saa ngapi, na alifanya kosa la kutopatia.

Maria alisema, "Alinipiga kwa nguvu kiasi cha kuanguka na kugonga kichwa changu kwenye sofa. Halafu alianza kunipiga mateke. Niliogopa kiasi cha kujikojolea."

Unyanyasaji uliendelea lakini Maria hakudhani kuwa anaweza kumweleza mtu yeyote. Sikutaka kumwambia mtu yeyote shuleni wala kumwambia mama yangu, kwa sababu alikuwa na matatizo mengi ya kuyashughulikia. Niliogopa sana kumwambia mtu yeyote kile kilichotokea, endapo baba yangu wa kambo angesikia na kunigeukia mimi na mama yangu".

Unyanyasaji umeathiri vipengele vyote vya maisha ya Maria na maendeleo yake shuleni yalianza kuathiriwa.

"Nilikosa shule kwa miaka mitatu kwa sababu nilikuwa na wasiwasi kuhusu kumwacha mama yangu peke yake na baba yangu wa kambo. Pia iliathiri kujistahi kwangu na niliwaachia watoto wengine shuleni kuninyanyasa na kunionea. Sikutaka kuzungumza na mtu yeyote shuleni au kumwambia chochote mama yangu, kwa sababu alikuwa na matatizo mengi ya kushughulikia".

Hatimaye shule nayo ikafuatilia, Maria alipofika darasa la 9, akiwa na umri wa miaka 13 waliandaa Mnasihi. Kwanza Maria alihisi kwamba hataweza kuzungumza kamwe na Mnasihi wake, lakini hatimaye aliongea naye.

"Kwanza sikumwamini, baada ya mwaka mmoja, nilimwambia kila kitu kilichokuwa kikitokea kwangu".

"Alikuwa kama rafiki yangu mpendwa na kuhisi kwamba ningemwambia kila kitu na hakuna aliyejua nilichokuwa nikimwambia".

Lakini ingawa alikuwa akiendelea kumwona mnasihi wake, Maria alimeza dawa nyingi na hivyo kulazwa kwa wiki moja. Alisema, "Nilikuwa nimekata tamaa na maisha na kuhisi kwamba hakuna sababu ya kuendelea".

Maria alipewa Mnasihi mwingine na pia kupata matibabu kutoka kwa mtaalamu wa maradhi ya akili na daktari wa kumsaidia kupona.

Maria aliseama: "Unasihi na msaada kutoka kwa mtaalamu wa maradhi ya akili na daktari kwa kweli vimenisaidia. Pia, kusoma vitabu na magazeti nimetambua kuwa sikuwa peke yangu niliyekuwa nikikabiliwa na tatizo hili. Wazo kwamba sikuwa peke yangu katika kushughulikia tatizo hili kilikuwa chanzo kikubwa cha faraja"

> Je, ungefanya nini katika hali ya Maria?
> Je, unadhani maisha yake yanaweza kuathirika na kile kilichomtokea?
> Je, watoto wanawezaje kulindwa dhidi ya ukatili wa nyumbani?
> Je, hali ya sheria ikoje nchini kwako kwa watoto wanaoishi kwenye mazingira ya ukatili ikiwemo nyumbani kwao?
> Je, watoto walindwe vipi na walindwe na nani dhidi ya ukatili wa nyumbani?
> Je, unao marafiki darasani kwako wanaokabiliwa na ukatili na kudhalilishwa nyumbani?
> Utafanya nini kuwasaidia na kutoa msaada wa marika?
> Je, unadhani kwamba wasichana wako hatarini zaidi kuliko wavulana kuhusu ukatili? Kwa nini?
> Je, una mifano ya uonevu shuleni? Je, utauzuiaje?

# Mitanziko ya Uadilifu

Mtanziko wa Uadilifu unaeleza hali inayohitaji kutatuliwa. Kama tatizo ni mtanziko, ina maana kuna uchaguzi wa hali ambazo huonekana kwamba hazipendezi, iwe kwa kipindi kifupi au kwa kipindi kirefu. Kutatua mitanziko mara nyingi kunaweza kuhusisha maswali magumu ya Kimaadili.

**Ufuataو ni mwongozo** wa namna wa kutengeneza mitanziko ya uadilifu wako:

- Hakikisha kuwa mtanziko huo unahusisha hali ambapo washiriki wanatakiwa kufanya uamuzi wao wenyewe. Kumbuka umuhimu wa kuwapa fursa vijana kuchagua.
- Eleza hali inayoruhusu kukiuka sheria.
- Wasilisha hali ambapo washiriki inawabidi kuhoji kilicho sahihi na kilicho kosa.
- Waongoze hadi kufikia hatua ambapo ufumbuzi mzuri zaidi unaonekana kuwa ni ule unaowanufaisha wao, lakini pia unawaathiri wengine.

## Mtanziko wa Uadilifu 1 – Kuokoa Maisha

Watu wawili wanasafiri jangwani. Wana chupa moja tu ya maji kwa ajili yao. Kama watashirikiana, wote watakufa. Kama mmoja wao atakunywa maji, atanusurika, lakini mwenzake hatanusurika.

Je, watafanya nini? Maoni ya upande mmoja ni kwamba, hawana budi kushirikiana maji yao, ili hakuna atakayeshuhudia kifo cha mwenzake. Wazo jingine ni kwamba, mwenye chupa, aliyefikiria kuileta, hana budi kunywa maji hayo.

Tuna tafsiri mbili zinazotofautiana. Je, tunawezaje kufikiria mawazo yaliyotofautiana? Ni maisha ya nani yanayopewa kipaumbele? Je itakuweje kama msafiri mmoja ni mtoto na mwingine ni mtu mzima? Itakuweje kama wasafiri hao ni mwanamume na mwanamke? Je, tunapimaje thamani ya maisha?

## Mtanziko wa Uadilifu 2 – Mchezo wa Mpira wa Kikapu

Mashindano ya Mpira wa Kikapu ya shule ya Olimpiki (Inter Schools Basketball Olympics) yanakaribia kuanza mjini kwako. Timu yako ilishinda Olimpiki mwaka jana na ilipewa medali ya dhahabu kwa mchezo mzuri.

Mwaka huu, kuna timu nyingi za shule. Wachezaji wawili bora hawapo tena shuleni kwako na unahitaji watu wawili wapya kuziba nafasi zao. Kocha wako hatakuwapo kwa wiki tatu na amekupa jukumu la kuchagua wachezaji wapya wawili kwa vigezo utakavyotumia kama timu. Hata hivyo ametoa mapendekezo: hakikisha kwamba wachezaji watakaochaguliwa wanaelewa na kukubali sheria za timu kabla ya kukubaliwa, na hakikisha kuwa unachagua wachezaji bora zaidi.

Umetangaza mchakato wa uchaguzi wa wachezaji hao na ni wachezaji watatu tu wameonyesha shauku ya kujiandikisha. Huna muda wa kuanzisha mchakato mpya kwa hiyo inakubidi uwachague kutokana na hao watatu.

Waombaji hao watatu ni:

Christian: Umri wa Miaka 14.
Hana uzoefu wa kucheza mpira wa kikapu. Angependa kujifunza kucheza.
Anapatikana kwa mazoezi: kila adhuhuri na kuendelea.

Hiran: Umri wa miaka 16.
Ana uzoefu wa miaka miwili. Alikuwa miongoni mwa timu bora ya pili ya shule katika michezo ya shule ya Olimpiki ya mwaka jana, lakini alifukuzwa kwenye timu kutokana na mchezo mbaya. Baadhi ya watu wanadhani kwamba kwa kuwa alifukuzwa atakuwa ameanza kutumia dawa za kulevya.

Anapatikana kwa mazoezi: mara nne kwa wiki.

Andres: Umri wa miaka 15.
Ana uzoefu wa mwaka mmoja.
Anapatikana kwa mazoezi: mara tatu kwa wiki.

Wakati timu ilipoendesha usaili, walieleza sheria za timu:

> Wanaojiunga na timu wawe na umri wa kati ya miaka 15 na 18
> Kuna mafunzo ya saa tatu mara tatu kwa wiki
> Kila jumamosi, timu inapata mafunzo ya uongozi. Mafunzo hayo ni lazima kwa wachezaji wote
> Kila mchezaji lazima ahudhurie Kambi za Kujenga Timu kila mwisho wa wiki ya kwanza ya kila baada ya miezi miwili
> Udhuru unakubaliwa tu kwa ugonjwa au matatizo ya familia

**Christian** amesema atatimiza umri wa miaka 15 baada ya miezi mitatu na kwamba hawezi kuhudhuria mafunzo siku za ijumaa kwa sababu kuna mikutano iliyopangwa na kamati ya wanafunzi ya shule.

**Hiran** hana kipingamizi chochote, anakubaliana na sheria zote.

**Andres** anaeleza kuwa hataweza kuhudhuria programu za mwiso wa juma kwa kutokana na sheria za dini. Yeye ni Myahudi na Sabato(Jumamosi) ni siku ya Mungu (Ibada).

> Je, utamchagua nani kuwa sehemu ya timu yako?
> Je, sheria za timu zinatosha kuweza kufanya uamuzi?
> Si Christian wala Andres wanaoweza kutii sheria za timu, je unawezaje kuwianisha uamuzi wako na masharti yaliyowekwa na kocha wako: "hakikisha kwamba wanakubaliana na kuelewa sheria za timu?
> Kama umeamua kutomkubali Hiran, je utatoa sababu gani? Je, kufukuzwa kwake kwenye timu yake ya zamani inaweza kuwa sababu ya kumzuia asijiunge na timu yako? Je, tetesi kuhusu matumizi ya dawa za kulevya itakuwa ni sababu ya kutomkubali?
> Kama umeamua kutomkubali Andres, je utakuwa na sababu gani?

## Mtanziko wa Uadilifu 3 – Kulinda Uongo

Judy ni msichana mwenye umri wa miaka 12. Mama yake alimwahidi kwamba atakwenda kwenye onyesho maalumu la muziki litakalofanyika mjini kwao kama ataweka akiba ya fedha za kutosha kutoka kwenye ujira wa uyaya na fedha za chakula cha mchana kununulia tiketi. Alifanikiwa kuweka $20 ambazo zingetosha kabisa kukatia tiketi ambayo ni $15. Hata hivyo baadaye mama yake Judy alibadili mawazo na kumwambia bora atumie fedha hizo kwa kununulia vitabu vya shule.

Judy hakufurahi na aliamua kwenda kwenye onyesho kwa hali yoyote. Alikata tiketi na kumwambia mama yake kuwa ameweza kuweka akiba ya dola tano tu. Jumamosi hiyo alikwenda kwenye onyesho na kumwambia mama yake atatoka na rafiki yake. Wiki ikapita bila mama yake kugundua.

Halafu Judy alimwambia dada yake mkubwa, Louise, kwamba alikwenda kwenye onyesho na alimdanganya mama yake kuhusu safari hiyo. Louise, hana hakika kama amwambie mama yao kuhusu alichofanya Judy.

1. Je, Louise, dada mkubwa, amwambie mama yao kuwa Judy alimdanganya kuhusu fedha na onyesho – au anyamaze? Je, afanye uamuzi kwa msingi gani?
2. Je, Louise awe mwaminifu zaidi kwa mama yake au dada yake? Kwa nini?
3. Je, ukweli kwamba Judy alijitafutia mwenyewe fedha ni muhimu katika hali hii? Kwa nini?
4. Mama alimwahidi Judy kuwa atakwenda kwenye onyesho iwapo atajitafutia mwenyewe fedha hizo. Je, ukweli kwamba mama yake kapuuza ahadi yake ni uamuzi muhimu? Kwa nini?
5. Kwa jumla, je, ahadi ni lazima itimizwe? Kwa nini?
6. Je, kuna tofauti yoyote iwapo mtu aliyeahidiwa kitu ni ndugu wa karibu au ndugu mgeni?
7. Je, nini jambo muhimu zaidi kwa Louise kufanya katika hali hii?

*Imechukuliwa kutoka: Moral Reasoning na Victor Grassian, Prentice Hall, 1981.*

## Mtanziko wa Uadilifu 4 – Gharama ya Maisha

Barani Ulaya, mwanamke alikuwa akisumbuliwa na saratani na kung'ang'ania maisha. Aina moja ya dawa inaweza kuokoa maisha yake, aina ya "radium" ambayo mfamasia wa mjini kwao ameigundua hivi karibuni. Mfamasia huyo anahitaji $ 2000, kwa dawa hiyo, mara 10 zaidi ya gharama za uzalishaji za dawa hiyo.

Mume wa mwanamke anayeumwa, Heinz, aliwatembelea marafiki na familia kuazima fedha , hata hivyo aliweza kukusanya kiasi cha $ 1000 tu. Alimwambia mfamasia kwamba mke wake atakufa na kumwomba ampunguzie au ampe mkopo kwa muda. Mfamasia alikataa.

Mume wake alifadhaika na kuamua kuvunja duka la mfamasia na kuiba dawa kwa ajili ya mke wake.

> Je, muuza dawa alikuwa sahihi kumnyima dawa Heinz? Kwa nini?
> Je, mume alikuwa sahihi kuvunja duka la dawa? Kwa nini?
> Je, mume alikuwa na hatua nyingine za kuchukua?
> Je, ungefanya nini kama ungekuwa Yule mume na kukabiliwa na hali kama hiyo?

*Imechukuliwa kutoka Kohlberg, Lawrence, Collected Papers on Moral Development and Moral Education, Cambridge: Moral Education and Research Foundation, Harvard University Education Foundation, 1973.*

## Mtanziko wa Uadilifu 5 – Mashua ya Kuokolea

Mwaka 1842, meli iligonga mwamba wa barafu majini na zaidi ya watu 30 walionusurika walijazana katika mashua ya kuokolea iliyokusudiwa kuchukua watu saba tu.

Kadiri tufani ilipozidi kutisha, ilikuwa dhahiri kwamba mashua ya kuokolea ilitakiwa ipunguze uzito kama kulikuwa na atakayenusurika. Nahodha alisema jambo linalofaa kufanya na kuwalazimisha baadhi ya watu wapungue na kuzama. Hatua hiyo, alijitetea kuwa si ya uonevu kwa wale waliotupwa baharini kwa sababu watazama kwa vyovyote vile. Hata hivyo kama asingefanya chochote, angechukua jukumu kwa vifo vya wale ambao angewaokoa.

Baadhi ya watu wamepinga uamuzi wa nahodha. Wamedai kuwa kama hakuna kilichofanyika na kila mmoja angekufa kutokana na hali hiyo, hakuna ambaye angelaumiwa kwa vifo hivyo. Kwa upande mwingine kama nahodha angejaribu kuokoa baadhi ya maisha, angefanya hivyo tu kwa kuwaua wengine na vifo vyao lingekuwa jukumu lake.

Nahodha alipinga sababu hii. Kwa kuwa uwezekano pekee wa kuwaokoa ulihitaji juhudi kubwa ya kupiga makasia, nahodha aliamua kuwa aliye dhaifu zaidi ingebidi atolewe mhanga. Katika hali hii, alifikiri kuwa ingekuwa upuuzi kuhangaika na watu wengi ambao wangetupwa baharini: Hatimaye aliwalazimisha waliokuwa dhaifu kutupwa baharini.

Kadiri hali ilivyokuwa, baada ya siku nyingi za upigaji makasia, walionusurika waliokolewa na nahodha alishtakiwa kwa kitendo alichofanya.

- Kama ungelikuwa kwenye boti, je, ungelitumia hoja gani, kama:
  - (a) Ungekuwa na uwezekano wa kutupwa baharini; au
  - (b) Ungekuwa miongoni mwa waliokuwa na nguvu ambao wangebaki kwenye boti?
- Kama ungekuwa katika jopo la majaji la kuamua kesi ya nahodha, je, ungeamua nini kuhusu hatia hiyo?
- Kama kuna adhabu unadhani nahodha angestahili kupata adhabu gani?
- Je, ungefanya nini kama ungekuwa katika nafasi ya nahodha?

*Imechukuliwa kutoka Moral Reasoning by Victor Grassian, Prentice Hall, 1981.*

## Mtanziko wa Uadilifu 6 – Kudanganya

Sona ana matatizo ya kujifunza Kemia na hajapata matokeo mazuri katika mazoezi yaliyopita.

Hata hivyo, Sona anajifunza kwa bidii kwa ajili ya mazoezi yake ya mwisho na ana imani kuwa atafanya vizuri. Zoezi ni refu sana lakini Sona anajibu maswali yote na mpaka sasa anafanya vizuri. Hata hivyo, kuna swali moja ambalo hawezi kulijibu. Swali hili lina 25% ya alama. Muda unakwisha.

Mtu aliye karibu na Sona amemaliza zoezi lake na ana fursa ya kunakili jibu la swali analolikosa. Profesa ametingwa kwa kujibu maswali kutoka kwa mwanafunzi mwingine na Sona anajua anaweza kunakili jibu kwa haraka sana.

Kama Sona atapata jibu la swali lake la mwisho, atafaulu mtihani na somo pia. Kama atashindwa kujibu swali hili la mwisho, atafeli na atalazimika kurudia somo hili wakati wa muhula ujao.

- Je, unadhani Sona atafanya nini?
- Ungefanya nini kama ungekuwa katika nafasi ya Sona?
- Tuchukulie kwamba umedanganya, kama mwalimu angekuuliza siku inayofuata kama umedanganya au hapana, je, ungeweza kukiri kosa na kuomba msamaha au kufanya jambo lolote?
- Kama mtu mmoja anadanganya darasani, je, unadhani mtu mwingine yeyote anaathiriwa? Vipi na kwa namna gani? Kwa nini si hivyo?

# Filamu na Video

Filamu na video zinaweza kuwasaidia washiriki kuingia katika ulimwengu mwingine na kujifunza kuhusu maisha ya watu wengine na hali zao. Kutegemea stadi za watengenezaji wa filamu, washiriki wanaweza pia kutafakari hoja mbalimbali, motisha kwa ajili ya kuchukua hatua na utata wa hali tunazokabiliana nazo.


Waelimishaji na wawezeshaji wanaweza kuwasiliana kwa urahisi na watoto na vijana kwa kutumia filamu au picha za kuelimisha zinazowasilisha masuala ya kijamii ya hivi sasa. Kuangalia filamu kunawahimiza washiriki kuuliza maswali kuhusu hali halisi katika sehemu tofauti za dunia, kuweza kuwa karibu na masuala ya haki za binadamu na kujifunza kuhusu mibadala isiyo na ugomvi katika mgogoro.

Filamu ni sehemu ya utamaduni unaopendwa na kutoa mchango muhimu katika burudani ya vijana; kwa hiyo zinaweza kuwaleta vijana na watoto karibu zaidi kwenye mada kwa namna ya kuvutia na kuchangamsha. Majadiliano kuhusu filamu yanaweza kuwasaidia washiriki kuonyesha hofu, fikra, hisia na kuelewa hali. Kipengele cha ziada ni kujadili nafasi ya vyombo vya habari katika utamaduni wa kiulaji.

Orodha ifuatayo ya filamu imechaguliwa ili kuwasaidia wawezeshaji na walimu kutumia filamu zinazohusiana na haki za binadamu, elimu ya amani, kujifunza utamaduni na dini mbalimbali. Zinapangwa daraja kwa mujibu wa Chama cha Filamu (Motion Pictures Association – MPA) kinachozingatia mada, lugha, ukatili, utupu, ngono na matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa maeneo mengine ya maudhui kufanya uamuzi kuhusu upangaji daraja. Upangaji huu wa daraja kwa kawaida huwa unafanywa na wazazi na itakuwa njia nzuri kuamua kufaa kwa filamu kwa umri wa kikundi unachoshirikiana nacho. Baadhi ya filamu hazipangwi daraja na MPA, kwa hali kama hizo, ridhaa ya mwezeshaji inatakiwa kama kutumia filamu au tusitumie.

Filamu zinapangwa daraja kwa namna ifuatayo:

| | |
|---|---|
| G | Watazamaji wa kawaida, umri wote unaruhusiwa. |
| PG | Ridhaa ya wazazi inapendekezwa, baadhi ya filamu hazitafaa kwa watoto. |
| PG-13 | Wazazi wanatahadharishwa sana, baadhi ya filamu hazifai kwa watoto chini ya umri wa miaka 13. |
| R | Imekatazwa, watoto chini ya umri wa miaka 17 wanahitaji kufuatana na wazazi au mlezi mtu mzima. |
| NC-17 | Hairuhusiwi kwa mtoto wa umri wa miaka 17 na chini yake. |



| Jina | Mwongozaji | Hadhi | Maelezo mafupi |
|---|---|---|---|
| *Au revoir, les enfants* | Louis Malle | PG | Madhari ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia, shule ya bweni ya Kikatoliki ya kijijini Ufaransa, inahusu wavulana wawili, mmoja wapo ni Myahudi aliyefichwa dhidi ya Wanazi na Watawa wa kiume wanaoendesha shule. Filamu hii inahusu uzoefu binafsi wa Malle. |
| *The Believer* | Henry Bean | | Safari binafsi ya utafiti ya mwanafunzi wa Kiyahudi wa New York kuelewa maana ya dini ya Kiyahudi maishani mwake. Inachunguza mada za dini na familia. Ni uchunguzi wa kisaikolojia kwenye nguvu za kukosa ustahamilivu, kwa mtu binafsi na kwa jamii kwa jumla. |
| *Blood Diamond* | Edward Zwick | R – Ukatili mkubwa na lugha ya kutisha | Wakati wa vita vya wenyewe kwa wenyewe na ghasia nchini SierraLeone, miaka ya 1990, Waafrika wawili Danny Archer, askari wa kukodiwa kutoka Zimbabwe- na Solomon Vandy, mvuvi wa kabila la Mende, wameanza safari ya kutafuta na kupata almasi adimu ya rangi ya pinki ambayo Solomon ametafuta na kuificha. Wakisaidiwa na mwandishi wa Habari wa Kimarekani, Maddy Bowen, watu wawili hao wamejusuru safari ya hatari ambayo ingeokoa familia ya Solomon na kumuahidi Archer ukombozi. |
| *Central Station* | Walter Salles | R – Lugha ya kutisha | Dora, mwalimu wa shule wa zamani, ajuza mwenye uchungu anayefanya kazi katika Kituo Kikuu cha Treni cha Rio de Janeiro, kuwaandikia barua wateja wasiojua kusoma na kuandika. Josue', mvulana mwenye umri wa miaka 9, hajawahi kuonana na baba yake bali mama yake anamwandikia kupitia kwa Dora. Dora anamchukua Josue' kumtafuta baba yake katika safari inayobadili maisha yao wote. |
| *Cry Freedom* | Richard Attenborough | PG | Mandhari ya Afrika Kusini wakati wa siasa ya Ubaguzi wa rangi, ni kisa cha Donald Woods, Mhariri Mkuu wa gazeti lisilofungamana na mtazamo wa ubaguzi la Daily Dispatch la Afrika Kusini na mwanaharakati Steve Biko. Wakati Steve Biko alipofariki kwenye kituo cha polisi, Woods anaandika kitabu kumhusu Biko na njia pekee ya kuweza kuchapishwa ni kwa Woods na familia yake, kutoroka nchini. |
| *Dead Poets Sosciety* | Peter Weir | PG | Hadithi ya watu wanaotafuta ujasiri wa kuchagua njia yao wenyewe. Profesa Keating, mwalimu mpya wa Kiingereza, anawashawishi wavulana katika shule ya maandalizi ya Kimarekani ya kifahari kuugomea uongozi . Kila mmoja kwa namna yao, wanafanya hivyo, na wanabadilishwa katika maisha yao yote. |

| Jina | Mwongozaji | Hadhi | Maelezo mafupi |
|---|---|---|---|
| *Gandhi* | Richard Attenborough | G | Maisha ya Gandhi yalikuwa miongoni mwa uanaharakati wa haki za binadamu, na ustahimilivu wa kisiasa na kidini. Filamu inayomwonyesha mtu asiye wa kawaida anafanya mapambano yasiyotumia nguvu yanayotetea kuishi kwa pamoja kwa amani na demokrasia. |
| *Hotel Rwanda* | Terry George | PG-13 – Ukatili, taswira zinazotia wasiwasi na lugha fupi na ya kutisha | Nchini Rwanda mwaka 1994, vitendo vya mauaji ya Kimbari vilifanyika kwa kiwango kisichofahamika tangu maangamizi makubwa ya Wayahudi. Katika kipindi cha miezi mitatu tu, watu milioni moja waliuawa kikatili. Akivutwa na mapenzi yake kwa familia, mtu wa kawaida anaokoa maisha ya wakimbizi zaidi ya elfu moja, wasio na uwezo kwa kuwapa makazi kwenye hoteli anayosimamia. |
| *In the name of God* | Anand Patwardhan | G | Tangu kupata uhuru mwaka 1947, India imekuwa nchi isiyo na uhusiano wa kidini. Hatari kubwa kwa taifa lenye mfumo wa kijamii uliozidiwa sana siku hizi inatoka kwa waumini wenye imani kali ya kidini ya Hindu wanaodai wingi wa 83% ya wahindi walio waumini wa Hindu kuitaka India ijulikane kama taifa la dini ya Hindu. |
| *The Kite Runner* | Marc Foster | | Kisa cha filamu kinafuata kile cha riwaya ya Khaled Hosseini. Kinaeleza hadithi ya Amir, anayesumbuliwa na hatia ya kumsaliti rafiki wake wa utotoni, Hassan, mtoto wa mtumishi wa baba yake. Anarudi Afghanistan na kutumaini kupata msamaha kwa uchaguzi aliofanya alipokuwa kijana. Hata hivyo, Afghanistan anakotaka, kurudi hivi sasa inadhibitiwa na Taliban. |
| *Kolya* | Jan Svera'k | PG-13 – Aina fulani ya upendaji wa starehe | Franta Louka, mpiga fidla kubwa kwenye onyesho la muziki nchini Czechoslovakia iliyovamiwa na Soviet, anapoteza nafasi katika kikundi cha muziki cha taifa. Ana deni kubwa na wakati rafiki yake alipopendekeza kumwoa mwanamke wa Kirusi ili apate hati za Czech, anakubali kwa shingo upande. Anatumia hali hiyo kuhamia kwa mpenzi wake Ujerumani ya Magharibi na kumwachia bibi yake mtoto wake mwenye umri wa miaka mitano. Anapofariki bibi yake, Kolya anakuja kuishi na baba yake wa kambo Louka. |
| *Kundun* | Martin Scorsese | PG-13 – Baadhi ya taswira za ukatili | Filamu inayoeleza maisha ya Dalai Lama. Wakati akiwa mdogo kwenye mkoa wa pembezoni wa Tibet, masufii waliamua kuwa yeye ndiyo mzaliwa upya wa 14 wa Buddha wa Huruma. Wakati Vita Vikuu vya Pili vya Dunia vilipomalizika alilazimika kushughulikia uvamizi wa Wakomunisti wa Kichina dhidi yaTibet. Malalamiko yalipuuzwa kwa kuwa Mao aliendelea kuimarisha jeshi Tibet na hatimaye Dalai Lama alilazimika kukimbilia Dharmsala, India. |

| Jina | Mwongozaji | Hadhi | Maelezo mafupi |
|---|---|---|---|
| *Life is Beautiful* | Roberto Benigni | PG-13 – vipengele muhimu vinavyohusiana na maangamizi makubwa ya Wayahudi | Myahudi na mshairi,Guido Orefice, mke wake na mtoto wanaishi kwa furaha mpaka Wajerumani walipowakamata na kuwaweka kwenye kambi ya mateso. Alimlinda mtoto wake Giosue dhidi ya ukweli mgumu, Guido anamwambia kwamba wako kwenye mapumziko makubwa na kuifanya kambi kubwa ni mchezo mkubwa na kudai kuwa lazima washinde alama 1000 kushinda mahabusi halisi na kuondoka. Ni filamu yenye utatanishi na kuonekana na wengine kama inayokufuru Mungu kwa "kufanya mzaha" kuhusu maangamizi na wengine kama inavyohusu kutoshindwa kwa nafsi ya mwanadamu. |
| *Lions for Lambs* | Robert Redford | R – Baadhi ya ukatili wa kivita na lugha ya kutisha | Wakitiwa moyo na Profesa wao Dkt. Malley, wanafunzi wawili wanaamua kujiunga na vita nchini Afghanistan. Mapambano yao ya kunusurika kwenye uwanja wa vita Afghanistan yanakuwa ndiyo kamba ya kuunganisha pamoja visa viwili vinavyotofautiana sana. Huko Califonia, Malley anajaribu kufikia mwanafunzi aliyebahatika lakini asiyeridhika, wakati Washington D.C. mgombea uraisi mwenye matarajio ya kushinda Seneta Jasper Irving, anakaribia kutoa hotuba kali kwa mwandishi mchunguzi wa TV itakayoathiri majaliwa ya mtoto. Hadithi tatu zote zimefumwa pamoja, zikieleza namna kila mmoja wa wamarekani hawa anavyokuwa na athari kubwa kwa kila mmoja – na ulimwengu. |
| *Malcolm X* | Spike Lee | | Wasifu wa Malcolm X, kiongozi maarufu wa Wamarekani Weusi. Jina la kuzaliwa likiwa Malcolm Little, baba yake mchungaji aliuawa na Ku Klux Klan. Alikuwa jambazi, na alipokuwa jela aligundua maandiko ya Taifa la Kiislamu ya Elijah Muhammad. Baada ya kutoka jela alihubiri mafundisho lakini akiwa kwenye hija katika mji wa Mecca alisilimishwa kuingia dini halisi ya Kiislamu na kuwa muislamu wa Sunni. Alibadili jina lake kuwa El – Hajj Malik Al-Shabazz na kusitisha mafundisho yake yanayopinga wazungu. Hatimaye aliuawa na kufa kama Shujaa wa Kiislamu. |
| *Mother Teresa: In the name of God's poor* | Kevin Cannor | G | Hiki ni kisa cha kweli cha Mother Teresa, kinachoanzia Calcutta, India anakokabili dhiki kutoka kila upande na ambako anaweka msingi wa jihadi yake ya kusaidia watu maskini zaidi miongoni mwa maskini wa Mungu. |

| Jina | Mwongozaji | Hadhi | Maelezo mafupi |
|---|---|---|---|
| *Motorcycle Diaries*<br><br>*(Diarios de Motocicleta)* | Walter Salles | R – Lugha | Motorcycle Diaries imetokana na jarida lililoandikwa na Ernesto 'Che' Guevara de la Serna alipokuwa na umri wa miaka 23. Filamu hiyo inahusu safari zake kwenye nchi za Amerika ya Kusini akiwa na rafiki yake Alberto Granado kwa pikipiki ya modeli ya 1939 Norton 500. Akiwa amezaliwa kwenye familia ya juu kiasi, hii ilikuwa safari yake ya kwanza ya haraka katika nchi za Amerika ya Kusini. Anashuhudia wajibu na maisha ya wenyeji wa vijijini wakiwemo wafanyakazi wa migodini na Wakomunisti walioteswa na kukimbia makazi yao. Hii ilisababisha tamko la 'Che' la kuwa tayari kupambana na kufa kwa ajili ya wafanyakazi katika bara la Amerika ya Kusini. |
| *Pay it Foward* | Mimi Leder | PG-13 – Vipengele muhimu vya watu wazima vikiwemo matumizi ya dawa za kulevya, kupata nafuu tena, baadhi ya matukio ya kingono, lugha fupi na ya ugomvi | Kijana Trevor Mckinney anakabiliwa na zoezi la kuvutia kutoka kwa mwalimu wake mpya wa elimu ya jamii, Mr. Simonet. Zoezi hilo: Fikiria jambo la kubadili ulimwengu na kuliingiza katika utekelezaji. Trevor anasisitiza wazo la kulipa upendeleo si nyuma bali mbele – kulipa matendo mazuri si kwa kurudisha fadhila, bali kwa matendo mema yaliyofanywa kwa watu watatu wapya. |
| *Pelle Conqueror* | Bille August | | Mwishoni mwa karne ya 19, mashua iliyojaa wahamiaji wa Sweden inakuja kwenye Kisiwa cha Bornholm cha Denmark. Miongoni mwao ni Lasse na mwanawe Pelle. Wanapata ajira kwenye shamba kubwa lakini wanafanyiwa kuonekana kuwa ni aina ya viumbe duni. Pelle anaanza kuzungumza Kideni lakini ananyanyaswa kama mgeni lakini hakuna hata mmoja wao anayeacha ndoto yao ya kutafuta maisha bora zaidi ya maisha waliyoyaacha Sweden. |
| *Schindler's List* | Steven Spielberg 1973 | R – lugha, mambo ya ngono kidogo na ukatili halisi | Schindler's list inatueleza hadithi ya Oskar Schindler, mfanyabiashara wa Kijerumani aliyeokoa maisha ya Wayahudi wa Kipolandi zaidi ya elfu moja wakati wa maangamizi ya Wayahudi. Inatokana na kitabu cha Schindler's Ark cha Thomas Keneally. |

| Jina | Mwongozaji | Hadhi | Maelezo mafupi |
|---|---|---|---|
| *The Sea Inside* | Alejandro Amena'ba | | Hadithi ya maisha ya Mhispania Ramo'n Sampedro, aliyefanya kampeni ya miaka 30 kushinda haki ya kumaliza maisha yake kwa hadhi. Filamu inatafuta uhusiano wa Ramo'n na wanawake wawili. Julia, mwanasheria anayeunga mkono kampeni yake, na Rosa, mwanamke wa kawaida anayetaka kumthibitishia kwamba maisha ni mazuri. Kupitia kipaji cha mapenzi yake, wanawake hawa wawili wanavutiwa kukamilisha mambo ambayo hawakuwahi kufikiria kama inawezekana. Licha ya kutaka kufa, Ramo'n alimfundisha kila mtu aliyekutana naye, maana, thamani na tunu ya maisha. |
| *Silent Waters* | Sabiha Sumar | | Filamu inaonyesha athari ya maisha nchini Pakistan mwaka 1979 chini ya utawala wa Kijeshi wa Jenerali, Rais Zia-ul-Haq. Inaeleza maisha ya Ayesha, mjane ambaye maisha yake yanategemea mtoto wake wa kiume, Saleem mpole, mwenye macho ya kusinzia wa umri wa miaka 18 anayependa Zubeida. Saleem anajihusisha kwa kina na kikundi cha wanaharakati wa Kiislamu wenye imani kali ya kumwacha Zubeida. Matukio yanapamba moto wakati, mahujaji wa Kisingasinga kutoka India wanapomiminika kwenye kijiji, mmoja wao alianza kumtafuta dada yake aliyetoroshwa mwaka 1947. Tukio hili linaamsha hisia kali za moyoni. |
| *Veer-Zaara* | Yash Chopra | | Saamiya Siddiqui, ni wakili wa kike kijana mwenye shauku ya kazi yake, amepewa dhima ya kuangalia haki za binadamu kwa wafungwa wa nchini Pakistani. Mojawapo ya kesi hizo ni Rajesh Rathore alituhumiwa ujasusi kwa jeshi la India aliyekutwa akifanya ujasusi na kuhukumiwa kifungo cha maisha. Saamiya anabaini kwamba huyu si jasusi bali ni Singasinga anayempenda mwanamke wa Kiislamu. Alijikuta kwenye mtandao wa ulaghai na usaliti na kulazimishwa kutia saini "kukiri kosa" kulikomfanya afungwe kwa miaka 22. Saamiya anathibitisha kwamba Veer amefungwa kwa makosa lakini wenzake hawapendi mwanamke anayefanya kazi ya mwanamume". |

| Jina | Mwongozaji | Hadhi | Maelezo mafupi |
|---|---|---|---|
| *Whale Rider* | Niki Caro | | Katika mwambao mwa mashariki ya New Zealand, Whangara wanaamini kuwapo kwao kunaanzia miaka elfu moja iliyopita kwa babu aitwae Paikea, aliyekwepa kuuawa wakati mtumbwi wake ulipopinduka kwa kusafiri hadi mwambao kwa kupanda kwenye mgongo wa nyangumi. Kuanzia wakati huo na kuendelea Watemi wa Whangara, ambaye kwa kawaida ni mtoto wa kiume anayezaliwa mwanzo, wamehesabiwa kuwa warithi wa moja kwa moja wa Paikea. Pai, msichana mwenye umri wa miaka 11, anaamini kwamba ndiye anayestahili kuwa mtemi mpya lakini babu yake Karo anabanwa na mila ya kumchagua kiongozi wa kiume. Pai anampenda Karo zaidi ya mtu yeyote duniani, lakini lazima akabiliane nae na mila ya miaka elfu moja ili kutimiza majaaliwa yake. |
| *Yenti* | Barbara Steisand | PG | Yente, mwanamke kijana wa Kiyahudi, alijifanya mvulana ili kupata udahili kwenye Yeshiva, ili kujifunza “Torah”, “Talmud”, nk.<br><br>Uigizaji wa “Yente, the Yeshiva Boy,” na Isaac Bashevis Singer (1902-1991) |

# Nyimbo


Kutumia muziki katika vipindi vya elimu kunachochea uzingativu na ubunifu wa watoto. Muziki unawasaidia watoto kuburudika na kushusha viwango vya msongo vinavyokwaza kujifunza kwao. Kusikiliza aina fulani ya muziki kunaweza kuamsha kutolewa kwa 'endorphins', kemikali ya kwenye ubongo, kuleta hali ya utulivu ambayo husababisha kujifunza kwa haraka.

Kupitia muziki watoto wanaweza kueleza hisia zao, kurudisha kumbukumbu na fikra na kupata hisia za utulivu, uhuru na starehe. Itasaidia kuimarisha njia za mawasiliano yasiyo ya mazungumzo na kuhimiza umoja na watu ambao hawajawahi kukutana kabla. Walimu na wawezeshaji wanaweza kutumia nyimbo kama mbadala usiotumia nguvu kupinga maovu, udhalilishaji na ukatili.

Kusikiliza wimbo kunaweza kusababisha majadiliano kuhusu masuala yaliyo muhimu sana kwa watoto na vijana siku hizi. Inaweza kusaidia kutayarisha nafasi ya kusikiliza, mazungumzo, kushirikiana na kuleta mjumuiko wa kuheshimika miongoni mwa washiriki.

Orodha ya nyimbo ifuatayo inaweza kutumika katika programu za kujifunza tamaduni na dini mbalimbali ili kuwamotisha washiriki kujifunza kuhusu imani za watu, tamaduni na dini nyingine. Nyimbo hizi pia zinaweza kuwa mahali pa kuanzia kujadili matatizo ambayo dunia inayakabili siku hizi, hisia na kukosa maelewano miongoni mwa watu. Unaweza kuwafundisha washiriki wako nyimbo na pengine kuzitafsiri kwenye lugha yako ya asili au ya nchi.





| Jina | Mwimbaji | Albamu | Nchi |
|---|---|---|---|
| Al-dameer El-Arabi. (The Arabic Consciousness) | Arab Singers | Single, 2008 | Arab counries |
| A Daniel, un chico de la guerra | Alberto Cortez | Entre Lineas, 1985 | Argentina |
| Color Esperanza | Diego Torres | Un Mundo Diferente 2002 | Argentina |
| Shosholoza | Helmut Lotti | Out of Africa, 2004 | Belgium |
| Canso sense nom | Lluis Liach | L'estaca., 1973 | Brazil |
| Breaking the Silence | Loreena Mckennit | Parallel dreams, 1989 | Canada |
| Gracias a la Vida | Mercedes Ossa | Las Ultimas Composiciones, 1966 | Chile |
| Sobreviviendo | Victor Heredia | Solo quiero la vida, 1984 | Chile |
| Solo le pido a Dios | Leon Gieco | El Encuentro | Chile |
| Fijate Bien | Juanes | Fijate Bien, 2000 | Colombia |
| Clandestino | Manu Chao | Clandestino, 2000 | France |
| Je crois que ca va pas etre possible | Zebda | Essence ordinaire, Barday, 1998 | France |
| Million Voices | Wyclef Jean | Hotel Rwanda: Music from the film, 2004 | Haiti |
| Sunday Blood Sunday | U2 | War, 1983 | Ireland |
| War Child | The Cranberrries | To The Faithful Departed, 1996 | Ireland |
| Shalom Shalom | Noa | Noa Gold | Israel |
| Shir Lashalom (Song for Peace) | Miri Aloni | Golden Hits Of The Nahal. | Israel |
| Buffalo Soldier | Bob Marley | One Love: The very Best of Bob Marley, 2001 | Jamaica |
| Hana (Flower) | Kina Shokichi | The Best Of Shokichi Kicha & Champloose | Japan |
| Jawaz al-Safr Passport | Marcel Khalifa | Promises of the Storm, 1999 | Lebanon |
| Khoufi Aa Wladi (My Fear For My Children) | Julia Boutros | Ta'awdna Alaik, 2006 | Lebanon |
| Folon | Salif Keita | The Past, 1995 | Mali |
| Me voy a convertir en un ave | Mana | Suenos Liquidos, 1997 | Mexico |
| Unknown Soldier | Fela Kuti | Unknown Soldier | Nigeria |
| Junoon | No More | Best of Junoon | Pakistan |
| Desapariciones | Ruben Blades | Buscando America, 1984 | Panama |

| Jina | Mwimbaji | Albamu | Nchi |
|---|---|---|---|
| Mama Afrika | Akon | Konvicted, 2007 | Senegal |
| Lokayak Nasannata | Sunil Edirisinghe | Mage Senehasa, 1985 | Sri Lanka |
| Hiroshima | Bjorn Afzelius | Exil, 1984 | Sweden |
| Brothers in Arms | Dire Straits | Brothers in Arms, 1985 | United Kingdom |
| Give peace a chance | John Lennon | Give Peace a Chance, 1969 | United Kingdom |
| Let there be Peace on Earth | Jill Jackson and Sy Miller | Circa, 1955 | United Kingdom |
| Peace Train | Cat Stevens | Teaser and the Firecat, 1971 | United Kingdom |
| The Specials | Free Nelson Mandela | In the Studio, 1984 | United Kingdom |
| The Way of Love | Olivia Newton – John | Gaia One Woman's Journey, 1993 | United Kingdom |
| A Summer Prayer for Peace | Archies | Sunshine, 1970 | United States |
| Masters of War | Bob Dylan | The Freewheelin' Bob Dylan, 1963 | United States |
| My Rainbow Race | Pete Seeger | Pete, 1966 | United States |
| Under the Rainbow | Joyce Rouse | Under the Rainbow, 2004 | United States |
| War | Bruce Springsteen | Live 1975-85 | United States |
| The Sounds of Silence | Paul Simon, Art Garfunkel | Wednesday Morning, 3 A.M, 1966 | United States |
| We are the World | Michael Jackson and Lionel Richie | We are the World, 1985 | United States |
| What a wonderful world | Louis Armstrong | What a wonderful world | United States |
| Where is the love? | Black Eyed Peas | Elephunk, 2003 | United States |
| Why can't we live together | Tim Thomas | Why Can't We live Together, 1964 | United States |

# Mashairi

Ushairi neno lenye asili ya Kigiriki, lenye maana ya "kutengeneza" au "kubuni" ni aina ya sanaa ambapo lugha inatumika kutokana na sifa za umbuji na kuleta hisia pamoja na, au badala ya, maana yake dhahiri.

Kusoma ushairi kwa watoto na vijana kunaongeza sifa za ubunifu, kisanii na kihemko katika namna ambazo vitabu vya riwaya haviwezi kuwasilisha. Vina na mizani vinatoa muktadha ambao watoto wanaweza kutabiri ni nini kinachofuata kwenye mistari ya shairi. Vinaonyesha usalama kutokana na mapigo yao ya kubembeleza ambayo ni muhimu kukuza amani ya ndani ya nafsi na starehe.

Mashairi yanasaidia kupanua maana halisi ya neno na kuamsha miitiko ya kihemko kwa njozi au ukweli. Matumizi ya utata, picha au kejeli hulipa shairi fursa ya kuwa na tafsiri mbalimbali, kwa hiyo, kuchochea ubunifu wa watoto na uwezo wa kutafuta uwezekano mbalimbali.

Mashairi yanaonyesha mistari ya upinzani na utekwaji wa fikra au shughuli, kukataliwa na kukumbatia, ya kutoa na kuchukua nafasi hiyo ya fikra kati ya ukinzani ambao huleta maana tu ndani ya mfumo wa ulimwengu uliobuniwa wa shairi. Hii inaimarisha uwezo wa watoto kuelewa uhalisia kutoka mitazamo tofauti bila ya kujali uhalisia huo unavyopingana.

Ushairi unaweza kufahamika kama mazungumzo ya aina moja na mfululizo wa aina ya mlolongo wa hadithi ambao ndio hasa tabia ya ushairi wenyewe ambayo inahusu maisha ya mtu.

Mara mtoto anapojiona mwenyewe katika shairi, anaweza kuanza kugundua maajabu ya maneno na uwezo wa ushairi. Shairi linaweza kukaririwa au kuimbwa au kuchukuliwa papo hapo, moyoni na akilini.

Mashairi yanaweza kutumiwa ama kabla, wakati au baada ya shughuli za kujipima na kujichunguza au kushawishi wakati wa kutafakari na ukimya kabla ya kuanza programu yako.

## Chumvi ya nafsi

Rafiki wapendwa,
Ni mara chache sana mnatenga muda wa kuongea nami… naikosa sana,
Ni hisia adimu zinazonifanya niwe mchangamfu nazo… mnazichukua,
Ni nyakati chache sana tunapokuwa pamoja… na nazitamani sana,
Ninapokugusa kwa muda mfupi hupata mhemko mkali na unahisi tupo karibu zaidi,
Ndiye mimi, ambaye kilio kimo ndani ya nafsi na hisia hukufanya utabasamu,
Ndiye mimi ambaye hunitambui kuwa ni injini ya maisha yako.
Nafsi yako

## Zungumza nasi kuhusu watoto

Na mwanamke aliyemweka mtoto kifuani kwake alisema, "Zungumza nasi kuhusu watoto."
Na alisema:
Watoto wako si wako.
Ni wana na mabinti wa maisha yanayowatamani kwa ajili yake.
Wanakuja kupitia kwako lakini si kutoka kwako,
Na ingawa uko pamoja nao, lakini si wako.
Unaweza kuwapa upendo wako, lakini si mawazo yako,
Kwa kuwa wana mawazo yao.
Unaweza kutunza miili yao lakini si nafsi zao,
Kwa kuwa nafsi zao zinaishi katika nyumba ya baadaye
ambayo huwezi kuitembelea, hata katika ndoto zako,
Unaweza kujitahidi kuwa kama wao, lakini huwezi kuwafanya kama wewe,
Kwa kuwa maisha hayarudi nyuma wala hayakawii kama jana…

*Khalil Gibran, "Mtume" sura ijulikanayo kwa jina "Watoto"*

## Watoto wanajifunza wanavyoishi

Kama watoto wanaishi kwa kukosolewa
Wanajifunza kulaani;
Kama wanaishi kwa uhasama
Wanajifunza kupambana;
Kama watoto wanaishi kwa dhihaka
Wanajifunza kuona haya;
Kama watoto wanaishi kwa aibu
Wanajifunza kuhisi kuwa wenye hatia;

(Lakini,)

Kama watoto wanaishi kwa uvumilivu
Wanajifunza kuwa wenye subira;
Kama wanaishi kwa kutiwa moyo
Wanajifunza kujiamini;
Kama watoto wanaishi kwa sifa,
Wanajifunza kufurahia;
Kama wanaishi bila upendeleo,
Wanajifunza haki;
Kama watoto wanaishi kwa usalam,
Wanajifunza kuwa na imani;
Kama watoto wanaishi kwa idhini
Wanajifunza kujipenda;
Kama watoto wanaishi kwa kukubalika na urafiki
Wanajifinza kutafuta upendo duniani.

*Dorothy Law Nolte*

## Hakuna nafasi ya chuki

Hakuna nafasi moyoni mwangu
kwa kulipa kisasi, ugomvi au chuki
hakuna nafasi akilini mwangu
kwa fikra kama hizi.

Sipati maneno ya kusema,
namna ninavyohisi
lakini naelewa kutokana na maumivu makali
ni lazima nitafute msamaha.

Maumivu tuliyofanyiwa
yamekata kidonda kama kisu,
lakini tusilipize kamwe
kwa kitendo tulichofanyiwa.

Badala yake tujitahidi na kutafuta
namna iliyo ngumu,
na kufikia mikono yetu ya upendo
kutafuta urafiki sasa.

Hakuna uponyaji zaidi wa mambo
Kuliko kufumbua macho yetu zaidi
na kuona kuwa watu wengine wote
ni kama sisi tu.

*David Gould*
*Aliandika baada ya binti yake kuuliwa katika Mabomu ya Mjini London, Julai 7, 2005*

## Mpakani

"Ndicho kituo cha mwisho cha kukaguliwa unapoingia nchini humu!"
Tulichukua kinywaji.
Baada ya muda kila kitu kitakuwa na ladha tofauti.

Ardhi tuliyokanyaga iliendelea,
kugawanywa kwa mnyonyoro mnene wa chuma.

Dada yangu anaweka miguu yake kutambuka mnyonyoro huo.
"Angalieni hapa" alitwambia,
"mguu wangu wa kulia uko katika nchi hii na mguu wangu wa
kushoto uko nchi nyingine."
Walinzi wa mpakani walimwambia aondoke.

Mama yangu aliniambia: Tunakwenda nyumbani.
Alisema kuwa barabara ni safi zaidi,
mandhari ya nchi yanapendeza zaidi,
na watu ni wakarimu zaidi.

Familia nyingi zilisubiri mvuani.
"Nasikia harufu ya nyumbani," mtu mmoja alisema.
Hivi sasa mama zetu walikuwa wanalia. Nilikuwa na umri wa miaka mitano,
nikiwa nimesimama kando ya kituo cha kukaguliwa,
nikilinganisha pande zote za mpaka.

Udongo wa majira na kupukutika majani uliendelea upande wa pili,
rangi na umbile sawa.
Mvua ilinyesha pande zote za mnyororo.

Tulisubiri wakati hati zetu zilipokuwa zikikaguliwa,
nyuso zetu zilikaguliwa kwa makini.
Halafu mnyororo uliondolewa kuturuhusu kupita.
Mwanamume mmoja aliinama na kuibusu ardhi ya nchi yake yenye tope.
Safu ile ile ya milima ilituzunguka wote.

*Choman Hardi*
*Mshairi Kijana wa Kikurdi wa London anayeandika kwa Kiingereza na lugha yake ya Kikurdi.*

## Dunia yenye matumaini zaidi

Ni kipindi cha Krismasi na natakiwa nifikirie kuwa furaha ni ya kwangu
Kila kitu ni shamrashamra, kila kitu ni cha kifahari, lakini roho yangu haiwezi kung'ara
Naendelea kufikiria namna watoto walivyo uchi na wagonjwa
Wana hamu ya haki na njaa ya chakula

Njaa, umaskini na vita ni mzigo unaobebwa na binadamu
Nilijiuliza, amani iko wapi? Upendo uko wapi?
Na kwanini huruma haitufikii?
Nakasirika na kukatishwa tamaa kushughulikia ulimwengu wenye matumaini zaidi

Wakati huo huo mdogo wangu wa kike alitembea kunifuata
Akiwa na tabasamu ya kuvutia, aliniomba nibusu mwanasesere wake,
Wakati akiigiza kunyonyesha maziwa mwanasesere
Aliniambia: tafadhali nisaidie kumnyonyesha, mpendwa Hind

Ilinigusa kama radi, jibu la huzuni na hasira zangu
Nilitambua kuwa jibu ni kufanya unaloweza na si kukata tama
Kama kila mtu anatoa mchango wake, watoto watakuwa na mahali pa amani pa kuishi
Watakuwa na dunia yenye matumaini zaidi, fursa mpya na matumaini

Tupende familia zetu, majirani na marafiki
Tumhudumie kila mtu na kufanya zaidi kutoka nyoyoni mwetu
Tufanye kadiri ya uwezo wetu kuboresha maisha yao, na matarajio ya mtoto
Tujenge dunia yenye matumaini zaidi ambayo watoto watapata upendo.

*Hind Farahat*
*Mjumbe wa Fishers Programme na mshiriki kijana wa GNRC, nchini Jordan*



## Shiriki katika mabadiliko unayotaka kuona

Sote tulikuwa pamoja wakati tuliposimama kidete kupambana na Waingereza,
Hutukujali tulikotoka, dini tuliyokuwa nayo, fikra au imani
Tulipata uhuru kutoka kwa Waingereza, tulikuwa tayari kuanza kwa nchi mpya
Viongozi wetu wenyewe walichukua madaraka na kutaka serikali ya kuongoza
Hawakujali walikotoka, dini waliyokuwa nayo, fikra au imani,

Lakini,
Haja ya kuwa na madaraka ilikuja, viongozi walikuwa na shauku ya kuongoza
Wazalendo walikuwa na uchu wa madaraka, vita vilianza kuchochewa,
Mahitaji na mitazamo ilibadilika, ubinafsi ulianza kujengeka,
Viongozi walifanya mabadiliko makubwa kwa muda mfupi

Mgawanyiko uliochochewa na lugha zilizosemwa kwenye nchi hii ndogo
Ulisababisha mgogoro wa kisiasa na matatizo ya kila mtu kuelewana na mwingine
Watu walianza kuwachukia wale wanaozungumza lugha ya "upande" mwingine
Mambo yalizidi kuwa mabaya,
Wale walioshikamana na kupigania uhuru walianza kugawanyika,
Vurugu ziliongezeka, watu walianza kuuana na amani ikapotea

Vikundi mbalimbali viliundwa kupigania haki zao, vurugu ziliongezeka na kuwa vita,
Watu wengi waliyakimbia makazi yao na kuacha kazi na familia zao,
Hakuna hata kiongozi mmoja aliyetambua makosa yaliofanyika zamani
Waliyatumia makosa hayo kubaki madarakani na kupata manufaa kwa ajili yao

Mpaka leo hatuna jibu la vita hii, wala hakuna anayejua kwa nini kuna vita.
Je, viongozi wetu walitumia lugha zetu tofauti kuchochea mfarakano?
Je, ilikuwaje kwa watu waliopigania uhuru pamoja na zaidi?

Hatimaye hivi sasa kunatokea nini?
Je tunataka kusahau yaliyopita?
Je, tunawaheshimu na kuwajali wengine?
Je, tunataka kushirikiana?

Sote tunajua kuwa tunataka kuishi na kufanya kazi pamoja,
Lakini hatuko tayari kufanya hivyo,
Watu wanataka wasahau yaliyopita na kusahau vita,
Lakini ubinafsi wetu umekua sana
Miaka elfu moja ya manung'uniko hayawezi kutanzuliwa kwa miaka kumi na zaidi,
Hatutaweza kubadili mambo sasa, kwa sababu usasa umepondwa

Lakini,
Tutakuwa viongozi wa kesho na kuweka mstakabali wetu wenyewe,
Tutafanya kazi kwa nchi ambapo kila mmoja anamheshimu mwenzake na kuendelea,
Tutajifunza kuwa pamoja na kuwezesha amani kuzaliwa

Tunaweza kujibadili wenyewe kabla ya kubadili ulimwengu,
Tunaweza kutanzua matatizo yetu kabla ya watu wengine kujaribu kutanzua,

Tunaweza kuwa na nchi ambapo kila mtu anaweza kuishi kwa amani,
Tusilaumiane bali tujaribu angalau kutafuta ufumbuzi,
Si Brits walioleta hali hii;
Hawakuwapo wakati madaraka tulipoyasheherekea,

Kama una ari ya kubadili ulimwengu, anza na wewe mwenyewe,
Huwezi kutarajia mabadiliko kuonyesha matokeo yenyewe,
Mtu ni lazima ajitolee mhanga na kufanya kwa kuleta mabadiliko
Starehe na maslahi binafsi havina nafasi hapa

Hakuna nchi iliyokamilika; unahitaji kuikamilisha…
"Muda ndio mponyaji, lakini muda unakwenda,
Muda haumsubiri mtu, lakini mambo yanahitaji kubadili mwelekeo wake"

Tunahitaji kubadilika katika amani
Sisi tunatakiwa kuwa mabadiliko tunayotaka kuyaona.

*Nooranie Muthaliph*
*Mwanachama Kijana wa GNRC, Sri Lanka*

## Sauti ya Watoto wa Afrika

Amani, Amani, Amani kwenye familia zetu,
Amani kwa kila mmoja anayetuzunguka,
Amani ni chanzo cha maendeleo,
Amani inaleta upendo na furaha.

Vurugu, Vurugu ziondoke kwenye jamii zetu,
Vurugu ni kilio kwa wasio na hatia,
Vurugu husababisha familia kuvunjika na kutengana,
Vurugu ni dalili za ukali na ukatili.

Amani na maliasili vimeharibiwa nchini kwetu
Angalia watoto nchini Somalia wanaoshika bunduki
Nenda Ethiopia au Angola, watu wanakufa njaa na katika mapigano
Watoto wa Afrika wanakata tamaa kuhusu maisha yao ya baadaye

Njoo Tanzania, watoto wengi wanaishi mitaani,
Wanatoroka kwao, kutafuta aina tofauti ya maisha
Familia zao zimetengana
Na haki zao zimekiukwa

Hakuna anayewasaidia,
Watu wanajifanya hawawaoni,
Wanawabeza namna wanavyofanya,
Wakati wanapoomba na kuiba mitaani.

Ardhi yetu yenye amani,
Imegeuka kuwa mahali pa mapigano,
Watu wameharibu maliasili yake ya kuvutia,
Ee Mola, "Tutarithi nini?"

Sauti hii ni kwa watoto wa Afrika,
Tumechoka kuwaona watu wakifa mbele yetu,
Tunataka bara tofauti,
Tunataka kurejesha amani yetu.

*Clara Mduma*
*Mwanachama Kijana wa GNRC, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania*

# Sala za Amani

**"Tunataka kwa dhati, tunapinga na kudhamiria…"**

Wakati wa mkutano wa dini mbalimbali katika Baraza la Makanisa Duniani mwaka 2005, kikundi wakilishi cha jumuiya za kidini walikutanika kwa kero moja kuu kuhusu aina ya ulimwengu tutakaourithisha kwa vijana na watoto wetu. Walisumbuliwa sana na kuenea kwa ugomvi na utamaduni wa kutenga na choyo vinavyoenea ulimwenguni. "Kwa hiyo tunatambua", walisema "umuhimu mkubwa wa mafunzo ya dini kwa ajili ya kurithisha hazina za urithi wetu kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Ni muhimu kwa kila jumuiya ya kidini kuelewa haja ya kuwawezesha vijana kushiriki katika mageuzi ya urithi wao yanayoendelea…

"Pia tunaangalia mchakato wa kujifunza utakaojenga mtazamo jumuishi, wa wazi na wenye huruma kwa wengine kwa msingi wa imani na dini ya mtu anayehusika. Pia tunaona umuhimu wa kuwa na uelewa unaofahamu mila na desturi za dini ya kila mtu, ili tusiwe na taswira za wengine kutokana na chuki za muda mrefu na upotoshaji unaofanywa na vyombo vya habari."

"Kutambua kuwa uhusiano kati ya dini na vurugu umekuwa miongoni mwa masuala muhimu ya siku hizi, kikundi kilisema: "Tunaamini kwamba, hakuna mila na desturi ya dini yoyote inayoona vurugu kama wema au unyofu wa dini na tunajua kwamba vurugu si asili ya dini yoyote. Kinyume chake, upendo, huruma na kuishi kwa pamoja kwa amani ni maadili ambayo mila na desturi zetu zote zinazingatia. Kwa hiyo tunapinga dhana ya vurugu katika dini na tunajitahidi kuelekea katika kutimiza uwezekano wa kuwa na amani na kutokuwa na vurugu vinavyoshikiliwa kuwa ni maadili ya msingi katika mila na desturi zetu."

## Ahadi za Pamoja

"Tunatambua kwamba changamoto tunazokabiliana nazo duniani zina nguvu sana kwa mila na desturi yetu yoyote kushughulikia, na kwamba tunahitajiana katika juhudi zetu za kuzishughulikia. Kwa hiyo, tusifanye peke yetu vile tunavyoweza kufanya pamoja. Ni katika uwezekano wa kutambua na kutenda kwa pamoja ndipo tunaweza kugundua kweli kila mmoja wetu, na ni katika kufanya ahadi za pamoja ndipo tutakapokua pamoja. Kwa hiyo, tunatoa matamko na ahadi zifuatazo:

**Tunatamka kwa dhati kwamba**, wanadamu wanaotokana na watu wengi, mataifa, mbari, rangi, utamaduni na mila na desturi za dini mbalimbali ni familia moja ya kibinadamu.

Kwa hiyo **tunapinga** juhudi zote za kuweka vizuizi vyovyote kati ya mila na desturi za kidini kwa kuziwakilisha kama jumuiya za kipekee zinazoafikiana.

**Tunaahidi** kujifunza zaidi kuhusu kila mmoja wetu, kujifunza kutokana na kila mmoja na kujigundua tena sisi wenyewe kuhusiana na wengine.

**Tunatamka kwa dhati** kwamba katika kiini cha mila na desturi zetu kuna upendo, huruma, kujitolea nafsi, na maadili yanayodumisha maisha na maisha katika jumuiya.

**Kwa hiyo tunapinga** tafsiri zote za mafundisho ya dini zinazojenga chuki, uadui au kuwatenga wengine.

**Tunaahidi** kukuza na kuendeleza mafundisho na desturi kwenye mila za dini zetu zinazostawisha maisha na kukuza jamii.

**Tunatamka kwa dhati** kwamba vurugu na vita ni kinyume na mafundisho ya dini zetu na hakuna hata mila na desturi za dini zetu zinazounga mkono usuluhishi wa migogoro kwa njia ya kutumia nguvu.

**Kwa hiyo tunapinga**_vurugu zote zinazotumiwa kwa kisingizio cha dini, tafsiri zote za dini zinazounga mkono vita na juhudi zote za kufasiri maandiko yetu matakatifu kuunga mkono migogoro.

**Tunaahidi** kutafsiri, kufundisha na kufanya mila na desturi za dini zetu kwa ajili ya kukuza amani na utulivu.

**Tunatamka kwa dhati** kwamba ubaguzi kwa msingi wa mbari, tabaka, hadhi ya kijamii, uwezo wa mwili na akili, mbari, jinsia n.k. ni kinyume na mafundisho yote ya dini zetu. Kwa hiyo tunapinga aina zozote za ubaguzi na kuwatenga wengine.

**Tunaahidi** kujitahidi kujenga jumuiya jumuishi na kupambana dhidi ya tafsiri za imani, dini na maandiko matakatifu yetu zinazohalalisha ubaguzi.

**Tunatamka kwa dhati**_kwamba haki na kutokuwa na upendeleo ni muhimu kwa maisha ya dini, kwamba umaskini, upotoshaji, njaa na maradhi ni vichocheo vinavyopunguza utu wa mtu na uwezo wake.

Kwa hiyo **tunapinga** mpangilio wa maisha ya kiuchumi na kisiasa unaoleta udhalimu, kutokuwa na usawa, na uchimbaji wa maliasili za ardhini kupita kiasi kwa choyo cha binadamu

**Tunaahidi** kulinda na kutetea utu na haki za binadamu, kijamii na kiuchumi za watu wote na umoja wa dunia.

**Tunathibitisha** kutetea haki za vijana na watoto na vipawa wanavyoleta kwa uelewa na desturi za maisha ya dini.

**Kwa hiyo tunapinga** juhudi zote za kuwatenga kwenye mkondo mkuu wa maisha ya dini.



**Tunaahidi** kukuza jumuiya jumuishi zitakazoshirikisha vijana na watoto kwa ukamilifu kuwawezesha kuleta vipawa vyao kwenye maisha yetu ya pamoja.

Imesemwa kwamba safari ya umbali wa maili elfu moja huanza kwa hatua moja. Tunaona ahadi hizi kama hatua tunazochukua kutimiza dira ya kuwa na ulimwengu ambao watu wataishi kwa haki na amani. Tunatoa wito kwa jumuiya zote za kidini kufanya matendo ya ahadi zote kuwa ni zao na kuendeleza dira ya kiroho itakayoleta uponyaji na ukamilifu kwa ulimwengu wetu ulio na mpasuko."[1]

Ni muhimu kwamba matamko na uthibitisho huu vimetokana na hisia ya haraka ya haja ya watu kutoka kwenye mila na desturi zote za dini kusema na kutenda kwa pamoja kuhusu masuala yanayoathiri maisha yao ya pamoja! Hata hivyo,haraka hiyo haionekani tu na jumuiya za kidini bali pia na wale wanaopata msukumo wao kutokana na maadili ya binadamu na mambo ya kiroho yasiyofahamika kwa lugha ya kidini.

1 Kutoka hati, *Religious Life: A Commitment and Calling*, kupitia mchakato wa mahusiano ya dini mbalimbali ulioandaliwa na WCC, 2005.

## Sala ya dini mbalimbali kwa amani

Ewe Mwenyenzi Mungu, wewe ni chanzo cha maisha na amani.
Jina lako litukuzwe daima.
Tunajua kuwa ni wewe unayebadili akili zetu kwenye fikra za amani.
Sikiliza sala yetu katika kipindi hiki cha hali ya wasiwasi mkubwa.
Uwezo wako unabadili nyoyo.

Waislamu, Wakristo na Wayahudi kumbuka na kutamka kwa dhati,
kwamba ni wafuasi wa Mungu mmoja,
Watoto wa Ibrahimu, kina kaka na kina dada;
maadui wanaanza kuzungumza pamoja;
wale waliofarakana shikaneni mikono kwa urafiki;
mataifa yanatafuta njia ya amani pamoja.

Imarisha kusudio letu kutoa ushahidi kwa
ukweli huu kwa namna tunavyoishi.
Tupatie:
Uelewa utakaomaliza ugomvi;
Rehema itakayoondoa chuki, na
Msamaha utakaoshinda kisasi.
Wawezeshe watu wote waishi katika sheria yako ya upendo
Amina.

*(Pax Christi)*



## Ewe Busara ya Milele

Ewe busara ya milele
ambaye tunakujua kiasi
na kiasi fulani hatukuji;
Ewe haki ya milele
ambaye tunakukiri kiasi
lakini hatukutii kwa ukamilifu;
Ewe upendo wa milele
ambaye tunakupenda kidogo
lakini tunaogopa kukupenda sana;
Tufungulie akili zetu
ili tuweze kuelewa;
Tufanye kazi kwa nia zetu
tunazoweza kutii;
Angaza nyoyo zetu
ili tuweze kukupenda wewe.

*(Sala katika sherehe za dini mbalimbali na kuadhimisha miaka 70 ya kuzaliwa kwa Askofu, Profesa, Krister Stendahl, 21 Aprili, 1991)*

## Nifanye kuwa zana ya amani yako

Ee Mola, nifanye kuwa zana ya amani yako;
pale penye chuki, niweze kupanda upendo;
panapotokea dhara, samehe;
pale penye shaka, imani;
pale penye kukata tamaa, matumaini;
pale penye giza, nuru;
na pale penye huzuni, furaha.
Nipe kile ambacho sitahitaji zaidi
kufarijiwa kama nitakavyofariji;
kueleweka kama nitakavyoelewa,
kupendwa, kama nitakavyopenda;
ni kwa kutoa, ndipo tutakavyopokea,
ni katika kusamehe, ndipo tunaposamehewa,
na ni katika kufa (sisi wenyewe) ndipo tutakapozaliwa katika maisha ya milele.

*(St. Francis of Assisi)*

## Naomba Niwe Wakati Wote

Naomba niwe wakati wote, sasa na daima
Mlinzi wa wale wasio na ulinzi
Kiongozi kwa wale waliopotea njia,
Meli kwa wale wenye bahari za kuvuka
Daraja kwa wale wenye mito ya kuvuka
Kimbilio, kwa wale walio hatarini
Taa, kwa wale wasio na mwanga
Mahali pa kujihifadhi, kwa wale wasio na makazi
Na mtumishi wa wote wenye shida.

*(Dalai Lama wa XIV, Novemba, 6, 2000)*

## Kuwa Mkarimu

Kuwa mkarimu katika ustawi, mwenye shukurani wakati wa dhiki. Usiwe na upendeleo katika uamuzi wako, na kulindwa katika kauli yako. Kuwa mwanga kwa wale wanaotembea gizani, na maskani kwa wageni. Kuwa macho kwa vipofu, na mwanga wa kuongozea miguu ya waliopotea. Kuwa pumzi ya maisha katika mwili wa binadamu, umande kwenye udongo wa moyo wa binadamu, na tunda kwenye mti wa unyenyekevu.

*(Baha 'u' llah)*

## Amani Duniani

Kama kunatakiwa kuwa na amani duniani,
Lazima kuwe na amani katika mataifa.

Kama kunatakiwa kuwa na amani katika mataifa,
Lazima kuwe na amani katika miji.

Kama kunatakiwa kuwa na amani katika miji,
Lazima kuwe na amani miongoni mwa majirani.

Kama kunatakiwa kuwa na amani miongoni mwa majirani,
Lazima kuwe na amani nyumbani.
Kama kunatakiwa kuwa na amani nyumbani,
Lazima kuwe na amani moyoni.

*(Lao – Tse)*

## Njia ya Utakatifu

Kama kuna mtu yeyote anayekusema kwa ubaya,
Wasifu daima.
Kama kuna mtu yeyote anayekukosea,
Watendee mema.
Kama kuna mtu yeyote anayekuadhibu,
Wasaidie kwa kila hali,
Utapata
nguvu nyingi.
Utadhibiti hasira na fahari.
Utafurahia
amani, utulivu na shwari.
Utakuwa mtakatifu.

*(Swami Sivananda)*

## Sala ya Wote kwa Amani

Niongoze kutoka kifo hadi maisha;
kutoka uongo hadi ukweli.
niongoze kutoka kukata tamaa hadi matumaini;
kutoka hofu hadi imani.
Niongoze kutoka chuki hadi upendo;
kutoka vita hadi amani.
Wezesha amani ijaze nyoyo zetu,
Dunia yetu, ulimwengu wetu.

*(Wiki ya Sala ya Amani Duniani, iliyochukuliwa kutoka wimbo wa zamani wa Jain)*

## Tujalie Amani ya Kweli

Ee Mwenyenzi Mungu! Ee Bwana Wetu. Wewe ni maisha ya milele na amani ya kudumu kutokana na asili yako na sifa. Amani ya kudumu inatoka kwako na inarudi kwako. Ewe Mhimili wetu! Tujalie maisha ya amani ya kweli na tuongoze kwenye maisha ya amani. Ewe Mtukufu na Mwingi wa Ukarimu! Umebarikiwa na Utukufu.

*Allahumma ya mowlana antas-salaam, wa minkas-salaam, wa ilaika yarjaus-salaam, haiyyina rabbana bis-salaam, wa adkhilna daras-salaam, tabarakta rabbana wa-ta' laita, ya zal jalali wal ikram*

## Sala ya Amani

Na kama hao maadui wakielekea katika amani, nawe pia uelekee na mtegemee Mwenyenzi Mungu. Hakika yeye ndiye asikiaye na ajuaye.

Sura ya 8, al- Anfal (Mali iliyotolewa vitani) aya ya 61.

Tafsiri ya Kiingereza ilikuwa ya A. Yusuf Ali

## Mambo ya Wema ya Buddha

Hivi ndivyo inavyotakiwa kufanyika
na yule stadi wa wema,
Na anayejua njia ya amani…

Kusiwe na hata mtu wa kumdanganya mwigine,
Au kumdharau yeyote aliye katika hali yoyote.
Kamwe kwa njia ya hasira au nia mbaya
Usimtakie mabaya mtu mwingine.
Hata kama mama analinda maisha yake
Mtoto wake, mtoto pekee,
Kwa hiyo kwa moyo mkunjufu
Mtu hana budi kuwahifadhi kwa upendo binadamu wote:
Kueneza wema duniani kote
Kusambaa kuelekea juu mbinguni
Na kuelekea vina vya chini ya ardhi;
Nje bila ya mipaka,
Kuondolewa chuki na nia mbaya.
Awe amesimama au anatembea, amekaa au amelala
Asiwe na usingizi,
Mtu hana budi kuhimili kumbukumbu hii.
Hii ni kwa walioambiwa kuwa watukufu wanaotii,
Kwa kutoshikilia mawazo mgando,
Wenye nyoyo safi, wenye ubayana wa dira,
Kuwa huru kutokana na hisia zote za matamanio,
Hajazaliwa tena kwenye ulimwengu huu.

*(Sutta Nipata, 145)*

## Siku za "Kuogofya"

Katika kalenda ya Kiyahudi ni wale walio karibu na sherehe takatifu ya Yom Kippur, muda wa upatanisho kwa dhambi zake.

Ewe chanzo cha Amani, tuongoze kwenye Amani, amani muhimu na ya kweli;
tuongoze katika uponyaji, kumudu yale yote yanayotusababishia vita
ndani yetu na wengine.
Tunaomba matendo yetu yatuandike kwenye Kitabu cha Uzima na Baraka,
uadilifu na amani!
Ewe chanzo cha Amani, tubarikie amani.

*(Stern, Chain (ed) Gates of Repentance)*

## Sala ya Dini Mbalimbali kabla ya Mkutano wa Amani Duniani wa Milenia wa viongozi

### wa kidini na kiroho katika Umoja wa Mataifa, Agosti, 2000

Tuzike silaha zetu za vita
Ili ziweze kugeuzwa kuwa maua ya utulivu na furaha;
Tuweke silaha zetu chini
Tuinue mikono yetu kwa Muumba
Sala zetu na tafakari zigeuze ulimwengu huu
Kuwa bustani ya furaha ya milele;
Na kila mmoja wetu aeneze Mwanga na Upendo,
Kuleta amani duniani kote.

*(Sant Rajinder Singh Ji Maharaj)*



## Sala katika eneo lililolipuliwa bomu la atomiki, Hiroshima, Japan

Kwako Muumba wa Ulimwengu na viumbe, kwa ukweli na uzuri Naomba:

Sikiliza sauti yangu, kwa sababu ni sauti ya waathirika wa vita vyote na vurugu miongoni mwa watu na mataifa,

Sikiliza sauti yangu kwa sababu ni sauti ya watoto wote wanaoteseka na watakaoteseka wakati watu wanapoweka imani zao kwenye silaha na vita.

Sikiliza sauti yangu wakati ninapokuomba kujaza mioyoni mwa wanadamu wote busara ya amani, nguvu ya haki na furaha ya urafiki.

Sikiliza sauti yangu kwa sababu nazungumza na umati katika kila nchi na katika kila kipindi cha historia, wasiotaka vita na wako tayari kutembea barabara ya amani.

Sikiliza sauti yangu na nipe utambuzi na nguvu ili daima tuweze kushughulikia chuki kwa upendo, ukosefu wa haki kwa kujitoa kwa ajili ya haki, mahitaji kwa kushirikiana na nafsi, na vita kwa amani.

*(Pope John Paul II)*

## Naomba kuwe na Amani

Naomba kuwe na Amai, Ewe Mtoto – Usiruhusu kuwapo kwa vita.
Weka chini mkuki wako na uache kama ishara –
Kwamba watoto wako wataona ushahidi.
Nenda kwa babu yako – kwa Auruia
Ili aweze kukufundisha wewe katika korero.

Naomba kusiwe na vita; kwa sababu mpenda vita hatosheki;
Lakini naomba mtoto wangu badala yake awe mtu mweye busara na mwenye kujifunza,
Mtunzaji wa mila nyumbani kwake.
Kusiwe na vita.
Pandikiza ndani zaidi moyo wa amani
Ili utawala wako uweze kufahamika –
Nchi inayozingirwa – na amani kote.

*(Wimbo kutoka Kisiwa cha Rarotonga, Polynesia)*

## Moyo wangu umeweza

Moyo wangu umeweza namna zote:
Ni malisho ya swala na nyumba ya Watawa wa Kikristo,
Hekalu la sanamu na Ka’ ba ya hija,
Meza za sheria na Kitabu cha Qurani.
Natangaza dini ya Upendo, na kwa upande wowote
Farasi wake atakaoelekea, upendo ni dini na imani yangu.

*(Ibn Arabi, 1165 – 1240)*

# Igizo Dhima

Igizo dhima ni njia inayofaa sana kuwasaidia washiriki kuona mambo kwa mtazamo mwingine.

*"Kama ungekuwa wewe ungefanyaje" ni ushauri mzuri. Watoto wetu watajifunza kuwaheshimu wengine kama wamezoea kujifikiria wao wenyewe katika nafasi ya mtu mwingine.* [1]

Igizo dhima kwa wakati huo linafurahisha na linafaa kwa sababu linawapa changamoto washiriki kushughulikia matatizo magumu bila ya 'jibu' hata moja na kutumia stadi za aina mbalimbali.

Mazoezi ya igizo dhima yanahitaji maandalizi na kuwa mwangalifu wakati wa utekelezaji, hata hivyo kazi hiyo inaelekea kulipa kutokana na motisha ya washiriki na ukamilishaji.

Ni muhimu kueleza madhumuni katika kuamua ni mada gani za kushughulikiwa kwenye zoezi. Bainisha tatizo linalohusiana na mada iliyochaguliwa na kupanga wahusika. Ni wazo zuri kufanya igizo kuwa halisi, lakini si lazima kuwa halisi.

Fanya malengo ya mhusika na inakuwaje kama mhusika hafikii malengo yaliyowekwa. Tafuta taarifa ya awali ya kila mhusika.

Washirikishe wahusika katika igizo kwa kueleza igizo lilivyo na tatizo. Wape taarifa kuhusu wahusika: malengo na taarifa ya awali. Baini ni wahusika wangapi wamewahi kufanya igizo dhima kabla na eleza namna itakavyokuwa kwa zoezi hili.

Washiriki watakaocheza wahusika wanahitaji muda mfupi wa kuangalia wahusika wao na kuchukua nafasi zao kwa ajili ya zoezi. Washiriki wanaweza kuwa na maoni kuhusu wahusika waliopangiwa au kuhusu malengo yao. Inafaa kujua hayo kabla ya kuanza igizo dhima.

Igizo dhima linahitaji kufuatiwa na kuwahoji washiriki waeleze walichojifunza na kuiwekea mkazo. Hatua hii inaweza kufanywa kwa majadiliano, kwa kutafakari au baada ya muda kwa kila mmoja kuandika kwenye logu ya Kujifunza. Wale wanaocheza wahusika wanaweza kuzungumzia kuhusu wahusika wao na pia kuchangia mawazo kuhusu kama kweli walikuwa wakieleza wanachohisi au kuzungumza tu katika uhusika. Wale waliokuwa wakitazama wanaweza kuuliza maswali kwa wahusika, kama uhusikawao "kiti moto" na kama wao wakati mwingine hujulikana kama wenyewe – walijihisi vipi kuwa katika nafasi mahusussi.

Baadhi ya maigizo dhima yameonyeshwa hapa, lakini kwa kufanya mazoezi, ni rahisi sana kuyabuni wewe mwenyewe kutokana na matukio ya mada.

1 *Neil Kurshan, Raising Your child to Be a Mensch, ch 4, 1987*

## Kadi ya 1 ya Igizo Dhima

Punjama ni msichana mwenye umri wa miaka 17. Anaishi na baba, mama na kaka zake wawili. Kwa kuwa ni msichana pekee, wazazi wake wanamlinda sana na hawataki awe na rafiki wa kiume. Familia ya Punjama ni wahafidhina sana na wanadumisha mila na desturi za dini na utamaduni wao. Punjama alikutana na Mathew, rafiki mkubwa wa kaka yake na akaanza kumwomba miadi bila ya kuwaambia wazazi wake au kaka zake. Mathew si muunini wa dini moja na Punjama na hawatoki nchi moja.

Siku moja, mmoja wa kaka zake Punjama alimwona dada yake akiwa ameshikana mikono na Mathew mtaani na kuwaambia wazazi wake. Walimkasirikia sana Punjama na walimsubiri mpaka arudi nyumbani. Aliporudi nyumbani, mama yake alianza kumgombeza na kumwambia amewaaibisha na kwamba hastahili kuendelea kuwa binti yao. Kaka zake Punjama waliwapendekezea wazazi wao wamfungie Punjama nyumbani ili asimwone tena Mathew. Baba yake akiwa amejawa na hasira alimfuata Punjama kwa kasi na kumpiga makofi, alikimbilia chumba kingine lakini kaka zake walimfuata na kumrudisha kwa wazazi wake.

## Kadi ya 2 ya Igizo Dhima

Sarah, Lina na Lucy ni marafiki wakubwa shuleni. Daima wako pamoja na kufurahia kuwacheka wasichana wanaoona aibu au wanaofanya mambo yasiyowapendeza

Farzina na Laura ni wanafunzi wapya shuleni. Bado hawana marafiki wengi, lakini ni wacheshi na wanafunzi wengine.

Siku moja Farzina na Laura walikuwa wakicheza mpira wa kikapu uwanjani wakati Sarah, Lina na Lucy walipowafuata. Waliwaambia Farzina na Laura waondoke uwanjani na mpira wao kwa sababu wanataka kucheza. Farzina aliwaambia kwamba ndiyo kwanza wameanza kucheza na wangependa kucheza kwa muda zaidi. Sarah alikasirika sana na kumsukuma. Farzina naye alijibu, akamsukuma Sarah nyuma na halafu Lina na Lucy nao wakaingia katika mapigano. Laura alikuwa na wasiwasi kuwa wanaweza kumwumiza Farzina na alimtupia mpira kwa nguvu Sarah kichwani na akaanguka. Sarah alicharuka kwa hasira na kumwendea Laura moja kwa moja na kumpiga.

# Kadi za Habari za Amani

Kadi hizi zitumike pamoja na shughuli ya Habari za Amani kwenye ukurasa 93. Madhumuni ya kadi ni kueleza hali zinazohusisha ukosefu wa heshima au/na ubaguzi, ambavyo washiriki wanatakiwa watafute ufumbuzi chanya. Washiriki wanatakiwa watoe taarifa kuhusu ufumbuzi wao kama vile ni habari kuu kwenye taarifa ya habari ya TV. Watawasilisha habari kuu kwa kuigiza hali hiyo na/au kuwahoji watu waliohusika.

Unaweza kuandika kadi zako mwenyewe na habari za amani kuhusu hali zinazohusiana na masuala ya mjini kwako au kitongoji cha jirani.

## Kadi ya 1 ya Habari za Amani

Asilimia 5 ya watu wa mjini kwako ni wahamiaji. Wiki chache zilizopita kulitokea vurugu miongoni mwa wahamiaji na wenyeji.

Watoto watatu wahamiaji kutoka kitongoji cha jirani ya mji wako walikamatwa wakiiba mkoba dukani. Wenyeji walilalamika kwamba hiyo haikuwa mara ya kwanza kutokea na kwamba hawahitaji tena wahamiaji kuishi kwenye kitongoji cha mji wao.

Kumekuwa na mvutano kati ya wenyeji na wahamiaji uliosababisha ugomvi na vurugu. Wenyeji waliitaka serikali kuhamisha wahamiaji kwenda mahali pengine na wawe na kitongoji chao. Wamelalamika kuwa kiwango cha ukosefu wa amani na usalama na uhalifu kimeongezeka kitongojini kwao tangu wahamiaji wengi zaidi walipowasili.

Wahamiaji wamelalamika kwamba wanabaguliwa sana na si rahisi kwao kupata ajira na kujumuishwa kwenye jamii. Wamekuwa wakilalamika jijini kila siku wiki yote iliyopita.

Serikali imepata ufumbuzi, na ni habari kuu...

## Kadi ya 2 ya Habari za Amani

Wanafunzi watatu wapya wamewasili shuleni kwako. Wanatoka nchi nyingine na wana imani tofauti za dini kuliko wanafunzi wengine wengi. Wazazi wao wamelalamika shuleni kwamba chakula kinachotolewa kwenye bwalo kwa mlo wa mchana hakitimizi masharti ya mlo wa watoto wasiokula nyama.

Waliwaambia shule iwape mlo wa wasiokula nyama. Hata hivyo Mkurugenzi wa shule hakukubali, alisema kwamba ni ghali sana kwa shule kutoa aina tofauti ya mlo kwa watoto watatu tu na hakukuwa na fedha zilizotengwa kwa ajili hiyo. Alipendekeza wanafunzi hao walete chakula chao kutoka nyumbani.

Familia ilishutumu shule kwa tabia za ubaguzi na kumtishia mkurugenzi kwamba wataishitaki shule, kama haitawapatia wanafunzi hao mlo usio na nyama

Tatizo limetanzuliwa, na ufumbuzi huo ni habari kuu…

## Kadi ya 3 ya Habari za Amani

Katika nchi ambayo wanajaribu kutenganisha dini na dola, msichana wa miaka 13 ameanza kuja shule akivalia hijab kamili, ikiwemo mtandio usoni mwake.

Amesema hivi sasa ameshafikia umri wa kuvunja ungo kwa hiyo ni lazima afunike sura na uso na mwili wake. Amesema pia kwamba haileti tofauti yoyote kutokana na namna anavyofanya mazoezi ya shule nyumbani.

Hata hivyo mkuu wake wa shule amemrudisha nyumbani na kumwambia asirudi mpaka avue hijab yake yote. Mkuu wa shule amesema inaweza kuwa hatari, kwa mfano kwenye maabara ya sayansi na pia inaleta dini katika shule ambayo haiendeshwi kidini.

Wazazi wa msichana wamesisitiza kwamba binti yao aje shule akivaa hijab na wametishia kuishtaki shule mahakamani.

Hii imepatiwa ufumbuzi, na ufumbuzi huo ni habari kuu…

## Kadi ya 4 ya Habari za Amani

Shule inalalamika sana kutokana na kufika wanafunzi wengi ambao ni wageni waliowasili nchini hivi karibuni.

Vijana hawa hawawezi kuzungumza lugha vizuri au hawawezi kabisa. Wanafunzi wana wasiwasi kuwa hawatapata masomo vizuri kwa kuwa walimu watatumia muda wao mwingi kuwasaidia wale wasioelewa.

Wanafunzi wana wasiwasi kwamba viwango vyao vitashuka na hawataenda kwenye vyuo watakavyochagua.

Wameanza kuwa jeuri kwa wanafunzi wapya na kulalamika kwa walimu.

Tatizo hili limefumbuliwa na ufumbuzi ni habari kuu…

# Muhtasari wa Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto (Ibara ya 1 hadi 42)

Katika Makubaliano haya neno 'mtoto' maana yake ni yeyote mwenye umri wa chini ya miaka 18.

**Ibara ya 1**
Kila mtu mwenye umri wa chini ya miaka 18 ana haki zote katika Makubaliano haya.

**Ibara ya 2**
Makubaliano haya yanatumika kwa kila mtu bila ya kujali mbari, dini, uwezo, kila wanachofikiri au kusema, aina yoyote ya familia wanayotoka.

**Ibara ya 3**
Mashirika yote yanayohusika na watoto hayana budi kufanya kadiri iwezekanavyo kuhakikisha kuwa kila mtoto anatendewa haki.

**Ibara ya 4**
Serikali zihakikishe kwamba watoto wanapatiwa haki hizi.

**Ibara ya 5**
Serikali hazina budi kuheshimu haki na wajibu wa familia kuwaelekeza na kuwaongoza watoto wao ili kadiri wanavyokua, wawe wanajifunza kutumia haki zao ipasavyo.

**Ibara ya 6**
Watoto wote wana haki ya kuishi Serikali zihakikishe kuwa watoto wanaishi na kukua kiafya.

**Ibara ya 7**
Watoto wote wana haki ya kuwa na jina lililosajiliwa kisheria, haki ya utaifa, haki ya kujua na kadiri iwezekanavyo, kutunzwa na wazazi wao.

**Ibara ya 8**
Serikali hazina budi kuheshimu haki za watoto kuwa na jina, utaifa na uhusiano wa kifamilia.

**Ibara ya 9**
Watoto wasitenganishwe na wazazi wao isipokuwa kwa manufaa yao, kwa mfano iwapo mzazi anamtesa au kumtelekeza mtoto. Watoto ambao wazazi wao wametengana wana haki ya kuwa karibu na wazazi wao wote isipokuwa kama kwa kufanya hivyo kutawaathiri watoto.

**Ibara ya 10**
Familia zinazoishi nchi tofauti ziruhusiwe kusafiri kati ya nchi hizo ili wazazi na watoto waweze kuishi kwa kuwasiliana au kurudi kama familia.

**Ibara ya 11**
Serikali zichukue hatua kuzuia watoto wasichukuliwe nje ya nchi zao kinyume cha sharia.

**Ibara ya 12**
Watoto wana haki ya kusema wanachodhani kuwa kitatokea, wakati watoto wanapofanya uamuzi utakaowaathiri, na maoni yao yazingatiwe.

**Ibara ya 13**
Watoto wana haki ya kupata na kushirikiana habari, alimradi habari hiyo haiwaathiri wao au wengine.

**Ibara ya 14**
Watoto wana haki ya kufikiri na kuamini kile wanachotaka na kufuata dini yao, alimradi hawawazuii watu wengine kufurahia haki zao. Wazazi hawana budi kuwaongoza watoto wao kuhusu mambo haya.

**Ibara ya 15**
Watoto wana haki ya kukutana pamoja na kujiunga na vikundi na vyama, alimradi kufanya hivyo hakuwazuii watu wengine kufurahia haki zao.

**Ibara ya 16**
Watoto wana haki ya faragha. Sheria iwalinde dhidi ya mashambulizi yanayopinga mtindo wa maisha yao, jina lao zuri, familia zao na nyumba zao.

**Ibara ya 17**
Watoto wana haki ya taarifa ya kuaminika kutoka vyombo vya habari. Televisheni, redio na magazeti vitoe taarifa ambazo watoto watazielewa na visieneze habari zinazoweza kuwadhuru watoto.

**Ibara ya 18**
Wazazi wote wana wajibu wa kuwalea watoto wao, na lazima wafikirie kilicho bora zaidi kwa kila mtoto. Serikali iwasaidie wazazi kwa kuwapa huduma za kuwasaidia, hasa kama wazazi wote wanafanya kazi.

**Ibara ya 19**
Serikali ihakikishe kwamba watoto wanatunzwa vizuri, na kuwalinda dhidi ya ugomvi, unyanyasaji na kutelekezwa na wazazi wao au mtu mwingine yeyote anayewalea.

**Ibara ya 20**
Watoto wasioweza kutunzwa na familia zao, lazima watunzwe ipasavyo na watu wanaoheshimu dini yao, utamaduni na lugha.



**Ibara ya 21**
Kama watoto wanaasiliwa, jambo la kwanza ni kujua nini kinachowafaa zaidi. Sheria hizo hizo ni lazima zitumike iwe watoto wameasiliwa katika nchi waliyozaliwa au kuchukuliwa kuishi nchi nyingine.

**Ibara ya 22**
Watoto wanaoingia nchini kama wakimbizi lazima wawe na haki sawa kama watoto waliozaliwa katika nchi hiyo.

**Ibara ya 23**
Watoto wenye ulemavu wa aina yoyote lazima wapewe matunzo maalumu na msaada ili waweze kuendesha maisha kamili na huru.

**Ibara ya 24**
Watoto wana haki ya matunzo bora ya afya na maji safi, chakula bora na mazingira safi ili waishi wenye afya. Nchi tajiri zisaidie nchi maskini kufikia haki hizo.

**Ibara ya 25**
Watoto wanaolelewa na mamlaka za serikali zao za mitaa badala ya wazazi wao lazima hali yao iangaliwe mara kwa mara.

**Ibara ya 26**
Serikali haina budi kutenga fedha za ziada kwa watoto wa familia maskini.

**Ibara ya 27**
Watoto wana haki ya kiwango cha maisha kinachofaa kukidhi mahitaji yao ya mwili na akili. Serikali izisaidie familia zisizomudu kutoa huduma hizo.

**Ibara ya 28**
Watoto wana haki ya kupewa elimu. Nidhamu shuleni haina budi kuheshimu utu wa mtoto. Elimu ya msingi iwe bure. Nchi tajiri zisisaidie nchi maskini kufikia haki hii.

**Ibara ya 29**
Elimu haina budi kukuza haiba na kipaji cha mtoto kwa ukamilifu. Iwahimize watoto kuwaheshimu wazazi wao, kuheshimu nafsi zao na utamaduni mwingine.

**Ibara ya 30**
Watoto wana haki ya kujifunza na kutumia lugha na mila na desturi za familia zao iwe zinashirikiana na wingi wa watu nchini au hapana.

**Ibara ya 31**
Watoto wote wana haki ya kuburudika na kucheza, na kujiunga na shughuli nyingi.

**Ibara ya 32**
Serikali iwalinde watoto dhidi ya kazi za hatari, vinginevyo wanaweza kudhuru afya zao au elimu yao.

**Ibara ya 33**
Serikali iwe na utaratibu wa kuwalinda watoto dhidi ya dawa za kulevya.

**Ibara ya 34**
Serikali iwalinde watoto dhidi ya unyanyasaji wa kingono.

**Ibara ya 35**
Serikali ihakikishe kuwa watoto hawatekwi nyara wala kuuzwa.

**Ibara ya 36**
Watoto walindwe dhidi ya shughuli zozote zinazoweza kudhuru maendeleo yao.

**Ibara ya 37**
Watoto wanaovunja sheria wasitendewe kwa ukatili. Wasifungwe gerezani na watu wazima na waweze kuwasiliana na familia zao.

**Ibara ya 38**
Serikali isiwaruhusu watoto chini ya umri wa miaka 15 kujiunga na jeshi. Watoto kwenye maeneo ya vita wapewe ulinzi maalumu.

**Ibara ya 39**
Watoto waliotelekezwa au kunyanyaswa wapewe msaada maalumu kurudisha heshima yao.

**Ibara ya 40**
Watoto waliotuhumiwa kuvunja sheria lazima wapate msaada wa sheria. Hukumu za vifungo vya watoto lazima zitumiwe kwa makosa makubwa zaidi.

**Ibara ya 41**
Kama sheria za nchi mahususi zinawalinda watoto vizuri zaidi kuliko Ibara za Makubaliano haya, basi sheria hizo zibaki.

**Ibara ya 42**
Serikali hazina budi kufanya makubaliano haya yafahamike kwa wazazi wote na watoto.

# Muhtasari wa Tamko la Kimataifa la haki za Binadamu

## Lilipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1948

**Kila mmoja…**

Amezaliwa huru na anastahili kutendewa kwa haki, na usawa.

Ni sawa ingawa anatofautiana kwa lugha, rangi, jinsia, dini, utaifa.

Ana haki ya kuishi na kuishi kwa uhuru na usalama.

Hana haki ya kuwekwa utumwa.

Hana haki ya kuumizwa na kuteswa.

Ana haki ya kutambuliwa mbele ya sharia.

Ana haki ya kutendewa kwa usawa mbele ya sheria.

Ana haki ya kuomba msaada wa sheria wakati haki zao zisipoheshimiwa.

Ana haki ya kutokamatwa na kufungwa jela kwa uonevu, au kuishi uhamishoni.

Ana haki ya kusikilizwa na kuhukumiwa.

Ana haki ya kuhesabiwa hana hatia mpaka pale inapothibitika kisheria.

Ana haki ya faragha.

Ana haki ya uhuru wa kwenda atakako na kuishi katika mipaka ya nchi yake.

Ana haki ya kutafuta hifadhi katika nchi nyingine kuepuka kuuawa.

Ana haki ya uraia.

Ana haki ya kuoa na kuolewa na kuanzisha familia.

Ana haki ya kumiliki mali.

Ana haki ya uhuru wa kufikiri na imani.

Ana haki ya uhuru wa kutoa maoni na kujieleza.

Ana haki ya kukutana na wengine.

Ana haki ya kushiriki katika serikali na kupiga kura.

Ana haki ya kupata hifadhi ya jamii.

Ana haki ya kufanya kazi, kupata malipo ya haki, mazingira salama ya kazi na haki ya kujiunga na chama cha wafanyakazi.

Ana haki ya kupumzika na siku za sikukuu.

Ana haki ya kutosha ya kuishi kama binadamu, ikiwemo chakula, nyumba, mavazi na msaada wa matibabu.

Ana haki ya kupata elimu.

Ana haki ya kushiriki katika masuala ya utamaduni ya jumuiya yake.

Anastahili utulivu katika jamii yake na kimataifa ambapo haki na uhuru wake uliotolewa katika tamko hili utapatikana.

Ana haki ya kuchukua wajibu unaopasa kuheshimu haki za wengine.


Hakuna mwenye haki ya kutenda kitendo chochote chenye kuvunja haki yoyote kati ya hizi.

# Namna ya Kukunja Korongo wa Karatasi

*Imechukuliwa kutoka http://www.sadako.org/foldingcranes.html*


## Hatua ya 1

Kunja nusu kimshazari.




## Hatua ya 2

Kunja tena nusu kimshazari.




## Hatua ya 3

Kunjua mfuko nje kutoka ndani na kunja kufanya mraba mdogo.




## Hatua ya 4

Geuza.



## Hatua ya 5


Rudia hatua ya 4.



## Hatua ya 6


Hii ni sehemu inayotatanisha (ambayo inaweza kurukwa mpaka Hatua ya 9).

Kunja pembe za kushoto na kulia kuelekea mstari wa katikati kwenye mstari mwekundu wa bonde na halafu kunja pembe ya juu katika mstari wa bluu wa bonde. Zingatia kwamba mikunjo itafanya mkunjo mkali.




## Hatua ya 7

Umbo litakuwa kama hivi.




## Hatua ya 8

Sasa fungua mfuko kwa kuvuta juu pembe ya chini, halafu kunja ndani kufuta mkunjo mkali (baadhi ya mikunjo itageuzwa).




## Hatua ya 9

Umbo litakuwa hivi. Kuwa makini kukunja pembe na kingo kwa usahihi. Geuza na rudia (hatua ya 6, 7, 8).




## Hatua ya 10

Sasa una msingi. Umefikia nusu, na sehemu iliyobaki ni rahisi sana.




## Hatua ya 11

Kuhakikisha kuwa una upande sahihi juu, kunja bonde kwenye mistari ya nukta kwa kutumia tabaka ya juu tu.




## Hatua ya 12

Umbo halina budi kuwa kama hili. Geuza.




## Hatua ya 13

Rudia hatua ya 11. Je, inazidi kuwa vigumu kukunja? Unakaribia kumaliza.




## Hatua ya 14

Geuza mkunjo kwenye mistari ya nukta kuunda kichwa.



## Hatua ya 15


Fungua upande kidogo na lete sehemu ya kichwa kama hivi.



## Hatua ya 16


Lete juu mpaka hatua hii na halafu bonyeza chini.

Rudia kufanya hivyo kuunda mkia upande wa pili.




## Hatua ya 17

Geuza mkunjo katika mistari ya nukta kuunda mdomo. Unaweza kuchagua urefu wa mdomo.




## Hatua ya 18

Kunja mbawa nje kwenye nafasi sahihi. Unaweza kupuzia upepo polepole kutokea chini.



## Hatua ya 19

Korongo aliyekamilika.



## Sehemu ya 6

# Tulifanya Kama Hivi

**Namna tulivyotumia *Kujifunza Kuishi Pamoja* na njia zake katika kanda mbalimbali na mazingira na watu kutoka utamaduni na imani mbalimbali**





Mchakato wa kutayarisha kitabu hiki cha kiada umekuwa wa safari ndefu. Ni matunda ya ushirikiano wa watu wa dini na utamaduni mbalimbali. *Kujifunza Kuishi Pamoja* kulijaribiwa katika kanda tano, nchi kumi na mazingira tofauti kwa kutumia zaidi ya washiriki 300 kutoka Argentina, Azerbajan, Bolivia, Canada, Colombia, Costa Rica, Denmark, Ecuador, El Salvador, Finland, Ghana, Guatemala, Honduras, India, Israel, Japan, Jordan, Kenya, Lebanon, Maldives, Nepal, Panama, Spain, Sri Lanka, Sweden, Uingereza (UK), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Venezuela.

Wawakilishi kutoka Dini za Kimila za Kiafrika, Dini ya Baha'I, Kibuddha, Kikristo, Kihindu, Mila za Kiasili, Kiislamu, Dini ya Kiyahudi, Wajumbe wa Brahma Kumaris na watu wenye fikra zisizokuwa za dini walihudhuria warsha na majaribio, zilizotoa fursa za kujifunza kutoka kwa kila mmoja. Kitabu hiki cha kiada kiliboreshwa sana na maoni na mawazo yao yalichangia katika kupata kitabu kinachokubali mabadiliko kulingana na hali na chenye mpangilio unaozingatia ulimwengu lakini kinachohimiza utekelezaji wa eneo linalohusika.

Uzoefu uliopatikana kwenye kila warsha uliingizwa kwenye toleo hili la mwisho: maoni ya wawezeshaji; mapendekezo ya watu wazima waliohudhuria mikutano inayofanana na iliyoendeshwa wakati mmoja, walichojifunza watoto na vijana; mapendekezo ya wataalamu wa elimu, maadili na kujifunza dini mbalimbali na ya wajumbe wa GNRC, na uvumbuzi tulifanya wakati wa mchakato wa warsha.

Katika kurasa zifuatazo, utaona maelezo ya kila warsha, njia zilizotumiwa, walichojifunza washiriki, athari ya warsha, na maoni muhimu yaliyoingizwa kwenye kitabu hiki cha kiada. Utaona namna kila warsha ilivyochangia kwenye matokeo ya mwisho. Utaweza kuvuta taswira ya mchakato tulioitia tangu warsha ya kwanza na namna kila moja alivyosaidia kutayarisha kitabu cha utamaduni na dini mbalimbali kitakachoweza kutumika katika mazingira mbalimbali.

Sehemu hii pia itakupa picha kamili ya namna programu hii ilivyotumika katika kanda mbalimbali na kukusaidia kukitumia wewe binafsi.

Tunakuomba kutunza kumbukumbu ya uzoefu wako kwa kutumia kitabu hiki cha kiada na athari yake kwa washiriki wako. Bila ya shaka kitakuwa marejeo yanayofaa ambayo asasi yako inaweza ikaandika programu ya elimu ya maadili na kupitia mchakato wa kujifunza kwa washiriki.



# Warsha kuhusu Elimu ya Maadili

## Lidingö, Sweden

## 18-20 Novemba, 2005

Kwa muda wa siku tatu, washiriki kutoka Denmark , Finland, Sweden na Uingereza (UK) walikusanyika kujadili masuala yanayohusu h*eshima*, *ushirikali* na *dhima*. Washiriki waligawanywa katika vikundi vitatu, kila kikundi kilijadili mojawapo ya maadili ya hapo juu. Kila kikundi kikiwa na vijana na watu wazima, walijadili maadili hayo, namna yanavyotumika katika jamii zao na namna yanavyoweza kuendelezwa.



Kikundi cha kwanza kilijadili **ushirikali** kutoka mitazamo mbalimbali. Kupitia mchanganuo wa picha za mateso, kukosa heshima, chuki, upendo, kuelewana na kujali, washiriki walishawishika kuchunguza zaidi umuhimu wa ushirikali katika jamii yetu, na haja ya desturi zinazokuza na kuhimiza huruma na heshima kwa wengine.

Kwa kuchukua hali ya watu wengine na kupitia mazoezi ya uaminifu (wakati watu wamefungwa kitambaa machoni); washiriki waligundua maana ya kuwa mshirikali na namna mtazamo wa namna hii utakavyosaidia kuchukua hatua ya kuwasaidia wengine. Uchunguzi kifani kuhusiana na masuala ya uhamiaji barani Ulaya ulitoa msingi wa majadiliano kuhusu ushirikali katika jamii.

Kikundi cha pili kilizingatia maadili ya **dhima**. Washiriki walichanganua wajibu wao, maoni na uzoefu katika jamii kutoka mitazamo yao. Walijadili masuala yanayoathiri nchi za Nordic na dhima ya mtu mmojammoja na ya pamoja waliyonayo kama raia. Kupitia uchunguzi kifani na majadiliano, safari iliwasaidia kutambua uwezo wao wa kushughulikia uonevu na mahitaji ya nchi zao.





Kikundi cha mwisho kilishughulikia mada ya **heshima**. Baada ya kujadiliana maana ya heshima namna inavyoendelezwa na namna inavyokiukwa, washiriki walitayarisha filamu ya vikaragosi kuhusu mada hii kwa kutumia vifaa vya msingi kama vile kalamu, kadibodi na mikasi. Njia hii iliendeleza ubunifu wa washiriki na fikra tunduizi kuhusu tabia na mienendo yao.

Warsha ilimalizika kwa sala ya dini mbalimbali iliyotayarishwa na washiriki ambapo kila mmoja wao alisali, kuimba au kukariri kwa moyo, maandiko kutoka kwenye dini yao mahususi. Ulikuwa wakati wa kutafakari kuhusu ushiriki wao, kujifunza kwao na uzoefu.

## Kujifunza na Matokeo

Washiriki walihisi kuwa majadiliano yao yamepanua ufahamu wao kuhusu baadhi ya masuala ya kijamii yanayokabiliwa siku hizi katika nchi za Nordic. Mwingiliano wa watu kutoka dini mbalimbali pia ulikuwa changamoto kwa maoni yao na uliwasaidia kuona umuhimu wa maadili yanayoelezwa wakati wa kujumuika na watu. Hoja nyingine za kujifunza zilihusu umuhimu wa kufikiria kuwa katika nafsi ya mtu mwingine na kulaumu chuki na upendeleo wa nafsi zao.

## Je, warsha hii ilichangiaje katika kutayarisha kitabu hiki cha kiada?

Hii ilikuwa mara ya kwanza ya kujaribu rasimu ya kitabu hiki, na katika hatua hii ni sehemu ya utangulizi tu ndiyo iliyokuwa imeandikwa. Tathmini ya warsha ilileta hoja nyingi muhimu za kujifunza zilizosaidia kuboresha kitabu hiki cha kiada na maudhui yake. Yafuatayo ni mawazo makuu yaliyoingizwa kwenye toleo la mwisho:

> Njia shirikishi kwa ukamilifu ni muhimu kwa kuendeleza unyoofu wa maadili.
> Wape watoto na vijana nafasi yao kushirikiana na kujifunza.
> Maadili yasiwe yamegawanywa bali yawe yanahusiana.
> Kitabu cha kiada kiwe na mkabala wa kanda zaidi na lazima kuwe na nafasi ya kuingiza maoni na nyenzo za kanda.
> Kitabu cha kiada hakina budi kushughulikia masuala ya kijamii na kuwasaidia watoto na vijana kuelewa matatizo ya ndani ya jamii zao.
> Maadili yanaelezwa tu, hayawezi kufundishwa.
> Kunahitajika nafasi na muda zaidi kwa watu kuendeleza mambo yao ya kiroho.
> Jumuisha nyenzo kama vile muhtasari wa shughuli, hadithi na uchunguzi kifani.

| Taarifa kuhusu Warsha | |
|---|---|
| Mahali | Taasisi ya Ekumeni, Lidingo |
| Idadi ya Washiriki/Wawezeshaji | 33/3 |
| Idadi ya Watu wazima | 27 |
| Idadi ya Vijana (miaka 15 – 19) | 6 |
| Siku za Warsha | Siku 3 |
| Lugha Iliyotumika | Kiingereza |
| Nchi walizotoka washiriki | Chile, Ecuador, Denmark, Finland, India, Israel, Japan, Jordan, Sri Lanka, Sweden, Uingereza (UK) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| Imani za Washiriki | Ubudha, Ukristo, Uhindu, Uislamu na Kiyahudi. Watu wasio na fikra za kidini |
| Mbinu za Ufundishaji | Sanaa<br>Kubadilishana uzoefu<br>Vikao vya majadiliano |








# Warsha kuhusu Uhamaji na Kuhamishwa

## Bogotá, Colombia

## 5-8 Desemba, 2005

Watoto na vijana na watu wazima kutoka Argentina, Bolivia, Colombia, Ecuador na Venezuela walikutana kwa siku nne kujadili namna *heshima, ushirikali, mapatano na dhima* vinavyoweza kutumiwa kwa muktadha wa nchi zao, na hasa kwa masuala ya uhamaji na kuhamishwa yanayoathiri ukanda wa Andean.

Warsha hii ilikusudiwa kwa waelimishaji kujifunza shughuli mpya halisi na njia za kufundishia zinazozingatia maadili yanayopendekezwa na kutafuta mapendekezo kwa ajili ya uendelezaji zaidi wa kitabu cha kiada.

Siku ya kwanza washiriki walijadili **utambulisho** wao. Walingundua mengi zaidi kuhusu wao wenyewe kuhusiana na wengine kwa kuchora mti wa familia ulioeleza chimbuko lao, wao ni kina nani na wanachotaka kupata maishani mwao. Shughuli nzito kuhusu kutafuta **tofauti** na **kufanana** miongoni mwa washiriki pia ilitumika kujadili zaidi maelewano ya pande mbili.






**Ushirikali** ulijadiliwa kupitia shughuli ya **tafakuri** kuhusu hisia za washiriki. Zoezi hili liliwasaidia washiriki **kuhusiana** na Dunia na watu waliopo. Kwa kujiweka katika taswira ya umbo la mtu mwingine, washiriki waliweza kutafakari kuhusu umuhimu wa ushirikali. Baada ya shughuli, majadiliano yalionyesha ugumu wa kuwa mshirikali na wale waliokiuka haki za watu wengine. Washiriki walitafakari kuhusu haja ya **kuona ubinadamu wa wengine** hata kama wamefanya uhalifu mbaya.



Kupitia uchanganuzi wa mchakato wa **upatanishi**, washiriki walikiri kwamba mgogoro ni sehemu ya uhalisia wetu na kwamba kuna haja ya **kubadili migogoro kwa amani**. Washiriki walitumia uchunguzi kifani kuhusu usuluhishi na kusisitiza umuhimu wa **mazungumzo** kama watu wanataka kuishi pamoja.

Siku ya mwisho, washiriki walichanganua suala la kuhamishwa katika kanda. Dhima na nafasi ya kila mtendaji katika jamii ilitambuliwa. Hii ilisababisha kutayarishwa mpango wa kazi kwa utekelezaji wa elimu ya maadili kwa muktadha wa kuhamishwa. Warsha ilianza kila asubuhi kwa sala ya amani, ambapo washiriki waliimba na kuungana na wakati wa kukaa kimya.

## Kujifunza na Matokeo

Baada ya kila shughuli, kikundi kilijikusanya na kutafakari maadili na kufikiria kuhusu walichojifunza. Watu wazima wengi walibaini kuwa warsha ilikuwa ya kusisimua na kuonyesha shauku katika kujifunza namna ya kutayarisha programu za elimu ya maadili kwa msingi wa njia shirikishi. Wakati wa kutafakari kuhusu matatizo ya kuwa mshirikali na mwenye huruma kuhusu wakosaji wagomvi, mwanafunzi mmoja alishtua watu wazima kwa kuwauliza, "Katika haya yote, Mungu yuko wapi? Aliwataka washiriki kuona ubinadamu wa watu wengine na kusamehe ili kuleta amani katika jamii."

## Je, warsha hii ilichangiaje katika kutayarisha kitabu hiki cha kiada?

Matokeo ya warsha, njia za kufundishia zilizotumika, maoni ya washiriki na mawazo ya kikundi, vyote vilichangia katika kutayarisha moduli ambazo hivi sasa zimo kwenye kitabu cha kiada. Yafuatayo ni maoni makuu yaliyoingizwa kwenye toleo la mwisho la kitabu cha kiada:

> Mchanganyiko wa watoto na watu wazima ni mzuri kwa baadhi ya shughuli.

> Ingiza shughuli motomoto na shirikishi na mazoezi kama vile muziki, michezo, maigizo dhima na filamu.

> Maadili manne yanaweza kuingizwa kwenye moduli ili kuleta unyumbufu na kuwezesha uhusiano kati yao.

> Kubadilishana uzoefu na muda wa kutafakari vilifurahiwa na havina budi kupewa kipaumbele.

> Umuhimu wa njia za kufundishia zinazotoa fursa kwa watoto kuvumbuana, kutafakari kuhusu wao wenyewe na kuhusu ulimwengu.

| Taarifa kuhusu Warsha | |
|---|---|
| Mahali | Retreat Centre, San Pedro Claver, Bogotá |
| Idadi ya Washiriki/Wawezeshaji | 49/4 |
| Idadi ya Watu wazima | 35 |
| Idadi ya Watoto (miaka 9 – 13) | 5 |
| Idadi ya Vijana (miaka 14 – 18) | 9 |
| Siku za Warsha | Siku 3 |
| Lugha Iliyotumika | Kihispaniola |
| Nchi walizotoka washiriki | Argentina, Bolivia, Colombia, Ecuador, France, Venezuela |
| Imani za Washiriki | Ukristo: Anglikana, Wakatoliki, Waluteri, Mennonites na Presbyterians |
| Mbinu za Ufundishaji | Kubadilishana uzoefu<br>michezo, tafakuri<br>mazungumzo |





# Kujenga GNRC ya vijana kwa pamoja

## Geneva, Uswisi

## 13-15 Julai, 2006

Warsha ya kimataifa yenye washiriki kutoka Azerbaijan, Colombia, Honduras, India, Israel, Jordan, Kenya, Lebanon, Sri Lanka, Sweden, Uingereza (UK) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliandaliwa kama warsha ya kwanza ya majaribio ya toleo la kwanza la kitabu kamili.

Vijana wenye umri wa miaka 14 hadi 16 walishiriki katika majadiliano kuhusu dini zao. Kwa kushirikiana ufahamu wa wao wa dini na taratibu za kidini walishiriki katika majadiliano moto moto yaliyowasaidia kuhusiana baina yao. **Ziara za Dini Mbalimbali**, zilitayarishwa, na kuwapa fursa washiriki kufikiria kuwa katika nafasi ya watu wengine.

Wakati wa **Kuchora kwenye Fulana**, washiriki walitafakari uhusiano wao na wengine na hali wanazokabiliana nazo. Walionyesha shauku yao ya kuleta amani duniani, kwa njia ya umoja, kujali, upendo na heshima. **Vikundi vya majadiliano** vilivyozingatia kuheshimiana, shuleni, familia na ujirani viliwasaidia kuchanganua namna heshima inavyoweza kutumiwa kwa vitendo.






**Mikusanyiko ya usiku ya utamaduni** ilitayarishwa kwa ushirikianaji wa baadhi ya vijana kutoka Geneva. Washiriki walikuwa na fursa ya kushirikiana taarifa kuhusu utamaduni wao na imani za dini zao. Wawakilishi wa vijana kutoka Israel waliacha ujumbe wa amani wakati walipokuwa wakizungumzia kuhusu shughuli walizokuwa wakishiriki katika kukuza kuishi pamoja na kuelewana katika jamii yao nchini Israel.



Siku ya mwisho, washiriki walijifunza kuhusu aina mbalimbali za migogoro na namna migogoro hiyo inavyoweza kuwa ugomvi na ghasia. Walitafakari kuhusu **mitazamo ya upatanishi** ili kuweza kubadili migogoro hiyo. Mmojawapo wa vijana alitoa changamoto kwa kikundi kuwa watafanya nini kama wangekuwa waathirika wa ugomvi unaofanywa na vijana wengine.

Baadhi ya washiriki walikumbuka uzoefu ambapo ilikuwa vigumu kushughulikia kwa amani na kutahadharisha kwamba wakati mwingine si rahisi kuepuka ugomvi. Wakati wa majadiliano, mmoja wa washiriki kutoka India alieleza namna Gandhi alivyoleta amani nchini India kupitia **upinzani wa amani**. Mwisho wa warsha washiriki walitafakari kuhusu haja ya kukuza amani ndani ya jamii ili kuweza kushughulikia hali ngumu zaidi.

Mwisho wa warsha, washiriki waliahidi kufanya mikutano nchini kwao na vijana wengine kujadili maadili yaliyojadiliwa wakati wa warsha.

## Kujifunza na Matokeo

Washiriki wengi walifikiri kwamba ziara za dini mbalimbali zinaongeza maarifa na zimeboresha uelewa wao kuhusu imani na dini za watu wengine. Mikusanyiko ya usiku ya utamaduni iliwasaidia kushirikiana kuhusu uhalisia wa watu wengine na kukubali utambulisho na utamaduni wa watu wengine. Baada ya warsha,washiriki kutoka Kenya na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walianzisha Klabu za Amani shuleni kwao katika nchi zao. Washiriki kutoka Azerbaijan walibadilishana mafunzo yao na vikundi vya vijana nchini Baku na Washiriki kutoka Jordan na Lebanon walibadilishana mafunzo yao na Fishers Programme mjini Jordan.

## Je, warsha hii ilichangiaje katika kutayarisha kitabu hiki cha kiada?

Kwa mara ya kwanza, moduli za mafunzo zilijadiliwa katika mazingira ya dini na utamaduni mbalimbali wa kimataifa. Hii ilituwezesha kubainisha mambo ya msingi na changamoto katika utekelezaji wa kitabu cha kiada. Yafuatayo ni maoni makuu yaliyoingizwa kwenye kitabu cha kiada:

> Tayarisha mwendeleo rahisi wa kutoka moduli ya kwanza kwenda ya pili.
> Tenganisha masomo kwa watu wazima kuwafahamisha kitabu hiki cha kiada.
> Muda na nafasi ya kutosha ya kukuza mambo ya kiroho kupitia shughuli kuhusu kujipima na kujifikiria mtu mwenyewe.
> Wape muda na nafasi washiriki wazungumzie kuhusu utamaduni na imani za dini zao.
> Haja ya kuhusisha shughuli katika mazingira ya mahali na hali halisi za jamii.
> Tumia mbinu zaidi za ufundishaji kuwashirikisha watoto na vijana katika kutafakari.

| Taarifa kuhusu Warsha | |
|---|---|
| Mahali | John Knox Center, Geneva |
| Idadi ya Washiriki/Wawezeshaji | 16/4 |
| Idadi ya Vijana (miaka 15 – 19) | 16 |
| Siku za Warsha | Siku 3 |
| Lugha Iliyotumika | Kiingereza/Kihispaniola |
| Nchi walizotoka washiriki | Azerbaijan, Colombia,Honduras, India, Israel, Jordan, Kenya, Lebanon, Sri Lanka, Sweden, Uingereza (UK) na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| Imani za Washiriki | Ubuddha, Ukristo (Anglikana, Wakatoliki, Orthodox), Uhindu, Uislamu na Uyahudi. |
| Mbinu za Ufundishaji | Sanaa<br>Kubadilishana uzoefu<br>Vikudi lengwa vya majadiliano<br>ziara za ugani<br>michezo |








# Warsha kuhusu Elimu ya Maadili

## Coimbatore, India

## 2-5 Agosti, 2006

India palikuwa mahali maalumu kwa mkutano kwa ajili ya warsha hii ya majaribio ya kitabu. Mazingira ya dini mbalimbali, jamii yenye harakati nyingi, masuala ya kijamii yanayoathiri nchi na ari ya ujasiriamali wa watu wake vimeunda mazingira ya kuvutia sana ya kuwashughulisha washiriki wa warsha katika uzoefu wa kujifunza mambo ya kiroho.

Washiriki kutoka Canada, India, Jordan, Lebanon, Maldives, Nepal na Sri Lanka walifunga safari ya kuvumbua zaidi kuhusu nafsi zao wenyewe kuhusiana na wengine na kukuza mambo yao ya kiroho. Kila asubuhi washiriki walikusanyika pamoja kwa ajili ya sala na tafakuri. Siku ya kwanza walifanya kazi kwa vikundi **kujadili** haja ya heshima kwenye jamii zao na mitazamo na tabia na mienendo inayohitajika kuishi na dini, watu, utamaduni anuwai.



**Ziara za dini mbalimbali** ziliandaliwa na washiriki walipata fursa ya kutembelea msikiti, hekalu na Jain, Msikiti wa wasingasinga, kanisa na hekalu la Kihindu. Kila ziara iliwapa fursa washiriki kuuliza maswali, kupata muda wa sala, muziki au kimya na kubainisha tofauti na kufanana kati ya dini mbalimbali.

**Shughuli**, *Chemshabongo – Je, ninaelewanini kuhusu dini nyingine?* ilitayarishwa, na kwa vikundi, washiriki walijibu maswali kuhusu mahali pa ibada walikotembelea. Washiriki walijadili haja ya mapatano na heshima.

Washiriki waliandika kwenye *logu zao za kujifunza* walichoona na walichohisi zaidi wakati wa warsha.





Siku ya tatu, ilitayarishwa ziara ya kwenye vijiji vya wenyeji. Watoto waliweza kujifunza kuhusu miradi inayoendeshwa na wanajamii, programu za kielimu zilizotayarishwa na AZISE na shughuli zinazofanywa na watu mmoja mmoja walio tayari kubadilisha jamii yao. **Shughuli hii inayotokana na uzoefu** imewawezesha washiriki kugundua kwamba dhima ya mtu na ya pamoja, huleta mabadiliko duniani.

Muziki, ngoma na mashairi vilichanganywa kwenye **usiku wa utamaduni**, ambapo washiriki walionyesha vipaji vyao na kushirikiana vipengele vya utamaduni wao. Siku ya mwisho ya warsha, washiriki walishiriki katika Tamasha la Amani la Coimbatore, na pamoja na zaidi ya watoto 250 **walijadili** haja ya unyoofu wa kimaadili kwenye jamii zao na namna wanavyoweza kufanya kama wajenzi wa amani. Warsha ilikwisha kwa maonyesho ya washiriki, na washiriki wakiimba **wimbo** waliojifunza wakati wa warsha na unaohimiza udugu na amani.

## Kujifunza na Matokeo

Wakati wa majadiliano mwisho wa warsha, washiriki walieleza kiasi walichojifunza na namna mtazamo wao kuhusu ulimwengu na kuhusu dini nyingine imepewa changamoto na mjumuiko wao na watu wa utamaduni, dini na imani tofauti. Mshiriki mmoja alisema, "*Nilikwishajua kuhusu kuwaheshimu wengine, nilipokuja hapa, lakini sasa nimeanz kujifunza kuhusu maana yake kwa uhalisia na kinachotakiwa katika mtazamo na vitendo ikiwa sisi kama vijana wa Kihindu, Kiislamu na Kikristo tunataka kufanya mambo pamoja kuboresha jumuiya zetu.*"



## Je, warsha hii itachangiaje katika kutayarisha kitabu hiki cha kiada?

Njia zilizotumika, mazingira ya kiroho yaliyoizunguka warsha, vimetusaidia kubainisha vipengele muhimu vitakavyojumuishwa katika kitabu cha kiada:

- Ushirikishwaji wa washiriki katika hali halisi ya mahali na jamii kupitia ziara za ugani na ujumuikaji na wenyeji.
- Ziara za dini mbalimbali na namna ya kutayarisha shughuli zinazotokana na uzoefu.
- Kuingiza muda zaidi kwa ajili ya ukimya, muziki, sala na tafakuri kukuza mambo ya kiroho.
- Haja ya kugundua matumizi ya maadili katika hali halisi.
- Utumikaji wa programu za maadili kwenye masuala yanayoihusu jamii.

| Taarifa kuhusu Warsha | |
|---|---|
| Mahali | Shanti Ashram, Coimbatore |
| Idadi ya Washiriki/Wawezeshaji | 65/5 |
| Idadi ya Watoto (miaka 10 – 19) | 65 |
| Siku za Warsha | Siku 3 |
| Lugha Iliyotumika | Kiingereza/Wakalimani wa Kitamili |
| Nchi walizotoka washiriki | Canada, India, Jordan, Lebanon, Maldives, Sri Lanka na Nepal |
| Imani za Washiriki | Ubuddha, Ukristo, Uhindu na Uislamu |
| Mbinu za Ufundishaji | Sanaa<br>Majadiliano<br>Kubadilishana uzoefu<br>Ziara za ugani<br>Michezo, Tafakuri<br>Kutamba hadithi |














# Warsha kuhusu Elimu ya Maadili

## Salamanca, Hispania

## 31 Agosti – 2 Septemba, 2006

Warsha ya nchini Hispania iliwakutanisha watu wazima na watoto kutoka sehemu mbalimbali za nchi, waliowakilisha Wakristo, Jumuiya ya Baha'i na asasi ya Brahma Kumaris. Hii ilikuwa mara ya kwanza kwa kitabu cha kiada kujaribiwa na washiriki wa nchi moja tu.

Watu wazima na vijana waligawanywa katika makundi mawili tofauti. Makundi yote hayo yalishughulikia moduli ya kwanza ya kitabu cha kiada, *kujielewa binafsi na wengine* na walipata fursa ya kujadili maudhui yake na kutoa maoni kwa ajili ya kuiboresha zaidi.

Katika siku ya kwanza, vijana walijadili aina mbalimbali za dini duniani kupitia zoezi la mchoro wa ramani, na walijadili dini mbalimbali na kanda dini hizo zinakofuatwa. Walipata uelewa mpya wa namna wingi na aina mbalimbali za dini zilivyosaidia kuubadili ulimwengu na namna nchi zilizokuwa na dini moja tu zinavyozidi kuingiza dini nyingi zaidi.



Kupitia **mchezo** washiriki walijadili hadhi ya mtu na kugundua haja ya kuheshimiana na kuelewana;



Wakati wa kubadilishana mawazo, washiriki walizungumza kuhusu **chuki** kwa utamaduni na dini nyingine na kuhusu haja ya kuwaelewa watu wanaotofautiana nao**. Walichanganua** sababu za masuala ya kijamii nchini Hispania na namna zinavyoathiri jamii yao kwa jumla. Walijadili namna wanavyoweza kuwa wazi zaidi kwa watu wanaotengwa au wanaodharauliwa.

Wakati wa jioni, watu wazima na watoto walikusanyika kwa ajili ya **mazungumzo ya pamoja** ambapo walijadiliana kuhusu kanuni, mwenendo na mitazamo vinavyohitajika kuishi pamoja kwa uelewano na watu kutoka imani na utamaduni mbalimbali. Hii ilifuatiwa na **usiku wa utamaduni** ambapo watoto waliandaa shughuli, dansi na hadithi mbalimbali kutoka katika mikoa yao.



Siku ya mwisho washiriki walitafakari kuhusu haja ya kutafuta amani na kujifikiria kuwa katika nafasi ya watu wengine. Kwa kutumia **tafakuri ya kutembea**, washiriki walipata uhusiano na maumbile, na washiriki wengine na kutafakari kuhusu hisia zao na dhima ili kusaidia kutanzua matatizo na kushughulikia kwa amani mahitaji ya wengine.

## Kujifunza na Matokeo

Watoto wa Kikatoliki walionyesha jinsi ilivyokuwa muhimu kwao kupata fursa ya kuwajua watoto kutoka madhehebu ya Baha'i na walikuwa na shauku ya kushirikiana na kutayarisha shughuli pamoja kuhimiza kuelewana. Washiriki wa madhehebu ya Baha'I waliahidi kushirikiana walichojifunza katika warsha na waumini wengine wa dini yao watakaporudi kwao, pia wamethibitisha utayari wao wa kutayarisha shughuli za dini mbalimbali za vijana ili kusaidia kuhimiza amani na umoja nchini Hispania.



## Je, warsha hii ilichangiaje katika kutayarisha kitabu hiki cha kiada?

Warsha iliruhusu kujaribiwa kwa shughuli mpya na njia ambazo sasa zimeingizwa katika kitabu cha kiada. Pia ilikuwa fursa nzuri kupitia upya maudhui na kuingiza mawazo mapya. Yafuatayo ni mawazo muhimu yaliyokusanywa:

> *Kujifunza Kuishi Pamoja*, pia kunaweza kutumiwa na watu wazima. Shughuli zinaweza kutumiwa na umri mbalimbali.

> Majadiliano kuhusu masuala mapya ya uhalisia wa jamii wa vijana yanahitaji kushughulikiwa kwenye kitabu cha kiada.

> Tumia shughuli zinazotokana na uzoefu wa kati wa kujadili uhalisia wa kijamii ili kufanya kujifunza kuwe na maana zaidi.

> Mawazo ya kutumia kitabu cha kiada kwenye kikundi chenye ulinganifu au usawa wa dini.

> Shughuli zinazohusu watu wenyewe zinawasaidia washiriki kufanya mafunzo yawe yao zaidi na kutafakari kuhusu uzoefu wao wenyewe.

| Taarifa kuhusu Warsha | |
|---|---|
| Mahali | Tianococo Residence,Salamanca |
| Idadi ya Washiriki/Wawezeshaji | 20/3 |
| Idadi ya Watu Wazima | 12 |
| Idadi ya Vijana (14 – 18) | 8 |
| Siku za Warsha | Siku 3 |
| Lugha Iliyotumika | Kihispaniola |
| Nchi walizotoka washiriki | Hispania |
| Imani za Washiriki | Madhehebu ya Baha'i, Kikristo (wakatoliki, Waanglikana) waumini wa Asasi ya Brahma Kumaris |
| Mbinu za Ufundishaji | Michezo<br>Vikundi lengwa vya majadiliano<br>Kubadilishana Uzoefu<br>Tafakuri<br>Mazungumzo ya Pamoja |











# Warsha kuhusu Elimu ya Maadili

## Kyoto, Japan

## Agosti, 2006

Warsha ya siku moja ilitayarishwa mjini Kyoto kwa watoto na vijana kutoka GNRC za kanda zote duniani na nchi, ikiwemo Ghana, Israel, Jordan, Sri Lanka na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Warsha iliendeshwa sawia na Mkutano Mkuu wa nane wa Dunia wa Mkutano wa Dunia wa Dini kwa ajili ya Amani (WCRP).

Watoto sita wanaowakilisha Dini za Kimila za Kiafrika, Kibuddha, Kihindu, Uislamu na Dini ya Kiyahudi walikutana kujifunza, kwa njia ya kubadilishana mawazo, kuhusu wao wenyewe na wengine. Kwa njia ya ufundishaji kuhusu nafsi zao, walitafakari kuhusu uhusiano wao na wengine.



Warsha ilianza na shughuli mbalimbali ambazo ziliwawezesha washiriki kujuana na kujadili kwa nini walihudhuria na walitarajia nini. Somo hili la utangulizi lilisaidia kupata nafasi salama kwa ajili ya majadiliano yatakayofuata.

Watoto waliambiwa wachore mti, unaowakilisha asili na chimbuko lao, familia zao, maslahi yao, ni mambo gani yanayowafurahisha na kuwahuzunisha na walichofurahia zaidi. Zoezi la mti wa **Historia ya Maisha Yangu** liliwapa muda wa kukaa kimya na kutafakari na kujipima na kujichunguza. Mwisho wa zoezi, walijadiliana kuhusu michoro yao na washiriki wengine na kuchunguza **tofauti zao na kufanana kwao**.

Kwa kutumia zoezi la **Visiwa Vinavyotoweka**, watoto waligundua haja ya kushirikiana na kuwasaidia wengine. Walijadili namna wao wote wanavyounda sehemu ya ubinadamu na umuhimu wa kuwaheshimu wengine na kujifikiria kuwa katika nafasi ya mtu mwingine.

Watoto walijadili migogoro na namna watu wanavyoishughulikia katika hali mbalimbali. Walijifunza **njia nyingine zisizotumia ugomvi** na walifanya mazoezi mbalimbali kugundua njia mbalimbali wanazoweza kutumia kuubadili ulimwengu hivi sasa na siku zijazo.



**Wakati wa kubadilishana mawazo na kutafakari kwa pamoja,** watoto walitambulishwa **Hadithi ya Sadako**, msichana wa Kijapani, aliyefariki kwa ugonjwa wa saratani ya damu kutokana na athari za maafa ya bomu la nyuklia la Hiroshima. Katika mwaka wake wa mwisho wa maisha yake, Sadako alitengeneza zaidi ya Korongo wa Karatasi 1000 kwa matumaini kwamba angepewa matamanio. Watoto walisikiliza kwa makini hadithi hiyo na halafu walijifunza namna ya **Kutengeneza Korongo wa Karatasi.**

Watoto walitafakari kuhusu namna Korongo wa Karatasi walivyokuwa alama ya sala ya amani duniani kote. Walipewa muda wa kuandika sala yao ya amani kwenye karatasi waliyotumia kutengeneza Korongo. Hii ilitoa nafasi ya kutafakari na kufanya ukunjaji wa Korongo wa Karatasi kuwa kipindi cha kiroho, ambapo washiriki wangefikiria kuhusu Hadithi ya Sadako na athari za maafa ya nyuklia ya mji wa Hiroshima.

## Kujifunza na Matokeo

Watoto walizungumzia kuhusu matatizo mengi duniani yaliyosababishwa na kukosa kuelewa. Walikiri haja ya kuwapo kwa njia za amani za kubadili migogoro binafsi na ya kijamii. Waliahidi kuwahurumia zaidi wengine na kuwaheshimu watu walio tofauti nao.

## Je, warsha hii ilichangiaje katika kutayarisha kitabu hiki cha kiada?



Ilikuwa mara ya kwanza kitabu cha kiada kujaribiwa na watoto wachache katika kikundi chenye utamaduni mbalimbali. Ilikuwa warsha fupi iliyoleta mawazo mazuri kwa programu:

- Umuhimu wa kutumia hadithi halisi kushawishi mawazo.
- Utayari wa kutumia njia za kufundishia kulingana na umri wa washiriki.
- Ujumuishaji wa njia za kufundishia zinazokuza ubunifu na hisia za kisanaa za washiriki.
- Haja ya kuweka muda na nafasi salama kwa watoto kuzungumza na marika yao, bila ya kusumbuliwa au kuvurugwa mawazo.

| Taarifa kuhusu Warsha | |
|---|---|
| Mahali | The International Conference Centre, Kyoto |
| Idadi ya Washiriki/Wawezeshaji | 6/2 |
| Idadi ya Watoto (miaka 9 – 13) | 6 |
| Siku za Warsha | Siku 1 |
| Lugha iliyotumika | Kiingereza |
| Nchi walizotoka washiriki | Ghana, Israel, Japan, Jordan, Sri Lanka na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania |
| Imani za Washiriki | Dini za Kimila za Kiafrika, Kibuddha, Kikristo, Kihindu, Uislamu na Dini ya Kiyahudi |
| Mbinu za Ufundishaji | Sanaa<br>Majadiliano<br>Kubadilishana uzoefu<br>Michezo |







# Kusafiri pamoja kwa Kuleta Amani

## Dar Es Salaam, Tanzania

## 7-10 Desemba, 2006

Kusafiri pamoja kwa Kuleta Amani ni jina la Warsha ya Dar es salaam, ambapo washiriki kutoka Kenya, Uganda, na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania walikutana kugundua namna wanavyoweza kuwa wajenzi wa amani na wahimizaji wa uelewano katika nchi zao.

Warsha ilitayarishwa kulingana na mazingira na utamaduni wa kanda na ilihusishwa na shughuli za wenyeji na masuala ya kijamii katika hali ya hali Afrika Mashariki. Wawakilishi kutoka dini mbalimbali wanaohusika pia na mazungumzo baina ya dini waliwahutubia washiriki kuwahimiza kuzingatia kuwapo kwa dini nyingi na kuwa wazi na kuwahurumia wengine.

Safari ilianza na kipindi cha kutambua nafsi zao na kuwafahamu wengine. Shughuli zilizofanywa zilisisitiza **utambulisho** wao na **tofauti na kufanana** kwao na wengine. **Majadiliano** kuhusu tofauti zao yaliwafanya washiriki watafakari matatizo katika jamii zao yanayotokea kutokana na kukosekana kwa kuheshimiana. Kupitia zoezi la **kutanzua tatizo**, **benki ya maadili**, washiriki walibainisha uovu wa jamii, kama rushwa na mateso dhidi ya watoto, na walitafakari namna matendo hayo yanavyoharibu utu. Pia walijadili aina za ubunifu za kusaidia kubadili hali hizo.



Washiriki walitayarisha **maigizo dhima** kuonyesha namna hali ngumu zinavyoweza kubadilishwa kwa amani. Watoto walijadili uonevu, kutengwa kijamii na ubaguzi, miongoni mwa masuala mengine, na walitafakari kuhusu tabia na mienendo na mitazamo yao. Walitaja umuhimu wa ushirikali na kupitia **michezo** na **kuigiza hali halisi,** walijifunza kuingia katika utamaduni wa watu wengine kukataa chuki zao na kujifunza kutokana na utajiri wa wingi wa dini na tamaduni.

Washiriki walipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali ya dini na kupima maono na mawazo yao. Walieleza kwamba, **ziara za dini mbalimbali** zimewawezesha kugundua namna kuwapo kwa Mungu kunavyoweza kuchukua sura nyingi na kueleweka kwa namna mbalimbali na watu tofauti.

Siku ya mwisho, washiriki walijifunza kuhusu ubadilishaji wa migogoro na namna migogoro inavyoweza kueleweka na kuchanganuliwa. Zoezi la **visiwa vinavyotoweka** liliwapa changamoto washiriki kufikiria namna, wakati mwingine, bila kukusudia tunawabagua watu wengine kupata tunachotaka au kuhitaji. Walitafakari umuhimu wa kushirikiana na kuwakumbatia wengine. Ulitengwa muda wa kubadilishana mawazo kuzungumza na mwanzilishi wa klabu za amani za GNRC katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mshiriki huyu kijana, ambaye maisha yake yamekabiliwa na matatizo mengi na hali zenye changamoto, alieleza uzoefu wake na kueleza namna nia yake ilivyomsaidia kuhimiza jitihada za haki za mtoto na amani miongoni mwa vijana wengine katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Warsha ilimalizika kwa **kipindi cha moto wa kambi** ambapo watoto na watu wazima walikusanyika kwenye moto wa kambi kwa mila ya Kiafrika kwa kutumia ngoma kufikisha ujumbe na burudani. Shangwe na burudani iliyopatikana ilikuwa kumbukumbu ya urithi wa Kiafrika ambapo nafasi na wasaa wa kiroho ulijengwa na wazee kurithisha maadili ya kiunyoofu na kusuluhisha pande zinazogombana.



## Kujifunza na matokeo

Watoto wengi walisema kuwa uelewa wao wa utamaduni na dini nyingine umepanuka. Baadhi yao waliahidi kuanzisha klabu za amani shuleni kwao; tangu wakati huo, klabu ya amani mpya imeanzishwa na washiriki mjini Dar es salaam. Wote waliahidi kushirikiana walichojifunza na marafiki wao na familia na kueleza utayari zaidi wa kushiriki katika shughuli za siku zijazo.

## Je, warsha hii ilichangiaje katika kutayarisha kitabu hiki cha kiada?

Aina mbalimbali za shughuli zilizofanywa katika warsha zilileta maoni mengi kwenye kitabu cha kiada. Mawazo yafuatayo yalikuwa na msaada mahususi:

- Toa nafasi na muda kwa washiriki kujumuika na watu wanaoweza kuwa kama mifano ya kuigwa na kuwashawishi kuleta mabadiliko.
- Ujumuishaji wa shughuli za kujenga jamii, k.m moto wa kambi na miduara ya kupiga ngoma.
- Ujumuishaji wa njia za kufundishia zinazoshawishi fikra tunduizi/ubunifu za washiriki.

| **Taarifa kuhusu Warsha** | |
|---|---|
| Mahali | Tanzania Episcopal Conference Centre,<br>Dar es salaam |
| Idadi ya Washiriki/Wawezeshaji | 24/3 |
| Idadi ya Watoto (miaka 15 – 19) | 24 |
| Siku za Warsha | Siku 3 |
| Lugha Iliyotumika | Kiingereza |
| Nchi walizotoka washiriki | Kenya, Uganda, Jamhuri wa Muungano wa Tanzania |
| Imani za Washiriki | Madhehebu ya Baha'i, Kibuddha, Kikristo, Kihindu na Uislamu |
| Mbinu za Ufundishaji | Kubadilishana uzoefu<br>Ziara za Ugani<br>Michezo<br>Kutanzua matatizo<br>Igizo Dhima |








# Warsha kuhusu Uhamiaji na Kuhamishwa

## San Lorenzo, Ecuador

## 23-25 Januari, 2007

Warsha kuhusu kuhamishwa na uhamiaji ilikusanya pamoja wazazi, vijana na watoto wa Wakolombia na Waikwedo. Kitabu cha kiada kilitayarishwa kulingana na mada ya warsha, washiriki kutoka madhehebu mbalimbali ya Kikristo na kutoka madhehebu ya Baha'i walijadili changamoto za kimaadili zinazowakabili watu wanaoishi katika ukanda wa mpakani wenye hatari sana kati ya Colombia na Ecuador.



Kila asubuhi, kabla ya kuanza shughuli, washiriki walijiunga na muda wa ukimya, tafakuri na sala ya amani katika ukanda wao. Baadhi ya vipindi vilifanywa na watoto na watu wazima pamoja, wakati vingine vilivyohitaji muda zaidi wa kutafuta na kujadiliana, vilifanywa tofauti.



Warsha ilifunguliwa kwa kipindi kilichohusu **utambulisho** wa utamaduni. Washiriki waligawanyika katika vikundi na kutakiwa wachore ramani ya Colombia au ya Ecuador, na kuonyesha viwakilishi vikuu vya nchi hizo, shughuli, chakula na taswira. Washiriki walijihusisha na majadiliano kuhusu chimbuko na asili ya nchi zote na **tofauti na kufanana** kwao. Zoezi hili liliwasaidia kujenga mazingira ya uhusiano na kushirikiana.



Mchana, washiriki walishughulikia mazoezi ya **uanuwai.** Walitafakari kuhusu masuala ya uhamaji na kuhamishwa kutokana na uzoefu wao, maoni ya dini na maadili na historia ya kijamii. Uanuwai ulikubaliwa kuwa ni uhalisia unaotajirisha wote na unaohitaji kukumbatiwa.

**Usiku wa utamaduni** ulitayarishwa, na kwa kutumia mapigo ya muziki wa Kiikwado na Kikolombia, washiriki walicheza, kuimba na kutamba hadithi. Ilikuwa fursa ya pekee kushirikiana katika usiku halisi wa Kilatini na kuweka fungamano kati ya washiriki. Siku iliyofuata, washiriki walitembelea mojawapo ya jamii za wenyeji karibu ya San Lorenzo. Hii ilisaidia kuongeza uelewa wao wa hali zinazowakabili Wakolombia na Waikwedo wanaoishi hapa. Walikuwa na nafasi ya kujumuika na wenyeji, kujadili masuala ya kijamii na viongozi wao wa jamii na kujifunza kuhusu jitihada na miradi yao.



Siku ya mwisho, washiriki walibainisha migogoro mbalimbali inayotokea kati ya Wakolombia na Waikwedo kwenye ukanda huu. Kupitia **uchunguzi kifani na igizo dhima,** walichambua sababu na matokeo yanayoweza kutokea na walijifunza kuhusu **njia zisizotumia ugomvi** kubadili migogoro hiyo. Watoto walieleza hali za ugomvi wanazozikabili kila siku shuleni na katika jamii. Walijadili ufumbuzi unaoweza kupatikana na kutafakari kuhusu dhima zao.

## Kujifunza na Matokeo

Athari za migogoro yenye ugomvi nchini Colombia imetopea kwenye tabia na mienendo na mitazamo ya baadhi ya watoto wanaoathiriwa moja kwa moja na hali. Inaweza kuwafanya wachukizwe na kutowavumilia wengine. Wakati wa warsha, watoto walieleza uzoefu wao na hofu, na walipendekeza wao wenyewe njia za kuheshimu zaidi wengine, kukubali tofauti na kukubali njia isiyotumia ugomvi hata kama haki zao zinakiukwa. Waligundua kwamba wanaweza kuwa sehemu ya ufumbuzi kuliko sehemu ya tatizo.

## Je, warsha hii ilichangiaje katika kutayarisha kitabu hiki cha kiada?

Hii ilikuwa mara ya kwanza kitabu hiki cha kiada kutumika kwa mada mahususi ya kijamii. Mkabala huu ulisaidia kutayarisha urahisi wa kubadilika kwa kitabu na kutafuta njia nyingine zinazoweza pia kutumika. Yafuatayo ni maoni muhimu yaliyoingizwa kwenye kitabu cha kiada:

> Miongozo ya kutayarisha ziara za ugani.

> Namna ya kutumia kitabu cha kiada kwa mada mahususi, kama vile kuhamishwa.

> Matumizi ya kitabu cha kiada kuhimiza ushirikiano wa dini mbalimbali kuhusu suala mahususi la kijamii.

> Kujumuisha njia zaidi za ufundishaji zinazohimiza ushirikishwaji na ujumuikaji.

> Umuhimu wa kuwatayarisha watu wazima, walimu na wawezeshaji kutumia kitabu hiki kwenye hali na mazingira tofauti.

| **Taarifa kuhusu Warsha** | |
|---|---|
| Mahali | Hotel San Lorenzo, San Lorenzo |
| Idadi ya Washiriki/Wawezeshaji | 37/4 |
| Idadi ya Watu Wazima | 25 |
| Idadi ya Vijana (miaka 14 – 18) | 12 |
| Siku za Warsha | Siku 3 |
| Lugha Iliyotumika | Kihispaniola |
| Nchi walizotoka washiriki | Colombia na Ecuador |
| Imani za Washiriki | Madhehebu ya Baha'I na Kikristo(Wakatoliki, Walokole, Waluteri, Mennonites na Presbyterians) |
| Mbinu za Ufundishaji | Sanaa<br>Kubadilishana uzoefu<br>Ziara za Ugani<br>Michezo<br>Kutanzua matatizo<br>Igizo Dhima |







# Warsha kuhusu Vurugu ya Vijana

## San Salvador, El Salvador

## 1-5 Novemba, 2007

Watoto 25 kutoka El Salvador waliowakilisha Madhehebu ya Baha'i, Kibuddha, Kikristo, Dini za Asili, Uislamu na Dini ya Kiyahudi walikutana na watu wazima wanaowakilisha asasi za dini kukuza mambo yao ya kiroho kwa kujifunza kuelewana zaidi. Kupitia warsha, waligundua njia za amani za kubadili hali za ugomvi na kukuza uwezo wao wa kufanya kazi pamoja kuleta amani kwenye jamii yao, licha ya tofauti zao.



Siku ya kwanza, washiriki walichora taswira zao na kujadili wao ni nani na namna utambulisho wao unajengwa na uzoefu wao. Walibadilishana mawazo yao. **Mchezo wa ushirika** ulitayarishwa kutafuta namna ya kufanya kazi pamoja kwa lengo moja na kujadili kuhusu upekee wa kila mtu. Washiriki walihitimisha kwamba inawezekana kufanya kazi pamoja wakati wanapojifunza kuheshimiana na wakati wanapowakubali wengine kwa moyo na akili isiyo ya kinyongo.

Baada ya zoezi hili, washiriki waligawanywa katika vikundi na walitakiwa watayarishe nasaba ya uelekeo katika familia kuonyesha tofauti na kufanana kati ya washiriki wa kila kikundi. Zoezi hili limewasaidia kufahamiana zaidi na kuangalia zaidi ya umbo na sura zao. Mwisho washiriki walijadili umuhimu wa wingi wa dini tofauti duniani na katika jamii.



Majadiliano kuhusu uhalisia wa changamoto za washiriki yaliwasaidia kuwa wazi kujadili uzoefu wao binafsi. Matatizo ya familia, watoto ambao ni sehemu ya Maras (magenge) na hali za vurugu, yalijadiliwa.



Vipindi mbalimbali viliendeshwa kujadili migogoro yenye ugomvi kuhusu El Salvador na **njia zisizotumia ugomvi**. Vipindi hivi vilihimiza ubunifu na fikra tunduizi kwa washiriki kutanzua tofauti zao na wengine na kujifunza namna ya kukataa chuki na mambo yasiyobadilika yanayojirudia rudia. Kwa kutumia **uchunguzi kifani, maigizo dhima na majadiliano**, walionyesha migogoro inayowaathiri na kubainisha njia zinazoweza kutumika kubadili migogoro hiyo kwa amani.

Kwa kutumia safari ya kimya, washiriki walitembelea maeneo mbalimbali ya mahali pa mkutano, na kubainisha kila moja kwa rangi tofauti mahususi. Kila rangi iliwawezesha kutafakari kuhusu maisha yao, uhusiano wao na wengine, hali na mitazamo ya suluhisho inayotakiwa kuleta amani kwa jamii zao. Harufu, milio ya ngoma, na muziki vilisaidia mchakato wa kujichunguza na kupima na kuwaruhusu washiriki kujitenga na ratiba ya shughuli nyingi za maisha yao ya kila siku.

Sala kutoka dini mbalimbali **na muda wa kukaa kimya** ulisaidia kujenga mazingira ya kuleta mambo ya kiroho ya washiriki na kugundua haja ya kutafuta amani ndani na kuweza kuleta amani kwa jamii zao.





## Kujifunza na Matokeo

Lilitolewa pendekezo la kutembelea maeneo ya dini kama ahadi ya kuendelea na safari hii ya dini mbalimbali kuendelea kutafuta njia za kushirikiana katika masuala yanayowaathiri watoto na vijana. Watoto walipendekeza kuongeza michezo zaidi na muda wa sala katika warsha zijazo na watu wazima walipendekeza kuendesha mikutano kuhusu elimu ya maadili kwa wazazi. Baada ya warsha, washiriki vijana walitayarisha tovuti (http://www.gnrcelsavador.blogspot.com ) kubadilishana uzoefu wao na kuendeleza mawasiliano yao.

## Je, warsha hii ilichangiaje katika kutayarisha kitabu hiki cha kiada?

Yafuatao ni maoni muhimu yaliyoingizwa kwenye kitabu cha kiada:

> Kanuni za kimya za kuhimiza kujipima na kujichunguza na kuwashawishi watoto watafakari kuhusu mitazamo yao na uhusiano wao na wengine.

> Umuhimu wa kutoa nafasi na wasaa wa sala ili kuelewa imani za wengine.

> Kujumuisha igizo dhima kama njia ya kutafuta namna nyingine zisizo za ugomvi kwenye njia ya kubadili migogoro.

| Taarifa kuhusu Warsha | |
|---|---|
| Mahali | Templo del sol, Jumuiya ya Kibuddha, San Salvador |
| Idadi ya Washiriki/Wawezeshaji | 43/5 |
| Idadi ya Watu Wazima | 18 |
| Idadi ya Vijana (miaka 14 – 18) | 25 |
| Siku za Warsha | Siku 3 |
| Lugha Iliyotumika | Kihispaniola |
| Nchi walizotoka washiriki | El Salvador, Guatemala na Honduras |
| Imani za Washiriki | Madhehebu ya Baha'i na Kikristo(Wakatoliki, Walokole, Waluteri, na Presbyterians), Dini za Kimila, Uislamu na Dini ya Kiyahudi |
| Mbinu za Ufundishaji | Sanaa<br>Kubadilishana uzoefu<br>Michezo<br>Tafakuri<br>Kutanzua matatizo<br>Igizo Dhima |







# Warsha kuhusu Vurugu ya Vijana

## Capira, Panama

## 21-23 Januari, 2008

Watu wazima 38 na watoto wanaowakilisha Madhehebu ya Baha'i, madhehebu mbalimbali ya Kikristo, madhehebu ya Hare Krishna na dini ya Kiyahudi walikutana kwa siku tatu kuchambua na kutafakari kuhusu suala la vurugu za vijana nchini Panama.



Siku ya kwanza **moto wa kambi** ulitayarishwa kuwakaribisha washiriki vijana. Nyimbo, magita, matuwazi, vicheko, sala, vilichanganywa kuleta mazingira ya ushirikiano na kuheshimiana.

Washiriki walijadili haja ya kuheshimu maoni ya kuelewana kupitia zoezi linaloitwa **Natetea**. Walieleza hoja zao mbalimbali kuhusu mada zinazowaathiri na kutoa msimamo wa kile wanachoamini. Hii ilitoa changamoto kwa maoni yao ya kuwahimiza waheshimu mawazo ya watu wengine hata wakati wasipokubaliana.



Washiriki pia walijadili **mitanziko ya kimaadili** mbalimbali na kutafakari kuhusu namna ya kufanya uamuzi wa kimaadili. Kwa kubadilishana uzoefu wao, walitafakari kuhusu haja ya ushirikali na mitazamo yenye heshima kuweza kufanya uamuzi wenye busara.

Walibainisha aina ya vurugu ambazo vijana wanapata, wanachochea au kufanya na wao ni waathirika kwenye mazingira yao. Waliangalia sababu, matokeo na uwezo walionao kubadili hali hizo. Familia zisizofuata utaratibu wa kijamii na kusababisha tabia isiyoridhisha, wazazi wagomvi, mifano mibaya ilitajwa kama baadhi ya sababu kuu kwa vurugu za vijana. Kwa kutumia igizo dhima, washiriki wamechambua **njia nyingine zisizo na ugomvi** kukabili hali za ugomvi na kupunguza kiwango cha vurugu kinachowaathiri katika maisha yao ya kila siku.

**Usiku wa utamaduni** ulitayarishwa ambapo washiriki waliwasilisha mila na desturi za Colombia, Costa Rica, Panama na Uruguay. Washiriki vijana waliimba na kucheza ngoma halisi kutoka Panama na kujifunza kutokana na mila na desturi za utamaduni zilizopo.

Katika siku ya mwisho ya warsha, **zoezi la kujipima na kujichunguza** lilifanywa kuwawezesha washiriki kuiga na kutafakari kuhusu maisha yao, uhusiano wao na wengine na mitazamo yao. Washiriki walibadilishana mawazo yao na kuhitimisha kuhusu umuhimu wa kuelewa wao ni kina nani na namna wanavyohusiana na wengine.



## Kujifunza na Matokeo

Katika mojawapo ya vipindi vya kubadilishana uzoefu, mshiriki mmoja alieleza hadithi ya *Knight in Rusty Armour* (Shujaa Alievalia Vazi la Kujihami lenye Kutu), kueleza aina ya mavazi tunayobeba kutulinda dhidi ya wengine na yanayotuzuia tusionyeshe sisi ni nani hasa. Aliwahimiza washiriki kuwa wazi kwa wengine na kugundua utambulisho wao halisi na maana ya maisha. Ilikuwa fursa nzuri kwa vijana kutafakari kuhusu nafsi zao na ujumuikaji wao na watu wengine.

Watu wazima wametoa wito wa utayarishaji wa programu za elimu ya maadili kwa familia na zijumuishe wazazi katika majadiliano na watoto kuhusu maadili. Wawakilishi kutoka Wiraza ya Mambo ya Jamii na Afya nchini Panama walionyesha shauku yao ya kushirikiana na GNRC katika kuhimiza elimu ya maadili kuzuia vurugu za vijana nchini.



## Je, warsha hii ilichangiaje katika kutayarisha kitabu hiki cha kiada?

Hii ilikuwa warsha ya mwisho kuendeshwa kupima kitabu hiki. Ilikuwa fursa ya pekee kujaribu makala yaliyoboreshwa na kutumia mazoezi mapya na mbinu. Mawazo yafuatayo yalijumuishwa kwenye kitabu cha kiada:

- Matumizi ya maulizo ya kupenda kuchambua matatizo ya migogoro.
- Matumizi ya mandalas (michoro ya dini ya Kihindi na Kibuddha) kuwasaidia watoto kutafakari kuhusu maisha na madhumuni.
- Matumizi ya mitanziko ya uadilifu kuhimiza fikra tunduizi na kuhoji maoni ya watoto kuhusu maana ya uamuzi wa kimaadili.

| Taarifa kuhusu Warsha | |
|---|---|
| Mahali | Hogar Javier, Capira |
| Idadi ya Washiriki/Wawezeshaji | 38/3 |
| Idadi ya Watu Wazima | 18 |
| Idadi ya Vijana (miaka 14 – 18) | 20 |
| Siku za Warsha | Siku 2 |
| Lugha Iliyotumika | Kihispaniola |
| Nchi walizotoka washiriki | Costa Rica na Panama |
| Imani za Washiriki | Madhehebu ya Baha'i, (Balboa Union Church, Wakatoliki naMennonites), Hare Krishna Movement na Dini ya Kiyahudi |
| Mbinu za Ufundishaji | Kubadilishana uzoefu<br>Michezo<br>Tafakuri<br>Kutanzua tatizo<br>Maulizo ya kufurahia<br>Igizo Dhima |











# Sehemu ya 7

# Marejeo

## Nyenzo

### Hadithi

Ngano ya Kichina – Unseth, Benjamin (edit). Honesty, Little Books of Virtue, Series One. Garborg's Inc., Bloomington, 1995, uk. 11-13.

Mtoto aliyepiga mayowe ya "Uongo" – Unseth, Benjamin (edit). Honesty, Little Books of Virtues, Series One. Garborg's Inc., Bloomington, 1995, uk. 34-36.

Ujasiri unaotakiwa kuwa nao – Imechukuliwa kutoka hadithi ya Peggy Monague, Christian Island, Ontario. Wilson, Lois Miriam, Mary and Me. Wood Lake Books Inc., Winfield, 1992, uk. 62.

Panya waliokula Chuma – Panchatantra – The mice tha ate Iron (1999). Inapatikana katika:http://www.indiaparenting.com/stores/panchatantra/panch009.shtml

Ombaomba – Elbert Hubbard's Scrap Book. Wm. H. Wise & Co., Roycroft Distributors, New York City, 1923, uk. 9.

The nothing beyond – Kenneth Cragg: The Wisdom of the Sufis, London, 76, uk. 8.

Mwanasesere wa Chumvi – Anthony Bloom: Living Prayer, Libra, London, 1966, uk. 105-106.

Kula chakula pamoja na Jenerali – Inapatikana kutoka http://www.geocities.com/Tokyo/Courtyard/1652/MilitaryDiner.html

Zimwi – Na Taghreed A. Najjar, Al-Salwa Publishing House, published 2002, Stand no.5.0 D 953.

Wanaume vipofu na tembo – Kuo, Louise and Kuo, Yuan-Hsi (1976), "Chinese Folk Tales," Celestial Arts: 231 Adrian Road, Millbrae, CA 94030, uk. 83-85. Vifuatavyo vinaunganisha matokeo mengine ya hadithi:

Mbwa mwitu na korongo. Aesopo

Jirani. Inapatikana kutoka http://www.ezsoftech.com/stories/mis40.asp

Kiti cha Pweza – Imechukuliwa kutoka: The Star Thrower by Loren Eiseley (1907-1977).

### Mashairi

Zungumza nasi kuhusu watoto. Khalil Gibran, "Mtume" sura ijulikanayo kwa jina "Watoto". Arrow Books Ltd. New York, 1991.

Watoto wanajifunza wanavyoishi. Dorothy Law Nolte. Workman Publishing Company. New York, 1998.

Ushairi kutoka kwa vijana wa GNRC.

## Sala za Amani

Pathways to Peace. Interreligious readings and reflections. A. Jean Lesher. Cowley Publications. Cambridge, Massachusetts, 2005.

Religious Life: A Commitment and Calling. Imekuzwa kupitia mchakato wa dini mbalimbali ulioandaliwa na Baraza la Makanisa Ulimwenguni.

Prayer Library na http://www.beliefnet.com

Stern, Chaim (ed). Shaarai Teshuva: Gates of Repentance. The New Union Prayerbook for the Days of Awe. Central Conference of American Rabbis: 1978, 1999.

## Uchunguzi kifani

Uchunguzi Kifani 1 Asubuhi mbaya ya Chris, uk. 139 – Imedhaminiwa kutoka kwa Learning the Skills of Peacemaking, Naomi Drew, Jalmar Press, Rolling Hills Estates, California, 1987.

Uchunguzi Kifani 3 Hadithi ya Anna, uk. 141 – Imedhaminiwa kutoka Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu kwa watu waliokimbia makazi yao, http://www.cicr.org/web/spa/sitespa0.nsf/iwpList2/ Home?OpenDocument

## Mitanziko ya Uadilifu

Mtanziko wa Uadilifu 3, uk. 145 na 147 – Imedhaminiwa kutoka kwa *Moral Reasoning*, na Victor Grassian, Prentice Hall, 1981, 1992.

Gharama ya Maisha, uk. 146 – Imechukuliwa kutoka Kohlberg, Lawrence. *Collected Papers on Moral Development and Moral Education.* Cambridge: Moral Education and Research Foundation, Harvard University Education Foundation, 1973.



## Maandiko ya Msaada kwa Ajili ya Shughuli

Muhtasari wa Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto http://www.unhchr.ch/html/menu3/b/k2crc.htm, au toleo la kirafiki la mtoto http://www.rcmp-grc.gc.ca/pdfs/NCD-poster_e.pdf

Muhtasari wa Tamko la Kimataifa la haki za Binadamu na http://www.un.org/Overview/rights.html au toleo la kirafiki la mtoto, http://www.amnesty.ie/amnesty/upload/images/attachdocuments/Universal%20Declaration%20of%20Human%20Rights%20-%20child%20friendly%20version.pdf

Muhtasari wa Muhtasari wa Makubaliano kuhusu Haki za Mtoto na Muhtasari wa Tamko la Kimataifa la haki za Binadamu uliochukuliwa kutoka Under the UN Flag, Assemblies for citizenship in Secondary Schools, UNICEF UK, 2005.

Utafiti wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa juu ya Ukatili dhidi ya Watoto, http://www.violencestudy.org

A Human Rights-Based Approach to Education for All, http://www.unicef.org/publications/files/A_Human_Rights_Based_Approach_to_Education_for_All.pdf

Will you listen? Young voices from conflict zones, http://www.unicef.org/publications/files/Will_You_Listen_eng.pdf

Uzuiaji wa machafuko na ujenzi wa amani, http://www.unicef.org/lifeskills/index_violence_peace.html

Handbook for Story Tellers. Inez Ramsey, Professor Emeritus James Madison University, http://falcon.jmu.edu/~ramseyil/storyhandbook.htm

Jinsi ya kuwasha moto kwenye kambi, http://www.luontoon.fi/page.asp?Section=8497

12 Skills for Conflict Transformation. Imedhaminiwa kutoka toleo lilitumika na Ms. Amada Benavides. Escuelas de Paz, Colombia.

World Schools Debating Championships, http://www.schoolsdebate.com/guides.asp

Taarifa juu ya mijadala, http://www.idebate.org/debate/what.php

Habari kuhusu Mandalas, http://www.mandalaproject.org/Index.html

Hadithi ya Sadako, www.sadako.org

Utengenezaji wa Filamu, http://www.filmyourissue.com/making/index.shtml

*Safe you, Safe Me*, rasilimali kwa ajili ya usalama wa mtoto. Save the Children. Mchango wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa juu ya Ukatili dhidi ya watoto, 2006. http://www.violencestudy.org/IMG/pdf/safeyoufinal.pdf

Michezo kama njia ya kuleta amani na maridhiano, http://www.toolkitsportdevelopment.org

Service Learning: Lessons, Plans and Projects. Human Rights Education Program, Amnesty International and Human Rights Education Associates, HREA, March 2007.

Appreciative Enquiry, http://appreciativeinquiry.case.edu/



## Shukurani na Marejeo kwa Ajili ya Shughuli

Mti wa Historia ya Maisha Yangu, uk. 65 – Imedhaminiwa kutoka kwa Jag & Du, Dioceses of Lund, 2004.

Kufikia Nyota, uk. 77 – Chanzo asilia kutoka toleo lilotumiwa na Fundación Escuelas de Paz, Bogotá – Colombia.

Kujiweka Katika nafasi ya Mwingine, uk. 85 – Chanzo asilia kutoka toleo lilotumiwa na Centro San Bartolomé de las Casas. El Salvador.

Taswira Yako ni Yangu, uk. 69 – Chanzo asilia kutoka toleo lilotumiwa na by Fundación Escuelas de Paz, Bogotá – Colombia.

Nderemo za kuridhika, uk. 105 – Imedhaminiwa kutoka somo la Dhamma lililofundishwa na Thai master.

Visiwa Vinavyotoweka, uk. 114 – Imedhaminiwa kutoka toleo lililotumika na Dr. Mustafa Ali, Jamhuri wa Muungano wa Tanzania, Afrika.

Mpira Hewani, uk. 115 – Chanzo asilia kutoka toleo lilotumiwa na Centro San Bartolomé de las Casas. El Salvador.

## Faharasa

**Maadili:** Ni tawi kuu la falsafa. Ni taaluma ya unyofu na mila na desturi za mtu au kikundi na hushughulikia uchanganuzi na matumizi ya dhana kama vile lililo sahihi na lisilo sahihi, wema na ubaya na dhima. Maadili ni imani, mawazo, nadharia na tafakuri ya msingi kuhusu masuala ya lazima, vinavyowezesha kuweka viwango.

**Uadilifu:** Unahusu tabia na mwenendo wa mtu, inahususha kilicho chema na kilicho kiovu, matumizi, kinachoonekana, kitendo. Uadilifu unaelezwa katika kanuni za maadili mema, mwonekano wa uadilifu mwema unaitwa "nemsi". Kuna kipengele binafsi au cha mtu kinachomaanishwa kwenye dhana ya uadilifu. Uadilifu una kipengele cha vitendo, kinachomwelekeza mtu nini cha kufanya na nini hakifai kufanywa.

**Unyofu:** Maadili mema yanayokubaliwa na mtu au kikundi – (binafsi na kitamaduni); kanuni, viwango au sifa zinazoelekeza matendo ya ubinaadamu.

### Unyofu wa mtu binafsi

Unyofu wa mtu binafsi unatokana na uzoefu na ulimwengu wa nje na unaweza kubadilika baada ya muda. Uaminifu katika matumizi ya unyofu unahusu mwendelezo wake; mtu ni mwaminifu kama anatumia unyofu wake ipasavyo licha ya upinzani au shinikizo hasi kutoka kwa watu wengine. Unyofu wa mtu binafsi unahusiana moja kwa moja na chaguo; unyofu binafsi unaelekeza uamuzi kwa kuruhusu chaguo la mtu kulinganishwa na kila unyofu unaohusiana na chaguo.

Unyofu wa mtu binafsi uliyojengwa tangu utotoni hauwezi kukubali mabadiliko. Unyofu huo unaweza kutokana na ule wa makundi mahususi au mifumo, kama vile utamaduni, dini na chama cha siasa. Hata hivyo unyofu wa mtu binafsi si wa kila mahali; jene za mtu, familia, taifa na mazingira ya historia huamua unyofu wa mtu binafsi. Hii haina maana kwamba dhana za unyofu zenyewe si za kila mahali, ukweli ni kwamba kila mtu ana fikra ya kipekee ya dhana hizo, k.v. maarifa binafsi ya unyofu unaofaa kwa jene zao; hisia na uzoefu.

### Unyofu wa Kiutamaduni

Vikundi, jamii, dini na utamaduni vina unyofu ambao hutumiwa na watu wao. Watu wanashirikiana utamaduni hata kama unyofu wa kila mtu binafsi haukubaliani moja kwa moja na baadhi ya unyofu linganifu ulioidhinishwa katika utamaduni. Hii inaonyesha uwezo wa kuunganisha vitu mbalimbali na kuchopoa vipengele vyenye manufaa kwao kutoka utamaduni mdogo mdogo wa aina mbalimbali unaowahusu.

Kama mtu anaonyesha maadili yanayotofautiana na desturi za kikundi chao, mamlaka ya kikundi yanaweza kufanya namna mbalimbali ya kumnyanyapaa au kumlazimisha mtu. Kwa mfano, kifungo cha gerezani kinaweza kutokana na mgongano wa desturi za kijamii zilizowekwa kama sheria.

### Makundi

Unyofu unaweza kupangwa katika makundi, kila kundi linaweza kujadiliwa.

> Unyoofu wa kiafya na tabia – unyofu wa kupenda starehe na anasa na Unyofu wa Kiutendaji – Unyofu wa kupenda anasa na starehe ni maadili ya mtu binafsi na hufanya kazi au kutofuata utaratibu wa jamii na kusababisha tabia ya maisha yasiyoridhisha kwa maisha ya mtu. Huwa unafanya kazi au haufanyi kazi kutegemea ukuaji wa mwili wa mtu. Unyofu wa kiafya na tabia hupatikana kupitia kuridhika kwa mtu, kutenda na uzoefu binafsi.

> Unyofu wa maadili na desturi – Unyofu wa Kijamii na Kidini/Kimila – Unyofu wa kijamii ni unyofu wa familia/kikundi na hufanya kazi au kutofuata utaratibu wa jamii na kusababisha tabia ya maisha yasiyoridhisha kwa maisha ya familia/kikundi. Huwa unaendeleza au kudhamiria mafanikio kutegemea ukomavu wa kijamii wa familia/kikundi. Unyofu wa kidini/kimila ni wa ndani ya mtu na hufanya kazi au kutofuata utaratibu wa jamii na kusababisha tabia ya maisha yasiyoridhisha kwa maisha yasiyoathiriwa na hisia nje ya familia/kikundi. Nitahamilivu au kutostahimili kutegemea ukomavu wa dini/mila. Unyoofu wa uadilifu hupatikana kupitia kutiwa moyo, mafundisho na uzoefu baina ya watu.

> Unyofu wa Kimaadili na Tabia na Mwenendo – Unyofu wa Kiuchumi na Kisiasa – Unyofu wa kiuchumi ni unyofu wa kitaifa na hufanya kazi au kutofuata utaratibu wa jamii na kusababisha tabia ya maisha yasiyoridhisha kwa uhai wa taifa. Kuzalisha mali au kutozalisha mali hutegemea maendeleo ya kiuchumi ya taifa. Unyofu wa kisiasa ni unyofu wa kitaifa na hufanya kazi au kutofuata utaratibu wa jamii na kusababisha tabia ya maisha yasiyoridhisha kwa uhai wa taifa. Kuendelea au kurudi nyuma hutegemea maendeleo ya kisiasa ya taifa. Unyofu wa kimaadili hupatikana kupitia tunzo, elimu na uzoefu usioathiriwa na hisia.

> Unyofu wa Kihistoria na Mwenendo – Unyofu wa Umbuji na Unyofu wa Kinadharia – Unyofu wa umbuji na unyofu wa binaadamu hufanya kazi au kutofuata utaratibu wa jamii na kusababisha tabia ya maisha yasiyoridhisha kwa binaadamu. Ni mzuri au mbaya (wenye maana au usio na maana) kutegemea maendeleo ya kisanaa ya binaadamu. Unyofu wa kinadharia ni unyofu wa binadamu unaoweza kuwa wa kweli au uongo (wenye makusudio au usio na maana) kwa uhai wa binadamu kutegemea maendeleo ya kisayansi ya binadamu. Unyofu wa kihistoria hupatikana kupitia msukumo (utambuzi na uzoefu wa kiubunifu).

Unyofu wote unatokana na hisia za nafsi iliyofichika na kudhamiria.

**Nemsi:** Uadilifu wa mtu wa hali ya juu. Nemsi ni tabia iliyothaminiwa kuwa bora. Kinyume cha dhana ya nemsi ni tabia mbaya.

**Dini mbalimbali:** Inahusu mjumuiko na ushirika chanya kati ya watu wa imani za dini mbalimbali (k.v. "imani") katika ngazi ya mtu binafsi na kitaasisi, na kusababisha ustahimilivu na kuheshimiana. Inatofautiana "syncretism" (mseto wa dini mbalimbali) au dini mbadala, kwamba mazungumzo huhimiza uelewano kati ya dini mbalimbali kuongeza heshima kwa wengine, kuliko kuunganisha na kupata imani mpya.

## Vifupisho

| | |
|---|---|
| **CRC** | Makubaliano kuhusu haki za Mtoto |
| **GNRC** | Mtandao wa Kimataifa wa Dini kwa Watoto |
| **MPA** | Chama cha Filamu za Sinema |
| **SMART** | Mahususi, Inayopimika, Inayotekelezeka, Halisi, Inazingatia muda |
| **UDHR** | Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu |
| **UNESCO** | Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni |
| **UNICEF** | Mfuko wa Watoto wa Umoja wa Mataifa |
| **WCC** | Baraza la Makanisa Duniani |
| **WCRP** | Mkutano wa Dunia wa Dini kwa Amani |

## Orodha ya Wajumbe wa Baraza la Dini Mbalimbali

### Mshauri wa Heshima

HRH Prince El Hassan bin Talal
Chairman, Royal Institute for Inter-Faith Studies, Jordan

### Wajumbe wa Baraza

Dr. A. T. Ariyaratne
Founder and President of the Sarvodaya Shramadana Movement, Sri Lanka

Mr. Adolfo Perez Esquivel
President of Servicio Paz y Justicia, Nobel Peace Prize Laureate, Argentina

Mr. Kul Gautam
Deputy Executive Director of the United Nations Children's Fund (UNICEF), United States

Dr. Hans Kung
President of the Global Ethic Foundation, Germany

Ms. Bibifatemeh Mousavi Nezhad
Manager, Institute for Interreligious Dialogue, Iran

Dr. Alice Shalvi
Former Chairwoman and President of the Schechter Institute of Jewish Studies, Israel

Ms. Didi Athavale Talwalkar
Leader of the Swadhyay Parivar Movement, India

Most Rev. Anastasios Yannoulatos
Archbishop of Tirana, Durres and All Albania, Greek Orthodox Church, Albania

### Wajumbe wa Baraza la Vijana

Ms. Nour Ammari
Fisher's Youth Programme, Jordan

Mr. Emanuel Mathias
Founder Movement of Youth and Children Peace Club, Tanzania

## Orodha ya Wajumbe wa Kamati ya Baraza la Dini Mbalimbali Kuhusu Elimu Maadili kwa Watoto

HE Ambassador Hasan Abu Nimah
Director, Royal Institute for Inter-Faith Studies
Advisor to HRH Prince El Hassan bin Talal, Jordan

Swami Agnivesh
Former Chairperson, United Nations Trust Fund on Contemporary Forms of Slavery, India

Ms. Charanjit AjitSingh
Freelance Inspector / Educational and Management Consultant Trustee and Vice Chair /
International Interfaith Centre, Oxford, United Kingdom

Ms. Farida Ali
Programme Officer, Office of Public Partnerships, UNICEF, United States

HE Mr. Ibrahim Al-Sheddi
Secretary-General, Saudi National Commission for Education, Culture and Science, Saudi Arabia.

Dr. Kezevino Aram
Director, Shanti Ashram, Indi

Dr. Wesley Ariarajah
Professor, Ecumenical Theology, Drew University Graduate and Theological Schools, United States

Professor Alicia Cabezudo
Director, Educating Cities Latin America, Argentina.

Ms. Meg Gardinier
Managing Director, Education and Community Partnerships, US Fund for UNICEF, United States

Mr. Andres Guerrero.
Partnerships Manager, Office of Public Partnerships, UNICEF Geneva, Switzerland.

Dr. Magnus Haavelsrud
Professor, Department of Education, Norwegian University of Science and Technology, Norway.

Dr. Heidi Hadsell
President, Hartford Seminary, United States

Mr. Vinod Hallan
Project Director, Department of Education and Skills, United Kingdom

Dr. Stuart Hart
Deputy Director, International Institute for Child Rights Development, United States/Canada

Dr. Azza Karam
Senior Culture Adviser, United National Population Fund, United States

Bishop Method Kilaini
Auxiliary Bishop of Dar es Salaam, United Republic of Tanzania

Ms. Marlene Silbert
Education Director, Cape Town Holocaust Centre, South Africa

Rev. Dr. Hans Ucko
Programme Secretary, Interreligious Relations, World Council of Churches, Switzerland

Dr. Deborah Weissman
Former Director, Kerem Institute for Teacher Training for Humanist-Jewish Education, Israel

Dr. Sunil Wijesiriwardhana
Consultant (peace, culture, media), Sarvodaya Shramadana Movement, Sri Lanka

## Waratibu wa GNRC

### Afrika
Dr. Mustafa Yusuf Ali
GNRC Office Coordinator, GNRC Africa Secretariat

### Ukanda wa Nchi za Kiarabu
Rev. Dr. Qais Sadiq
President of the Ecumenical Studies Center in Jordan

### Asia ya kati na Jamii ya Wazungu – Wahindi
Ms. Razia Sultan Ismail Abbasi
International Convenor and Founding Charter Member, Women's Coalition for Peace and Development with Dignity

### Ulaya
Ms. Marta Palma
Advisor on Children's Issues to the General Secretary of the World Council of Churches

### Amerika ya Kusini na Karibiani
Ms. Mercedes Roman
Women and Children's Desk, Maryknoll Office for Global Concerns

### Asia ya Kusini
Dr. Vinya S. Ariyaratne
Executive Director, Sarvodaya Shramadana Movement of Sri Lanka

### Israeli
Ms. Dorit Shippin
Coordinator Doumia – Sakinah. The Pluralistic Spiritual Center, Neve-Shalom / Wahat al-Salam

# VIAMBATISHO

## FOMU YA TATHMINI

### LOJISTIKI

| | Alama 1-5 (5 ndiyo ya juu) | Maoni |
|---|---|---|
| Mahali pa mkutano | | |
| Malazi | | |
| Chakula | | |
| Vifaa | | |
| Maoni mengine | | |

### MAUDHUI

| | |
|---|---|
| Je, madhumuni ya warsha yalieleweka? | |
| Je, maudhui ya vipindi yalikuwa na maana kwako? | |
| Je, mbinu za ufundishaji zilizotumika zilifaa kwa mada? | |
| Je, ulipata ugumu wowote wakati wa vipindi? Fafanua. | |

## KUJIFUNZA

| | |
|---|---|
| Ni jambo gani kuu ulilojifunza katika warsha? | |
| Je, unaweza kutumia ulichojifunza kwa muktadha wako mwenyewe?<br><br>(binafsi, kijamii, kitaalamu, kitaasisi). | |
| MAPENDEKEZO | |

## MATRIKI KWA AJILI YA TATHMINI YA MATOKEO

| A. Ninachokijua | | | |
|---|---|---|---|
| | Ndiyo | Hapana | Maoni |
| Najua uwezo na stadi zangu | | | Kama jibu lako ni ndiyo, je unavitumiaje? |
| Naona fahari kwangu mwenyewe, familia yangu, utamaduni wangu na imani zangu | | | Eleza |
| Nawajua watu wa utamaduni na imani za kidini nyingine | | | Kama jibu lako ni ndiyo, je, unaelewa nini kuhusu watu hao? |
| Najua tofauti kati ya utamaduni wangu mwenyewe na imani na ule wa watu wengine | | | Kama jibu lako ni ndiyo, taja tofauti mbili za baadhi ya utamaduni na imani za kidini ulizowahi kusikia |
| Naelewa matatizo ya ugomvi na kukosa kuelewana shuleni kwangu na maeneo ya jirani | | | Kama jibu lako ni ndiyo, ni matatizo gani hayo? |
| Naelewa sababu za migogoro mikuu na dhuluma katika jamii yangu | | | Kama jibu lako ni ndiyo, taja mfano mmoja na andika sababu zake |
| Najua kuhusu juhudi za kuleta amani katika jamii yangu | | | Kama jibu lako ni ndiyo, ni juhudi zipi hizo? |

| B. Jibu si kweli au kweli kwa maelezo yafuatayo na thibitisha majibu yako | | | |
|---|---|---|---|
| Maelezo | Si kweli | Kweli | Kwa nini? |
| Ni vizuri mtu kuficha mawazo na imani yake kama watu wengi waliopo wana maoni na mawazo tofauti | | | |
| Wakati mtu anapozungumza nami nasikiliza kwa makini lugha yake ya mwili, mkao, anavyoangalia, kiimbo, sauti, ishara ya uso, n.k, sana kama ninavyozingatia maneno | | | |
| Ni rahisi kuwa rafiki na mtu mnayeshirikiana naye imani na namna ninavyofikiri | | | |
| Ni vizuri kupuuza mawazo ya watu yanapogongana na imani na kanuni zangu | | | |
| Mtu wa barabarani aliyevaa kimaskini huenda akaniumiza au kuniibia kitu fulani | | | |
| Uamuzi ni lazima ufanywe kwa msingi wa namna unavyoathiri watu wengine | | | |
| Ninapokasirika natumia muda kutafakari na kutuliza hasira kabla ya kufanya chochote | | | |

| C. Fikiria kuhusu hali zifuatazo na eleza namna utakavyofanya au kushughulikia hali hizo | |
|---|---|
| Mtu fulani anafanyia mzaha imani yako na mila na desturi za utamaduni wa familia yako. Je, utafanya nini? | |
| Inakubidi ufanye kazi katika timu ya mtu usiyependa namna anavyotenda na hukubaliani na mawazo yake. Utawezaje kuifanya kazi hiyo? | |
| Unabishana na rafiki aliyekuudhi. Huelewi kwa nini rafiki huyo amekufanyia hivyo. Je, unajaribu kutanzua tatizo hilo? Kama ni hivyo, utajaribu vipi kulitanzua? | |
| Darasani kwako kuna tatizo la ubaguzi, lisilokuhusu moja kwa moja. Je, utajaribu kufanya lolote kuhusu tatizo hilo? Kama ndiyo, utafanya nini na kwa nini? | |
| Mtu kutoka utamaduni, dini na imani tofauti anawasili shuleni kwako. Wanafunzi wengine wote wanazungumza mambo mabaya kuhusu mtu huyo. Anavaa au kufanya tofauti kwa wanafunzi wengine wengi shuleni kwako. Hufurahishwi na mtu huyo ingawa anajaribu kuwa rafiki yako. Unajua kwamba, kama utakuwa rafiki yake, marafiki wako wengine hawatapenda kudumisha urafiki wako. Utafanya nini? | |
| Umefanya uamuzi unaowaathiri vibaya watu wengine. Hutaadhibiwa kama utaamua kutofanya lolote kuhusu jambo hilo. Je, utafanya jambo lolote kurekebisha madhara uliyosababisha? Kama utafanya hivyo, ni jambo gani utakalofanya? | |

## Maelezo

## Maelezo

***Kujifunza Kuishi Pamoja ni Programu*** ya utamaduni na dini mbalimbali kwa elimu ya maadili, iliyotayarishwa kwa kuchangia katikautimizaji wa haki za mtoto na maendeleo kamili na yenye afya ya mwili,akili, roho, uadilifu na kijamii na kupata elimu kama ilivyoandikwakwenye Makubaliano ya Umoja wa Mataifa kuhusu Haki za Mtoto (CRC), katika ibara ya 26.1 ya Tamko la Kimataifa la Haki za Binadami (UDHR), katika Azimio la Dunia kuhusu Elimu kwa wote na Malengo ya Maendeleo ya Milenia (MDG).

***Kujifunza Kuishi Pamoja ni Programu*** kinawapa viongozi wa vijana na waelimishaji duniani kote zana kwa ajili ya program ya utamaduni ni dini mbalimbali na elimu ya maadili, ambapo watoto na vijana wataweza kukuza hisia thabiti ya maadili. Kimetayarishwa kwa ajili ya kuwasaidia vijana kuelewa na kuwaheshimu watu wa utamaduni na dini nyingine na kulea hisia zao kuhusu jumuiya ya dunia. Katabu hiki cha kiada kimetayarishwa kwa ushirikiano wa karibu na UNESCO na UNICEF.